Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 4 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Silvester M. Mabumba) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. ABDULKARIM I. H. SHAH – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Kuhusu Makadirio ya Makamu wa Rais (Mazinigira) kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 128

### Fedha kwa Ajili ya Fidia ya 20% ya Vyanzo vya Mapato Vilivyofutwa na Serikali.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU** aliuliza:-

Taaarifa rasmi ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida inaonyesha kuwa imepokea toka Serikalini shilingi 302,000,000/= katika mwaka wa fedha 2008/2009 za kulipa vijiji vyote vya Halmashauri kama fidia 20 % ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa na Serikali miaka ya nyuma.

Kati ya pesa hizo shilingi 96,000,000/= tu zililipwa zikabaki Shs 205,000,000/= ambazo hazijulikani zimetumika vipi lakini ukweli ni kwamba hakuna kijiji hata kimoja katika Jimbo la Singida Mashariki, kimepata fedha yoyote kwa mwaka 2008/2009.

(a) Je, fedha hizo za fidia ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilikiri kupokea zilipelekwa wapi na nani au kwa mamlaka ipi iliyoidhinisha matumizi mengine ya fedha hizo?

(b) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Singida imepokea kiasi gani cha 20% ya fedha ya fidia kwa mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011?

(c) Je, ni vijiji vipi katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambavyo vimelipwa fedha yoyote kwa fidia tangu mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kwamba kwa kipindi cha 2008/2009 hadi 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilitakiwa kupeleka shilingi 302,000,000/= kwenye vijiji ambazo ni 20% ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa. Aidha ni kweli shilingi 96,000,000/= tu zilipelekwa katika Vijiji na shilingi 205,000,000/= hazikupelekwa kupitia ridhaa ya Baraza la Madiwani, Halmashauri ilituma fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari, kukamilisha ujenzi wa miradi ya maji ya vijiji, kuendesha vikao vya kisheria ngazi ya Halmashauri na kugharamia shughuli za ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na fedha hizo kutopelekwa katika vijiji, Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa tarehe 27 Oktoba, 2011 na tarehe 20 Machi, 2012 iliagiza Halmashauri kuhakikisha fedha hizo zinapelekwa kwenye vijiji kama

ilivyokusudiwa. Aidha, OWM - TAMISEMI kupitia barua yenye kumb.Na.CBC.239/265.01 ya tarehe 2 Julai, 2012 iliagiza Halmashauri hiyo kuhakikisha fedha hizo zinapelekwa kama ilivyo katika maelezo ya Kamati na Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilipokea fedha shilingi 302,000,000/= za fidia kutoka HAZINA kwa mchanganuo ufuatao:- 2008/2009 shilingi 110,836,600/=, 2009/2010 shilingi 106,813,9988 na mwaka 2010/2011 shilingi 84,349,412/=.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopelekwa katika Kata za Jimbo la Singida Mashariki kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:-

Nitataja zile Kata tu Kata ya Mungonyi ilipelekewa shilingi milioni mbili na pointi moja, Kata ya Musigaha ilipelekewa shilingi milioni mbili na pointi sita, Kata ya Igungi Ilipelekewa shilingi milioni mbili na pointi moja, Kata ya Mtuntu mbili na pointi moja, Kata Mngaa ilipelekewa shilingi milioni mbili na pointi saba, Kata ya Iuyu ilipelekewa shilingi milioni tatu na pointi tisa, Dungunyi Shilingi milioni moja na pointi tisa na Isuna ni Shilingi Milioni moja na pointi inane jumla ni shilingi milioni kumi na tisa, laki tano na themanini na tisa mia nne na kumi na moja takwimu zingine kama benki na akaunti nimezionyesha.

**MHE. TUNDU A.M LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida nimeingia kwenye Bunge na

kwenye Kamati hiyo nimefuatilia hizo fedha. Hakuna kijiji hata kimoja ambacho kimewahi kupewa hata senti moja ya hizi fedha ambazo Waziri anadai zimepelekwa viijijini sasa maswali yangu ni mawili.

(a) Kwanza ni je, Serikali iko tayari kuamuru uchunguzi maalum yaani *special audit* kwa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuhusiana na fedha hizi?

(b) Swali la pili ni je, kama ni kweli hizi fedha zimepelekwa kwenye Kata kwa nini wakati waraka wa Serikali unaagiza zipelekwe kwenye vijiji siyo kwenye Kata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *concerns* za Mheshimiwa Lissu mimi ninazielewa nimewaita mimi ofisini kwangu toka juzi na jana mpaka Mwenyekiti wa Halmashauri mwaka huo wa 2008. Humu ndani ninapokiri hapa nina *quote* mimi ripoti ya *CAG,* nina *quote* mimi ripoti ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida, nina *quote* mimi hata taarifa iliyoletwa na *Local Authorities accounts Committee* iko hapa na zote nimekuja nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokubaliana naye ni hiki na ninataka kieleweka hapa ukitafuta hela zilizokwenda kwa maana ya 20% kwa ajili ya kwenda ku- *run office* kule hutaiona, hutaiona hiyo hela, ukitafuta kwa maana ya miradi iliyokwenda pale na orodha yote kwasababu yeye anauliza pale Singida Mashariki na wakati huo Singida Mashariki haikuwepo. Kulikuwa kuna Singida Kaskazini na Singida Kusini ikaja

ikavunjika lakini mimi nikatafuta pia kwenye hiyo Singida Mashariki wakati huu wa sasa je ni vijiji gani vimeguswa hapo ndiyo kikaja na hiki kiasi anachozungumza hapa Mheshimiwa Lissu.

Tumezungumza na *Regional Commissioner* nikamwambia ni kinyume cha utaratibu kutokupeleka hizo shilingi milioni mia mbili na tano ninataka niiweke vizuri hapa ili iweze kueleweka vizuri.

Ukisema hela zimeibiwa hapa nimeonyesha na namba za akaunti ambazo hela hizo zimeingia na Mheshimiwa Lissu nimekupa nina orodha yote ya Halmashauri nzima kwa kipindi chote kinachozungumzwa ninayo hapa.

Sasa habari ya kusema tunaenda kufanya uchunguzi ninayo taarifa ya *CAG* Wabunge tutafute kwenye taarifa ya *CAG ,CAG* ana *confess* anatamka hizi hela kuwa zilizokwenda pale ni milioni tisini na sita tu, milioni mia mbili na tano hazikwenda ambapo Mheshimiwa Tundu Lissu yuko *right* ni kusema hivi *reallocation* hiyo ni nani alitoa kibali hicho ndicho ninachokizungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sisi tunakiri hapa hela zilizokuja kwa ajili ya kujenga madarasa na kwa ajili ya kujenga vituo vya Afya Halmashauri ikakaa chini na Madiwani wakati huo Mheshimiwa Lissu hakuwa Mbunge.

Jambo hili ni jambo ambalo limezungumzwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida na jambo hili ni jambo ambalo limezungumzwa katika Halmashauri

ya Wilaya ya Singida na maoni yangu katika hili kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali hili lilipaswa lijibiwe hukohuko kwenye Halmashauri husika.

Halmashauri ndiyo wao wenye *mandate* kuchukua Sheria Namba 7 na Namba 8 ya mwaka 1982 ambayo ilikuja ikarejeshwa tena mwaka 2002 chenye Mamlaka na Madaraka ya kuamua hela hizi zilitumikaje ni Halmashauri lakini kwa utaratibu ufuatao:-

Kupata ridhaa ya Mkuu wa Mkoa, kupeleka kwa *Permanent Secretary* katika TAMISEMI *in corroboration* na Katibu Mkuu wa *Treasury* wao ndio wakubali hela zibadilishwe. Ndiyo maana nimeagiza na nilitaka nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunasema hapa kuwa ni marufuku na Halmashauri haiwezi kubadili matumizi ya hela za Serikali kinyume na ilivyopitishwa hapa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti la pili, ninamalizia kwa kuwa ninajua lilikuwa na *sensitivity act* na wale wengine wanaofanya hivyo tumeshawaonya na barua tumeandika kwa nini zilikwenda kwenye Kata.

Ukiangalia ripoti waliotuletea tumetafuta hivi vijiji vyote alivyovisema Mheshimiwa Lissu na hili ninalisema kabisa rafiki yangu Lissu mimi kwenye hili wala sikupingi nimekwenda na kutafuta vijiji vyote vile havina akaunti, vijiji vilivyokuwa na akaunti, akaunti zile kwasababu zilikuwa haziingizwi hela ziko *dormant* wakawa wana peleka kwenye Kata kwasababu kwenye Kata ndiko kulikokuwa na akaunti ambazo zinaonekana kuwa ziko *active.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeandika hapa namba na akaunti zilizoingia kama bado Mheshimiwa Mbunge bado ana *doubt* jambo hili Ofisi ya Waziri Mkuu iko tayari kuendelea kushirikiana na wewe mpaka tupate ukweli wa jambo hili. Lakini ninataka nikuthibitishie kuwa mimi nimewa *squeeze* wale jamaa wote wamekuja pale na ninataka nikuambie nina uhakika na jambo ninalolizungumza. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, kwa vile tatizo la Singida ni sawa na Mbarali na Halmashauri nyingi zimekuwa ni vigumu sana kutenga hizo 20%.

Je, wakati sasa umefika wa kurejesha mfumo wa zamani kwamba vijiji vibaki na mapato yao kuliko hivi sasa vinapata shida sana kuendesha ofisi zao ukizingatia kuwa inatakiwa wawalipe Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa vijiji wapate angalau hata sabuni sasa hivi inashindikana.

Je, Serikali iko tayari sasa kuona kuwa utaratibu wa zamani wa kuacha vyanzo vya mapato kwenye vijiji ili vijiendeshe kwamba umefika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawali linalofuata hapa atajibu naibu Waziri wa Fedha. *General purpose grand* imekwisharejeshwa imerudi tena na Serikali imekubali ombi letu kuwa turejeshewe tena hizi hela na ziende kwa utaratibu ule uliokuwa unatumika toka huko nyuma. Ninataka nimthibitishie Mbunge kuwa akisema tunarudisha vile vyanzo aelewe kuwa vyanzo

vilivyofutwa vilikuwa ni vile vyanzo vinavyohusu vitumbua, maandazi, samaki wa kukaanga, mchicha ambavyo vilionekana kuwa vina kero. Sasa leo tukisema tunarudisha tena maana yake ni kuwa tunarudisha tena kero ile ile hatuwezi kurudi tena huko.

Tanzania hapa tunaelewa kuwa tunayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inayowajali watu wanyonge. Hawa siyo watu wanaofanya biashara ili kupata faida kibao, hawa ni watu ambao wanaangalia watoto wao na hawa akina Mama hawawezi kuonewa na hakuna kuwarudishia tena hizo kero lakini tumerudisha *General Purpose Grand* na haya makisio yatakuwa yanakwenda kule na tutaagiza hapa kuwa hela ziende moja kwa moja mpaka vijijini naomba Wabunge mtusaidie asiyepeleka pale tutashuka naye jumla jumla. *(Vicheko)*

Na. 129

**Kuondolewa kwa Fidia ya Mapato ya Halmashauri**

**Mhe. Zabein M. Mhita** aliuliza:-

Serikali Kuu imeondoa fidia ya mapato ya 20% iliyokkuwa inatolewa bila kujali kuwa uwezo wa mapato wa Halmashauri nyingi ni mdogo:-

Je, Serikali haioni kwamba kuwa hatua hiyo inadhoofisha utendaji wa miradi mingi ya maendeleo kutotekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu swali namba 31 katika Mkutano wa saba wa Bunge ambalo lilikuwa na maudhui sawa na swali hili, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri iliyopunguzwa imerejeshwa katika Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Kiwango kilichotengwa kimeongezeka kutoka shilingi 10.8 bilioni zilizotengwa mwaka 2022/20212 hadi shilingi 63.5 bilioni zilizotengwa mwaka huu 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshwaji wa fidia hii ulifanyika baada ya kutathimini athari za kupunguzwa kiwango hicho cha ruzuku, hususan kwa Halmashauri nyingi kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji hali ambayo siyo tu ilidhoofisha utekelezaji wa shughuli bali iliathiri utendaji wa siku hadi siku wa shughuli nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali kuwa hatua hii ya kurejesha ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato ikienda sambamba na Halmashauri hizi kuzidisha jitihada ya kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani itaziwezesha Halmashauri hizi

kuwa na mapato zaidi yatakayoziongezea uwezo wa kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Awali ya yote naomba niishukuru Serikali yetu kwa kurudisha fidia hii ambayo wameona ni ya msingi kabisa, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeona umuhimu wa kurejesha fidia hii. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kufidia fidia hii ambayo iliondolewa mwaka jana wa fedha 2011/2012, kwa sababu kuna madhara makubwa ambayo yametokea katika Halmashauri ya Kondoa. Mfano, Halmashauri ilishindwa kulipa madeni ya wazabuni, Halmashauri ilishindwa kulipa madeni ya watumishi, Halmashauri ilishindwa pia kupeleka ile asilimia 20 vijijini.

(i) Je, Serikali sasa itafidia fidia hii kutokana na umuhimu wake?

(ii) Kama alivyokiri Waziri umuhimu wa fidia hii. Je, sasa Serikali itapeleka hiki kiasi cha fidia ambayo imetengwa kama ilivyo badala ya kupeleka pungufu na kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Kondoa ilipaswa kupata milioni 654.9.

**MWENYEKITI:** Mhehsimiwa uliza swali usitoe hotuba.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ikapeleka milioni 180. Je, sasa Serikali itapeleka fidia hiyo kama ilivyopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Serikali kuwa tayari kufidia viwango vya mwaka jana, kwa mwaka huu wa Bajeti inazungumzia kurejesha asilimia 20 kuanzia Bajeti ya mwaka huu. Lakini pamoja na hayo Serikali inaweza ikaliangalia kama inawezekana na iko katika uwezo wa Bajeti kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukafidia yale maeneo ambayo ni muhimu na yameshindikana kabisa kutekelezwa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri swali la pili linahusiana na hilo la kwanza kwa hiyo itabidi kuangalia na mimi nipo tayari kukaa na Mbunge kuangalia uwezekano wa kufanya hivyo.(*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Suala hili la ushuru kweney Halmashauri zetu kwa kweli ni suala nyeti na ya muhimu sana.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea imekuwa ikizalisha chakula na kwa mwaka jana imezalisha karibu tani 67,000 za mahindi na kuwalisha Watanzania na hivyo kupunguza tatizo la njaa, na kwa kuwa zao hili la mahindi limekuwa ni zao la biashara katika Halmashauri yetu na linatakiwa lipatiwe ushuru (*SES)* katika Halmashauri hii.

*NFRA* ndiyo wanaotakiwa kutulipa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Serikali ingawa mpaka sasa hawajatulipa jumla ya milioni mia tatu sitini na mbili, laki saba na arobaini na nne. Mpaka sasa katika Halmashauri yetu na kutusababishia hasara kubwa.

Je, Waziri yupo tayari sasa kutulipa ushuru huo ili kuendelea kuipa moyo Halmashauri yangu kuendelea kuzalisha chakula kuilisha nchi hii kuondokana na njaa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri na ni kweli kama ni wajibu wa NFRA kulipa deni hili basi tutakaa tuangalie uwezekano wa kuongea nao ili ushuru huu ulipiwe kama ambavyo sheria inasema. *(Makofi)*

Na. 130

**Matangazo ya Udanganyifu na Upotoshaji katika Vyombo vya habari.**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la matangazo mengi katika vyombo vya habari yaliyojaa udanganyifu na upotoshaji wa jamii kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo ambalo linazidi kukua?

(b) Je, ni lini sera mpya ya Utangazaji na sheria mpya ya vyombo vya Habari zitakuwa

tayari ili kuziba mianya yote inayosababisha udanganyifu huo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya vyombo vya Habari, magazeti, radio na televisheni vinatoa matangazo yaliyojaa udanganyifu na yanayopotosha jamii. Wizara yangu kupitia kwa Msajili wa Magazeti imekuwa ikiwaita wahusika na kuwataka kuyafanyia marekebisho matangazo yaliyojaa udanganyifu kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazolinda maadili ya taalum hiyo pamoja na nchi kwa ujumla.

Kwa wale wanaokaidi Wizara yangu imekuwa ikiwachukuliwa hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaonya, kuyafungia kwa muda au kuyafuta katika orodha ya gazeti la msajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa radio na televisheni Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *TCRA* kupitia Kamati ya maudhui, inafuatilia maudhui ya matangazo yanayotolewa.

Endapo matangazo yenye mwelekeo wa upotoshaji wa jamii kinyume na sheria na kanuni za utangazaji yanapojitokeza, chombo husika huitwa mbele ya Kamati ya maudhui na kikipatikana na makosa hatua mbalimbali huchukuliwa ikiwemo karipio, onyo, au faini na hata kunyanga'anywa leseni.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya habari na utangazaji ipo kuanzia mwaka 2003. Sera hiyo inayosimamia utangazaji imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara kutegemeana na mahitaji ya nyakati na mabadiliko ya teknolojia. Hivi sasa sera hiyo inasubiri kufanyiwa marekebisho kidogo ili kukidhi mahitaji ya itifaki ya soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Kwa upande wa sheria mpya ya vyombo vya habari ni kwamba rasimu ya sheria ya kusimamia vyombo vya habari imekamilika katika ngazi ya Wizara. Mapendekezo haya yanasubiri maamuzi ya ngazi za juu Serikalini. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ya ufanisi, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa pamoja na kuwepo kwa sheria hizi zinazohusu usalama wa chakula, *Consumer Prote*ction na usalama kwenye madawa, bado tunaendelea kushuhudia matangazo mengi yanayopotosha Umma na hivyo kuwaondolea haki ya kupata taarifa sahihi watumiaji wa huduma hizi?

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni vizuri ikaanzisha mfumo ambao utakuwa ni *self regulating* kwa kuanzisha chombo ambacho kitakuwa ni *advertising standard council* ambacho katika nchi 71 Ulimwenguni kimeweza kuleta mafanikio makubwa kuondokana na tatizo hili?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka niseme kwamba Serikali inapokea ushauri wake na tutaendelea kuufanyia kazi. Lakini nataka nisistize tu kwamba wamiliki wa vyombo vya habari na magazeti wazingatie sera, sheria na kanuni za uandishi wa habari. Hili ni pamoja pia na kuhakikisha kwamba vyombo hivi vinakuwa na waandishi wenye taaluma na uweledi wa tasnia ya utangazaji. Lakini pia kuhakikisha kwamba wanazingatia maadili na miiko ya utangazaji na uandishi wa Habari.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Waandishi wa Habari wamekuwa wakifanyakazi katika mazingira magumu sana, na waandishi wa Habari wengine huandika taarifa za jamii katika kurubuniwa ili kupata chochote.

Je, Serikali ina mikakati gani kuwawezesha Waandishi wa Habari nao waweze kuandika habari zao kwa ufasaha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lipo tatizo la Waandishi wa Habari na Serikali jambo la kwanza ni

kuona kwamba tunakuja na sheria hapa Bungeni nzuri kwa vyombo vya habari. Lakini pia niwaombe wamiliki wa vyombo vya habari kuona kwamba wanawaajiri na kuwalipa vizuri waandishi wao wa habari na waandishi wenyewe pia kuepuka suala la rushwa katika uandishi wa habari.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina swali moja dogo la nyongeza kuhusu vyombo vya habari. Katika televisheni vipindi vingi au baadhi ya vipindi vya burudani huwa haviendi sambamba na utamaduni wanchi yetu.

Je, Serikali kupitia Wizara yetu hii inachukua hatua gani ili kuondosha vipindi hivyo na kurejesha hali ya utamaduni wa nchi yetu kama ilivyokuwa hapo zamani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara imejipanga na ina chombo cha Kamati ya maudhui na Tume ya mawasiliano kuchunguza endapo kuna filamu au vipindi vinavyokiuka na inapotokea basi wahusika huitwa na kuonywa au kupewa faini au karipio kali.

Na. 131

**Sheria iliyounda TFC Kubadilishwa**.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

T.F.C. ni chombo cha Serikali kinachoweza kuwezeshwa na kusambaza mbolea yenye ubora na kwa wakati; na kwa kuwa sasa kuna gesi ambayo inaweza kusaidia uanzishwaji wa mbolea za kemikali:-

Je, kwa nini sheria iliyounda *T.F.C.* isibadilishwe ili chombo hiki sasa kitafute wadau na kuanzisha kiwanda cha mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maamuzi ya kufunga kiwanda cha uzalishaji wa mbolea kilichokuwa Tanga mwaka 1995, kitengo cha mauzo cha kampuni ya mbolea Tanzania *(TFC)* Dar es Salaam kiliundwa upya na kuwa kampuni kwa kutumia sheria ya makampuni *(Company Ordinance Act, Cap. 212).*

Hii ilitokana na uwezo mkubwa wa *TFC* katika miundombinu ya usambazaji, wataalam wenye uzoefu na imani kubwa iliyo nayo kwa wakulima. Kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa mbolea bora kwa wakulima na kwa wakati, Serikali iliamua pia kutobinafsisha au kuuza mali zilizokuwa za kiwanda cha *TFC* za usambazaji mbolea ili kampuni ya TFC iliyoundwa iendelee kutumia mali hizo katika kutekeleza jukumu lake hilo ambalo ni nyeti sana kwa

uchumi wa nchi. Kampuni ya *TFC* imeendelea kuwa shirika la umma chini ya Serikali hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Serikali ilikwishajitoa katika uzalishaji na uendeleshaji wa moja kwa moja wa biashara na kuachia sekta binafsi jukumu hilo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha vivutio vilivyoko nchini ili sekta binafsi ichukue jukumu la kuwekeza.

Hii ni pamoja na kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda mbalimbali hasa vinavyotumia mali ghafi zinazopatikana nchini ikiwa ni pamoja viwanda vya mbolea vinavyotokana na madini ya fosfeti ya Minjingu na viwanda vitakavyotumia gesi asili kama malighafi, Serikali imekuwa inahamasisha uwekezaji katika sekta hiyo.

Juhudi hizo zinaendelezwa na kuna mategemeo makubwa ya kuanzishwa kiwanda cha kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi asili katika siku za usoni, jambo ambalo litawezesha uzalishaji humu nchini wa mbolea kuu kwa maana ya *(super fertilizer - NPK)* inayotegemea malighafi yake kwa kiasi kikubwa kutokana na rasilimali za humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, na kwa hali ilivyo hivi sasa, ni vizuri kampuni ya *TFC* ikaendelea na jukumu lake la kusambaza mbolea nchini hasa sehemu ambazo hazifikiki kirahisi ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbolea kwa wakati. Suala la kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mbolea ni zuri ila katika mazingira ya sasa ushiriki wa *TFC* utakuwa na tija

zaidi kama ukizingatia ushiriki wa pamoja wa sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*). *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bado hata sioni ni kwa sababu gani *TFC* iendelee kupewa jukumu la kusambaza mbolea wakati hata hiyo mbolea yenyewe inayosambazwa haipo na haipatikani.

Lakini tulishapitisha sheria ya *PPP* hapa Bungeni, ambayo inairuhusu Serikali kuingia ubia na wawekezaji wengine wowote katika kuimarisha miradi mikubwa ya kuibua uchumi, kwa imani yangu miradi ya kuinua uchumi ni pamoja na kilimo. Kwa kuwa, tatizo hili la upatikanaji wa mbolea tena kwa bei kubwa sabisa limekuwa ni mzigo mkubwa kwa wakulima wa Tanzania na malighafi kama gesi na fosfeti kule Minjingu imeshapatikana. *(Makofi)*

Je, kwa nini Serikali isifanye maamuzi magumu na ya haraka kujenga kiwanda cha mbolea kule Mtwara kwa kutumia gesi hasa kwa kushirikisha mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo tunayo na ingeweza kuokoa wakulima maskini wa nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali imeonesha kabisa kwamba wakulima wetu wamekuwa wakisambaziwa mbolea ambazo hazina ubora wakiwemo wakulima wengi wa Jimbo la Peramiho.

Je, Serikali kwa kuwa sasa haijajenga kiwanda imeacha biashara ya mbolea kuwa huria, iko tayari kuwafidia wakulima wanaposambaziwa mbolea ambazo hazina kiwango, kwa kuwa hatuna kiwanda nchini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyojielekeza kwenye majibu yangu ya msingi nilisema Serikali kwa sasa hivi tumejitoa moja kwa moja kushiriki kwenye masuala ya *production* kwa maana ya kuingilia kati moja kwa moja, lakini mshirika wa *TFC* kwa niaba ya sekta ya Umma na ndiyo msingi wa *PPP.*

Mheshimiwa Mbunge amesema kama kuna sheria ya *PPP* kwa nini haifanyi kazi. Sheria ya *PPP* inafanyakazi kwa hiari ya pande zote mbili.

Kwa sasa hivi naomba nimhakikishie kwanza kabisa kwamba kiwanda cha Minjingu kinazalisha hiyo mbolea ya *super fertilizer* ya *NPK* sasa hivi, ambayo ina naitrojeni, fosfeti na potashium na sulfa na vitu vile vyote.

Mbolea ambayo sasa imetoa ile mbolea ya kawaida ya *rock fosfeti* kwenda kwenye *super fertilizer* ambako ndiko tunakotaka tuelekee. Sasa kwa huko mbele ya safari kwa sasa hivi ile *combination* ya *UREA* inatoka nje ya nchi lakini tukifika huko mbele ya safari ambapo tunatarajia tuwe na uzalishaji wa *UREA* ambayo ni mbolea inayotokana na gesi asili ikizalishwa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema fikra ya mbele ni kwamba ile *super fertilizer NPK* itazalishwa nchini kutokana na rasilimali zinazotokana humu nchini.

Kwa sasa hivi tuna mbolea ya *NPK*, Minjingu mazao inazalishwa Tanzania kampuni inasema ina uwezo wa kuzalisha mpaka tani laki moja, lakini ile *element* ya *urea* inayochanganywa mle ndani inatoka nje. Kwa hiyo, fikra ni kwamba tutakapokuwa na uzalishaji wa gesi asili na kampuni nyingi zimeonesha nia ya kuzalisha *Urea* Mtwara.

Tutakapokuwa na *combination* hiyo naamini ile *combination* ya *NPK* ambayo kwa sasa inazalishwa na Minjingu Mazao kwa gharama ambayo bado ni ndogo kuliko inayotoka nchi za nje bado itakuwa na gharama ndogo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imefanya maamuzi itasapoti kiwanda cha Minjingu lakini pia kutengeneza mbolea ya *NPK,* lakini pia ita-*support* mtu yeyote atakayekuja na watu kama watatu au wannne wameshakuja kwa fikra ya kuzalisha *Urea Mtwara.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kwamba mbolea hazina ubora, hili naomba niungane na Mheshimiwa Jenista moja kwa moja. Kwa mkakati huu sheria ya pembejeo ya mwaka 2009 na sheria ambayo tutakuja kuiboresha Bungeni *Inshallah* mwezi wa kumi na moja, tunakuja na mdhibiti wa mbolea.

Kama tulivyokuwa na *EWURA* kwenye mafuta sasa tunakuja na mdhibiti wa mbolea. Tayari Mdhibiti wa Mbolea imeanza kufanyakazi na hivi ninavyozungumza Mdhibiti Mkuu wa mbolea Mama Suzan Ekera yupo Mkoa wa Ruvuma hivi sasa anafuatilia mbolea yote inayosambazwa Mkoa wa Ruvuma ili tujihakikishie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana na Wakuu wa Mikoa wiki iliyopita kwamba atakapotoka Mdhibiti wa Mbolea na Wakuu wa Mikoa waende ili kuhakikisha kwamba huu mchezo wa kuepeleka mbolea ya ovyo ovyo kwa wakulima.

Watu wanatengeneza hela za ajabu kupitia migongo ya wakulima ife kabisa na tunaamini kwamba tutakapopitisha Bajeti yetu hapa Wabunge mkatuunga mkono, tunaamini kwamba Mama Suzan Ekera na watu wake wote watapata pesa za kutosha ili kumaliza mchezo huu *once and for all. (Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona, ningependa kujua Serikali ina mkakati gani sasa wa kuharakisha utaratibu wa upelekaji wa pembejeo katika maeneo haya ya kilimo hasa ukizingatia sasa hivi maeneo yote ya Ukanda wa Kusini hatujapata sulphur kwa ajili ya Mikorosho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mangungu kwamba tatizo la kuchelewa kwa *Sulphur* kama alivyo yeye mdau wa kKorosho na mimi pia ni mdau wa Korosho. Tatizo la kuchelewa mbolea ya Sulphur ni tatizo la *syndication.* Tuna wafanyabiashara wachache ambao wamedhibiti biashara ile ya *sulphur* na matokeo yake wanaleta *Sulphur* kwa wakati wanaotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekutana na Mama Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho na Wajumbe wake tumekubaliana kwamba kwa mwaka ujao wa fedha huu tunaokwenda 2012/2013 ifikapo mwezi wa tatu, mwezi wa nne, mtu hajaleta *Sulphur* mkataba umekufa. Huwezi kuleta *Sulphur* mwezi wa 8 wakati watu wanahitaji Sulphur mwezi wa sita. Kwa hiyo, mchezo huu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Murtaza kwamba kuanzia Bodi, Mfuko na Wizara tunajipanga ili mchezo huu mwaka huu uwe mwisho. (*Makofi*)

Na. 132

**Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Serikali inakosea inapoandaa mipango ya kilimo nchini bila kuzingatia kuwa misimu ya mvua hutofautiana kutoka mkoa au Ukanda mmoja kwenda mwingine:-

Je, Serikali itarekebisha lini hali hiyo ili kuwawezesha wakulima kupata mbolea mapema kabla ya msimu wa mvua wa eneo husika haujaanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba misimu ya mvua inatofautiana kutoka ukanda mmoja kwenda mwingine. Kwa mfano, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini msimu wa kilimo huanzia mwezi Septemba hadi Novemba wakati Kanda ya Kaskazini msimu wake huanza mwezi Februari hadi Aprili. Hali hiyo hupelekea kuwepo na mahitaji tofauti ya pembejeo kwa wakulima katika kanda hizo, kutokana na mazoea ya wakulima kutonunua pembejeo hadi msimu wa mvua unapokaribia na wengine kusubiri hadi vocha za ruzuku ya pembejeo ziwafikie, kunachangia makampuni ya usambazaji pembejeo kuona kuwa ni hasara kuhifadhi pembejeo kwenye maghala ambayo yanakodishwa kwa muda mrefu kwani huwasababishia hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na kuchelewa kwa pembejeo za kilimo, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Wizara yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuendelea kuyashawishi makampuni ya pembejeo kuhakikisha kwamba pembejeo zinakuwepo

Mikoani na Wilayani maana ile *(storing facility)* kwa kipindi muafaka kwa kuzingatia mahitaji ya kupandia na kukuzia ili kuwawezesha wakulima kuzipata muda watakapozihitaji.

Pili, kuishauri Mikoa kuhakikisha kwamba wanahakiki kiasi cha pembejeo kilichoko katika Mikoa yao na endapo kutakuwa na dalili za upungufu wawasiliane na Wizara pamoja na kampuni za pembejeo moja kwa moja. Aidha, Mikoa na Wilaya imehimizwa kuwaelimisha wakulima kujenga mazoea ya kununua pembejeo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Wizara kwamba endapo ufuatiliaji huu wa pamoja utatekelezwa kwa ufanisi baina ya pande zote husika, tatizo hili litapungua kama siyo kuliondoa kabisa. Aidha, pia ni matarajio yetu kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge pamoja na na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa tutanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha azma hii ya kuwafikishia wakulima pembejeo kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekuwa inachangia wakati mwingine kuweza kuya-*discourage* makampuni ambayo yamekuwa yaki-*supply* pembejeo kama mbolea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa mfano mwaka jana makampuni yaliweza ku-*supply* mbolea hadi leo hii baadhi hawajalipwa na sababu ni kutokana na

*voucher* kuchelewa. Naomba kauli ya Serikali ni kwa nini hali hiyo bado inaendelea kujitokeza kwa kuwa Serikali imekuwa inatoa majibu kwamba watarekebisha suala hilo na hata mwaka jana nimekuwa nikiuliza maswali haya lakini mpaka leo bado hali hiyo ina- *exists*?

(b) Suala la pembejeo linapaswa kwenda sambamba na suala la wakulima wetu kuweza kupatiwa ardhi ya kutosha. Mwaka jana mwezi wa Novemba, 2011 wananchi wa Wilaya ya Kasulu ambao walikuwa wakilima katika mapori ya Kagera Nkanda Serikali iliamua kuweza kuondoa kwa kusema kwamba ni maeneo ambayo ni ya hifadhi na kuahidi kwamba ingeweza kushughulikia tatizo la wakulima kukosa ardhi na kuweza kuwapatia ardhi ambapo Mkuu wa Mkoa wa Kigoma alikuwepo, Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ujumla ya Mkoa wa Kigoma ikiongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, leo hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa.

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Mbunge, muda hatuna.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa hiyo, nilikuwa naomba kauli ya Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Uongozi wa Mkoa wa Kigoma ambao uliwaahidi wakulima wa Wilaya Kasulu kwamba ungetafuta ardhi mbadala ili kusudi wakulima wale wakaondolewa kule waweze kupata maeneo kwa ajili ya kulima kwa sababu

hakuna ambacho kimefanyika mpaka dakika hii? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu katika maswali mawili naomba kujibu hili moja la nyongeza la Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawa-*discourage* Makampuni yanayoleta mbolea hata siku moja. Tulichosema ni kwamba mwaka jana utaratibu wa *voucher* uliingia dosari na tatizo hili limechangiwa na watu tatizo siyo mfumo, tatizo ni sisi wenyewe wote mimi pamoja na wewe wote ambao tunasimamia mfumo huu. Kwa hiyo, maana yangu ni kwamba kama *voucher* zilichelewa mwaka huu kwa Mikoa ambayo msimu wa kupandia unaanza mwezi Septemba tumeshajipanga kwamba mpaka ifikapo mwisho wa mwezi huu wa saba, mikoa yote itakuwa imepatiwa utaratibu wa namna ya kufikishiwa *voucher* ili mbolea hizo ziwafikie wakulima kwa wakati. Kwa hiyo, taratibu na mianya ile yote ambayo watu wanatumia.

Sasa umezungumzia kwa nini watu hawajalipwa? Kusema kweli hili tatizo baina ya wale wanaoleta mbolea na mawakala na kadhalika, kwa hiyo, hili linafanyiwa kazi kupitia Wizara yangu, Wizara ya Fedha na wahusika wote ili tatizo hili liondoke. Mwaka huu hatutakuwa na tatizo hilo kwa sababu mawakala watakuwa dhamana ya *main suppliers* wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la pembejeo pamoja na ardhi kwa upande wa Jimbo la Kasulu mimi

naamini hili liko kwake mwenyewe Kigoma, kwa hiyo tusema *RC* wa Kigoma anashughulikia liko kwenye *RCC.* Lakini kwa kuwa wewe na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika wote ni wadau wa Mkoa wa Kigoma na hili linawahusu moja kwa moja, naomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika anipokee katika hili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu sahihi kabisa. Labda kwa haraka tu niseme Mheshimiwa Machali nadhani unachanganya kidogo makampuni hayajawa *discouraged* nafikiri Mheshimiwa Machali amechanganya kati ya makampuni na mawakala, watu ambao wanadai ni mawakala waliosambaza pembejeo. Ndio mfumo wa sasa tumesema makampuni yatawajibika kuchagua mawakala wao wenyewe kuliko mfumo tunaotumia. Kwa hiyo, watu ambao hawajalipwa ni mawakala. Lakini kwa upande huo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Machali kwamba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akihitimisha hotuba yake hapa nilitoa ufafanuzi kwamba Serikali tayari imepeleka shilingi bilioni 53 kwenye mabenki na sasa hivi mchakato unaendelea wa kuwalipa mawakala. Wale ambao hawalipi ujue kuna matatizo yao pengine walikuwa na matatizo mambo waliyoyafanya bado wana kesi ndio hawapi. Lakini fedha sasa zimepelekwa ili waweze kulipwa.

Hili la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Machali kwamba tutaishughulikia kule kwetu pamoja na Mkuu wa Mkoa na Wizara ya Maliasili. Lakini

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alikuwa hapa juzi na tulikutana na nilitegemea Mheshimiwa Machali na wewe uwepo tuzungumzie mambo haya bahati mbaya ulikuwa na majukumu mengine. Lakini tutalishughulikia. *(Makofi)*

Na. 133

**Askari wa Jeshi la Polisi Walioajiriwa Mwaka 2011/2012**

**MHE. RASHID A. OMAR** aliuliza:-

(a) Je, ni askari wangapi wa Jeshi la Polisi walioajiriwa katika mwaka wa Fedha 2011/2012?

(b) Je, kati yao ni wangapi kutoka Tanzania Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niab a ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya askari wapya 3,294 waliajiriwa. Kati yao 168 ni kutoka Tanzania Zanzibar. Hii ni sawa na asilimia 5.1 ya askari wote walioajiriwa kwa mwaka huo.

**MHE. RASHID A. OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano; na kwa kuwa idadi ya Askari walioajiriwa mwaka 2011/2012 ni askari 3294 na kwa kuwa idadi hii ya askari walioajiriwa Zanzibar 168 tu ni idadi ndogo ukilinganisha na idadi ya askari wote walioajiriwa. Je, Serikali haioni kwamba ni kuwatendea dhuluma Wazanzibar katika sekta hii ya ajira ya Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Ali Omar, kama ifuatavyo:-

Ndani ya Jeshi la Polisi ajira hazijatolewa moja kwa moja kusema wangapi Wazanzibar wa Tanzania Bara; wa sehemu nyingine. Kinachofanywa baada ya kupata idadi na kibali cha ajira ni kugawa kwa Mikoa kila Mikoa kulingana na idadi ya wananchi ambao wako pale hupewa mgao wake na hivyo ndivyo inavyofanyika bila kuangalia ni upande upi wa Muungano au upande wa pili. Kwa hiyo, kwa misingi ya taratibu ambazo zipo nafikiri hii si dhuluma lakini ni utaratibu ambao umekubaliwa na unatekelezwa.

Na. 134

**Mamlaka ya Ujenzi (*TBA*) Kujenga Nyumba kwa Ajili ya Watumishi wa Serikali ya Muungano Zanzibar**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA (K.n.y. MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA)** aliuliza:-

Serikali kupitia Mamlaka ya Ujenzi (*TBA*) inao utaratibu wa kujenga nyumba kwa ajili ya Muungano upande wa Zanzibar:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba kwa ajili ya watumishi wa Serikali ya Muungano upande wa Zanzibar?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba Zanzibar kwa ajili ya watumishi wa Serikali ya Muungano wanaoenda Zanzibar kikazi kama walivyojengewa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaumbwa Makame Mbaraka, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakati wote ni kuona kuwa watumishi wake wote wanaishi katika nyumba zilizo bora wakiwa kazini na hata baada ya kustaafu. Hii ndiyo sababu pamoja na ufinyu wa Bajeti, Serikali kupitia kwa wakala wa majengo (*TBA*), inaendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi wake kila mwaka upande wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Upande wa Tanzania Zanzibar, utaratibu huu haujaanza kutokana na ukweli kuwa *TBA* iko chini ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya ujenzi si Wizara ya Muungano.

Kwa sasa watumishi wa Serikali ya Muungano wanaokwenda Zanzibar kikazi taasisi zao zitaendelea kuwagharamia kulingana na taratibu za utumishi wa umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa karibuni kumekuwa na Wilaya mbalimbali mpya ambapo hakuna kabisa majengo ya wafanyakazi wa Serikali. Je, kuna utaratibu gani ambao mmejiandaa ili kuhakikisha kwamba katika Wilaya hizi kama vile Itilima tunakuwa na nyumba ambazo zimejengwa na *TBA* kwa ajili ya watumishi wa Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cheyo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa, Wilaya 19 na kuna bajeti ya maendeleo ambayo pamoja na kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga Ofisi za Serikali. Wakala wa Majengo *TBA* itapewa jukumu hilo la kusimamia ujenzi wa nyumba hizo. *(Makofi)*

Na. 135

## Ukali wa Mgao wa Umeme Kinondoni

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Mgao wa umeme katika Jimbo la Kinondoni, katika Jiji la Dar es Salaam ni mkali sana.

(a) Je, ni lini mgao huo utaisha?

(b) Je, kwa nini uwiano wa mgao huo hauko sawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mbunge wa Kinondoni lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kinondoni na Jiji la Dar es Salaam, kwa ujumla katika kipindi cha tangu mwezi Februari, 2012 hadi sasa hakuna mgao wa umeme kabisa.

Inapotokea umeme umekatika ni kwa sababu ya hitilafu ya mitambo, nguzo za umeme kuanguka, miti kuangukia nyaya za umeme, hitilafu kwenye *Grid* ya Taifa au matengenezo ya miundombinu. Aidha, taarifa hutolewa kwenye vyombo vya habari siku mbili hadi tatu kabla ya kuzima umeme, kwa tatizo linalojulikana na siku hiyo hiyo kwa tatizo la ghafla.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kusisitiza kwamba hatuna mpango wa mgao wa umeme nchini na Wizara yangu tumejipanga kuhakikisha kwamba tunafanya kila jitihada kuhakikisha mgao hautokei ili shughuli za uchumi ziweze kuendelea kama ilivyopangwa.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* kwa kukomesha tatizo la mgao wa umeme nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Suala la kukatika umeme katika Jiji la Dar es Salaam hususan katika Wilaya ya Kinondoni bado linaendelea na umeme huwa unakatika ovyo ovyo na hakuna taarifa zozote zinazotolewa. Je, ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha inakomesha kukatika katika umeme huko kunaendelea hivi sasa?

(b) Kwa kuwa kukatika katika umeme huko kwa ovyo ovyo kuleta athari kubwa sana kwa wananchi hususan kuharibu vifaa vyao kutokana na umeme kurudi kwa nguvu. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuangalia uwezekano wa kulipa fidia kwa wale ambao watathibitika kwamba vifaa vyao vimeharibika kutokana na tatizo la umeme kama ambavyo nchi nyingine zinafanya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Idd Azzan kama ifuatavyo:-

Kuhusu kukatika katika kwa umeme kama nilivyosema kwa sasa kwa Dar es Salaam *TANESCO* wamefanya kazi kubwa wakishirikiana na Serikali ambayo imerekebisha hali ya udhaifu wa miundombinu iliyokuwepo na sasa hivi umeme Dar es Salaam uko *very stable,* umetulia kabisa.

Sasa kwa umeme bado unakatikakatika ovyo zinaweza kuwa sababu kama nilizoziseme katika jibu langu la msingi. Lakini moja ambayo siwezi kuikubali sana ni hii inatokana na uzembe wa watendaji wetu.

Napenda nichukue nafasi hii kuwaomba sana Mameneja wa *TANESCO* na nimwagize hapa Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* kwamba pale ambapo sababu zitakuwa ni za msingi tutakubali. Lakini pale ambapo sababu siyo za msingi basi wanaosababisha udhaifu huo wa umeme kutokuweko maeneo fulani kwa sababu tu wamechelewa *action* ya tatizo dogo kama la waya kugusana basi hatua kali zichukuliwe dhidi ya uzembe huo. (*Makofi*)

Lakini la pili, ni juu ya hasara zinazotokana na umeme kurudi kwa nguvu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Idd Azzan kwamba anajitahidi sana kufuatilia juu ya masuala ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Lakini hapa pia niwaombe sana wananchi watumiaji wa umeme kwamba umeme unapokatika basi ni vizuri wakachukua utaratibu wa kuzima sehemu zote ambako umeme unaingia ili utakaporudi usiweze kuleta madhara.

Kwa kusema hivyo basi niwaombe sana na hata wenzetu watendaji au wataalamu wa umeme, watoaji wa umeme kwa maana ya mafundi wa *TANESCO* wanaporejesha umeme basi warejeshe kwa utaratibu mzuri ambao hautaleta madhara.

Lakini pia zipo Sheria ambazo endapo mtu amepata hasara anaweza akadai. Sheria hizi zipo na zinaweza zikafuatwa na wananchi ili kuweza kurejeshewa fidia zao kutokana na hasara wanazozipata. (*Makofi*)

Na.136

## Ahadi ya Kuwapatia Umeme Wananchi wa Kata ya Ruvu

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. HAMOUD ABUU JUMAA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika kampeni zake za uchaguzi wa mwaka 2010 aliahidi kuwapatia umeme wananchi wa Kata ya Ruvu na wananchi kwa kulijua hilo walianza kuweka mazingira ya kuupokea umeme huo kwa kujenga nyumba za kudumu, kuboresha kilimo na ufugaji, na kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo hayo kufanya shughuli za maendeleo kama vile ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao, nyama, mbogamboga na samaki wanaopatikana Mto Ruvu, lakini hadi sasa umeme huo haujapatikana:-

Je, Serikali ina mpango gani katika kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini kwa ajili ya kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu ilifanyika mwezi Februari, 2012. Gharama za kupeleka umeme katika Kata hiyo zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.5. Fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 33 yenye urefu wa kilomita 28 kuanzia Mlandizi hadi Mzenga.

Jumla ya *transfoma* nane(8) zitafungwa na mradi unatarajiwa kuwapatia umeme wateja wapatao 400. Sehemu ya mradi wa umeme katika Kata ya Ruvu iko katika miradi ya *REA* inayoendelea kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha, yaani Vijiji vya Kikongo na Lupunga. Vijiji vilivyoko Kata ya Ruvu *Station* na Kitomondo vimeingizwa katika miradi ya *REA phase* II, inayotegemewa kuanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais katika Kata ya Ruvu imeshaanza kutekelezwa na ni dhamira ya Serikali kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yanayoridhisha ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge amependa kuisisitiza Serikali ihakikishe kwamba mradi huu unafanyika kwa haraka maana yake wananchi wamesubiri kwa kipindi kirefu?

Lakini tatizo linalopatikana katika eneo la Kibaha Vijijini linawiana sana na kule Kilwa Kaskazini. Mradi wa *REA* ambao umeahidiwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo yake tunataka kujua ni lini utatekelezwa pamoja na fidia ya watu wa maeneo ya Malendegu na Manzese ambao muda mrefu wamekuwa wakidai fidia ya kupisha mradi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mangungu, Mbunge wa Kilwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu uhakika, nimhakikishie kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa eneo hilo la Kibaha itatekelezwa na itakamilika katika muda stahiki.

(b) Lakini la pili la fidia ya watu wa Jimbo lake katika Vijiji hivyo alivyovitaja, napenda nimhakikishie kwamba nimelichukua na hivi karibuni nilikuwa nafikiria kutembelea maeneo ya Mtwara na Lindi, naomba tuwasiliane na Wabunge wa maeneo hayo ili niweze kwenda kuona na kujiridhisha matatizo yote yalioko

kule ikiwa ni pamoja na hili la fidia kwa watu ambao *line* ya msongo wa umeme utapita.

Na. 137

**Takwimu ya Idadi ya Watanzania Wanaofanya Kazi Nje ya Nchi**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. VICKY P. KAMATA**) aliuliza:-

Maendeleo ya nchi yanatokana na juhudu na mchango wa wananchi kwa ujumla ikiwemo wale wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi (*Diaspora*) ikiwemo India, Ufilipino na kadhalika. Je, ni wapi katika mipango yetu ya maendeleo inaonyesha takwimu za idadi ya Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba maendeleo ya nchi yanatokana na mchango wa wananchi kwa ujumla wao ikiwa ni pamoja na wale wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi (*Diaspora*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kushirikisha Watanzania waishio Ughaibuni katika maendeleo ya nchi ni suala mtambuka. Jukumu kubwa la Wizara yangu ni kuratibu ushirikishwaji huo. Hivyo, Serikali imeanzisha kundi la wadau linalojumuisha Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Kazi na Ajira, Tume ya Mipango, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Idara ya Takwimu na kadhalika ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika na masuala ya Watanzania wanaoishi au wanaofanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina idadi kamili ya Watanzania waishio na kufanya kazi Ughaibuni. Hata hivyo, kutokana na mahusiano yetu nao katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, tunakisia kwamba tuna Watanzania wasiopungua milioni mbili (2,000,000) katika nchi mbalimbali duniani. Upo uwezekano mkubwa kwamba idadi yao ni kubwa kuliko hiyo ya milioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ikishirikiana na Benki ya Dunia, iko mbioni kuratibu mikakati ya kuwafikia Watanzania wote huko waliko kwa madhumuni ya kupata idadi yao, wasifu wao na pia mahitaji yao. Aidha, Idara ya Takwimu kwa kutambua umuhimu wa kuwa na taarifa hizo, imeweka maswali yanayohusu Watanzania waishio nje ya nchi katika sensa ya makazi na watu inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti mwaka huu. Sehemu H (swali 50 hadi 53) ya dodoso la sensa inahusu taarifa za Watanzania waishio nje ya nchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie kwamba Mheshimiwa Rais au Viongozi wa Kitaifa wanapofika kutembelea Diaspora huwahamasisha wananchi waishio kule ambao ni Watanzania kurudi nyumbani kwa ajili ya kuwekeza nyumbani.

Lakini wanapofika hapa, huwa wanapata misukosuko na matatizo mengi ya kuwakatisha tama kwa ajili ya kuwekeza hapa nyumbani.

Je, Mheshimiwa Waziri au Serikali iko tayari sasa kuanzisha dirisha maalum la kuwahudumia Wana-*Diaspora* hawa ili wapate fursa ya kuwekeza hapa nyumbani? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje naomba kumjibu Mheshimiwa Martha Mlata swali lake la nyongeza:-

Kwanza nikubaliane na maelezo yake kwamba Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine wanapokwenda nje na wanapopata fursa ya kukutana na Watanzania wanaoishi nje, wamekuwa wakiwahimiza katika kuchangia maendeleo nchini kwao Tanzania. Maendeleo hayo wanaweza kuchangia kwa either wao kurudi au kwa kusaidia ndugu zao waliopo huku. Lakini pia kwa kuleta mawazo mapya, taaluma na teknolojia ambayo wameipata wakiwa nje.

Ni kweli kumekuwa na mkakati na Serikali imekuwa ikijitahidi kuandaa mazingira mazuri zaidi kwa Watanzania wanaoishi nje wanaporudi nyumbani waweze kuwekeza bila usumbufu. Hatua hizo zimeanza kuchukuliwa na zinaendelea. Ahsante.(*Makofi*)

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza:-

Kwa kuwa elimu ni msingi wa maendeleo na kwa kuwa kumwelimisha mwanamke ni kuelimisha jamii nzima. Je, ni Balozi ngapi za Tanzania ambazo zina kitengo ambacho kinachoshughulikia kuendeleza wanawake wa Tanzania kielimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima nieleze hili suala linahusiana kwa mbali sana na lile swali la msingi. Lakini miongoni mwa majukumu ya Balozi zetu ni pamoja na kuwa-engage Watanzania wanaoishi huko na kuwahamasisha kujitafutia maendeleo yao na pia kutafuta maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, tumekuwa tukiwahamasisha wanawake wote wanaoishi nje ya nchi kutafuta elimu na kutafuta maendeleo kwa ajili yao na kwa ajili ya nchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru, muda wa maswali umekwisha sasa nina matangazo yafuatayo. Naomba kutanganza kwamba kuna wageni katika *gallery* ya Spika, tunae Ndugu Sazi Salula Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, ahsante karibu. Pia tuna Mhandisi

Mgosi Mwihala, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais. Tuna Ndugu Zahoro Haji, Katibu wa Makamu wa Rais, tunae Ndugu Seif Msongoro, Naibu Katibu wa Makamu wa Rais, Zanzibar. Tuna wasaidizi wa Makamu wa Rais, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais walipo wasimame, karibuni. Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna Ndugu Rashid Suluhu, Hassan Kaka yake Samia Suluhu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, karibu sana. Tuna watoto watatu wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, walipo wasimame, karibuni Baba anafanya kazi ya Serikali. Tuna wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, tuna Viongozi 30 wanawake wa Kanisa la *Adventist* Wasabato Tanzania wakiongozwa na Jobie Maroba ambaye ni Mkurugenzi wa *division* ya Afrika Mashariki na Kati pamoja na Bi. Winfrida Mitekaro, Mkurugenzi wa Tanzania Idara ya Huduma za Wanawake, karibuni sana. Tuna wanafunzi wanne kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* wakiongozwa na Jessica Anatori, walipo wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Felister Bura kutoka Butiama, Musoma walipo wasimame, karibuni sana. Tuna vijana wanne (4) waliotoka masomoni kutoka Jimbo la Iramba walipo wasimame, karibuni Mbunge wenu anafanya kazi Mheshimiwa Mwigulu. Tuna tangazo kutoka kwa kapiteni msaidizi wa timu ya Wabunge ya Yanga, anaomba washiriki mazoezi ili kuishinda timu ya Simba. Kwa hiyo mhudhurie mazoezi yenu. Matangazo yangu yamekwisha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7).

**MWENYEKITI**: Ebu isome.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anaesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili SPika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhisiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadae kadiri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako juu ya kauli ambazo zimekuwa zikitolewa hapa kila kukicha kuanzia wiki iliyopita mpaka na jana na juzi kuhusiana na Bunge hili kutopewa fursa ya kujadili jambo ambalo liko Mahakamani la mgomo wa Madaktari. Lakini taarifa nilizonazo hivi sasa ni kwamba tayari Mahakama ilikwishatoa uamuzi na kuwataka Madaktari watangaze kumaliza mgomo na ndiyo sababu Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na yeye akapata fursa kwenye Muhimili wa Serikali sasa kuzungumzia jambo hilo kwa wananchi.

Ninaomba mwongozo wako sasa kwamba ni wakati muafaka kwa sababu matatizo kwenye hospitali bado yanaendelea, bado migomo ya chini

kwa chini inaendelea, hatutawatendea haki Watanzania endapo Bunge hili ambalo ni chombo cha wananchi halitatunza heshima yake ya kujadili matatizo yanayowakabili Watanzania na kuweza kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako kama kuendelea kuzuia Bunge hili kujadili suala la Madaktari haliruhusiwi au linaruhusiwa. Naomba mwongo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Nakushukuru Mheshimiwa, ombi lako la mwongozo Kiti kimepokea, nitalitolea taarifa baadaye.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Nataka nitumie Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako ambayo hivi punde imesomwa sidhani kama nina sababu ya kuisoma. Lakini kwa mujibu ya Kanuni wa 101(2) ambayo tunahoji Serikali Bunge linapokuwa limekaa kama Kamati ya Matumizi, jana nilipotaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa Kanuni 101(2) nilihoji Serikali kwamba Sekretarieti ya Ajira..

**MWENYEKITI**: Naomba uisome.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 101inasema “Katika Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atawahoji Wajumbe kuhusu Kifungu kimoja kimoja cha makadirio ya matumizi ya mwaka na kila kifungu kitaafikiwa pekee yake “cha pili kidogo” Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika Kifungu chochote cha Fungu linalohusika wakati Kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jana nilihoji Serikali kuhusiana na vote ya 67 ambayo ni *Public Service Recruitment Secretariat* na nikasema sub-vote 220800 imetengewa shilingi milioni 6 tu, nikasema pesa hizi kimsingi ni kidogo sana kwa maana ya kuiwezesha Sekreterieti hii kuweza kupata mafunzo ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi. Sasa Mheshimiwa Waziri na mimi sina tatizo na Mheshimiwa Waziri naomba nimthibitishie lakini nasimama kwa sababu tu ya kuweka kumbukumbu sawasawa.

Alisema pesa zaidi za mafunzo kwa ajili ya Sekretarieti ziko kwenye kitabu cha nne ambacho ni kitabu cha maendeleo. Lakini hata nilipoenda kwenye kitabu cha maendeleo, hii *Public Service Recruitment Secretariat* haina vote hiyo, vote hiyo ya 67 kwenye kitabu cha nne haipo kabisa. Sasa naomba mwongozo wako kwa sababu haipo, Serikali ikiri upungufu na kwa maana hiyo kwamba hela hizo hazipo kwa sababu ni ukweli. Ukienda kitabu cha nne fungu 67 haipo kabisa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Zambi nimepokea ombi lako nitatolea mwongozo baadaye. Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013
## Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na ile iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitumie fursa hii, kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutupa tena dhamana ya kusimamia Masuala ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira, katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Vile vile, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo anayotupa katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kuratibu masuala ya Muungano na Uhifadhi wa Mazingira. Tunaahidi kuendelea kutumia kikamilifu fursa zote zilizopo, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na wenzangu kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais

kushika nyadhifa mbalimbali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naungana na wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla kwa vifo vya Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mheshimiwa Mussa Khamis Silima na Mheshimiwa Jeremia Solomon Sumari. Vifo vya waheshimiwa wabunge hao ni pigo kubwa kwa Taifa letu. Tutawakumbuka kwa juhudi zao na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutumia nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dokta William Augustao Mgimwa Mbunge, kwa kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge, pamoja na Mawaziri wote waliotangulia katika kuwasilisha hotuba zao za Bajeti ambao ni: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mbunge). Hotuba zao zimefafanua kwa kina mwelekeo wa Sera, mipango, Mikakati, Malengo na Kazi za Serikali kwa Mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge Viti

Maalum, kutoka Mkoa wa Iringa, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kwa ushirikiano, maoni na ushauri uliojaa hekima walioutoa katika kupitia na kuchambua taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, nawashukuru Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo Mbunge, waliokuwa wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, Kuhusu Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano na michango yao.

Aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Tundu Mughwai Antiphas Lissu, na Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, kwa kuteuliwa kuwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Masuala ya Muungano na Mazingira. Tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2011/2012 na Malengo ya Mwaka 2012/2013. Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2011/2012 imeendelea kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa ya kuratibu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano, pamoja na usimamizi wa Mazingira hapa nchini. Ofisi imetekeleza

majukumu hayo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania *(MKUKUTA II)*; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi *(CCM)* ya Mwaka 2010 hadi 2015; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ya awali, naomba sasa niwasilishe taarifa ya utekelezaji kwa kipindi hicho na malengo ya mwaka 2012/2013 katika Masuala ya Muungano na pia katika Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala ya Muungano. Utekelezaji wa Maendeleo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya Mwaka 2010 hadi 2015. Ibara 183 ya Ilani hiyo inaelekeza kuwa, ili kuimarisha Muungano Serikali itajenga mazingira endelevu na kuimarisha fursa za kiuchumi miongoni mwa wananchi wa kila upande, ili waone na kuamini kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sio tu ni ngao madhubuti ya Umoja, Amani na Mshikamano wao. Bali pia ni daraja lisilotetereka la kuwafikisha katika azma yao ya kuondokana na umaskini na kuharakisha maendeleo yao na ya Taifa kwa jumla. Aidha, katika Ibara ya 184 Serikali inaelekezwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa majengo na Taasisi za Muungano ambazo zimeanzishwa Tanzania Zanzibar;

(b) Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya kutatua changamoto za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya Kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa;

(c) Kuboresha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano;

(d) Kuzifanyia mapitio na uboreshaji Sheria na Kanuni za fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB)* upande wa Tanzania Zanzibar kwa lengo la kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo;

(e) Kuboresha Sheria, Kanuni na taratibu za ajira ya watumishi katika Taasisi za Muungano ili utumishi huo uwe na sura muafaka ya Muungano;

(f) Kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja zenye lengo la kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano; na

(g) Kuendeleza miradi ya pamoja ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii iliyoanzishwa ikiwemo ya *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* na *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi imeendelea kutekeleza llani ya

Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2010 – 2015 katika masuala ya Muungano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, “Kukamilisha ujenzi wa majengo na Taasisi za Muungano ambazo zimeanzishwa Tanzania Zanzibar”. Katika kipindi hiki, Ofisi imehamasisha Wizara, Idara na Taasisi za Muungano kujenga au kufungua Ofisi zao Tanzania Zanzibar. Ofisi ya Makamu wa Rais imekamilisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu - Zanzibar. Aidha, Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* na Tume ya Nguvu za Atomiki *(TAEC)* zimehamishia Ofisi zao kwa muda katika Jengo hilo.

Vile vile, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu Zanzibar umekamilika na ujenzi wa Ofisi ya Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyopo Buyu unaendelea. Taasisi ya kusimamia biashara za nje Tanzania, *(TanTrade)* imefungua Ofisi ya muda Zanzibar. Aidha, ujenzi wa Ofisi za uhamiaji Makao Makuu Zanzibar uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, “Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya kutatua changamoto za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya Kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa”. Katika kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya *SMT* na *SMZ* ya kutatua changamoto za Muungano, Ofisi imeandaa utaratibu wa kufanya vikao vya sekta. Lengo la vikao hivyo ni kuharakisha utekelezaji wa maamuzi ya Kamati hiyo. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, Ofisi imeratibu

vikao 7 kwa sekta zenye hoja, Pamoja na vikao viwili (2) vya Sekretariati ya kamati hiyo. Hoja hizo zinahusu Masuala ya Fedha, Nishati ya Umeme, Usajili wa vyombo vya moto na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Katika kipindi hicho, kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kilifanyika tarehe 28 Januari, 2012, Dar es Salaam. Hoja ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na hoja ya ongezeko kubwa la ankara za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kwenda Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO)* zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, “Kuboresha Uchangiaji na Mgawanyo wa Mapato ya Muungano”. Ofisi imeratibu kikao cha Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya fedha wa SMT na SMZ kilichofanyika tarehe 6 Oktoba, 2011. Kikao hicho kilijadili utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuhusu mgawanyo wa Mapato na kuchangia gharama za Muungano kwa Serikali zetu mbili. Kwa sasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko kwenye hatua za mwisho za kutoa maamuzi Kuhusu mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, “Kuzifanyia mapitio na uboreshaji Sheria na Kanuni za fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya *TRA* na *ZRB* upande wa Tanzania Zanzibar kwa lengo la kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo”. Serikali zetu mbili zimekubaliana kuwa, yafanyike marekebisho ya sheria

za Kodi ya Mapato ya Ajira (*Pay As You Earn (PAYE*) na Kodi ya Mapato inayozuiwa (*Withholding Tax*) ili kodi hiyo itumike pale inapokusanywa. Mswada wa marekebisho ya sheria hizo uwasilishwe kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge. Aidha, imekubaliwa kuwa, marekebisho ya Sheria za usajili wa vyombo vya moto yafanywe katika vikao vya Bunge na Baraza la wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Kuboresha Sheria, Kanuni na Taratibu za Ajira ya Watumishi katika Taasisi za Muungano ili utumishi huo uwe na sura muafaka ya ki-Muungano". Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeratibu vikao vya Kamati ya kuboresha Sheria na Sera za utumishi katika Taasisi za Muungano. Kutokana na mabadiliko yaliyotokea baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 na kusababisha baadhi ya Wizara na wajumbe wa kamati iliyoundwa kubadilishwa au kuhamishwa, Kamati ya mawaziri imeunda kamati nyingine ambayo imeelekezwa kukamilisha kazi ya kuainisha maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja zenye lengo la kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano". Katika kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano *SMT* na *SMZ* zimekubaliana kwa pamoja kutekeleza masuala ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania *(MKUKUTA)* na Mkakati wa Kuondoa Umaskini Zanzibar *(MKUZA)* na kupeana taarifa kuanzia hatua za awali, kushiriki kikamilifu katika

majadiliano na washirika wa maendeleo na kuainisha maeneo ya vipaumbele. Rasimu ya mwongozo wa ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yote ya Kimataifa imeandaliwa.

Miongoni mwa mambo yaliyozingatiwa katika mwongozo ni suala la utafutaji wa fedha za misaada au mikopo kutoka nje ya nchi. Mwongozo wa vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za *SMT* na *SMZ* umeandaliwa ili kuimarisha masuala ya sera, utaalam na wataalam kwa pande mbili za Muungano. Aidha, Ofisi imeratibu gawio la asilimia 4.5 la misaada ya kibajeti kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii iliyokwishaanzishwa ikiwemo ya *Tanzania Social Action Fund (TASAF) na Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*".Ofisi imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kiuchumi na kijamii kupitia ziara zilizofanywa tarehe 21 hadi 24 Februari 2012 na tarehe 12 hadi 16 Machi, 2012 Tanzania Zanzibar. Miradi hiyo inafadhiliwa na *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, *Marine and Coastal Environment Management Programme* (*MACEMP), Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Miradi yote iliyotembelewa imeonyesha kutekelezwa vizuri na kuwafaidisha wananchi kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2011/2012 na Malengo ya Mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufuatilia utekelezaji wa kila siku wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano ili kudumisha Muungano na ushirikiano wa Serikali zote mbili. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuondoa Vikwazo katika Utekelezaji wa Masuala ya Muungano. Kikao cha Kamati ya Pamoja ya *SMT* na *SMZ* kilifanyika tarehe 28 Januari, 2012, Dar-es-Salaam kwa madhumuni ya kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Kikao hiki kilitanguliwa na vikao viwili (2) vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja *SMT* na *SMZ* vilivyofanyika tarehe 20 Desemba, 2011 na 17 Januari, 2012. Hoja 13 zilijadiliwa katika kikao hicho na kati ya hizo, hoja mbili (2) zilipatiwa ufumbuzi na zilizobaki ziko katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda ZECO'. Kulikuwa na hoja kutoka *SMZ* kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* ilipandisha bei za umeme kwa wateja wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* likiwemo Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* mwezi Januari, 2008. Upandishwaji huo ulikuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 21.7 kwa wateja waliopo Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar

bei ya umeme ilipandishwa kwa asilimia 168. Baada ya majadiliano katika Kikao cha Mawaziri wa Sekta ya Nishati kilichofanyika tarehe 27 Januari, 2012 hoja hii ilipatiwa ufumbuzi kwa kushusha gharama za umeme kwenda *ZECO*. Hivyo, hoja hii imeondolewa kwenye orodha ya changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa SMT. Kulikuwa na hoja kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo umuhusishe mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kama mjumbe wa kudumu katika Kamati ya Mfuko huo ili kuweza kujua matumizi ya fedha za mipango ya maendeleo ya Jimbo. Wawakilishi wa viti maalum kutoka katika Baraza la Wawakilishi pia washirikishwe katika kupanga matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo. Hoja hii ilijadiliwa katika ngazi za wataalamu kwa kupitia Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya *SMT* kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kurekebisha sheria hiyo. Hata hivyo, hoja hii imeondolewa katika Orodha ya changamoto za Muungano baada ya *SMZ* kuanzisha sheria yake ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambazo ziko katika hatua za kutafutiwa ufumbuzi ni pamoja na:- Ushiriki wa Zanzibar katika Taasisi za Nje; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili; Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano; Hisa za *SMZ* zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki; Marekebisho ya Sheria ya usajili wa vyombo vya moto, Kodi ya Mapato inayozuia na Kodi ya Mapato ya Ajira (*PAYE)*; na Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutoa Elimu kwa Umma. Ofisi imetoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya Muungano kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Ofisi iliandaa na kusambaza nakala 8,000 za Jarida la Muungano Wetu; nakala 9,000 za vipeperushi; nakala 2,000 za kitabu cha miaka 50 ya Uhuru; na nakala 460 za kitabu cha Historia ya Muungano katika picha;

(b) Ofisi ilishiriki na kutoa elimu kwa Umma katika maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika Mjini Dodoma tarehe 1 hadi 8 Agosti, 2011 na maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Dar es Salaam tarehe 1 hadi 12 Desemba, 2011 na Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Mkoani Kilimanjaro mapema mwezi Juni, 2012; na

(c) Elimu ya Muungano ilitolewa kwa umma kupitia vipindi vya Redio na Televisheni vilivyorushwa hewani kupitia *TBC1, ITV, Radio Free Africa* na *Redio Clouds FM* pamoja na taarifa maalum ya miaka 48 ya Muungano iliyochapishwa katika magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisheria. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano alifanya ziara kwenye Taasisi zilizopo Dar es Salaam tarehe 18 hadi 20 Oktoba, 2011, tarehe 21 hadi 24 Februari, 2012, na tarehe 12 - 16 Machi, 2012 alitembelea taasisi na Miradi iliyoko

Zanzibar. Taasisi zilizotembelewa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA*, Tume ya Pamoja ya Fedha - *JFC*, Mamlaka ya Bandari Tanzania - *TPA*, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC)*, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Idara ya Uhamiaji Zanzibar na Taasisi ya Sayansi za Bahari. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kufanya ufuatiliaji katika Taasisi za Muungano na kuangalia utekelezaji wa shughuli za Muungano kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kiuchumi na kijamii Zanzibar inayotekelezwa chini ya ufadhili wa miradi ambayo fedha zake zinapatikana kupitia *SMT*. Miradi hiyo ni *TASAF, MACEMP, ASDP, ASSP* na *ASSPL*. Miradi hii imefanikiwa kuleta maendeleo kwa wananchi kwa kuondoa kero za huduma za jamii mfano ni ujenzi wa shule, visima vya maji, ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki na uzalishaji wa chumvi, zahanati, ufugaji wa nyuki na kilimo cha umwagiliaji. Aidha, miradi hii imewaongezea wananchi kipato, kuwajengea uwezo wa kusimamia, kutekeleza na kuendeleza miradi yao, elimu ya msingi ya ujasiriamali, elimu ya kuweka na kuwekeza, imetoa ajira za muda kwa wananchi na kuongeza ari ya kujitolea kwa wananchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kuratibu gawio la asilimia 4.5 la misaada ya wahisani na mikopo ya kibajeti. Hadi kufikia tarehe 15 Juni, 2012 SMZ imepokea shilingi 32,466,000,000/= badala ya shilingi 30,423,054,500/= zilizoidhinishwa na Bunge mwaka 2011/2012 sawa na asilimia 106. Ongezeko hili

limetokana na kuongezeka kwa misaada na mikopo ya kibajeti. Fedha hizi za gawio kwa SMZ hutumika kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi pia imeratibu upelekaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar. Hadi mwezi Aprili, 2012 Ofisi ilipokea shilingi 1,243,923,360/= kwa ajili ya Mikoa ya Unguja na Pemba. Fedha hizo zimepelekwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya *SMZ* kwa ajili ya majimbo husika. Aidha, Ofisi ilitembelea baadhi ya Majimbo na kujionea jinsi fedha za maendeleo ya jimbo kwa upande wa Zanzibar zilivyonufaisha wananchi wa majimbo hayo. Baadhi ya miradi iliyotembelewa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa ya skuli ya msingi ya Simai – Wingwi na skuli ya sekondari ya Mtambile; usambazaji wa umeme katika eneo la Michenzani katika Jimbo la Mkanyageni na uimarishaji wa jengo la chinjio Wete; ununuzi wa vifaa vya ufundi katika shule ya ufundi ya Jeshi la Kujenga Uchumi *(JKU)*; Uchimbaji na ujenzi wa kisima cha maji Mtoni Mazrui; na Mradi wa Barabara ya Chukwani yenye urefu wa takribani kilomita tatu (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano. Ofisi imeratibu ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa masuala yasiyo ya Muungano. Ushirikiano huu ni katika maeneo ya kubadilishana uzoefu, Sera, Sheria, utaalamu na wataalamu kati ya Serikali mbili; kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na ziara za kikazi za

mara kwa mara kati ya sekta zinazofanya shughuli zinazoshabihiana pamoja na kujadili kuhusu changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, mwongozo wa vikao vya ushirikiano kati ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za *SMT* na *SMZ* uliandaliwa, kuchapishwa na kusambazwa kwa Wizara na Sekta zote za *SMT* na *SMZ*. Mwongozo huu unaziwezesha Taasisi husika kuratibu kikamilifu vikao vya ushirikiano katika ngazi za Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam ili kuhakikisha utekelezaji wa mikakati na mipango iliyokusudiwa inafanikiwa. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi imeratibu vikao 10 vya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Maji za pande mbili za Muungano zilikutana tarehe 28 Februari, 2012. Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kujadili na kuridhia mapendekezo ya Mpango Kazi wa Ushirikiano wa Sekta ya Maji kati ya *SMT* na *SMZ* uliohusisha maeneo 9 ambayo ni Ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa kwa kutumia Mfumo Pepe (*MIS*); Mfumo wa kusimamia ubora wa maji; Uboreshaji wa huduma za maji mijini na vijijini; Kufanya tafiti mbalimbali za vyanzo vya maji pamoja na Teknolojia zinazotumika katika Sekta ya Maji; Mfumo wa kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu za rasilimali za maji; Uvunaji wa maji ya mvua; Kubadilishana taarifa mbalimbali za Sekta ya Maji (Sera, Mikakati, Sheria, Mapitio ya Sekta na kadhalika; na Ufuatiliaji na Tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa *(TAKUKURU)* chini ya Ofisi ya Rais *(SMT)* na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora *(SMZ)* zilikutana tarehe 15 Oktoba, 2011, tarehe 3 Novemba, 2011 na tarehe 19 Novemba 2011. Vikao hivyo vilijadili maeneo ya ushirikiano ikiwemo kuanzisha ushirikiano kati ya *TAKUKURU* na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inayotarajia kuanzishwa Zanzibar. Mapendekezo ya maeneo ya ushirikiano ni pamoja na; uandaaji na uwasilishaji taarifa katika ngazi za Kikanda na Kimataifa; Uchunguzi na ukusanyaji wa ushahidi kuhusu makosa ya rushwa ndani na nje ya Nchi; Ushirikiano wa kitaasisi kwa ngazi zote za mafunzo, Utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya miradi, vikao vya pamoja; na Ushirikiano katika kuandaa mikakati ya kupambana na rushwa. Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira *(SMT)* na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Idara ya Mazingira *(SMZ)* zilikutana tarehe 29 Septemba, 2011. Kikao kilikuwa ni cha Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalam wenye dhamana ya masuala ya Mazingira *SMT* na *SMZ*. Lengo lilikuwa ni kufahamiana, kubadilishana uzoefu pamoja na kuainisha maeneo ya ushirikiano katika sekta ya Mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais *(SMT)* na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) zenye dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano zilikutana mara mbili (2) tarehe 23 na 30 Novemba, 2011. Lengo la vikao hivyo lilikuwa ni kujadili namna ya kuboresha uratibu wa masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi *(SMT)* na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano *(SMZ)*

zilikutana 24 na 25 Oktoba, 2011. Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kujadiliana kuhusu huduma na usalama wa usafiri kwa njia ya maji ikiwemo kufanyia mapitio sheria mbili zinazosimamia usafiri majini nchini *Merchant Shipping Act.* ya mwaka 2003 kwa upande wa *SMT* na *Maritime Transport Act.* ya 2006 kwa upande wa *SMZ*; Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA)* na Mamlaka ya Usafiri Majini Zanzibar zishirikiane katika uteuzi wa kampuni/Wakala ambazo wamezikasimisha mamlaka ya kutekeleza shughuli zao; kuongeza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu usalama wa usafiri majini, anga na nchi kavu; pamoja na kuharakishwa kwa mchakato wa utungwaji wa sheria za shughuli za utafutaji na uokoaji majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu (*TAMISEMI)* na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi *(SMZ)* zilikutana tarehe 19 na 20 Desemba, 2011. Lengo la kikao hicho ilikuwa ni kubadilishana uzoefu kuhusu: Chaguzi za Serikali za Mitaa *SMT* na *SMZ*, mafanikio na changamoto zake; Uendeshaji wa shule za msingi na sekondari Tanzania Bara na Zanzibar, mafanikio na changamoto zake pamoja na masuala ya usafi kwa Majiji na Manispaa. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini *(SMT)* na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati *(SMZ)* zilikutana tarehe 27 Januari, 2012. Lengo la kikao hicho ilikuwa ni kujadili deni la *ZECO* kwa *TANESCO* na ongezeko la bei ya umeme kwa *ZECO* kutoka *TANESCO*. Vikao hivi vya kisekta vimeongeza ushirikiano kati ya *SMT* na *SMZ* hivyo kuimarisha Muungano. Hivyo natoa wito kwa Sekta zote na taasisi kuendelea kukutana na kujadili masuala muhimu kwa uhai wa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana zipo changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo wa masuala ya Muungano na utekelezaji wake hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa uundwaji wa Katiba Mpya. Aidha, mfumo tofauti wa Sheria kwa pande mbili za Muungano, hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika kutatua changamoto za Muungano mfano katika masuala ya usajili wa magari. Hata hivyo, Serikali zetu zinashirikiana ili kuoanisha Sheria zinazokwamisha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Mwaka 2012/2013. Kwa mwaka 2012/2013 Ofisi itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano;

(b) Kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisheria na mambo yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano;

(c) Kutoa elimu kwa Umma kupitia redio na runinga, Jarida, makala za magazeti, vipeperushi na kushiriki katika maonesho ya kitaifa; na

(d) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba Sekta, Wizara na Asasi zisizo za Muungano zinakutana angalau mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Mazingira. Utekelezaji wa Maelezo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya Mwaka 2010 hadi 2015. Katika masuala ya Hifadhi ya Mazingira, Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2010, Ibara 193 (uk. 92-93) inaelekeza kuwa, Chama kitahakikisha kuwa kazi iliyoanzwa ya Hifadhi ya Mazingira inakuwa endelevu. Aidha, katika Ibara hiyo Serikali inaelekezwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti hususan miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, Vituo vya Afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa;

(b) Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za Hifadhi ya Misitu;

(c) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya hifadhi ya mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji na mkakati wa usafi katika fukwe;

(d) Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira;

(e) Kupunguza gharama ya vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa;

(f) Kuhimiza na kuhamasisha ufugaji wa kisasa vijijini ili uwe kichocheo cha hifadhi ya mazingira;

(g) Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira;

(h) Kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano vya hifadhi ya mazingira (*eco-villages*);

(i) Vipeperushi vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira viandaliwe, vichapishwe kwa wingi na vitumike kwenye mafunzo ya elimu yenye manufaa nchini kote; na

(j) Kufanya tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2010 kama ifuatavyo: "Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, Vituo vya Afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ina jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika mwaka huu wa fedha, ofisi imeendelea kutekeleza jukumu hilo na kwa mujibu wa taarifa ya kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya miti 180,793,223 ilipandwa nchini kote na kati hiyo miti 141,470,900 ilipona, sawa na asilimia 78.2 ya miti iliyopandwa. Wilaya 33 zimevuka lengo la kupanda miti 1,500,000 lililoainishwa kwenye Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 zoezi la upandaji miti bado linaendelea. Kwa mwaka 2012/2013, ofisi itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa kampeni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka 2011/12, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kushirikisha Halmashauri za Wilaya na Manispaa. Aidha, katika kufanya hivyo, Ofisi imehimiza Wilaya na Manispaa kutunga Sheria Ndogo za Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Misitu, kufanya tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Vilevile baadhi ya vijiji vimeweka Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira; kwa mfano, Kijiji cha Ilagala, Wilaya ya Kigoma Vijijini - Mkoa wa Kigoma, Kijiji cha Mwese Wilaya ya Mpanda - Mkoa wa Katavi na Kisumba Wilaya ya Sumbawanga Vijijini - Mkoa wa Rukwa. Halmashauri tayari zimeandaa sheria ndogo ndogo na zimeanza kutumika kwa mfano; Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Wilaya ya

Njombe. Aidha, baadhi ya Vijiji vimeweka Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira kwenye vyanzo vya maji, kila wilaya inawajibika kutoa taarifa kuhusu hali ya hifadhi ya vyanzo vya maji. Kwa kutumia sheria hii, Wilaya zimeanza kuainisha vyanzo vya maji na kutumia Sheria Ndogo za Kuhifadhi Vyanzo hivyo, kwa mfano: Wilaya za Kondoa, Babati, Singida Vijijini, Iramba, Bahi, Mbeya Vijijini na Wilaya ya Mpanda. Aidha, katika kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Usafi katika Fukwe, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, iliendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa Kupitia Miradi mitano ambayo ni *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP); Tanzania Coastal Management Partneship (TCMP-PWANI); Western Indian Ocean Marine Highway Development;* na *Coastal and Marine Contamination Prevention Project (WIOMHP). Mingine ni Regional Programme for the Sustainable Management of the Coastal Zones of the Indian Ocean Countires - ReCoMaP* na *Agulhans and Somali Current Large Marine Ecosystems - ASCLME.* Miongoni mwa shughuli zilizofanywa na Miradi hii ni pamoja na kuhakikisha usafi na kuhifadhi mazingira ya bahari na fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi kupitia Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, umeiwezesha Wizara ya Nishati na Madini kuandaa Mpango wa Mazingira wa Sekta ya Madini na Nishati. Mpango huu pamoja na mambo mengine, unaweka

misingi ya kuongeza na kuboresha matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iko katika hatua za kuandaa Sera ya Nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2012/13 Serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vifaa vya gesi. Hatua hii ya Serikali itachangia kupambana na uharibifu wa mazingira utokanao na matumizi ya kuni na mkaa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi kwa kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira liliimarisha usimamizi wa viwanda, biashara na migodi ili shughuli hizo zisichafue mazingira. Baraza lilifanya ukaguzi wa viwanda, migodi, sehemu za biashara na uzalishaji ili kuhakikisha kuwa taratibu na kanuni za hifadhi ya mazingira zinafuatwa. Aidha, viwanda na taasisi 30 na migodi 13 ilikaguliwa na kupewa amri ya kuboresha mifumo ili kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2012/13, Ofisi itaimarisha utekelezwaji wa mambo yafuatayo: Ukaguzi wa mara kwa mara wa viwanda na biashara ili kuhakikisha kuwa vinatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye Hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na mipango yao ya hifadhi ya mazingira na uperembaji *(Environmental Management and Monitoring Plans);* Kusimamia na kukagua viwanda na biashara ili kuhakikisha utekelezaji wa katazo la Matumizi ya Mifuko ya Plastiki; Kuendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wa Mikoa na Maafisa

Mazingira wa Halmashari za Wilaya ili waweze kusimamia Sheria ya Mazingira; Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wenye viwanda na makampuni kuhusiana na namna salama ya kutupa au kuharibu taka hatarishi zenye kemikali mbalimbali zikiwemo vimiminika toka viwandani *(industrial effluents),* dawa za binadamu zilizoisha muda wake wa matumizi na viuatilifu chakavu *(obsolete pesticides).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jumuiya ya Ulaya ilitoa msaada wa kiasi cha *EURO* 2,205,816 kwa ajili ya miradi ya kuongeza uwezo wa jamii wa kupunguza na kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha vijiji vya mfano katika kanda mbalimbali vinavyojulikana kama *Eco villages*. Miradi hii inatekelezwa katika Mkoa wa Dodoma katika Kijiji cha Chololo; Mkoa wa Morogoro katika Tarafa ya Mgeta na Matombo katika Vijiji vya Matalawe, Londo, Luale, Tawa, Konde, Milawilila na Kibungo Juu; na Pemba katika Sheha za Uwandani (Kitongoji "A" na "B"), Pujimi, Fundo, Uvinje na Kokoto. Mradi unaotekelezwa katika Kijiji cha Chololo ulizinduliwa Septemba, 2011 na Mradi unaotekelezwa Pemba ulizinduliwa Oktoba, 2011. Mradi unaotekelezwa katika Vijiji vya Tarafa ya Mgeta ulizinduliwa mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzinduliwa kwa Miradi hii, watekelezaji wa Miradi walianza kufanya shughuli za uhamasishaji, mafunzo na kujenga uelewa wa Watendaji katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa, Viongozi wa Serikali za Vijiji na Wanavijiji ambamo Miradi hiyo inatekelezwa hususan kuhusu

malengo ya miradi, faida zake na ushiriki wao katika utekelezaji wake. Aidha, takwimu za awali kuhusu maeneo ya Miradi zilichukuliwa na maeneo ya kutekeleza Miradi hiyo kuainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Kilimo, hadi kufikia mwezi Mei 2012, wananchi 400 wa Kijiji cha Chololo walipatiwa mafunzo kuhusu jinsi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya eneo la kilimo; nafasi kati ya mmea mmoja hadi mwingine; kilimo mseto; hifadhi ya maji ya ardhini; na uzalishaji wa mbegu. Aidha, wakulima 80 walipatiwa mafunzo ya matumizi ya plau za kukokotwa na ng'ombe na wengine 532 walipatiwa mbegu za mtama, uwele, karanga, alizeti na mbaazi zinazostahimili ukame, kukomaa mapema na kutoa mazao mengi.

Mheshimiwa Mwenyekit, katika eneo la ufugaji, jumla ya wakulima 118 walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ngombe, mbuzi na kuku. Kati ya hao, Wakulima wanawake walikuwa 54 na wanaume walikuwa 64. Aidha, madume 30 ya ng'ombe aina ya Mpwapwa; madume 60 ya mbuzi wa maziwa na nyama aina ya Blended; na majogoo bora 123 yalisambazwa kwa wakulima kwa lengo la kuongeza ubora wa mifugo katika Kijiji cha Chololo. Wakulima waliopatiwa mifugo bora walipewa pia dawa za kupambana na kupe na dawa nyingine muhimu za mifugo. Aidha, mradi ulitenga ekari 10 na kupanda malisho, hususan nyasi aina ya *Cenchrus ciliaris;*

mikunde *(Clitoria ternatea);* na miti aina ya *Leucaena pallida.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulitoa mafunzo kwa viongozi na wanakijiji 133 wa Chololo kuhusu hifadhi ya misitu, upandaji wa miti na utunzaji wa vitalu vya miti. Aidha, mradi ulifanya ukarabati wa kisima cha kijiji na miundombinu ya usambazaji wa maji kijijini; kujenga miundombinu ya kukusanya maji ya mvua ambapo matanki matatu yenye uwezo wa kuhifadhi lita 60,000 yalijengwa katika Shule ya Msingi Chololo. Miche 3000 pia ilipandwa katika eneo la eka tatu kwa ajili ya hifadhi ya msitu wa kijiji na vitalu viwili vya miche ya miti vilianzishwa katika eneo la shule na eneo kandokando ya kisima cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Maji katika Kijiji cha Chololo shughuli za utambuzi wa maji ya ardhini na jinsi kina chake kilivyokuwa kinabadilika katika miaka ya hivi karibuni zilifanywa na mradi huu. Aidha, ukarabati wa kisima kirefu na miundombinu ya usambazaji wa maji; ujenzi wa miundombinu ya kukusanya maji ya mvua kwenye paa la shule ya msingi; na ujenzi wa bwawa dogo kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi maji ya mvua ulifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zinazoendelea kufanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kuhusu nishati mbadala, hususan kuhusu faida za matumizi ya majiko banifu na namna ya kutengeneza majiko hayo katika maeneo yao. Aidha, shughuli za ujenzi wa mitambo midogo ya uzalishaji wa gesi

itokanayo na kinyesi cha mifugo kwa ajili ya kupikia unaendelea katika Kijiji cha Chololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za maendeleo katika utekelezaji wa Mradi huu zinatolewa katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo Televisheni ya Taifa *(TBC),* redio na magazeti. Aidha, baadhi ya taarifa za mradi zinapatikana kwa njia ya vijarida, picha, video na kwenye tovuti zifuatazo: www.*chololoecovillage.wordpress.com* na ukurasa wa *Facebook* - *www.facebook.com/pages/Chololoecovillage/254704077908782.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya hifadhi ya mazingira imeendelea kutolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali kama vile Maadhimisho na Maonesho ya Siku ya Mazingira Afrika, Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Wakulima Nanenane na Siku ya Ozoni Duniani. Aidha, elimu itolewe pia kwa kutumia njia zifuatazo: Vipeperushi nakala 15,000, mabango 100 na vitini nakala 15,000; magari ya matangazo, televisheni, redio na makala 20 kwenye magazeti; na maonesho ya matumizi ya majiko banifu. Aidha, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika mwaka wa fedha 2011/12, liliandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau vipeperushi 20,000 vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira na Jarida la Baraza la mwezi Januari – Juni, 2012 nakala 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi limekuwa ni ajenda ya kudumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Miradi yote ya

mabadiliko ya tabianchi inayotekelezwa inawajibika kuwa na eneo la elimu ya mabadiliko ya tabianchi. Hii ni pamoja na Miradi ya MKUHUMI, Miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)* na Miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi ilitoa elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa wadau mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Elimu ya mazingira kwa ujumla ikiwemo suala la mabadiliko ya tabianchi ilitolewa katika Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Wakulima (Nanenane); Wiki ya Utumishi wa Umma; na Miaka Hamsini ya Uhuru;

(b) Kwa kushirikiana na Kituo cha Habari cha Umoja wa Mataifa *(United Nations Information Centre),* Ofisi ilitoa mafunzo kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini kwa lengo la kukuza weledi kwa watendaji hao;

(c) Ofisi ilitoa mafunzo kwa wanadiplomasia pamoja na Watendaji Wakuu 50. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na yalihusu athari na changamoto za mabadiliko ya tabianchi Tanzania na juhudi zinazochukuliwa Kitaifa na Kimataifa katika kukabiliana na tatizo hilo;

(d) Mafunzo kuhusu Miradi ya Upunguzaji Gesi Joto *(Clean Development Mechanism - CDM)*

yalitolewa kwa Wizara na Idara za Serikali pamoja na Sekta Binafsi. Mafunzo haya yalilenga kujenga uelewa kuhusu hatua muhimu za kupitia kabla mradi haujasajiliwa na miradi inayoweza kutambulika na kusajiliwa kama miradi ya kupunguza gesi joto;

(e) Mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabianchi yalitolewa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Mafunzo hayo yalitolewa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mjini Bagamoyo. Pia, Ofisi ilitoa mafunzo ya aina hii kwa Baraza la Wawakilishi Zanzíbar;

(f) Mafunzo kuhusu hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ambao barafu yake ipo hatarini kutoweka kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi yalitolewa kwa Vikundi 11 vya Mazingira vinavyozunguka Mlima huo kupitia Programu ya *COMPACT* na Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhi Mkoani Kilimanjaro; na

(g) Mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabianchi na usalama yalitolewa kwa Watumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha suala la mabadiliko ya tabianchi linasimamiwa vyema na pia kuhakikisha utoaji elimu na uhamasishaji kuhusu mabadiliko ya tabianchi unakuwa endelevu. Ofisi ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(National Climate Strategy)* na baadae Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi *(National Climate Change Communication Strategy).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hii imeandaliwa kwa lengo la kuwa na mkakati jumuishi wa mabadiliko ya tabianchi na kukuza uelewa wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika ngazi zote nchini. Aidha, ina nia ya kuhakikisha kuwa taarifa zinazohusu mabadiliko ya tabianchi zinakuwa sahihi na zinaifikia jamii na pia zinasaidia katika kutekeleza shughuli za kuhimili mabadiliko ya tabianchi na hata zile za upunguzaji wa gesi joto. Hata hivyo, shughuli za upunguzaji gesi joto kwa nchi maskini kama Tanzania zinaangaliwa katika muktadha wa kujiletea maendeleo endelevu na pia kupunguza umaskini. Aidha, Rasimu ya Makakati wa Taifa wa MKUHUMI imeandaliwa na inabainisha utoaji wa elimu sahihi kwa umma kama sehemu mojawapo ya utekelezaji wa Mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12 Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, limeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba Miradi ya Ujenzi inafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira (Sura ya 191). Katika kipindi hicho, Miradi 31 ya Ujenzi na Uendelezaji kwenye vivutio vya utalii ilifanyiwa TAM na kupata Hati za TAM *(EIA Certificates).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu yake *(Environmental Management Act - Implementation Support Programme-EMA-ISP).* Katika kipindi hiki Ofisi iliandaa kwa lugha nyepesi *(Popular Version)* Kanuni

tano za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili ziweze kueleweka kwa wananchi wengi zaidi. Kanuni hizi ni Kanuni za Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors Regulations);* Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Zenye Sumu *(Hazardous Waste Control and Management Regulations);* Kanuni za Ada na Tozo za Mazingira *(Environmental Management Act - Fees and Charges Regulations);* Kanuni za Mazingira za Viwango vya Kelele na Mitetemo *(Noise and Vibration Regulations);* na Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu *(Regulations on the Solid Waste Management).* Aidha, watumishi saba wamejengewa uwezo kuhusu uongozi katika usimamizi wa mazingira na mbinu zinazotumika katika Majadiliano ya Kimataifa ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi imekamilisha tafsiri ya Kanuni nane za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika Lugha ya Kiswahili. Kanuni hizi ni Kanuni za Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors Regulations);* Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Zenye Sumu *(Hazardous Waste Control and Management Regulations);* Kanuni za Ada na Tozo za Mazingira *(Environmental Management Act -Fees and Charges Regulations);* Kanuni za Viwango vya Kelele na Mitetemo *(Noise and Vibration Standards Regulations);* Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu *(Solid Waste Management);* Kanuni za Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni *(Environmental Management: Control of Importation, Exportation and Consumption of Ozone Depleting Substances);* Kanuni za Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira *(Regulations on Strategic Environmental*

*Assessment);* na Kanuni za Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa *(Biosafety Regulations for Handling, Use, Import or Export of Genetically Modified Organisms and Products)*. Tafsiri ya Kanuni hizi itatoa fursa kwa wananchi wengi kuzielewa na kuzitumia katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria hii. Vile vile, Ofisi ilizindua Kamati ya Ushauri ya Mazingira *(National Environmental Advisory Committee-NEAC).* Kamati hii itakuwa chombo muhimu cha kutoa ushauri katika maamuzi muhimu yanayohusu mazingira. Ofisi pia, imeanza kuandaa Ripoti ya Pili ya Hali ya Mazingira Nchini. Ripoti hii huandaliwa kila baada ya miaka miwili kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ili kutoa takwimu muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi yanayohusu usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki kanuni nne za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ziko katika hatua mbalimbali za maandalizi. Kanuni hizi zinahusu:-

Kusimamia na Kuhifadhi Bioanuai katika Maeneo Asilia na Yasiyoasili *(Environmental Management Regulations on Conservation of Biological Diversity In-Situ and Ex-Situ);* Kanuni za Kusimamia Viwango vya Ubora wa Mionzi *(Environmental Management Regulation on Radiation Quality Standards);* Kanuni za Kusimamia Viwango vya Harufu *(Environmental Management Regulations on Noxious Smell Emission Quality);* na Kanuni za Kudhibiti Upatikanaji wa Vinasaba kutoka kwenye Maliasili *(Environmental Management Regulations on Control of Access to Genetic Resources).* Aidha, miongozo minne ya Sheria ya Mazingira inaandaliwa. Miongozo hii inahusu

Uhuishaji wa Uzalishaji na Matumizi Endelevu katika Sera na Mipango ya Serikali na Makampuni binafsi *(Mainstreaming Sustainable Consumption and Production - SCP) into Government and Company Policies and Plans);* Kulinda Ukanda wa Ozoni *(Protection of the Ozone Layer and the Stratosphere);* Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu *(Handling and Disposal of Hazardous Waste)*; na Usimamizi wa Taka za Vimiminika *(Management of Liquid Waste)*. Kanuni na miongozo hii inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu yake kwa kuendelea kuandaa na kukamilisha Kanuni na Miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; kuanzisha Baraza la Rufaa za Mazingira; kuandaa kwa lugha nyepesi tafsiri za kanuni na miongozo; kuandaa na kurusha vipindi vya televisheni na radio kuhusu Sheria na Sera ya Mazingira; kuandaa vipeperushi, vitini na warsha za kuelimisha umma kuhusu Sera na Sheria; kutekeleza mkakati wa mawasiliano ya programu na mafunzo kwa watumishi; na kujenga uwezo wa watumishi kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi yangu inaratibu Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Tuzo hii ilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2010 katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika tarehe 5 Juni 2010 Wilayani Bahi, Mkoani Dodoma na itakuwa ikitolewa

kila baada ya miaka miwili. Katika kipindi cha 2011/12, Ofisi iliendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii, Taasisi na Watendaji katika Ngazi za Wilaya na Mikoa kuhusu kushiriki katika mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuzo hiyo imetolewa kwa mara ya pili na Mheshimiwa Rais, katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2012 katika Manispaa ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro ambapo Mikoa 19 ilishiriki ambayo ni Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Manyara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Washindi wa mwaka huu walitoka katika makundi tisa ya ushindani. Washindi Kitaifa wa Tuzo hii walikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kundi la kaya ni Bwana Sombi J. Sombi wa Kijiji cha Mtiti, Kata ya Mughawo, Tarafa ya Ilongero, Wilaya ya Singida Vijijini, Mkoa wa Singida aliyepata Cheti na Fedha shilingi 2,000,000;

(b) Kundi la Kijiji ni Kijiji cha Mwese Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi kilichopata Cheti, Kombe na fedha shilingi 3,000,000;

(c) Kundi la Kata ni Bomalang'ombe Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa ambayo imepata Cheti, Kombe na fedha shilingi 3,000,000;

(d) Kundi la Shule za Msingi ni Shule ya Msingi Bupigi iliyoko Wilaya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga ambayo imepata Cheti, Kombe na fedha shilingi 3,000,000;

(e) Kundi la Shule za Sekondari ni Shule ya Sekondari Qameyu Tarafa ya Bashnet, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara ambayo imepata Cheti, Kombe na fedha shilingi 3,000,000;

(f) Kundi la Vyuo vya Mafunzo na Utafiti ni Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine Wilaya ya Morogoro Mjini, Mkoa wa Morogoro ambacho kimepata Cheti, Kombe na fedha shilingi 3,000,000;

(g) Kundi la Asasi za Kijamii za Uhamasishaji ni *Tanzania Environment Action Conservation Association (TEACA)* iliyopo Mkoa wa Kilimanjaro ambayo imepata Cheti, Kombe na fedha shilingi 5,000,000;

(h) Kundi la Taasisi za Uwezeshaji ni Kampuni ya Wiliamson Diamonds iliyopo Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga ambayo imepata Cheti na Kombe; na

(i) Kundi la Wilaya ni Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa ambayo imepata Cheti, kombe na fedha shilingi 5,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mashindano ya Tuzo hii, Shule ya Sekondari ya Qameyu iliyopo Tarafa ya Bashnet, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, imeonesha ubunifu katika uvunaji wa maji. Ili kupambana na changamoto ya ukosefu wa maji,

Shule imebuni na kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya ukungu na hivyo kuwa mshindi wa jumla katika ngazi ya kitaifa na imejipatia zawadi ya Cheti, Ngao na fedha taslimu shilingi 10,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wananchi wote waliojitokeza kushiriki katika mashindano haya. Kwa wale ambao hawakufanikiwa kushinda Tuzo mwaka huu, waendelee kuongeza juhudi ili kujitokeza tena mwaka 2014 mashindano haya yatakapofanyika tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi itaendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii, taasisi na watendaji katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mashindano haya. Ni matarajio yangu kuwa, mikoa yote itashiriki katika mashindano haya yatakayofanyika tena mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu endelevu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika inayohusisha nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Programu hii inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)* na *NORDIC Fund*. Miradi mitatu inatekelezwa chini ya Programu hii ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Bonde *(Catchment Management),* Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji na Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi na Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, shughuli zilizotekelezwa ni uandaaji wa Mkakati Shirikishi wa Usimamizi wa Taka wa Manispaa ya Kigoma. Maandalizi ya Mkakati huu yalishirikisha wananchi 150 kutoka mitaa 68 ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Vile vile, Mradi umekamilisha maandalizi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji sita vya mfano na vimeidhinishwa katika ngazi ya kijiji na Wilaya. Hivi sasa mipango hiyo iko katika hatua za mwisho za kuidhinishwa katika ngazi ya Taifa. Aidha, semina moja kuhusu uanzishwaji vikundi vya ujasiriamali na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu za biashara iliendeshwa kwa wanavikundi 24 kutoka vijiji sita vya mfano. Aidha, elimu ya ufugaji nyuki ilitolewa kwa vikundi vya wafugaji nyuki na kuchakata mazao yatokanayo na nyuki katika Kijiji cha Kisumba ambapo jumla ya washiriki 17 walifaidika na mafunzo haya. Aidha, Mradi umetoa mizinga ya kisasa 10 ya nyuki kwa kikundi cha Amani cha ufugaji nyuki toka Kijiji cha Kagongo, Wilaya ya Kigoma. Mradi pia umetoa elimu kwa kaya 8,504 katika eneo lote la Mradi kuhusu kilimo endelevu na ufugaji bora kwa lengo kuhamasisha kilimo kinachozingatia hifadhi ya mazingira katika Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi pia umeendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Miundombinu hiyo ni ukamilishaji wa ujenzi vyumba viwili vya madarasa katika Kijiji cha Isengule, Wilaya ya Mpanda, Ujenzi wa kisima kirefu kina cha mita 60 kwa ajili ya wachakata mafuta ya mawese katika Kijiji cha Ilagala na ujenzi wa vyoo katika Vijiji vya Kagunga, Mwamgongo, Karago na

Muyobozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma; Ujenzi wa hosteli ya wasichana na nyumba moja ya mwalimu na visima vitatu vya maji katika Kijiji cha Kirando, Wilaya ya Nkasi. Katika kipindi hicho sensa ya uvuvi ilifanyika katika eneo lote la Mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa lengo la kupata takwimu za aina ya vyombo vya uvuvi, nyavu zinazotumika na idadi ya wavuvi waliopo kwa lengo la kutambua kiwango cha uvuvi kilichopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika. Shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kuimarisha hifadhi ya mazingira katika shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika; Kuendelea kujenga vyumba vya madarasa, zahanati, visima vya maji, hosteli na vyoo katika Wilaya za Sumbawanga, Nkasi, Mpanda, Kigoma na Kasulu chini ya miradi midogo *(Community Infrastructure)* na ujenzi wa soko la kisasa la samaki na chumba cha kuhifadhia samaki wabichi katika Mwalo wa Kibirizi, kukamilisha ujenzi wa kilomita 102 za barabara kwa kiwango cha changarawe katika mikoa husika; kukamilisha ujenzi wa mialo minne ya kisasa katika Wilaya za Mpanda, Nkasi na Kigoma; ununuzi wa boti nne za doria na kununua vifaa kwenye vituo vya doria na kukamilisha ukarabati wa Ofisi za *TAFIRI* na Uvuvi Kigoma; Ujenzi wa Ofisi ya Doria Buhingu katika Wilaya ya Kigoma; Ununuzi wa magari mawili na pikipiki nne kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi; na kuendelea kuhamasisha na kuelimisha Wananchi wa Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa kuhusu hifadhi na

utunzaji wa mazingira na kuimarisha hifadhi katika lindimaji *(catchment )* ya Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu nia ya kuanzisha Programu Endelevu ya Kuhifadhi Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa itakayohusisha nchi za Tanzania, Malawi na Msumbiji chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi ilendelea kufanya uhamasishaji wa wadau katika wilaya zinazopakana na Ziwa Nyasa ambazo ni Mbinga, Ludewa, Makete, Njombe na Kyela ili kujenga uelewa wa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika Programu hii. Aidha, mawasiliano ya kikanda yaliendelea kufanyika kati ya nchi yetu na nchi jirani za Malawi na Msumbiji kuhusu uanzishwaji wa Programu hii. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau wengine kupitia kikao cha wadau, imebainisha kuwa moja ya maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya ufadhili katika awamu ya tano ya Mfuko wa Mazingira Duniani ni hifadhi endelevu ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi itaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha zilizotengwa katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environmental Facility)* kwa ajili ya Mradi huo ambazo ni Dola za Marekani 1,500,000. Aidha, Ofisi itaendelea kuwasiliana na nchi washiriki na Benki ya Dunia kuhusu ukamilishwaji wa maandalizi ya Programu ya Pamoja ya Kuhifadhi Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Ofisi imeendelea kuratibu Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira inayotekelezwa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani *(USAID).* Mashirika hayo ni pamoja na *World Wide Fund for Nature (WWF); Jane Goodall Institute (JGI); University of Rhodes Island & Tanzania Coastal Management Partnership (URI/TCMP); University of Florida - Integrated Water Sanitation and Hygiene (iWASH), United States Department of Interior – International Technical Assistance Programme (DOI – ITAP)* na *African Wildlife Foundation (AWF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Programu hii, kwa kupitia Taasisi ya Jane Goodall Institute imeendelea kutekeleza Mradi wa kusaidia Jamii kuhifadhi Mazingira, hususan katika maeneo ya Mfumo-ikolojia wa Gombe na Masito katika Wilaya za Kigoma na Mpanda. Programu hii inayohusisha vijiji 49 katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Mpanda ina lengo la kuhudumia jamii ya watu wapatao 300,000. Katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zilifanyika: Mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 27 iliandaliwa; mafunzo ya wiki mbili yalitolewa kwa wahamasishaji 103 kuhusu matumizi ya majiko banifu; kampeni za kuzuia moto ziliendeshwa katika vijiji vitano ambapo watu 4,450 walishiriki; mafunzo kuhusu hifadhi ya maliasili vijijini yalitolewa kwa walinzi *(village game scouts)* 16 katika Chuo cha Wanyamapori Pansiasi Mwanza; mafunzo ya kilimo endelevu yalitolewa kwa wakulima 177 ambapo wakulima 54 katika vijiji vinane waliwezeshwa kuanzisha kilimo mseto na wengine 80

walipata mafunzo kuhusu utunzaji bora wa nyuki. Aidha, Mradi ulisambaza mizinga bora kwa vikundi vya kijamii 17 na majiko banifu kwenye kaya 170 katika vijiji sita vya Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *African Wildlife Foundation - AWF* ni Shirika ambalo linatekeleza shughuli zake katika maeneo ya Tarangire, Ziwa Manyara, Kilimanjaro Magharibi, Ziwa Natron, Kondoa, Monduli, Kiteto, Babati, Mbulu, Karatu, Longido na Simanjiro. Lengo lake ni kuhakikisha kuna utunzaji endelevu wa bioanuai katika maeneo muhimu ya mazingira kama vile Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwa kushirikiana na wakulima wadogowadogo na wafugaji ili kuinua vipato vyao. Katika kipindi hiki, shughuli zifuatazo zilifanyika: Kutoa elimu kwa jamii kuhusu VVU na UKIMWI; kutoa mafunzo ya ujasiriamali na hifadhi ya mazingira kwa wadau wa mradi hususan katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs); na kutoa huduma ya maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu na viumbe wengine katika maeneo yanayozunguka mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya kitaalamu kuhusu namna ya kutekeleza programu, mipango na Miradi ya Usimamizi wa Mazingira yametolewa na *United States Department of Interior – International Technical Assistance Programme - DOI - ITAP)* ikishirikiana na mashirika mengine yanayofadhiliwa na Serikali ya Marekani. Katika kipindi hiki, Programu hii ilitoa mafunzo kwa viongozi na walinzi-jamii *(village game scouts)* katika Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Burunge, Ikona, Pawaga-Idodi na

Enduimet kuhusu ulinzi na usimamizi wa rasilimali, ujasiriamali na uandaaji wa mabango ya kuelekeza wageni ndani ya maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori na vipeperushi vya kutangaza Jumuiya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya *Tanzania Integrated Water, Sanitation and Hygiene (IWASH)* inaendesha shughuli za kusaidia jamii kupata huduma za maji safi na salama na kuboresha usafi binafsi na usafi wa mazingira ulio endelevu na kuanzisha mipango shirikishi ya kuhifadhi rasilimali za maji, hususan katika jamii zinazoishi katika Bonde la Wami/Ruvu. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Programu hii ilitoa mafunzo kwa mafundi mchundo watano kuhusu namna ya kutengeneza pampu za maji na timu kumi za uchimbaji visima kuhusu namna ya kutengeneza visima vifupi. Maeneo 60 ya kutolea huduma ya maji yalitengenezwa ambapo takriban watu 16,500 wanapata huduma ya maji safi na salama kutoka katika vituo hivyo. Aidha, Programu hii ilitoa msaada wa pampu tano za maji za kutumia kamba na mitambo midogo 500 ya kuchujia maji ya kunywa ijulikanayo kama *Tulip Filters*. Mradi pia ulisaidia kujenga vyoo bora katika shule kumi za msingi, vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 5,500. Pia, wanafunzi wanne walipata ufadhili wa masomo katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam chini ya Programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Rhodes Island na *Tanzania Coastal Management Partnership (URI/TCMP)* wanaendesha shughuli zinazolenga katika hifadhi ya rasilimali muhimu za misitu ya Pwani,

wanyamapori na viumbe wa majini; hifadhi ya mifumo-ikolojia muhimu ya Pwani na viumbe walio katika hatari ya kutoweka mfano, kasa; pamoja na kuboresha afya na hali ya maisha ya watu wanaoishi katika mazingira ya Pwani. Shughuli hizi zinatekelezwa katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo (Tanzania Bara) na maeneo ya Fumba na Rasi ya Menai (Zanzibar).

Katika kipindi hiki vikundi vya hifadhi ya mazingira vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo kuhusu utunzaji wa miche ya miti, hifadhi ya mazingira ya Pwani na viumbe baharini hususan kasa, ujasiriamali, utunzaji wa kumbukumbu muhimu, uzazi wa mpango, Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uendeshaji wa *SACCOs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *World Wide Fund for Nature (WWF)* limeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa kutekeleza sera zinazohusu usimamizi wa mazingira na maliasili kwa njia ya mafunzo, ukuzaji wa uelewa na weledi. Shirika pia limeendelea kusaidia utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Jamii katika hifadhi ya mazingira, hususan katika maeneo yanayozunguka Mbuga na Hifadhi za Taifa na Wanyamapori kwa lengo la kuongeza kipato. Maeneo ya Mradi ni pamoja na Hifadhi za Taifa za Ruaha, Manyara, Tarangire na Serengeti; maeneo tengefu ya Selous-Niassa na Ugalla-Katavi-Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Mradi ulikamilisha shughuli zifuatazo: Ujenzi wa kituo cha watalii, vituo viwili vya ulinzi-jamii na milango *(Entrance*

*Gates)* minne ya kuingilia kwenye hifadhi na ukarabati wa barabara za ndani katika Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori *(Wildlife Management Area – WMA)* ya Burunge iliyopo katika Wilaya ya Babati; ujenzi wa vituo vinne vya ulinzi-jamii, malango manne ya kuingilia kwenye hifadhi na vituo vitatu vya kuangalia rasilimali za hifadhi *(observation centres)* katika Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet iliyopo katika Wilaya ya Longido; ujenzi wa vituo viwili vya ulinzi-jamii, visima viwili vya maji na kuweka mipaka eneo la kilometa za mraba 115 katika Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori la Ipole iliyopo katika Wilaya ya Sikonge; ujenzi wa vituo viwili kwa ajili ya ulinzi-jamii na malango mawili ya kuingia kwenye Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Ikona iliyopo katika Wilaya ya Serengeti; na ujenzi wa barabara ya changarawe yenye urefu wa kilometa 30, kituo kimoja cha ulinzi-jamii na lango moja la kuingia kwenye Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Matumizi Bora ya Maliasili - Idodi na Pawaga (MBOMIPA) katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu shughuli za Programu hii kwa kuzingatia mipango ya Miradi iliyopo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi iliyoandaliwa mwaka 2007, Mpango wa Kupunguza uzalishaji wa Hewa Ukaa unaotokana na Ukataji wa Miti na uharibifu wa Misitu (MKUHUMI), Programu na Miradi mbalimbali ya kuhimili mabadiliko

ya tabianchi na kupunguza gesijoto. Aidha, Ofisi ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa 17 wa Nchi Wanachama uliofanyika Durban Afrika ya Kusini Desemba mwaka 2011. Katika Mkutano huo, nchi ziliazimia kuwa na Mpango mpya utakaohusisha nchi zote kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi, utakaosimamiwa na *Ad-hoc Working Group on Durdan Platform for Enhanced Actions (ADP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(Africa Adaptation Programme)* unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Miradi minne ya majaribio katika upatikanaji wa maji iliendelea kutekelezwa katika Wilaya za Igunga Mkoani Tabora katika Vijiji vya Nanga, Igumbi, Majengo na Itunduru, Mbinga Mkoani Ruvuma Kijiji cha Ng'ombo, Misenyi Mkoani Kagera katika Vijiji vya Byeju, Mbale, Kanyigo, Kashasha, Bukwali na Kitobo na Wilaya ya Kaskazini A Kijiji cha Nungwi. Aidha, Miongozo miwili inayohusu Ujumuishaji wa Masuala ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Sera, Mipango na Programu za Wizara za Kisekta na Serikali za Mitaa iliandaliwa na Tathmini na Uperembaji wa Shughuli za Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Wilaya iliandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi uliendesha mafunzo ya muda mfupi katika nyanja za uongozi, mipango, utawala, uhasibu, bajeti, ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa watumishi 11 wa Ofisi. Kwa kupitia Mradi huu, mapitio ya Rasimu ya Mpango wa Taifa wa

Mazingira *(Draft National Environmental Action Plan-NEAP)* yalifanyika, ili kujumuisha masuala ya kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na maandalizi ya rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(National Climate Change Communication Strategy)* yamefanyika. Kazi hizi zinategemewa kukamilika katika mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/13, Ofisi itatekeleza shughuli zifuatazo chini ya Mradi huu: Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Mawasiliano wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango wa Taifa wa Mazingira; kutoa elimu kwa umma kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi wa Wizara mbalimbali kuhusu ujumuishaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika bajeti *(Medium Term Expenditure Frameworks - MTEF)* na Mipango Mkakati ya Wizara *(Strategic Plans);* kutoa elimu kwa umma kuhusu usimamizi Shirikishi katika Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi chini ya Mradi wa Kujenga Uwezo wa Serikali Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark. Katika kipindi hiki, Ofisi imekamilisha maandalizi ya rasimu ya mkakati huu unaolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika sekta zote na kuwahusisha wadau wote. Mkakati huu unabainisha hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na wadau mbalimbali katika kuhimili mabadiliko ya

tabianchi na kupata fursa za maendeleo kwa kushiriki katika juhudi za kimataifa za kupunguza gesijoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu - MKUHUMI. Awamu ya kwanza ya Mpango huu ilihusisha miradi tisa ya majaribio inayotekelezwa kupitia Asasi Zisizo za Serikali katika Wilaya za Kondoa, Kigoma, Kilosa, Kilwa, Lindi Vijijini, Rungwe, Muheza, Kisarawe, Shinyanga Vijijini na Kahama kwa upande wa Tanzania Bara na katika Wilaya za Chakechake, Wete, Mkoani, Micheweni, Kusini Unguja, Kati na Kaskazini B kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii inalenga kuhifadhi misitu ya asili, kupanda miti kwa ajili ya matumizi ya wananchi hususan nishati, ugawanaji bora wa mapato yatokanayo na mauzo ya Hewa ya Ukaa, kilimo bora, matumizi ya majiko banifu na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Awamu ya kwanza ilianza mwezi Aprili 2008 hadi Agosti 2011 na sasa imeingia awamu ya pili ya utekelezaji kuanzia Septemba 2011 hadi Septemba 2013, ambapo Halmashauri zitashirikishwa katika mpango huu ili kuona jinsi misitu iyopo chini ya Halmashauri inavyoweza kunufaika na MKUHUMI. Aidha, sekta binafsi inatarajiwa kushirikishwa na kuanzisha ushirikiano endelevu kati ya Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu unalenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika

Sekta ya Misitu kwa kujenga uwezo wa wananchi katika kutunza misitu na katika kufanya hivyo itasaidia kuwaongezea kipato na kujiletea maendeleo, kukuza uelewa kuhusu MKUHUMI na kujenga uwezo wa kushiriki katika kuutekeleza ili kuchangia katika kupambana na athari za mabadiliko ya Tabianchi kwa ujumla. Mpango huu kupitia miradi ya majaribio unalenga kubaini njia bora za kutoa motisha kwa wananchi na taasisi mbalimbali zinazotunza na kuhifadhi misitu na kuweka mfumo bora na madhubuti wa soko la biashara ya hewa ukaa katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi iliendelea kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI na mpango kazi wake. Rasimu ya pili ya Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI imekamilika na itawasilishwa kwa wadau ili waweze kutoa maoni yao. Aidha, utekelezaji wa miradi ya majaribio ya MKUHUMI kupitia Asasi zisizo za Serikali uliendelea katika Wilaya za Kondoa, Kigoma, Kilosa, Kilwa, Rungwe, Muheza, Kisarawe na Shinyanga kwa upande wa Tanzania Bara. Mradi wa majaribio wa MKUHUMI kwa upande wa Zanzibar uliendelea kutekelezwa katika Wilaya za Chakechake, Wete, Mkoani, Micheweni, Kusini Unguja, Kati na Kaskazini B. Miradi hii yote inaendelea vizuri na katika baadhi ya vijiji wananchi wameanza kufaidika na miradi hii kwa kupata fedha za MKUHUMI kama sehemu ya majaribio. Aidha, Watanzania, Wanafunzi 16 wa Shahada ya Uzamivu *(Ph.D)* na hamsini 50 wa Shahada ya Uzamili katika Sayansi *(M.Sc)* walipata ufadhili kusoma hapa nchini na nje ya nchi ili kujenga

uwezo katika eneo la mabadiliko ya Tabianchi hususan katika eneo la MKUHUMI.

Ofisi pia inaendelea kutoa machapisho anuai na kusambaza kwa wadau ili kutoa taarifa na kuelimisha jamii kwa ujumla. Machapisho haya ni pamoja na mkakati wa MKUHUMI nakala 2000 na kijarida cha utekelezaji wa shughuli za MKUHUMI Tanzania nakala 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Ofisi pia iliendelea na hatua za uanzishaji Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Uzalishaji wa Hewa Ukaa *(National Carbon Monitoring Centre-NCMC)* na Mfuko wa Kitaifa wa MKUHUMI *(National REDD+ Trust Fund-NRTF).* Andiko la uanzishaji wa Kituo cha Ufuatiliaji wa Uzalishaji wa Hewa Ukaa limekamilika na taratibu za kuanzisha kituo hiki kama Wakala wa Serikali zinaendelea. Kituo hiki kitakusanya taarifa kuhusu kiasi cha hewa ukaa kinachopunguzwa kutokana na shughuli za uhifadhi wa misitu na kufuatilia masuala yote yanayohusu upunguzaji wa hewa ukaa nchini.

Katika hatua za awali kituo hiki kitakuwa chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa muda na baadae kitajitegemea kama wakala kamili wa serikali. Kituo hiki pia kinategemewa kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa nchi nyingine kwa kuwa kitakuwa cha kipekee katika ukanda huu wa nchi za Afrika ya Mashariki. Aidha, Mfuko wa Kitaifa wa MKUHUMI utasimamia fedha zitakanazo na shughuli za MKUHUMI nchini na kuhakikisha kuwa wananchi wanaoshiriki kuhifadhi misitu kwa ajili ya upunguzaji wa hewa ukaa

wanapatiwa malipo stahili ili kuwahamasisha kuendelea na juhudi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za MKUHUMI ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo na kukuza uelewa kwa umma kuhusu MKUHUMI, kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI, kuendelea na taratibu za kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Uzalishaji hewa ukaa - *NCMC* na uanzishaji wa Mfuko wa MKUHUMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kuanza kutekelezwa kwa Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani wenye thamani ya takriban Dola za Marekani 3,100,000, fedha ambazo Tanzania imetengewa katika Mfuko wa Mazingira wa Nchi Maskini Duniani *(LDCF).* Utekelezaji wa Mradi huu haukuanza mwaka huu kama ilivyopangwa kutokana na kuchelewa kukamilika kwa taratibu za kusaini mikataba na wafadhili wa mradi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taratibu zote zimekamilika na mradi utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/13. Aidha, Bodi ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia wa Kuhimili Mbadiliko ya Tabianchi - *AFB* imekubali kufadhili Mradi mwingine wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Pwani katika Mkoa wa Dar es Salaam wenye thamani ya takriban Dola za Marekani 5,000,000 na mradi huu pia unategemewa kuanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2012/13, pindi taratibu hizo zitakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeandaa Mradi wa Kujumuisha Masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sera na Mipango ya Maendeleo wenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,900,000 unaofadhiliwa kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa-*UNDP.* Malengo ya Mradi huu ni kuhuisha masuala ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maandalizi ya mipango ya maendeleo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa MKUKUTA II; kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi; na kuanzisha utaratibu wa usimamizi wa fedha kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu ni wa miaka minne (2011-2015) na unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *NEMC* na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Ofisi pia ilishiriki kikamilifu katika mikutano ya Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Nchi Wanachama uliofanyika Changwon, Korea Kusini. Pamoja na maamuzi mengine yaliyochukuliwa, Mkutano huu ulielekeza Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)* utoe fedha zaidi za kuwezesha utekelezaji wa Mkataba huu. Aidha, Mkutano ulielekeza kuwa uhuishaji wa Programu ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(National Action Programme to Combat Desertification - NAP)* ufanyike ili sasa upimaji wa utekelezaji wa Mkataba uweze kulingana na Mkakati wa Miaka Kumi wa Mkataba wa *United Nations Convention to Combat Desertification - UNCCD.* Ili

kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa katika Mkutano huu, Ofisi inaendelea na juhudi za kuhuisha Programu ya Taifa ya Kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame ili iendane na Mkakati wa miaka kumi wa utekelezaji wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkataba inayoshughulikia upatikanaji wa fedha *(Global Mechanism)* iliyoko Rome, Italy, imeendelea na hatua za kuandaa Mkakati wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(Integrated Financing Strategy - IFS)* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi Mkoani Kilimanjaro *(Sustainable Land Management in the High Land Kilimanjaro)* chini ya Mpango Maalumu wa Afrika wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(TerrAfrica).* Baada ya kuzinduliwa rasmi mwezi Mei 2011, Ofisi ya Mradi imefunguliwa Mkoani Kilimanjaro na Mratibu wa Mradi ameteuliwa na utekelezaji wa Mradi huu umeanza. Sekta zinazohusika ni Kilimo, Nishati, Maliasili na Mazingira.

Malengo makuu ya Mradi huu ni kupunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni, mbao na uchomaji mkaa; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo; na kuwezesha maisha bora kutokana na huduma bora zitokanazo na mazingira bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi pamoja na kuratibu utekelezaji wa Miradi ambayo inaendelea, kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF),* itaratibu utekelezaji wa Mradi wa Uhuishaji wa Maendeleo Endelevu ya Misitu katika Ukanda Miombo katika Mikoa ya Tabora, Rukwa na Katavi. Mradi huu utagharimu Dola za Marekani 3,200,000 na utatekelezwa katika Tarafa za Usinge na Imalamakoye Wilayani Urambo, Mbola katika Wilaya ya Uyui na Inyonga katika Wilaya ya Mpanda. Jumla ya vijiji 28 vitashiriki katika utekelezaji wa Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu *(United Nations Commission for Sustainable Development):* Mwaka huu, jumuiya ya Kimataifa imeadhimisha miaka 20 tangu kufanyika Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu mwaka 1992 *(Earth Summit)* huko Rio de Janeiro, Brazil. Maadhimisho haya yajulikanayo kama *Rio + 20* yamefanyika Rio de Janeiro, Brazil kuanzia tarehe 20 hadi 22 Juni 2012. Malengo ya Mkutano huo pamoja na mambo mengine yalikuwa ni kutathmini kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Rio wa Mwaka 1992, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizobaki katika kufikia maazimio ya mkutano huo.

Mkutano wa *Rio +20* ulijikita katika dhima mbili kuu ambazo ni (a) Uchumi wa Kijani katika muktadha wa maendeleo endelevu na kupunguza umaskini (*Green economy in the context of sustainable development and poverty eradication)*; na (b) Muundo wa Kitaasisi

kwa ajili ya maendeleo endelevu *(The institutional framework for sustainable development).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya Mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Makubaliano yalifikiwa kuwa uchumi wa kijani uzingatie kupunguza umaskini na kuhakikisha usalama wa chakula na kuinua uchumi na hali ya maisha hasa kwa nchi zinazoendelea;

(ii) Kuimarisha muundo wa utekelezaji kwa kuziongezea nguvu zaidi Taasisi za Umoja wa Mataifa kama *UNEP* na kuimarisha ushiriki na mchango wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Serikali katika kuleta maendeleo endelevu;

(iii) Kuimarisha mafanikio ambayo yamepatikana tangu Mkutano wa Rio wa mwaka 1992 hadi sasa. Kwa Tanzania mafanikio hayo ni uundwaji wa Taasisi, Sera na Sheria zinazosimamia shughuli za maendeleo endelevu nchini. Mfano, kuanzishwa kwa Idara ya Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; kutungwa kwa Sera ya Mazingira (1997) na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004); kuandaliwa kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Maandalizi ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na uundwaji wa Sera na Sheria mbalimbali za Kisekta;

(iv) Kuimarisha Ushirikiano wa Kimataifa katika kutekeleza Maazimio ya Rio ya mwaka 1992. Maazimio haya ni Tamko la Rio kuhusu Dunia kuendelea kutekeleza shughuli za maendeleo kwa kuzingatia

misingi ya maendeleo endelevu; Misingi 27 ya Mkutano wa Rio; Ajenda Nambari 21; Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi; Mkataba wa Bioanuai na Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame;

(v) Kuimarisha utekelezaji wa azimio la nchi zilizoendelea kwa kuchangia asilimia 0.7 ya pato lao la ndani kwa nchi zinazoendelea hasa nchi za Afrika ili kuondoa umaskini; na

(v) Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano wa Rio+20 uende sanjari na utekelezaji wa Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, nchi yetu ni Mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Hifadhi ya Bioanuai *(Convention on Biological Diversity)* na Itifaki ya Cartagena. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Hifadhi ya Bioanuai kwa kushirikisha wadau kutoka Sekta za Kilimo, Misitu, Uvuvi na Wanyamapori katika maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Bioanuai kulingana na shabaha zilizopo kwenye Mpango Mkakati wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai ambao ni wa miaka kumi kuanzia 2011 hadi 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mkataba na maandalizi ya Mpango Mkakati wa Kitaifa chini ya ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendesha mafunzo ya siku tano ya utambuzi wa mimea/bidhaa ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki kwa wataalam 15 kutoka Mamlaka za udhibiti, Vyuo Vikuu na Vyuo vya Utafiti wa Kilimo. Taasisi zilizopewa mafunzo hayo ni pamoja na *Tropical Pest Research Institute - TPRI, Shirika la Viwango Tanzania - TBS, Tanzania Official Seed Certifying Institute - TOSCI,* Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali - *GCLA,* Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani - Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania - *TFDA,* Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine - SUA, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Plant Health Service of the Ministry of Agriculture.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kukuza uelewa kwa wananchi, Mfumo wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa *(National Biosafety Framework)* umetafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili kwa lengo la kujenga uwezo na upashanaji wa habari za matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Katika kipindi hiki, Ofisi pia imeendesha warsha moja katika Kanda ya Mashariki Jijini Dar es Salaam ili kukuza uelewa kwa wadau kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, mchakato wa kuandaa nyenzo muhimu za usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa umeanza na wataalam washauri wamewasilisha rasimu ya nyenzo hizo. Nyenzo hizo ni pamoja na:-

(i) Mwongozo kwa ajili ya kushughulikia dharura iwapo itatokea shughuli za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa *(Manual for GMOs emergency response);*

(ii) Mwongozo kwa ajili ya kuendesha majaribio yanayohusu mimea, bidhaa au viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki *(Manual on procedures for Laboratory/green house contained trial on GMOs for contained use);* na

(iii) Mwongozo wa masuala ya kijamii na kiuchumi ambayo ni muhimu kuzingatiwa wakati wa kufanya maamuzi ya shughuli za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa *(Manual of socio-economic priority issues to be taken into consideration for decision making process).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/13, Ofisi itatekeleza shughuli zifuatazo: Kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu utambuzi, udhibiti, tathmini na masuala ya kisheria kuhusu bidhaa na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki; na kuboresha maabara tano kati ya 11 zilizoainishwa kwenye mtandao unaojumuisha vituo kumi vya Tanzania Bara na kituo kimoja cha Zanzibar cha matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, Ofisi itahuisha shughuli za Mradi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia katika majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kuendesha warsha za wadau ili kuainisha majukumu yao katika utekelezaji endelevu wa shughuli za mradi baada ya muda wake kumalizika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu baina ya Nchi na Nchi (Mkataba wa Basel) na Mkataba Unaozuia Uingizaji wa Taka za Sumu Barani Afrika (Mkataba wa Bamako). Katika kipindi hiki, mradi wa kujenga uwezo wa nchi katika usimamizi wa usafirishaji wa taka sumu kupitia katika bandari umeandaliwa. Aidha, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya usafi wa mazingira katika Miji na Majiji nchini iliyozinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari 2011. Shughuli za usafi wa mazingira zinafanyika kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi nchini kote chini ya usimamizi wa TAMISEMI. Kampeni hii inalenga kuboresha hali ya usafi wa mazingira ya miji na kujenga utamaduni wa kuzingatia usafi wa mazingira miongoni mwa jamii. Matokeo ya juhudi za usafi yameanza kuonekana, kwa hiyo, natumia fursa hii kuwapongeza Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri mbalimbali kwa kuwa mstari wa mbele kusimamia masuala ya usafi; ni vyema juhudi hizo ziendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/13, shughuli zifuatazo zitatekelezwa: Kukusanya takwimu na taarifa za usimamizi wa taka za sumu na taka za kawaida katika Bandari za Dar es Salaam na Tanga; Kuratibu uandaaji wa Mpango Kabambe wa Usimamizi wa taka katika bandari hizo *(Port Waste Management Plan);* Kuandaa Mpango na kuendesha mafunzo kwa wadau wa sekta zinazojihusisha na taka za sumu katika bandari na kwingineko; Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa

Taka; Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Usafi wa Mazingira katika Miji na Majiji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa agizo la Serikali la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini iliyoanza kutumika Oktoba, 2006. Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Kanuni za mwaka 2006 zinazopiga marufuku utengenezaji, uingizaji, uuzaji na matumizi ya bidhaa za plastiki, Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko laini ya plastiki ili kulinda mazingira na afya ya binadamu kutokana na madhara ambayo yanajitokeza kwa kuendelea kutumia mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilipitia Kanuni za zamani na kuandaa Kanuni mpya kuhusu matumizi ya mifuko laini ya plastiki *(The Environmental Management Act, Control of Polyethylene Materials Regulations).* Kanuni hizi mpya zimetoa fursa kutumika kwa baadhi ya bidhaa za plastiki *(Polyethelyne Materials)* kwa ajili ya shughuli muhimu katika viwanda vya aina mbalimbali (mfano sekta ya maziwa na usindikaji wa vyakula). Kanuni hizi ziko kwenye utaratibu wa ukamilishaji kwa ajili ya kuanza kutumika. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu Kanuni hii na wajibu wao kuzizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Montreal kuhusu kuondoa matumizi ya Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Angani. Lengo la Programu hii ni kuendelea kupunguza matumizi ya kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni angani kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba huu na kukuza matumizi ya kemikali na teknolojia mbadala ambazo ni salama kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki shughuli zilizotekelezwa ni kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ozoni tarehe 16 Septemba, 2011. Maadhimisho haya yalifanyika Jijini Arusha kwa kufanya semina ya Mafundi Mchundo wa majokofu na viyoyozi kutoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Aidha, Mafundi Mchundo na Maafisa Mazingira 102 kutoka Mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa walishiriki katika mafunzo kuhusu teknolojia mbadala na njia bora za kuhudumia majokofu na viyoyozi. Mafunzo haya yanalenga katika kuwaongezea Mafundi Mchundo ufanisi katika kazi zao hususan kuzingatia utunzaji wa mazingira kwa kuepuka kuachia gesi zisizo rafiki wa Tabaka la Ozoni hewani wanapohudumia majokofu na viyoyozi. Vile vile, katika kipindi hiki takwimu za uagizaji nchini na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni angani zilikusanywa na kuandaliwa taarifa na kuwasilishwa katika Sekretarieti ya Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango huu kwa kutekeleza kazi

zifuatazo: Kuendesha mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira kuhusu majukumu yao katika utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni) za mwaka 2007; kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs* nchini kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; Kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba katika Sekretarati ya Mkataba; kuendelea kutoa mafunzo ya Mafundi Mchundo wa majokofu na viyoyozi kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo na ubadilishaji wa teknolojia za mitambo ya kupozea inayotumia gesi haribifu; na kutoa elimu kwa wadau na umma kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kulinda Tabaka la Ozoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Mkataba wa Stockhom kuhusu kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira. Katika kipindi hiki, Ofisi imekamilisha Mwongozo wa Usimamizi wa Mafuta yenye Kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls - PCBs* yanayotumika kupoza mitambo na vifaa vya kuzalisha umeme; Mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira, Sekta ya Kilimo na Afya kuhusu usimamizi wa kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira yameendeshwa. Mafunzo kuhusu teknolojia bora na utaratibu bora wa usimamizi wa mazingira dhidi ya kemikali zinazotokana na uchomaji taka na mchakato wa uzalishaji bidhaa viwandani aina ya *dioxins* na furans yameendeshwa katika Jiji la Mwanza na Arusha, washiriki walitoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kigoma,

Kilimanjaro, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tanga. Jumla ya washiriki 57 walinufaika na mafunzo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kuhusu madhara hususan ya kiafya yatokanayo na kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira yaliendeshwa Mjini Morogoro kwa wataalam 47 kutoka Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii na Kilimo, Chakula na Ushirika. Mafunzo haya yalijumuisha Waganga Wakuu wa Wilaya kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Aidha, kutokana na ukosefu wa vifaa, uchunguzi wa kimaabara wa mafuta yatumikayo kupoza mitambo na vifaa vya kusambaza umeme kama vile transformers na capacitors ili kujua uwepo wa kiwango cha kemikali aina ya *PCBs* haukufanyika kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Mkataba wa Stockholm ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo wa taasisi husika. Shughuli zitakazofanyika chini ya Mradi huu ni pamoja na kutoa mafunzo kuhusu madhara yatokanayo na uchomaji moto holela kama vile taka na misitu; Kusambaza Mwongozo wa Usimamizi wa Mafuta yenye Kemikali aina ya *PCBs* yanayotumika kupoza mitambo na vifaa vya kusambaza umeme. Aidha, Mpango wa Taifa wa Usimamizi na utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm utafanyiwa mapitio ili kuuboresha kwa kujumuisha kemikali zilizo katika makundi kumi zilizoongezwa katika

Mkataba huu Mwaka 2009 na Mwaka 2011. Kati ya kemikali hizi sita hutumika kama viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea, Kemikali tano hutumika katika mchakato wa kuzalisha bidhaa viwandani na kemikali tatu huzalishwa bila kukusudia *(by products)*. Aidha, kemikali moja inapatikana katika makundi yote matatu na kemikali mbili zinatumika viwandani na vile vile huzalishwa bila kukusudia. Katika mwaka 2012/13, Ofisi itaendelea kukuza uelewa wa umma kwa kusambaza taarifa kuhusu usimamizi bora wa kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/12, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Afrika ya Mtandao wa Hali ya Mazingira *(African Environmental Information Network)* chini ya Ufadhili wa *UNEP* kupitia *UNDP*. Lengo la Programu hii ni kuongeza uwezo wa nchi katika kupatikana kwa taarifa za hali ya Mazingira na kuwa na mtandao wa habari za Mazingira baina ya Nchi za Afrika, kubadilishana taarifa za hali ya Mazingira, kuandaa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mradi na Uandaaji wa Ripoti kuhusu Hali ya Mazingira nchini. Programu hii imekamilisha uandaaji wa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Jiji la Dar es Salaam *(Dar City Environmental Outlook Report).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi itasambaza Ripoti hii kwa wadau kwa lengo la kutoa mwongozo wa kutayarisha taarifa za namna hiyo kwa majiji na miji mingine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni kila mwaka ni Siku ya Mazingira Duniani, Tanzania huungana na Jumuiya ya Kimataifa katika kuadhimisha siku hii. Maadhimisho haya Kimataifa mwaka huu yalifanyika nchini Brazil na kwa hapa nchini yalifanyika Mjini Moshi Mkoani Kilimanjaro. Kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu Kimataifa ni Uchumi Kijani: Unakuhusu? *(Green Economy: Does it include you?).* Kitaifa Kaulimbiu yetu ilikuwa Hifadhi Mazingira: Jikite katika Uzalishaji Endelevu. Ujumbe huu ulilenga katika kuhamasisha Jamii ya Watanzania kuendesha shughuli za kiuchumi katika misingi na taratibu ambazo hazina athari kubwa kwa mazingira hususan katika uzalishaji viwandani, kilimo na uchimbaji madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho ya mwaka huu yaliambatana na shughuli mbalimbali zinazohusiana na hifadhi ya mazingira nchi nzima kwa kipindi cha wiki moja, kuanzia tarehe 1 Juni hadi siku ya kilele tarehe 5 Juni. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na upandaji na palizi ya miti, mafunzo mbalimbali kuhusu mazingira kupitia Maonesho na mashindano ya nyimbo na ngonjera ili kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa hifadhi na usafi wa mazingira. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi ya Mazingira kwa kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwashukuru wananchi na taasisi mbalimbali kwa kushiriki katika maadhimisho haya. Aidha, napenda kuwashukuru kwa namna ya pekee Viongozi na Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kukubali kuwa

wenyeji wa maadhimisho hayo na pia kwa ushirikiano wao uliofanikisha maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF),* unaoendelea nchini ikiwa ni pamoja na Miradi midogo chini ya *GEF Small Grant Programme*. Mfuko huu unafadhili maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni Hifadhi ya Bioanuai; Mabadiliko ya Tabianchi; Hifadhi ya Ardhi; Hifadhi ya Maji ya Kimataifa; Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni; na Kemikali Zinazodumu kwa Muda Mrefu katika Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, miradi sita iliwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Mfuko kwa ajili ya kufadhiliwa na awamu ya tano ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia *GEF-STAR* - 5. Miradi hiyo ni *Conservation and Management of Kihansi Ecosystem; Malawi/Mozambique/Tanzania Regional Lake Conservation and Development Project; Strengthening Implementation of Cartegena Protocol on Biosafety; Promotion of Renewable Energy Application for Rural lighting and Agro – Industral Sector in Tanzania; Promotion of Geothermal as Altenative Source of Electricity Generation in Tanzania & Enhancing the Forest Nature Reserves Network for Biodiversity Conservation in Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi

ya *GEF* na kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka *GEF-STAR 5* ili kutekeleza Miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni mwaka wa saba tangu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ianze kutekelezwa. Miongoni mwa wadau muhimu katika usimamizi na utelekelezaji wa Sheria hii ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* lenyewe. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12 Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997, Mpango Mkakati wa Baraza *(NEMC Strategic Plan 2010-2014)*, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, nyaraka na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira, kuondoa umaskini na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuhakikisha kuwa Sheria ya Mazingira inazingatiwa na inasimamiwa ipasavyo katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya uchumi. Baraza liliendelea kufanya ukaguzi wa kudumu katika maeneo yenye uchafuzi mkubwa wa mazingira. Aidha, Baraza lilifanya ukaguzi wa migodi, viwanda, sehemu za uzalishaji na gereji mbalimbali ili kuhimiza utekelezaji wa kanuni za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa viwanda vingi hapa nchini vimeanzishwa kabla ya kuwepo kwa Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, ambayo inaelekeza kuwa miradi yote hapa nchini ni lazima

ifanyiwe Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya utekelezaji wake. Kwa hiyo, kuna tatizo la kutozingatia misingi ya hifadhi ya mazingira hasa kuweka miundombinu ya usafishaji wa majitaka kutoka katika viwanda hivyo. Kutokana na upungufu huo, viwanda hivyo vimepewa notisi na kutakiwa kulipa tozo kwa mujibu wa kanuni za tozo za mazingira *(Environmental Management (Fees and Charges) Regulations 2008),* wametakiwa wale wote ambao miradi au viwanda vyao havikufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kufanya Ukaguzi wa Mazingira *(Environmental Audit),* kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, lilikagua viwanda 11 ambavyo vinachafua mazingira kutokana na umwagaji wa majitaka yasiyotibiwa na uchafuzi wa hewa. Viwanda vilivyokaguliwa katika Mkoa wa Dar-es-Salaam ni *Ruidar Plastic Recycling* - Mbagala; *Tanpack Industries* - Mikocheni; Kiboko Paints - Mikocheni; *Shelys Pharmaceuticals* - Mwenge; *Bidco Oil and Soap Industries* Mikocheni; na KTM – Mbagala, pamoja na *Bundaa Oil Mills* cha Bunda na *21st Century*, *Morogoro Canvas* na *Tanzania Hides* vilivyoko Kihonda, Morogoro. Viwanda vingine vilivyokaguliwa ni Kiwanda cha *Afritex,* Kiwanda cha Chokaa na Kiwanda cha *Tanga Fish* vilivyoko Mjini Tanga. Viwanda hivi vilipewa notisi ili kufanya marekebisho katika mfumo wa kutibu majitaka na vingine kwa kutokuwa na mifumo hiyo kabisa. Baraza pia lilifanya ukaguzi katika Migodi ya Buzwagi, Bulyankulu, Resolute, Buhemba na Mgodi wa North Mara. Baraza lilitoa maelekezo ya kudhibiti

uchafuzi wa mazingira uliobanika kutokana na shughuli za migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limefuatilia kwa karibu suala la kuhamishwa kwa Kiwanda cha *Azania Wheat Flour Ltd*. kilichopo Ubungo Riverside – Dar es Salaam kutokana na uchafuzi wa hewa unaosababishwa na shughuli za uzalishaji. Hata hivyo, Baraza limegundua kuwa kiwanda hicho kinachomilikiwa na Kampuni ya Makunguni Traders Ltd. walikuwa na vibali vyote vya kupewa eneo hilo na hivyo kisheria na hawana mpango wa kuhama. Hata hivyo, Baraza liliuagiza uongozi wa kiwanda hicho kutekeleza yafuatayo: Kuhakikisha vumbi na kelele toka kiwandani vinakidhi viwango vya mazingira; Kufanya utafiti na kuweka mitambo itakayodhibiti vumbi na kelele; na kufanya ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit)* ili kuzingatia viwango vya mazingira kikamilifu. Utafiti huo umekamilika na kiwanda kimefunga mitambo ya kuzuia vumbi na kelele kulingana na viwango vya taifa vya mazingira. Baraza litaendelea kufuatilia ili kuhakikisha mfumo huo unakidhi na kuzingatia sheria.

Baraza pia, lilifanya ukaguzi katika maeneo kadhaa ya makazi kufuatilia malalamiko ya wananchi kuhusu uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ujenzi katika mikondo ya mito na fukwe za baharí. Miongoni mwa maeneo yaliyokaguliwa ni kiwanja Na. 101 kilichopo Mtaa wa Migombani, Mbezi Beach, ambacho kililalamikiwa kwa ujenzi uliozuiba mkondo wa maji. Baraza lilisitisha ujenzi huo na kuamuru sehemu ya nyumba iliyoziba mkondo huo kubomolewa. Viwanja

vingine vilivyolalamikiwa katika Wilaya ya Kinondoni ni Viwanja Na. 2009, 2019 na 2020, ambavyo kwa mujibu wa Wizara ya Ardhi, havina hati miliki na havitambuliwi na mipango miji ya Wizara hiyo. Kwa hiyo, iliamuriwa kuwa nyumba hizo zibomolewe. Aidha, Kiwanja Na. 2002 kiligunduliwa kuwa na hati miliki halali, isipokuwa mipaka yake iko ndani ya mkondo wa Mto Mbezi. Kwa hiyo, iliamuriwa mipaka irekebishwe na ukuta ndani ya mto huo ubomolewe.

Kamati za Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kinondoni na ile ya Mkoa wa Dar es Salaam zimeridhia ubomoaji wa nyumba hizo ufanyike. Ubomoaji wa ukuta huo utafanyika mara tu maandalizi hayo yatakapokamilika. Kuhusu nyumba iliyojengwa katika Kiwanja Na. 2020 ambayo mmiliki wake amefungua kesi Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi, ubomoaji wa nyumba hiyo unasubiri uamuzi wa mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yaliyokaguliwa ni Eneo la Malolo na Mto Mlandizi, Wilaya ya Kibaha kutokana na umwagikaji wa mafuta kufuatia kupasuka kwa bomba la mafuta la *TAZAMA;* Eneo la matangi ya mafuta ya *Oilcom,* Kurasini kuhusu uchafuzi uliosababishwa na umwagaji wa mafuta machafu katika mazingira ya bahari eneo la *Kurasini Oil Jetty* ambapo Oilcom walilipa faini ya shilingi 30,000,000 na kusafisha eneo lililochafuliwa; na katika eneo la Wazo kuhusu uchimbaji wa mchanga ambapo malori manne ya mchanga yalikamatwa na kutozwa faini ya shilingi kati ya shilingi laki tano na milioni moja na kuagizwa kufukia mashimo yaliyosababishwa na uchimbaji mchanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi pia umefanyika katika eneo la Msasani kufuatia uchafuzi wa mazingira kutoka *Msasani Apartments*. Mwekezaji ameagizwa kusitisha utiririshaji wa maji taka kwa kujenga mfumo wa kuondoa maji hayo, kazi ambayo ameikamilisha. Vile vile, Baraza lilikagua na kutoa vibali 15 vya kukusanya mafuta machafu na vibali vinane vya kukusanya chuma chakavu kwa makampuni mbalimbali. Baraza pia lilifanya ukaguzi wa kushtukiza katika eneo la Tegeta na kukamata shehena ya vipodozi chakavu kutoka katika kiwanda cha *Chemi-Cotex Industries Ltd*. cha Mbezi Beach, Kinondoni kinyume cha sheria. Kiwanda hiki kilitozwa faini ya shilingi 10,000,000 iliyolipwa pamoja na kupewa onyo na shehena hiyo kuteketezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchafuzi wa mazingira unaofanywa na viwanda vya ngozi; Baraza limefuatilia kwa karibu viwanda hivi ambavyo vimelalamikiwa na wananchi kutokana na harufu mbaya ya uozo na kemikali zinazotumika katika kusindika ngozi. Viwanda vilivyokaguliwa ni vile vya Kibaha (Pwani), Kihonda (Morogoro) na Himo (Kilimanjaro). Viwanda hivi bado vinatumia teknolojia ya zamani, hivyo kutoweza kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Zipo teknolojia mpya za kutibu maji taka kwenye viwanda hivi ambazo kwa kiasi kikubwa zinapunguza harufu mbaya itokanayo na usindikaji wa ngozi. Baraza limeagiza viwanda hivi kuboresha teknolojia nafuu ili kupunguza harufu na pia kudhibiti taka ngumu wanazozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Baraza lilitoa mafunzo kuhusu Sheria ya Mazingira kwa Wataalamu wa Mazingira wa Mikoa na Maafisa Mazingira wa Wilaya 24 kutoka Halmashari za Wilaya za Kanda ya Kaskazini, iliyojumuisha Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Baraza pia liliendelea kukuza uwezo wa Serikali za Mitaa katika kusimamia ukusanyaji na utupaji wa taka za aina zote kwa kuendesha mafunzo kwa Maafisa Mazingira kutoka Serikali za Mitaa katika Kanda ya Mashariki (Pwani, Dar es Salaam na Morogoro) ili kukuza uelewa wa Sheria ya Mazingira na kuhimiza utekelezaji wake kwa vitendo. Baraza pia liliendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu utupaji au kuharibu taka hatarishi zenye kemikali kwa makampuni mbalimbali zikiwemo dawa za binadamu zilizoisha muda wake wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza kupitia Ofisi zake za Kanda ambazo ni Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda Kaskazini (Arusha) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), ziliendelea na zoezi la ukaguzi ili kutambua shughuli ambazo zitahusika katika tozo za hifadhi ya mazingira na kuanza zoezi la kukusanya tozo hizo kwa mujibu wa Kanuni za Tozo za Mwaka wa 2008. Jumla ya viwanda na migodi ipatayo 120 ilikaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/12, Baraza liliendelea kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Serikali uliozishirikisha sekta zote muhimu kuhakikisha kuwa uchafuzi uliotokea katika Mgodi wa North Mara unadhibitiwa na hautokei tena katika mgodi huo na katika migodi mingine nchini. Aidha, tayari mtambo wa kusafisha maji umejengwa na

mfumo wa kusafisha maji ya Gokona unafanya kazi. Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Ziwa na Ofisi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria, walichukua vipimo vya maji vya kila siku kwa mwezi mzima kutoka katika mtambo huo tangu tarehe 21 Februari, 2012. Sampuli zilizochukuliwa zinafanyiwa uchunguzi katika maabara na matokeo yanatarajiwa kupatikana mwezi Julai, 2012. Mara baada ya vipimo hivyo kukamilika, itatoa mwelekeo kuhusu viwango vya maji kwa matumizi ya binadamu na mtambo huo utazinduliwa mwishoni mwa Julai, 2012 na kuanza kusambaza maji kwa baadhi ya vijiji vinavyozunguka Mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya kiafya na vifo vinavyodaiwa kutokea North Mara kutokana na uharibifu wa mazingira, Serikali iliahidi kutoa taarifa. Natumia fursa hii kutoa taarifa kuwa uchunguzi uliofanywa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umebaini kuwa, sampuli za maji zilizochukuliwa kutoka katika visima mbalimbali katika maeneo yanayozunguka mgodi na yale yaliyo nje ya Mgodi wa Nyamongo zinaonesha kuwa zote zilikuwa na viwango vya juu vya Madini Tembo *(Heavy Metals).* Pia, uchunguzi wa sampuli za damu zilizochukuliwa kutoka kwa baadhi ya wakazi wa vijiji vinavyozunguka mgodi pamoja na mifugo ulionesha kuwepo kwa Madini Tembo hayo kwenye damu kwa viwango vya juu. Hali hii inaweza kuwa ilisababishwa na matumizi ya muda mrefu wa maji yenye Madini Tembo hayo. Mapitio ya machapisho ya tafiti mbalimbali zilizofanyika kwingineko duniani zinaonesha kuwa kuwepo kwa viwango vya juu vya Madini Tembo katika miili ya

binadamu kunaweza kusababisha athari za kiafya kama zile zilizojitokeza kwa baadhi ya wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka Mgodi wa North Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti huo, Serikali inapenda kutamka rasmi kuwa, hakuna ushahidi wowote wa kisayansi unaonesha mahusiano kati ya athari za kiafya zilizojitokeza kwa baadhi ya wananchi wa eneo la Nyamongo na tukio la kumwagika kwa tindikali kutoka kwenye mabwawa ya kuhifadhia tindikali hiyo katika mgodi wa dhahabu wa North Mara. Athari zilizojitokeza zinatokana na matumizi ya maji yenye Madini Tembo kwa muda mrefu, ambayo yalitokana na kuwepo kwa madini tembo hayo katika miamba ya asili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kugundulika kwa kiwango hicho cha Madini Tembo katika vyanzo vingi vya maji katika eneo la Nyamongo, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na uongozi wa mgodi walifanya jitihada za haraka kupata vyanzo vya maji mbadala kwa matumizi ya wananchi hao huku ufumbuzi wa kudumu ukifanyiwa kazi. Kwa hiyo, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na mgodi wamechimba visima vingine ambavyo maji yake yanaelekea kuwa na kiwango kidogo cha madini tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Mgodi umeanzisha mpango wa kuchimba visima virefu na tayari umefanya kazi zifuatazo: Kupeleka maji safi kwa Wakazi wa Nyamongo kwa magari kila siku kwa

matumizi yao kama mpango wa muda mfupi; mpango wa muda mrefu ni kuwapatia maji ya mtandao wa mabomba kutoka vyanzo vingine kama Mto Mara; Jumla ya visima 16 vimechimbwa katika vijiji vinavyozunguka Mgodi ambavyo ni Kewanja vitatu, Nyamwaga viwili, Nyakunguru viwili, Genkuru viwili, Kerende viwili, Matongo viwili na Nyangoto vitatu (kati yake viwili havina maji) na 14 kati ya hivyo vimetambuliwa kuwa na maji; Visima viwili katika Kijiji cha Matongo zimefungwa pampu na katika Vijiji vya Kewanja, Nyamwaga na Kerende kumefungwa pampu moja moja. Katika Kijiji cha Nyangoto mgodi umeanza kuchimba visima vifupi na viwili vimechimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Baraza litaendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa kufanya kaguzi na kufuatilia viwanda, migodi na miradi ili kuangalia kama utekelezaji wake unakidhi viwango vya mazingira na kutoa ushauri wa marekebisho. Pamoja na kazi zilizotajwa hapo juu, Baraza litaendelea kutekeleza kazi zifuatazo: Kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, Kitengo cha Polisi wa Mazingira kimeanzishwa ndani ya Jeshi la Polisi ambacho kitafanya kazi na Baraza; Kukubaliana na taasisi nyingine za Serikali jinsi ya kukagua na kusimamia Sheria ya Mazingira katika masuala yenye kuhitaji usimamizi wa pamoja na kuendeleza shughuli za Mtandao wa Afrika Mashariki wa uzingatiaji na utekelezaji wa sheria za Mazingira (*East African Networking on environmental Compliance and enforcement – EANECE, Tanzania*

*Chapter);* Kukuza weledi kwa maafisa mazingira wateule na wataalamu wa mazingira kutoka Kanda ya Kati (Mikoa ya Morogoro, Dodoma na Manyara) kuhusu wajibu na majukumu yao katika kutekeleza Sheria ya Mazingira, Sura ya 191; na kuainisha viwanda na shughuli zinazochafua mazingira katika mikoa sita (Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Mbeya, Arusha na Kagera) ili kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la Kiwanda cha *Kilombero Plantation Limited - KPL* kilichopo Mngeta-Morogoro kukausha mashamba ya wanakijiji kwa kunyunyiza dawa za kuua magugu. Baraza lilifuatilia suala hilo ili kubaini ukweli wa malalamiko ya wananchi katika Wilaya ya Kilombero. Kiwanda cha *KPL* kilianzishwa mwaka 2007 ili kuendeleza *Mngeta Farm* lililopo Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro. Baraza lilibaini kuwa mnamo tarehe 27 Desemba, 2010, wakulima wapatao 630 wa Kijiji cha Mkangawalo na Mngeta walitoa malalamiko yao kwenye Kampuni ya *Kilombero Plantation Limited (KPL)* kuhusu mashamba yao kuharibiwa na kemikali zinazotokana na kiwanda hicho kupulizia viuatilifu angani. Baada ya malalamiko hayo, ukaguzi ulifanyika kwa kuwashirikisha baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya *KPL* na Viongozi wa Vijiji na kubaini tatizo kuwa wananchi zaidi ya 500 walikuwa wameathirika kutokana na zoezi la upuliziaji wa viuatilifu angani. Kwa mantiki hiyo, *KPL* waliamua kuwalipa kama kifuta machozi *(gesture of goodwill)* wakazi wa vijiji viwili vya Mngeta na Mkangawalo kiasi cha takriban shilingi 50,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malipo hayo, Kampuni ilinunua eneo la ekari 1,900 lenye thamani ya shilingi 56,700,000 na kuligawa kwa familia 630 zilizohamishwa kutoka katika eneo la Kampuni na kila familia ilipewa ekari tatu za shamba, kulimiwa na kupewa mbegu za mpunga. Aidha, familia 80 zilizokuwa na nyumba katika eneo la kampuni, zilijengewa nyumba zenye thamani kati ya shilingi milioni tatu hadi 5,000,000 na kuchimbiwa visima vitatu vifupi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wananchi wa Kitongoji cha Mbasa kuwa na makazi ya kudumu katika eneo la kampuni lipatalo ekari 385, Kampuni iliamua kuwaachia eneo hilo na kusaidia kujenga madarasa mawili katika shule yao ya msingi, nyumba mbili za walimu na nyumba 20 za wananchi zilizokuwa katika hali mbaya. Kwa ujumla mgogoro huu umeisha na wananchi wote waliokuwa wamevamia eneo la kampuni wameondoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limeendelea kuratibu Programu ya *African Stockpiles (ASP)* ambayo inalenga kukusanya, kusafirisha, kuondosha na kuteketeza viuatilifu chakavu *(obsolete pesticides)* vilivyolundikana nchini; ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya udhibiti ili kuhakikisha kuwa mlundikano wa viuatilifu hautokei tena hapa nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, nililijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Baraza lilikamilisha zoezi la kubaini viuatilifu chakavu nchini kote na tani 700 zilibainishwa na kukusanywa katika maeneo 135 nchini kote. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12 Baraza lilikamilisha zoezi la

kukusanya shehena ya viuatilifu hivyo chakavu na kuviweka katika vituo vya kati sita vilivyopo hapa nchini, ambavyo vipo Arusha, Morogoro, Nzega, Mbeya, Kibiti na Mahonda (Zanzibar). Vituo hivi vya kati vimetumiwa kuhifadhia shehena ya viuatilifu chakavu vikisubiri kusafirishwa kwa ajili ya kuteketezwa nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza kwa kupitia Mradi wa ASP limempata Mkandarasi wa Kimataifa mwenye ujuzi wa kushughulikia mrundikano wa viuatilifu chakavu kwa njia ya zabuni ya kimataifa. Mkandarasi *M/S Veolia ES Ltd. kutoka* Uingereza aliibuka mshindi wa zabuni ya kimataifa ambapo alisaini mkataba wa kukusanya, kusafirisha na kuteketeza viuatilifu hivyo chakavu pamoja na tani nyingine 300 za udongo ulioathirika. Mkandarasi huyo ameonesha kwamba vifaa vya kufanikisha zoezi hilo ikiwa ni pamoja na mapipa, mifuko maalumu na vifaa vya kinga vimepakiwa kwenye meli na viko njiani kuletwa hapa nchini. Aidha, zoezi la kupakia na kusafirisha viuatilifu hivyo chakavu hadi kwenye mitambo mahususi huko Uingereza litafanyika kuanzia mwezi huu wa Julai, ambapo viuatilifu hivyo vitakuwa vimeondolewa hapa nchini ifikapo Desemba, 2012 kulingana na ratiba iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kupitia upya sheria ya kusimamia viuatilifu inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika limekamilika. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, linaendelea na mkakati wa kushughulikia vifungashio au mikebe iliyokuwa inahifadhia viuatilifu

chakavu. Aidha, tathmini ya athari ya mradi kwa mazingira ilifanyika mwaka 2010/11 na inatumika kama dira katika kusimamia zoezi la uondoshaji viuatilifu chakavu nchini. Aidha, Baraza limeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano wa *ASP Communication Strategy for Tanzania (ASP)* unaosaidia katika kuhakikisha kwamba wadau wanapata ujumbe kuhusu madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya viuatilifu na kuelimisha jamii itoe ushirikiano ili kuhakikisha kuwa mlundikano wa viuatilifu chakavu haujirudii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, jumla ya Miradi ya Maendeleo 412 ya wawekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Kati ya Miradi hiyo, Miradi 208 imefanyiwa TAM na ripoti zake kufanyiwa mapitio kwa ajili ya kupata Hati za TAM *(EIA Certificates).* Kati ya Miradi hii, Miradi 176 imepata Hati za TAM, baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni za TAM. Kati ya miradi iliyopata Hati ya TAM Miradi 34 ilikuwa ya mawasiliano, 31 ya ujenzi, 13 vivutio vya utalii, 11 miundombinu, 14 ya uchimbaji madini, 35 ni ya nishati, 31 ni ya viwanda, mmoja wa maji, miwili ya afya na minne ni ya kilimo na misitu. Aidha, Jumla ya miradi 236 inaendelea kufanyiwa kazi na wawekezaji na haijarejeshwa kwenye Baraza ili kuendeleza mchakato wa kupatiwa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio kwani kumekuwepo na ongezeko la miradi iliyofanyiwa mapitio na kupatiwa hati kutoka miradi 163 mwaka 2010/2011 hadi miradi miradi 176 mwaka 2011/12, sawa

na ongezeko la asilimia 4.1. Ongezeko hili linaonesha kuwa wawekezaji wengi wamepata mwamko wa kufuata na kutimiza matakwa ya Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, ambayo pamoja na mambo mengine inawataka wawekezaji kutimiza masharti ya TAM kabla na baada ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12 Baraza liliendesha mafunzo yenye lengo la kukuza weledi wa wadau kuhusu umuhimu na hatua za kuzingatia katika masuala ya TAM. Mafunzo ya TAM yalitolewa kwa Wahandisi na Mafundi Mchundo 40 wa barabara kwa miradi ya ujenzi wa barabara ambayo yalifanyika Morogoro. Asasi zisizo za kiserikali *(NGOs)* 16, walipata mafunzo ya Ukaguzi na Ufuatiliaji Mazingira *(Environmental Auditing and Monitoring).* Mafunzo haya yalifanyika Dar es Salaam na Kibaha.

Jumla ya Maafisa 30 wakiwemo Maafisa Mazingira na Timu ya Wawezeshaji wa Wilaya *(District Facilitation Team)* walipewa mafunzo huko Tabora yaliyohusu Uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Aidha, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira walifanyiwa semina inayohusu mradi wa uchimbaji na usafishaji wa madini ya uranium Mjini Dar es Salaam. Pia Wafanyakazi 15 wa Baraza walipewa mafunzo kuhusu uchimbaji wa mafuta na gesi kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Baraza lilipokea jumla ya maombi 135 kwa ajili ya usajili wa Wataalamu Waelekezi wa TAM *(EIA*

*Experts/Consultants)* na Ukaguzi wa Mazingira *(Environmental Auditors).* Maombi haya yalifanyiwa uchambuzi na tathmini ili kukamilisha usajili rasmi wa wataalamu hawa. Wataalamu 86 wa TAM na 39 wa Ukaguzi wa Mazingira wamesajiliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 1 Aprili, 2012. Vile vile, maombi ya makampuni 26 yanayotoa Utaalamu Elekezi wa TAM na Ukaguzi wa Mazingira yalipokelewa kwa ajili ya usajili. Kati ya hayo, makampuni 15 yalisajiliwa kwa ajili ya kufanya TAM na 11 yalisajiliwa kwa ajili ya kufanya Ukaguzi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuanzisha miradi ya kuchimba madini ya urani hapa nchini; mpaka sasa maeneo yaliyogunduliwa madini ya urani yapo Mto Mkuju Namtumbo (Ruvuma), Bahi (Dodoma) na Manyoni (Singida) na kwa ujumla inakadiriwa kuwa kuna kiasi cha kilo 24,700,000 za madini hayo. Makampuni yaliyojitokeza kuchimba ni *MANTRA* (Mkuju) na *URANEX* (Bahi na Manyoni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza kwa kushirikiana na Tume ya Nguvu za Atomiki *(Tanzania Atomic Energy Commission – TAEC),* linahakikisha kuwa taratibu zote za sheria ikiwa ni pamoja na zile za Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, zinafuatwa na kwamba Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) zinafanyika ili kuhakikisha kuwa wakati wa utekelezaji wa Miradi hii, mazingira na binadamu hawapati athari. Katika mchakato wa TAM, kazi muhimu ya Baraza ni kusimamia hatua zote pamoja na kufanya mapitio na baada ya kuridhika kuwa ripoti za tathmini zimejitosheleza na kukamilika na kumshauri Waziri mwenye dhamana ya mazingira

kuhusu Utoaji wa Hati au vinginevyo na baadaye kufanya uperembaji na ukaguzi wa mazingira wakati wa utekelezaji wa Mradi. *MANTRA* walianza utaratibu wa kupata Hati ya Mazingira mwaka 2009. Katika kufanya mapitio ya TAM ya Mradi wa *MANTRA,* Baraza lilishirikisha Wataalam wa TAEC katika hatua zote, ikiwa ni pamoja na kutembelea na kufanya uhakiki wa eneo la mradi tarajiwa *(site verification visit)* na kushiriki kwenye Mkutano wa Kamati ya Kitaalam ya Mapitio *(Technical Advisory Committee).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchakato huu wa TAM, Baraza lilibaini upungufu unaohitaji uamuzi wa kisera na hivyo kutaka mwongozo wa juu wa Serikali kuhusu upungufu huo, ambao ulijitokeza katika maeneo makubwa yafuatayo:-

(i) Kutokuwapo kwa Sheria na kanuni za kusimamia uchimbaji wa madini yatoayo mionzi *(radioactive minerals)* hususan urani;

(ii) Kutokuwepo kwa hati fungani ya utekelezaji dhidi ya mazingira *(environmental performance bond);*

(iii) Kutokuwepo kwa mwongozo kuhusu uchimbaji wa madini katika Pori la Akiba la Selous ambalo limetambuliwa kuwa sehemu ya urithi wa Dunia; na

(iv) Kutokana na Mradi huu kuwa mpya na wa aina yake nchini, ilibainika kuwa hakuna uwezo *(capacity)* wa kutosha wa kusimamia na kudhibiti utekelezaji miradi ya aina hii.

Ili kutatua upungufu uliojitokeza Serikali imefanya yafuatayo:-

Imetunga sheria na kanuni zifuatazo: Sheria ya Madini ya 2010 (*The Mining Act of 2010);* Kanuni za Madini Yatoayo Mionzi za 2010 *(The Mining (Radioactive Minerals) Regulations, 2010);* Kanuni za Nguvu ya Atomiki kuhusu uchimbaji wa madini yatoayo mionzi za 2011 *(The Atomic Energy (Radiation Safety in the Mining & Process of Radioactive Ores) Regulations, 2011);* Kanuni za Nguvu ya Atomiki kuhusu usafirishaji wa madini yatoayo mionzi za 2011 *(The Atomic Energy (Transporting and Packaging of Radioactive Materials) Regulations, 2011);* na Kanuni za Nguvu ya Atomiki kuhusu tozo za 2011 *(The Atomic Energy (Fees and Charges) Regulations 2011).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2012/13, Serikali itatayarisha kanuni za hati fungani kwa miradi inayosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira *(Environmental Performance Bond Regulations).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kupata ruhusa ya kuchimba urani katika Pori la Selous uko ukingoni baada ya kuwasiliana na *UNESCO* na *WHC* karibu kwa miaka miwili sasa. Aidha, uamuzi wa kutenga eneo linalohitajika na mradi kutoka katika eneo la urithi wa dunia ili kuruhusu uchimbaji ufanyike utafikiwa katika Kikao cha *WHC* kinachofanyika St.

Petersburg, Urusi, kuanzia tarehe 24 Juni hadi 6 Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa Sheria na Kanuni za Kusimamia Madini Yatoayo Mionzi, tunayo Kamisheni ya Tanzania ya Nguvu ya Atomiki *(Tanzania Atomic Energy Commission au - TAEC),* ambayo tunaamini wanao uwezo wa kitaalam kwa masuala yanayohusu urani pamoja na kujenga uwezo wa wadau wengine. Baraza litatumia *TAEC* kujenga uwezo wake na litaendelea kujenga uwezo kwa kutumia nafasi nyingine zitakazopatikana ikiwa ni pamoja na kuajiri wataalam katika fani husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Baraza litaendelea kufanya mapitio ya Taarifa za TAM, kusajili Wataalam wa TAM na Ukaguzi wa Mazingira na kukagua Miradi ya Maendeleo ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye Hati za TAM na Mipango ya Hifadhi ya Mazingira *(Environmental Management Plans).* Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wadau kuhusu masuala ya TAM ili kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo zinakuwa endelevu. Aidha, wataalam 20 wa Baraza watahudhuria mafunzo ya muda mfupi kuhusu masuala ya nguvu za nuklia/atomiki na mionzi yatakayofanyika mwezi huu wa Julai 2012 huko Arusha kwenye Makao Makuu ya *TAEC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya mazingira kwa umma ni muhimu sana ili jamii iweze kushiriki katika kufanya maamuzi sahihi yanayohusu matumizi endelevu ya maliasili na mazingira kwa ujumla. Katika

Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza lilitoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa kutumia vipeperushi, vijarida, mabango, maonesho, luninga, redio na magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza lilishiriki katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Nane Nane mwaka 2011 ili kukuza weledi kuhusu mahusiano kati ya kilimo na hifadhi ya mazingira yaliyofanyika Mkoani Dodoma, Mbeya na Mwanza. Pia, Baraza lilishiriki kwa siku kumi katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonesho ya Mwalimu J.K. Nyerere, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza lilitembelea Miradi ya Kuhifadhi Mazingira iliyokuwa inafadhiliwa na Serikali ya Uholanzi katika Wilaya za Tarime, Kilombero, Sumbawanga Kibaha na Siha, kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Miradi hiyo. Baraza liliandaa semina tatu zilizoshirikisha wadau mbalimbali kama vile Idara ya Mazingira, Hali ya Hewa, Wizara za Kilimo, Maji, Maliasili na Taasisi zisizo za Kiserikali, kwa ajili ya kutayarisha nyenzo zitakazotumika kuelimisha umma kuhusu uhimili wa mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza liliendesha semina ambazo pia zilihusisha mada zilizolenga kuwaelimisha Maafisa Mazingira katika Serikali za Mitaa katika Kanda za Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Tanga), Nyanda za juu

Kusini (Rukwa, Mbeya na Iringa) kuhusu ukusanyaji wa taarifa za mazingira kwa kutumia mfumo wa kompyuta kulingana na majukumu yao. Vile vile, katika kipindi cha mwezi Mei, 2012, Baraza liliendesha semina ya kukuza weledi miongoni mwa Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri za Wilaya za Karatu, Siha, Magu na Maswa, iliyohusu kujumuisha utunzaji wa mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya maendeleo. Aidha, Baraza liliendelea kukamilisha na kuboresha mifumo ya mawasiliano kati yake na wadau zikiwemo Tovuti ya Baraza *(www.nemc.or.tz).* Tovuti ya Mazingira ya Tanzania *(Tanzania Environment Web Portal - www.tanzaniaenvironment.go.tz)* na kuhamasisha matumizi ya mitandao hii miongoni mwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote za kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa umma; vitendo vya uchafuzi wa mazingira kama vile utupaji taka ovyo, utiririshaji wa maji machafu, matumizi na utupaji ovyo wa mifuko ya plastiki, ukataji miti na ujenzi holela kandokando ya mito na katika fukwe za bahari bado ni tatizo kwa baadhi ya maeneo. Napenda kutoa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika shughuli za hifadhi ya mazingira kwani suala hili ni letu sote na matokeo ya uharibifu wa mazingira hayana mipaka na yataathiri kizazi hiki na cha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Baraza litaendelea kuboresha mifumo ya mawasiliano kati yake na wadau wote wa mazingira, ikiwa ni pamoja na Tovuti ya Baraza, Tovuti ya Mazingira ya Tanzania na kuhamasisha matumizi ya

mitandao hii. Pia, Baraza litaongeza kasi ya kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu ya wadau katika hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza liliendesha warsha ya kujenga uwezo kwa Maafisa Mazingira wa Wilaya, Manispaa, Miji na Mikoa katika Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara na Singida) kuhusu vipaumbele vya utafiti katika eneo pana la mazingira. Warsha hii ililenga kuwapa uelewa kuhusu Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti katika Mazingira *(National Environment Research Agenda – NERA)* na kupeana mbinu za kutambua maeneo yanayostahili kufanyiwa utafiti katika maeneo yao ya kazi kwa kutumia *NERA* kama mwongozo. Warsha hii ilifanyika katika Mji wa Dodoma tarehe 18 hadi 20 Januari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza liliendesha semina mbili za siku tatu kila moja kwa Maafisa Mazingira wa Wilaya, Manispaa, Miji na Mikoa katika Kanda za Kusini (Ruvuma, Mtwara na Lindi) na Magharibi (Shinyanga, Tabora na Kigoma) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukusanya taarifa za hali ya milima na mifumo ikolojia yake na kupanua uelewa wao wa Sheria ya Mazingira, Sura Na.191, hususan katika masuala ya utafiti na mipango ya mazingira. Aidha, zoezi hili lilikuwa na umuhimu wa kipekee kwa sababu washiriki wengi ni wateuliwa wapya wa kada ya Afisa Mazingira. Semina hizo zilifanyika katika Miji ya Kahama na Songea mwezi Februari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza liliandaa Kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Utafiti wa Mazingira *(Environmental Research Advisory Committee – ERAC)* na kupitia Rasimu ya mwisho ya Mwongozo wa kutoa fedha za Utafiti wa Mazingira *(Environmental Research Guidelines & Grant Forms).* Mwongozo huu utatumiwa na Baraza kutathmini mapendekezo ya miradi ya utafiti katika utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utafiti *(NERA).* Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa *(UNDP),* limeanza kutekeleza baadhi ya majukumu yake katika eneo la Mabadiliko ya Tabianchi. Maeneo yanayopewa kipaumbele ni suala zima la kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu dhana hiyo; kutengeneza makala fupi za kisera kuhusu mabadiliko ya Tabia Nchi zitakazolenga watoa maamuzi katika ngazi mbalimbali; kuongeza uwezo wa Halmashauri kuelewa masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na kuhusu mbinu za kujikimu na kuonesha mahusiano kati ya tabianchi na maendeleo kwa njia ya ramani ili kuongeza uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza liliendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa kupitia Miradi mitano ya *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP),* unaotekelezwa katika wilaya zote za Pwani; *Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP-PWANI),* unaotekelezwa katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo kwa upande wa Tanzania Bara na Wilaya za Kusini, Magharibi, Mjini na Kati kwa upande wa Tanzania Visiwani (Unguja). Pia, Baraza linatekeleza

Mradi wa *Western Indian Ocean Marine Highway (WIOMHP),* unaoshughulikia udhibiti wa uchafuzi utokanao na vyombo vya usafirishaji Baharini ikiwemo udhibiti wa umwagikaji wa mafuta utokanao na vyombo hivyo. Katika Mradi huu, Shirika la nchi zilizo Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi limefadhili utengenezaji wa ramani za rasilimali bahari hasa kwa sehemu tekechu *(fragile)* na pia utengenezaji wa mpango wa dharura wa kudhibiti umwagikaji wa mafuta na dutu *(substances)* hatarishi baharini. Vile vile chini ya kikosi kazi kiitwacho *Tanzania Coral Reef Taskforce (TzCRTF),* Baraza limeweza kufuatilia na kusimamia utunzaji wa rasilimali za bahari yakiwemo matumbawe ambayo huharibiwa na uvuvi wa kutumia baruti. Kwa kushirikiana na Sekta nyingine kama vile Idara ya Uvuvi, Baraza linaendelea kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Baraza lilifanya uperembaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani katika Halmashauri zote 14 unakotekelezwa Mradi huu. Ili kupima mafanikio ya Mradi wa *MACEMP;* Baraza lilisambaza kwa wadau Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira ya Pwani *(State of the Coast Report).* Pia katika kipindi hicho, Baraza liliendelea kushiriki katika Programu ya *ReCoMaP* chini ya Shirika la Nchi zilizo Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Commission – IOC),* iliyofadhili jumla ya miradi midogo midogo 16 kwenye asasi za kijamii na zisizo za kiserikali. Maeneo ambayo yalipata Miradi ya *ReCoMaP* ni Kilimo cha Lulu inayotokana na chaza na unenepeshaji wa kaa *(Pearl Oyster Farming and Crab*

*Fattening)* wa Rufiji, Mafia na *Kilwa Complex - RUMAKI),* chini ya *WWF;* Usafi wa Mazingira Lindi Mjini kupitia Asasi lsiyo ya Kiserikali iitwayo *COBIHESA*; Ujenzi wa kingo za bahari huko Kigombe; mradi wa kuhifadhi kasa wa baharini huko Tanga na Temeke kupitia Sea Sence. Mradi mwingine ni kilimo cha mwani kinachofanyika katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba kupitia *WIOMSA*; na Urejeshwaji wa Mikoko Mkoani Tanga kupitia Asasi za *Envirocare* na *African Health Environment and Development (AHED) Trust.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/12, Baraza liliendelea kuratibu Mradi wa Hifadhi na Usimamizi Shirikishi wa Mazingira ya Pwani *(Tanzania Coastal Management Partneship - TCMP-PWANI)*; ni mradi wa miaka minne (Januari 2010 hadi Desemba 2013). Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa – *USAID,* kwa kiasi cha Dola za Marekani 3,800,000, unatekelezwa chini ya usimamizi wa Baraza na unaendeleza kazi zilizoanzishwa na Mradi wa *TCMP-SUCCESS* uliomalizika 2009. Kwa mwaka 2011/12 mradi uliendelea kutekeleza shughuli zake kama ilivyopangwa. Baadhi ya kazi zilizofanywa na mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na Kuziwezesha Wilaya za Pangani na Bagamoyo kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani na Bahari kwa kutekeleza Mipango Kazi iliyoainishwa na Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi ulijenga uwezo kwa Wilaya hizo mbili za Bara, nne za Zanzibar (Kusini, Kati, Magharibi na Mjini) na vijiji 27, vitongoji tisa na

Shehia 12 kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali watu 362 ambapo 65% walikuwa wanawake; Mradi umefadhili miradi midogo midogo ya kijamii katika Wilaya zilizotajwa kwa lengo la kuongeza kipato miongoni mwa jamii. Mradi umeweza kutoa mtaji pamoja na elimu kuhusu matumizi na utengenezaji wa majiko banifu (Pangani na Bagamoyo), uanzishwaji na uendeshwaji wa *SACCOS* (Bara na Unguja), kuanzisha utalii ikolojia (Bagamoyo), kuanzisha maeneo tengefu ya uvuvi *(No – Take Zones)* manne katika Shehia za Fumba Bondeni, Fumba Cheleni, Bweleo na Nyamanzi (Wilaya ya Magharibi - Unguja), uboreshaji wa kilimo cha mwani (Mlingotini – Bagamoyo), ufugaji wa nyuki na samaki ulio endelevu katika Wilaya za Bagamoyo na Pangani. Hadi sasa vipo vikundi 22 vya ujasiliamali (katika maeneo ya ufugaji nyuki, kilimo cha mwani, mapambo na lulu, uokaji mikate na utalii ikolojia) vyenye jumla ya wanachama 437.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha 2012/13 Mradi wa TCMP-Pwani utaendelea kutekeleza shughuli kubwa tano zifuatazo:-

Kusaidia uhifadhi wa mazingira ya Pwani na Bahari na ikologia yake katika eneo pana *(Land – Seascape)* la Bagamoyo na Pangani ikiwemo Hifadhi ya Saadani na eneo la Ghuba ya Menai (Zanzibar); Kuendeleza juhudi za hifadhi ya maeneo yaliyotengwa ya Matumbawe (Bagamoyo) na yale ya Chaza na uzalishaji wa lulu (Ghuba ya Menai) ili kuinua hali ya uchumi kwa wanavijiji wanaozunguuka maeneo hayo; Kukuza na kuendeleza utalii wa Pomboo *(Dolphin Tourism)* katika maeneo ya Ghuba ya Menai na Utalii

ikolojia/utamaduni katika maeneo ya Bagamoyo na Pangani; Kuzihakiki njia za kupitia wanyamapori zitakazobainishwa na setilaiti katika Hifadhi ya Saadani na kupendekeza usimamizi wa maeneo hayo ili kupunguza changamoto zilizopo kati ya wanyama na binadamu katika maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Saadani na eneo la wanyamapori la Wami – Mbiki; na Kushirikiana na wadau mbalimbali wa nje na ndani ya nchi kubuni mradi mwingine utakaoendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Mradi huu utakapomaliza muda wake na kuangalia uwezekano wa kupanua maeneo ya Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti wa chura na mazingira ya Kihansi, Kamati ya Kitaifa ya Kuangalia na Kusimamia Zoezi la Urejeshwaji wa Vyura *(Re-introduction Task Force),* ambayo inahusisha Wajumbe kutoka Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali, Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti na ambayo iliundwa mwezi Julai, 2009 inaendelea na kazi zake. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Wataalamu wa Vyuo Vikuu vya SUA na UDSM lilifanya utafiti na ufuatiliaji wa mifumo ikolojia ya Bonde la Kihansi kwa lengo la kubaini mazingira stahili kwa ajili ya kurejesha vyura katika mazingira yao ya asili. Hadi Juni 15, 2012 jumla ya vyura waliorejeshwa nchini (Chuo Kikuu Dar es Salaam na Kihansi) ni 1,646 na waliobaki Marekani *(Bronx na Toledo Zoos)* ni vyura 6,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza kwa kupitia Mradi huu lilijenga uwezo wa Wilaya zinazozunguka Bonde la Mto Kihansi, pamoja na Watendaji wa Wilaya, Kamati za Vijiji na Viongozi wa Kidini katika masuala ya hifadhi

ya mazingira na mbinu za kuboresha maisha ya jamii. Baraza pia lilikabidhi shughuli za uhifadhi kwa *TANESCO* ambayo ni mmiliki wa mradi akisaidiwa kiufundi na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI).* Hata hivyo, kwa makubaliano maalum, Baraza linaendelea kuisaidia *TANESCO* kuratibu utekelezaji wa shughuli za Mradi huo, hususan katika kipindi hiki cha mpito ikiwa ni pamoja na kusimamia mipango ya kurudisha baadhi ya vyura wanaohifadhiwa nchini Marekani. Shughuli za muda mrefu za hifadhi ya Bonde la Kihansi na bioanuai yake zinatarajiwa kuendelezwa kupitia fedha zitakazopatikana chini ya Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(G.E.F).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Baraza litaendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira *(National Environmental Reasearch Agenda - NERA)* na kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya, ili waweze kutekeleza *NERA* katika maeneo yao; litaendelea kufanya tafiti ili kupata taarifa zaidi kuhusu hali na ikolojia ya milima nchini; litaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi na mikakati ya kuhifadhi mazingira na litabuni miradi mingine ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Baraza liliendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa kufanya maandalizi ya awali ya kujenga Jengo la Makao Makuu ya kudumu. Aidha, Baraza lilikamilisha ukarabati wa jengo moja ili kuongeza ofisi na ukumbi wa mikutano katika kiwanja chake kilichopo Regent

Estate, Mikocheni. Tayari wafanyakazi wote wamehamia katika ofisi hizo na ukumbi wa mikutano na umeanza kutumika. Hata hivyo, kazi ya ujenzi wa ukuta uliobomoka kuzunguka eneo la kiwanja na michoro ya ujenzi wa jengo la kudumu la Baraza haikuwezekana kuanza kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza ufanisi wa kazi, Watumishi wa Baraza wamepewa fursa ya kujiendeleza kitaaluma. Aidha, Watumishi 14 wa Baraza wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na Watumishi kumi walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, Baraza limepewa nafasi 31 za ajira, nafasi 30 kwa ajili ya Maafisa Mazingira na moja ya Mkurugenzi wa Utawala na Fedha, nafasi hizi zimetangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa 2011/12, Baraza lilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ufinyu wa bajeti na uelewa mdogo wa jamii wa masuala ya mazingira. Hivyo, Baraza litaendelea kuongeza kasi ya kutekeleza mpango wake wa kupata mapato kutoka vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na tozo na kuibua miradi mipya inayoweza kupata wafadhili. Kuhusu uelewa mdogo wa jamii wa masuala mbalimbali ya Mazingira, Baraza litaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia Redio, Televisheni, Magazeti na Machapisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuendelea kutekeleza majukumu yake kisheria kama ilivyoelezwa hapo juu, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13 Baraza

limepanga pia kutekeleza yafuatayo: Litaongeza kasi ya utekelezaji wa Kanuni za Tozo (Fees and Charges Regulations 2008); kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuwajengea uwezo ili kuongeza motisha na ufanisi katika utendaji kazi; kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi zake na uzio na kuandaa michoro ya jengo la kudumu; kushirikiana na Jeshi la Polisi kuanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira; na kutathmini utekelezaji wa Mpango Kazi wa 2012/13 na Mpango Mkakati wake (2010 – 2014) ili kubaini changamoto zinazojitokeza na kuchukua hatua stahiki za maboresho kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata misingi ya Utawala Bora. Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma zilizingatiwa, kusimamiwa na kutekelezwa kikamilifu. Aidha, Ofisi iliendelea kulinda na kuwapatia watumishi wake haki na maslahi yao kwa kuzingatia wajibu wa kila mtumishi na majukumu ya Ofisi kupitia Vikao vya Baraza la Wafanyakazi na taratibu zingine za kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa jana, Ofisi imetekeleza mabadiliko ya Muundo wake mpya hasa baada ya kuongezeka kwa nafasi ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, Ofisi ilijaza nafasi moja ya Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu na nafasi tano za Wakurugenzi Wasaidizi zilizokuwa wazi. Nafasi mbili ni kwa ajili ya Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, mbili kwa ajili ya Idara ya Sera na Mipango na moja kwa ajili ya Idara ya Muungano. Ofisi

ilijaza nafasi za ajira mpya tano, nafasi mbili zilikuwa ni za ajira mpya na nafasi tatu za ajira mbadala za maafisa wa kawaida. Aidha, Ofisi iliwapandisha vyeo watumishi 28 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza tija na kuwaongeza watumishi uwezo katika utendaji wao, Ofisi iliwaongezea watumishi wake uwezo wa kielimu na utendaji kazi. Katika Mwaka wa Fedha 2011/12, Ofisi iligharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa watumishi wapatao 29 waliohudhuria mafunzo ya aina mbalimbali kwa kuzingatia majukumu yao kazini. Kati ya hao, watatu walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na ishirini na sita walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, muda umekwisha na hujaomba Bunge likuidhinishie pesa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi iliendelea kuimarisha mshikamano, ushirikiano na mahusiano kati ya watumishi wake na watumishi wa Ofisi nyingine za Serikali kwa kushiriki kikamilifu katika mabonanza na Michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Kitaifa Mkoani Tanga mwezi Novemba, 2011. Jumla ya watumishi 42 walishiriki. Aidha, Ofisi iliendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari. Katika kipindi hiki, watumishi 208 walipata mafunzo kuhusu UKIMWI na VVU na kati

ya hao 101 walijitokeza kupima afya zao kwa hiari na kupatiwa ushauri nasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, Ofisi iliendelea kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi. Ujenzi wa Jengo la Ofisi Awamu ya Pili katika Kiwanja Na.10 kilichopo katika Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam umeendelea kusimamiwa na kutekelezwa. Ujenzi huu unaendelea vizuri na unategemewa kukamilika mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu, yameanza kutumika na Watumishi wa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais waliopo Zanzibar wamehamia katika jengo hili. Vile vile baadhi ya vyumba vya jengo hili vimeanza kutumiwa na Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia, yaani Tume ya Sayansi na Teknolojia na Tume ya Nguvu za Atomiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zote zinazoongoza masuala ya kiutumishi hususan nidhamu, maslahi, mafunzo, ajira, haki na Maadili ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia watumishi vitendea kazi ili kuongeza ufanisi na tija. Vile vile, Ofisi imeweka mkakati wa kuhamasisha watumishi kuendelea kupima afya zao kwa hiari, hususan Virusi vya UKIMWI na kuwashauri

watumishi walioathirika kujitokeza ili Ofisi iweze kuwahudumia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mawaziri wenzangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa (Mb.), Waziri wa Nchi, Mazingira na Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini ambao umewezesha kuwasilisha hoja hii. Vile vile, napenda niwashukuru Katibu Mkuu, Bw. Sazi Bundara Salula; Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Ngosi Charlestino Mwihava; Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mhandisi Bonaventure Thobias Baya; Wakuu wa Idara na Vitengo na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Taasisi yake kwa juhudi zao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais inapenda kutumia fursa hii ya kipekee kutambua na kuwashukuru Washirika wote wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi, ambao kwa njia moja au nyingine walichangia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi. Washirika hao ni Serikali ya Norway, Mfuko wa Maendeleo wa Norway *(Nordic Development Fund);* Jamhuri ya Korea ya Kusini, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Mpango wa Mazingira la Umoja wa Mataifa *(UNEP),* Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF),* Benki ya Dunia, International Development Agency -

IDA, Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA), SADC-REEP, Wildlife Conservation Society - WCS, World Wildlife Fund - WWF,* Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO), Crop Life International - CLI,* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Shirika la Misaada ya Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)* na Asasi Zisizo za Kiserikali *(AZISE)* za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Washirika wote wa Maendeleo waendelee kushirikiana nasi zaidi katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini na juhudi za kuboresha maisha ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, tarehe 26 Aprili, 2012 tulishuhudia Muungano wetu ukitimiza miaka 48 yenye maendeleo katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo kwa kiwango kikubwa zimefanyiwa kazi. Changamoto zilizobaki zitaendelea kufanyiwa kazi ili kudumisha uhuru, umoja na mshikamano wetu. Aidha, sisi sote tunafahamu kuwa tumeanza mchakato wa uandaaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni nafasi ya kipekee, itakayotuwezesha kuimarisha na kujenga Muungano wetu katika hali endelevu ili uwe wa manufaa kwa kizazi cha sasa na cha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwasihi Wananchi wote wa Tanzania, kujitokeza kwa wingi na kutumia nafasi hii adhimu, kutoa hoja na maoni kuhusu Muungano na masuala mengine kwa

maslahi ya Taifa kwa uwazi, bila jazba, fujo wala ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, shughuli za binadamu zina mchango kubwa katika uharibifu na uhifadhi wa mazingira. Aidha, Jumuiya ya Kimataifa inaendelea kusisitiza Uchumi wa Kijani ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Miaka 20 baada ya Mkutano wa Kilele Kuhusu Maendeleo Endelevu uliofanyika hivi karibuni huko Rio de Janeiro, Brazil. Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuratibu usimamizi na hifadhi ya mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa sahihi kuhusu idadi ya watu na shughuli zao pamoja na takwimu zingine ni muhimu katika kuandaa mipango na mikakati endelevu ya maendeleo, yanayozingatia uchumi wa kijani *(Green Economy).* Hivyo basi, ni matarajio yangu kuwa, Sensa ya Watu itakayofanyika tarehe 26 Agosti, 2012 itatoa mchango mkubwa katika kupanga na kusimamia vyema hifadhi ya mazingira hapa nchini. Kwa hiyo, natumia fursa kuungana na Viongozi wenzangu kutoa wito kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Ofisi ya Makamu wa Rais iweze kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa na malengo yake ya mwaka wa fedha 2012/13 ambayo nimeyaelezea katika Hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 26 - Makamu wa Rais, shilingi 4,653,309,000, fedha za matumzi ya kawaida. Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi 42,694,540,000 fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 10,270,942,000 fedha za maendeleo. Aidha, makadirio ya fungu 31 yanajumuisha shilingi 32,625,766,000 fedha za mgao wa kibajeti kwa SMZ na shilingi 3,716,883,000 ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Nakushukuru kwa taarifa yako. *(Makofi)*

Kwanza, nifafanue kwamba, Mheshimiwa Waziri amewasilisha pamoja na Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Kwa hiyo, ame-*cover* ofisi mbili.

Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa niaba yake Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA**

**UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za 99(7) na 114(11), za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013, kwa Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, tarehe 31 Mei, 2012, Kamati ilikutana Dar es Salaam, ili kupokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2011/2012 na kupitia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao hicho, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), alieleza Majukumu, Dira na Dhima ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile, alieleza masuala yaliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Ofisi hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maeneo kadhaa muhimu sana ambayo Kamati iliyatolea maoni na ushauri, hayakupatiwa ufumbuzi. Maeneo hayo ni:-

(i) Ufumbuzi na matatizo ya Muungano. Kamati iliiomba Serikali kuongeza kasi katika mazungumzo kati ya pande mbili za Muungano katika kutafuta suluhisho za kero za Muungano na hivyo kuimarisha Muungano wetu.

Kamati inasikitika kuona kwamba pamoja na juhudi ambazo zimekuwa zinafanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), bado matokeo ya juhudi hizo hayajazaa matunda kwani vurugu na machafuko yanayotokea upande mmoja wa Muungano yanadhihirisha kwamba juhudi hizo hazijafanikiwa ili kupata suluhisho la kero za Muungano. Kamati inaishauri Serikali kuonesha dhamira ya dhati na kulichukulia suala la Muungano kama suala nyeti ili matatizo yaliyopo yapate ufumbuzi kwani hivi sasa imekuwa siyo kero tena bali bughudha kwa pande zote mbili za Muungano.

(ii) Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano. Kwa mujibu wa Ibara ya 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ni kazi ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuzishauri Serikali zote mbili juu ya masuala ya fedha *(fiscal policy)* ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa Mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuelezea masikitiko yake kuhusu jambo hili kwani kwa taarifa zilizotolewa mbele ya Kamati, inaonesha dhahiri kwamba agizo hili halijatekelezwa kwa sababu ambazo hazikuwekwa wazi mbele ya Kamati. Aidha, ilielezwa kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walishatoa mapendekezo yao kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha lakini wenzao wa Serikali ya Muungano hadi leo hawajawasilisha mapendekezo kwa upande wao. Kamati inapenda utolewe ufafanuzi wa kina; ni kwa nini hali hiyo imekuwa hivyo kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Vile vile Kamati ilipendekeza kuwa Sheria ya Pamoja ya Fedha ya Mwaka 1996 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa vifungu vinavyosababisha ongezeko la kero za Muungano. Aidha, Sheria inayoitaka Taarifa kupelekwa kwa Mawaziri wa Fedha kuboreshwa ili Bunge na Baraza la Wawakilishi vihusishwe kwa kupelekewa uamuzi uliofikiwa na pande mbili kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitika kwa mara nyingine kutaarifu kwamba ushauri na Maoni haya ya Kamati hayakutekelezwa, hivyo ni vyema Serikali ikatoa ufafanuzi wa jambo hili mbele ya Bunge lako Tukufu.

(iii) Mawaziri wa Fedha wa pande zote mbili za Muungano wakutane na kushauriana kuhusu hatua zilizofikiwa na pande zote mbili katika kushughulikia

mapendekezo ya Tume. Aidha, Tume ijulishwe hatua zilizofikiwa na pande mbili katika mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hata agizo hili nalo halikutekelezwa, pamoja na juhudi zote zilizofanyika na Ofisi ya Makamu wa Rais za kuitisha kikao cha Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya fedha kwa ajili ya kujadili hatua iliyofikiwa katika kutoa uamuzi wa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowakilishwa kwa Tume zote mbili. Kamati inapenda kupata ufafanuzi wa Serikali ni kwa nini Wizara ya fedha hasa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijawa tayari wa kushughulikia jambo hili.

(iv) Elimu zaidi kuhusu Muungano wetu itolewe kwa Umma kupitia Redio, Televisheni, Magazeti, Majarida, Vipeperushi, Machapisho na hata Makongamano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili Kamati inaipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa kuendelea kutoa elimu kwa Umma kupitia Vyombo vya Habari kuhusu umuhimu wa kuimarisha na kudumisha Muungano wetu kwa amani ya Taifa letu. Hata hivyo, Kamati inaamini kuwa bado juhudi zaidi za kutoa Elimu kwa Umma zinahitajika kupitia njia mbalimbali ili Umma wa Watanzania waweze kuuelewa Muungano vizuri.

Serikali kutenga fedha kwenye Bajeti ili samani za majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Zanzibar) ziweze kununuliwa na hivyo kumuwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais, kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wakati wote anapokuwa eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuhusu jambo hili Kamati ilitaarifiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi,Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, samani kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar zimenunuliwa na tayari Mheshimiwa Makamu wa Rais anatumia Ofisi na Makazi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto nyingi zinazopaswa kushughulikiwa kwa dhati. Mfano ni tatizo la Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, kuelimisha Umma kuhusu Muungano na kuimarisha ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii. Changamoto nyingine zinaainishwa kama ifuatavyo:-

(i) Vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushughulikia masuala ya Muungano kutofanyika kwa mujibu wa Ratiba kutokana na majukumu ya Viongozi wa Juu ambao ni wahusika Wakuu katika vikao hivi.

(ii) Kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha za Bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi kwani zinazopatikana zinakuwa ni kidogo na hivyo

kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(iii) Uhaba wa vitendea kazi hususan magari kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji wa Miradi ya Ofisi na shughuli za kila siku.

(iv) Ufinyu wa Bajeti ya Fungu 31 unaoikabili Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo ya Kamati: Kwa kuwa kwa kiasi kikubwa maagizo ya Kamati yaliyotolewa Mwaka jana hayakutekelezwa kama ilivyotarajiwa, Kamati inazidi kuagiza ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Kamati inaiagiza Serikali kutoa ufafanuzi ni kwa nini suala la Wafanyabiashara wa Zanzibar bado limeendelea kuwa kero kwa kutozwa kodi mara mbili na Taasisi za kutoza kodi pamoja na Taarifa iliyotolewa na Serikali mbele ya Kamati Mwaka jana kwamba Kero hii imepatiwa ufumbuzi na kwamba bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha utaratibu wa forodha kupitia kituo chochote cha forodha ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazipaswi tena kulipa kodi mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaomba pia kupata ufafanuzi wa hatua gani za kisheria/kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya Maafisa na Watendaji wa Serikali walioshindwa kutekeleza maagizo haya yaliyotolewa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Kamati inaamini kwamba, suala la mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada katika nchi za nje bado ni kero hasa kwa upande wa Tanzania Visiwani. Ili kuondoa utata kwa pande zote mbili za Muungano, Kamati inaiomba Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu jambo hili. Aidha, Kamati inazidi tena kusisitiza kuwa ni vyema Serikali kuzipitia upya Sekta zote zinazoonekana kuwa na matatizo ili kupata suluhisho kwa manufaa na ustawi wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Kamati inazidi kuiagiza Serikali kufanyia kazi kwa haraka mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yameshafikishwa Serikalini. Kamati inaamini kuwa, hili ni moja ya maeneo ambayo pamekuwa ni kero kubwa na hivyo kusababisha hali ya kutoeleweka miongoni mwa wananchi kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa akaunti ya fedha ya pamoja kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; Kamati inapenda kupata ufafanuzi wa Serikali ili kueleza sababu ambazo hadi leo zinafanya Mawaziri wa Fedha wa pande zote mbili za Muungano, washindwe kukutana na kushauriana kuhusu hatua zilizofikiwa na pande mbili katika kushughulikia Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha. Pamoja na hilo, Kamati inazidi kusisisitiza kuwa ni vyema Sheria inayotaka Taarifa kupelekwa kwa Mawaziri wa Fedha ibadilishwe ili Taarifa hizo

ziletwe Bungeni na kwenye Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; Kamati inaiasa Jamii ya pande zote mbili za Muungano kuheshimu Utawala wa Sheria na kuwa tayari kutoa Maoni kwenye Tume ya kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba, ambayo hivi sasa imeshaanza kazi yake ili kutoa mawazo yao kwa jambo lolote ambalo linaonekana kuwa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita; Kamati inashauri kwamba pamoja na kuongeza juhudi zaidi katika utoaji wa elimu kuhusu Muungano ni vyema mipango ikafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu ili kuangalia namna ambayo somo la Historia kuhusu Muungano linaweza kufundishwa kuanzia Shule za Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maoni na ushauri ambayo Kamati iliyatoa iliposhughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya ufafanuzi uliotolewa na Ofisi hiyo, hatimaye Kamati yangu iliyapitisha Matumizi ya Ofisi hiyo na kuruhusu yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu na kuniwezesha kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu

wa Rais (Muungano), Ndugu Sazi Bundala Salula, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Uendeshaji, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa John Paulo Lwanji - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Zahara Ali Hamadi, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert Bigumisa Blandes, Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed na Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda.

Napenda pia kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha na kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, namshukuru Ndugu Peter Magati - Katibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha

mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa Fungu 31 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kuidhinisha maombi ya fedha kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba (Mb), aliyekuwa Mjumbe wa Kamati, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kwa kuteuliwa kwao. Kamati inawataka kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu mkubwa kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Aidha, Kamati ilipokea muhtasari wa kazi zilizofanywa na Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kipindi kilichopita na mafanikio na changamoto zilizojitokeza mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Kamati ilipopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/2012, Kamati iliweza kukutana na Ofisi hii mara kadhaa na imekuwa ikitoa ushauri kuhusu maeneo mbalimbali kuhusu usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Ushauri ambao umekuwa ukizingatiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo machache ambayo Kamati ilishauri, lakini Serikali haikuzingatia ushauri huo hasa katika maeneo yaliyoainishwa kama ifuatavyo:-

Pamoja na Kamati kuishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, bado Serikali imetenga fedha kidogo (kutoka shilingi 52,822,422,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 hadi shilingi 52,965,482,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/ 2013, ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.27 tu), ambazo hazitoshelezi mahitaji halisi ya utekelezaji wa shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Kamati imesikitishwa na Bajeti hii, kwani inaonekana wazi kwamba, Serikali haijalipa kipaumbele suala la Mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, nakuona lakini naomba umwache aendelee kwanza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Ingawa Ofisi ya Makamu wa Rais

(Mazingira) imeendelea kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini, bado wananchi wengi hawajafikiwa na elimu hii hasa wananchi waishio vijijini.

Kamati inaamini kuwa, endapo juhudi zaidi zingefanyika, wananchi wengi wangefikiwa na elimu hii hivyo kuweza kutunza mazingira na kufaidika na uwepo wa vyanzo vya maji, malisho na mazao yatokanayo na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuisihi Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati ili kuweza kutunza na kuhifadhi mazingira kwa faida ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza mtoa hoja, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 7,100,000. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012, Ofisi ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 16,343,633, ikiwa hata hivyo ni ongezeko la asilimia 230 ya kiasi kilichokadiriwa. Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kuweza kukusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 200.

**MWENYEKITI:** Samahani, Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Matiko tafadhali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa naomba kuhusu utaratibu, lakini naona event yenyewe imekwisha-*expire.* Wakati

msomaji kuhusu Kamati ya Katiba na Sheria anachangia, na ninatumia Kanuni 66(3)(d), kuna Mbunge alikuwa anasoma gazeti muda wote wa kipindi hiki, Mheshimiwa Mussa Kombo. Saa zile alikuwa anasoma sasa hivi imekwisha-*expire* sijui utafanya nini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Utaratibu unaagiza hivi; wakati Bunge lipo kwenye kikao hairuhusiwi Kikanuni kusoma kitu ambacho ni tofauti na ajenda ambayo inaendelea. Kwa hiyo, hilo ni kosa.

Mheshimiwa Mbunge, naomba uendelee.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) iliidhinishiwa Shilingi 40,412,043,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,323,754,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 39,088,289,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kiasi hicho kinajumuisha shilingi 30,423,054,500, mgawo wa fedha za Bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za ruzuku za Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) shilingi 4,098,955,000. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012, Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 33,733,903,080 kwa ajili matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 83 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya shilingi 40,412,043,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, ziliidhinishwa jumla ya Shilingi 12,410,379,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,067,014,000 zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi 6,343,365,000 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012 jumla ya Shilingi 5,312,580,835.20 zilipokelewa, sawa na asilimia 36 ya Bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifurahishwa kuona Serikali imetenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo zaidi ya fedha za wafadhili. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na kiasi kidogo cha fedha za miradi ya maendeleo kilichotolewa na hii inadhihirisha jinsi gani Serikali inafanyia mzaha suala la Mazingira linaloambatana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012: Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) imefanikiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma kupitia maadhimisho na maonesho mbalimbali kwa njia ya vipeperushi, mabango, fulana na kofia, vitini, redio na televisheni;

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (1994) wa Rio de Janeiro;

(iii) Kuendelea kuandaa Kanuni na Miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ambapo Kanuni Mbalimbali zimeandaliwa ikiwa ni pamoja na Kanuni za Kudhibiti Matumizi ya Mifuko ya Plastiki na Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu;

(iv) Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuunda Kamati ya Ushauri ya Mazingira; kuandaa rasimu ya taarifa ya pili ya Hali ya Mazingira nchini; na kuidhinisha miradi 153 na kuipatia Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM); na

(v) Kuendelea kujenga uwezo kwa wataalam na wadau kuhusu Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, ufinyu wa Bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa. Aidha, changamoto mbalimbali zimeendelea kuikabili Ofisi ikiwa ni pamoja na zifuatazo: Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira; kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati; mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika hifadhi na utunzaji wa mazingira; upungufu wa wataalam wa fani ya Mazingira katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi

wa Mazingira *(NEMC);* na uhaba wa rasilimali watu katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2012/2013, Kamati imeona kuwa Ofisi ilizingatia Mwongozo wa Taifa wa Uandaaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013, Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), Dira ya Taifa ya Maendeleo – 2025 na maoni na mapendekezo ya Bunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Ofisi kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivyo basi, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kiasi cha shilingi 52,965,482,000 kinaombwa kwa ajili ya Fungu 31, ambapo kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 42,694, 540,000 na fedha za matumizi ya maendeleo shilingi 10,270,942,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha matumizi ya kawaida kinajumuisha fedha za mgao wa asilimia 4.5 ya Bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 32,625,766,000; hivyo, kiuhalisia matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) ni kiasi cha shilingi 10,068,774,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi 10,270,942,000 zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani

shilingi 4,500,000,000 na fedha za nje shilingi 5,770,942,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipitia kifungu kwa kifungu na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kuridhika nayo; na sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya shilingi 52,965,482,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuujadili Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kina, Kamati inatoa maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha za matumizi ya kawaida kwa Fungu 31, shilingi 5,372,218,000 tu ndiyo zimetengwa kati ya shilingi 42,694,540,000, kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ya Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Kamati inaona kiwango hiki ni kidogo sana kwa Idara na Baraza kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa sana na Bajeti ndogo ambayo Ofisi hii imepangiwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, pamoja na kwamba wakati wa kuchambua Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Kamati ilishauri Bajeti iongezwe kwa Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na faida zake. Aidha, ni mashahidi wa athari mbalimbali zinazotokana na uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji, ukataji ovyo wa misitu, ujenzi holela wa miji na utupaji ovyo wa taka, ambavyo vinachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali, ione umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kuitengea fedha za kutosha ambazo zitaiwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) pamoja na mambo mengine, kutoa elimu kwa umma hususan kwa wananchi walio vijijini kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* limetengewa kiasi cha Sh. 3,716,883,000 kwa ajili ya fedha za matumizi ya kawaida ikiwa ni pungufu ya asilimia tisa ya kiasi kilichotengwa (Sh. 4,098,955,000) kwa ajili ya Baraza katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* ndiyo Msimamizi Mkuu wa Mazingira Nchini, Serikali imeendelea kutenga bajeti ndogo sana kwa Baraza, hali iliyopelekea Baraza kushindwa kujiendesha na kushindwa kuajiri wataalamu wa kutosha katika fani ya Mazingira.

Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudi za ziada kuongeza bajeti hii ili Baraza liweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na suala la mabadiliko ya tabianchi kupewa kipaumbele katika nchi nyingi ulimwenguni, bado Serikali yetu haijalipa suala hili msukumo unaostahili. Kamati imesikitishwa sana kuona kwamba katika fedha za maendeleo kwa mradi wa mabadiliko ya tabianchi kiasi kilichotengwa cha shilingi 1,495,420,000 kitatoka kwa wahisani. Kamati bado inasisitiza kwamba, nchi haiwezi kuendelea kwa kutegemea wahisani; ni vyema Serikali ikatoa kipaumbele na kutenga angalau fedha za ndani kwa ajili ya kuendesha miradi kama hii yenye tija kwa Taifa kwani uzoefu umeonesha kuwa fedha nyingi zinazoahidiwa na wafadhili huwa hazitolewi kwa wakati mwafaka na wakati mwingine hazitolewi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia Sheria ya Mazingira kuanzisha Mfuko wa Mazingira. Kamati inaamini Mfuko huu ukianza kutumika, utasaidia sana katika kuboresha masuala mbalimbali yahusuyo usimamizi na uhifadhi wa Mazingira. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kutumia utaratibu mzuri ili Mfuko usimamiwe na watendaji waadilifu, makini na wenye weledi katika masuala ya Mazingira kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi nchini hasa maeneo ya mijini kumekuwepo na uchafuzi mkubwa wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki. Kwa kuwa nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki

zimekubaliana kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki iliyo kati ya kipimo cha kuanzia micro moja hadi 30, Kamati inaishauri Serikali kuisimamia Kanuni ya Kudhibiti Matumizi ya Mifuko hiyo ya Plastiki *(Control of Polyethylene Materials)* na kuhakikisha Kanuni hii inatekelezwa kama ilivyo katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan Nchi ya Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waratibu wa Mazingira wa Kisekta huteuliwa miongoni mwa Maafisa wa Wizara husika kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na hivyo Waratibu hao kuwa na majukumu mengine na kushindwa kutekeleza ipasavyo majukumu ya kusimamia mazingira, Kamati inashauri ni vyema kifungu husika (Kifungu Namba 33) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) kikarekebishwa na kutoa mamlaka kwa Wizara husika kuajiri wataalam wenye taaluma ya Mazingira kuwa Waratibu wa Mazingira na kusimamiwa na Katibu Mkuu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) iliweza kukutana na Halmashauri tatu tu za Karatu, Siha na Magu, kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira na kupata maelezo ya namna Halmashauri hizo zilivyojiandaa kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeonesha mwitikio mdogo katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni vyema kwa Mwaka huu wa Fedha, Ofisi hii ikakutana na Halmashauri nyingi zaidi ili kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo. Aidha, Kamati inashauri pamoja na

kukutana na Halmashauri hizo, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ifuatilie utungaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo za Mazingira katika Halmashauri za Miji, Majiji na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Ofisi hii, iliona kuna baadhi ya vifungu vilivyotengewa fedha kidogo sana. Kwa mfano, kifungu Kidogo cha 1006 - 221100 - *Travel out of Country* ni Sh. 50,000, ukilinganisha na mahitaji.

Kamati inashauri kuwa ni vyema kwa kila Mwaka wa Fedha, Ofisi ikaainisha maeneo ya kipaumbele na kutenga fedha za kutosha katika maeneo hayo ili kuepuka kutenga fedha kidogo katika baadhi ya vifungu ambapo utekelezaji wake hauwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la athari za mabadiliko ya tabianchi limeendelea kuleta matatizo nchini na duniani kote. Wote tumeona majanga yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini yaliyosababishwa na ukame, mvua zisizotabirika, maporomoko ya ardhi, mafuriko, kuongezeka kwa joto na kuongezeka kwa kina cha bahari, ambapo kwa kiasi kikubwa yameathiri shughuli za kijamii, kiuchumi na za binadamu.

Kamati inashauri Serikali kuendelea kukuza weledi kuhusu tatizo hili na jinsi ya kukabiliana nalo kwa wananchi wote na viongozi hasa wawakilishi wa wananchi kwani wao wataweza kufikisha elimu hii

katika maeneo yao. Aidha, Serikali ihuishe masuala ya tabianchi katika mipango yake ya maendeleo kwani ukisoma Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013, ukurasa wa 42, Serikali imeelezea jinsi mabadiliko ya tabianchi yaliyoambatana na ukame na mafuriko, yalivyoweza kuathiri shughuli za uzalishaji na uharibifu wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii na kupelekea kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2011/2012. Hali hii iliilazimu Serikali kuelekeza fedha za Miradi ya Maendeleo katika kukabiliana na majanga haya. Pamoja na Serikali kutambua athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, bado imeshindwa kuhusisha mipango yake ya maendeleo na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuitaka Serikali kuonesha nia ya dhati kwa kuongeza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka ujao wa Fedha (2013/2014) ili kuweza kukabiliana na changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa ukame, mafuriko na kina cha bahari. Kamati inaitaka Serikali kutambua mabadiliko ya tabianchi ni ya kweli na ya kudumu, yanayohitaji utayari wa Serikali, la sivyo yatakuwa na madhara makubwa kwa vizazi vijavyo ambavyo vitatumia gharama kubwa zaidi ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine ya muhimu ambayo Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu

wa Rais (Mazingira) kuyapa kipaumbele katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kila mtu ni shahidi kwamba miti ni muhimu katika utunzaji wa mazingira na kwa kuwa jukumu la kutunza mazingira ni wajibu wa kila mwananchi; Kamati inashauri kwamba, suala la upandaji miti lipewe kipaumbele hasa katika siku ya upandaji miti nchini, kwa kuwahamasisha wananchi kupanda miti na kuitunza kwani mazingira ni muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mikoa Mkoa wa Kilimanjaro umeonesha juhudi za wazi katika utunzaji wa mazingira, tunawapongeza sana. Kamati inashauri ni vyema Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ikawa na utaratibu wa kuandaa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Kitaifa katika Mikoa ambayo ipo nyuma katika suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Kwa kufanya hivyo, Ofisi itafanikiwa kutoa elimu kwa umma katika maeneo ambayo hayajatoa kipaumbele katika masuala ya mazingira. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na siku ya upandaji miti inayofanyika kila mwaka tarehe 1 Aprili. Pamoja na ubunifu huu, Kamati inashauri, ili kuongeza ufanisi siku hii ya upandaji miti ni vyema ikapangwa kulingana na vipindi vya mvua kwa kutegemea na eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kutekeleza utaratibu uliowekwa wa

kufanya usafi wa mazingira kila mwezi katika kila Halmashauri. Kamati inashauri suala la utunzaji wa mazingira liwe ni moja ya vigezo vya kupima ufanisi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Pia namshukuru sana Mwenyekiti wangu na Makamu Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii pia kuwakilisha. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Naibu Waziri Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga; Ndugu Sazi M. Salula - Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wataalamu wote wa Ofisi hii na Watendaji wote wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* kwa ushirikiano, ushauri na utaalamu wao ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti inayoombwa na hivyo kufanikisha Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji - Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri

Khatib Ameir, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ali khamis Seif, Mheshimiwa Suzan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Michael Lekule laizer, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Kamati - Ndugu Grace Bidya na Rachel Nyega, wakisaidiwa na Ndugu Lukindo Choholo, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa liipokee Taarifa hii na kukubali kuidhinisha Bajeti ya Ofisi wa Makamu wa Rais (Mazingira) kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, niwasilishe Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa mwaka 2012/2013. Naomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu Za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetimiza miaka arobaini na nane tangu kuzaliwa kwake, baada ya Rais wa Jamhuri ya Tanganyika Mwalimu Nyerere kutia saini Makubaliano ya Muungano na Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Sheikh Abedi Amani Karume, tarehe 22 Aprili, 1964. Wakati anawasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba "... katika kipindi hicho, Muungano wetu umekuwa na mafanikio katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa... Muungano wetu ndiyo nguzo kuu ya umoja na amani." Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba, licha ya

mafanikio hayo, "...zipo changamoto katika kumaliza vikwazo vinavyokwamisha shughuli za Muungano." Mheshimiwa Waziri hakuzitaja changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utangulizi wake kwa Chapisho la Pili la Mhadhara wa Kiprofesa (Professorial Inaugural Lecture), uliotolewa Januari 1990 na Profesa Issa G. Shivji na kupewa kichwa cha Tanzania: The Legal Foundations of the Union, Profesa Yash Ghai, aliyekuwa Mkuu wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa kwanza kutoka Afrika Mashariki anasema kwamba; kwa kuzingatia mazingira ya kuanzishwa kwa Muungano na historia yake, "...kitu cha ajabu siyo kwamba umekuwa na matatizo, bali umedumu (licha ya matatizo hayo) na kwenda kinyume na mwelekeo katika Afrika."

Muungano ulidumu misuguano ya miaka ya mwanzo kati ya Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume iliyohusu kuongezwa kwa masuala ya fedha na sarafu katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Aidha, Muungano ulidumu mauaji ya Viongozi Waandamizi na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi la kwanza la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Abdallah Kassim Hanga, Waziri wa Fedha Abdul Aziz Twala, Othman Sharrif, Mdungi Ussi, Saleh Saadalla na wengine wengi. Vile vile, Muungano ulidumu mauaji ya Sheikh Karume mwenyewe mwaka 1972; kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar iliyopelekea kung'olewa madarakani kwa Rais Aboud Jumbe mwaka 1984; na kile alichokiita Mwalimu Nyerere udhaifu wa Rais Mwinyi; na kifo cha Mwalimu Nyerere mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, mapito haya ya Muungano yamekuwa yanafichwa fichwa, licha ya kauli za mara kwa mara za kuelimisha umma juu ya Muungano. Kwa sababu hiyo, zaidi ya tendo la kuchanganya udongo na matukio mengine yaliyofanyika hadharani, historia halisi ya Muungano wetu haifahamiki kwa wananchi walio wengi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, wakati umefika sasa kwa Serikali kuweka wazi nyaraka mbalimbali zinazohusu historia ya Muungano wetu na mapito yake ili Watanzania waelewe masuala yote yaliyotokea yanayouhusu. Hii ni muhimu zaidi kwa kuzingatia ukweli kwamba, Mataifa ya Magharibi kama vile Marekani na Uingereza yalikwishatoa hadharani nyaraka za mashirika yao ya kijasusi pamoja na Balozi zao za Tanzania zinazoonesha jinsi ambavyo Serikali za Mataifa hayo zilihusika katika kuzaliwa kwa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanikwa kwa nyaraka zilizoko katika mamlaka mbalimbali za Serikali kutasaidia kuthibitisha au kukanusha taarifa ambazo chanzo chake ni nyaraka za kidiplomasia na kijasusi za nchi hizo kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulitokana na njama za kibeberu za kudhibiti ushawishi wa siasa za kimapinduzi za Chama cha Umma na Viongozi wake ndani ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar la wakati huo. Aidha, nyaraka hizo zitatoa mwanga juu ya kilichowasibu Viongozi Waandamizi wa Chama hicho ambao bila uwepo wao kutambuliwa rasmi, historia ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya

Muungano inabaki pungufu. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, miaka karibu hamsini ya Muungano ni umri wa kutosha kwa Taifa la Tanzania kuambiwa ukweli wote juu ya kuzaliwa kwake na mapito ambayo limepitia katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano ya Muungano ya tarehe 22 Aprili 1964 yalikuwa ni Mkataba wa Kimataifa kati ya nchi mbili huru zilizokubaliana kuunda nchi moja huru, kwa mujibu wa ibara ya (i) ya Hati ya Muungano. Ili kutekeleza Makubaliano ya Muungano, Bunge la Jamhuri ya Tanganyika lilitunga Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, 1964, Sura ya 557 ya Sheria za Tanzania.

Kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kilitangaza kuunganishwa kwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na kuwa Jamhuri moja huru itakayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kwa upande wa Zanzibar, Baraza la Mapinduzi, ambalo ndiyo lilikuwa Bunge la Zanzibar wakati huo, halikutunga Sheria ya Kuridhia Makubaliano ya Muungano. Jambo hili limekuwa chanzo cha mjadala mkali katika duru za kitaaluma na kisheria juu ya uhalali wa Muungano wenyewe. Kwa vyovyote vile, matokeo ya kusainiwa Makubaliano ya Muungano ni kwamba, Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zilikufa na nchi moja iliyokuja baadaye kuitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa aya ya (iv) ya Makubaliano ya Muungano na kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Muungano, Mambo ya Muungano yaliyokubaliwa kwenye Makubaliano ya Muungano yalikuwa kumi na moja. Haya ni mambo yaliyoko katika vipengele vya kwanza hadi cha kumi na moja vya Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Muungano ya sasa. Hata hivyo, kati ya mwaka 1964 na 1973 mambo mengine sita yanayoonekana katika vipengele vya 12 hadi 16 vya Nyongeza ya Kwanza yaliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Hivyo basi, mwaka 1965 masuala ya fedha, sarafu na benki yaliongezwa; mwaka 1967 leseni ya viwanda na takwimu, elimu ya juu na mambo yaliyokuwa katika Nyongeza ya X ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliongezwa; mwaka 1968 yaliongezwa mambo ya maliasili ya mafuta, petroli na gesi asilia; na mwaka 1973 mambo yanayohusu Baraza la Mitihani la Taifa yaliongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mabadiliko ya Tano ya Katiba ya mwaka 1984 yaligawa kipengele cha Nyongeza ya X ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutengeneza vipengele vinne vinavyojitegemea katika Orodha ya Mambo ya Muungano, yaani usafiri na usafirishaji wa anga, utafiti, utabiri wa hali ya hewa na takwimu. Vilevile, mabadiliko hayo yaliongeza kitu kipya katika orodha ya Mambo ya Muungano: Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Aidha, kipengele cha tatu, yaani Ulinzi, kilifanyiwa marekebisho na kuwa Ulinzi na Usalama. Na mwaka 1992 uandikishwaji wa Vyama vya Siasa nao uliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote yaliyoongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano baada ya mwaka 1964 yalikuwa nje ya Makubaliano ya Muungano na nje ya Sheria ya Muungano na kwa hiyo yalikuwa batili. Hii ni kwa sababu Sheria ya Muungano na siyo Katiba za Muda za 1964 au 1965 au ya sasa, ndiyo Sheria Mama iliyozaa Muungano na kuweka mgawanyo wa madaraka kati ya Mamlaka za Jamhuri ya Muungano na Mamlaka za Zanzibar.

Sheria ya Muungano ilitungwa na Bunge la Katiba tofauti na sheria za kawaida. Aidha, Katiba ya Muda, 1965 iliyotawala Tanzania hadi 1977, iliiweka Sheria hiyo ya Muungano kama Nyongeza ya Pili katika Katiba na kuweka masharti kwamba Sheria hiyo haiwezi kurekebishwa bila marekebisho hayo kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote wa Tanganyika na wale wa Zanzibar.

Vilevile, Katiba ya Muungano ya sasa inataja katika Orodha ya Kwanza ya Nyongeza ya Pili kwamba moja ya Sheria ambazo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote ni “Sura ya 557 (Toleo la 1965), Sheria ya Kuthibitisha Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya Mwaka 1964.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya, yanaifanya Sheria ya Muungano kuwa na haiba ya Katiba. Kama alivyosema Profesa Issa Shivji katika “The Legal Foundations of the Union: “Kila mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa sheria amefundishwa kwamba

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapatikana katika Waraka unaoitwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Nachelea kusema, kila mwanafunzi amefundishwa visivyo. Katiba ya Tanzania haipatikani katika Waraka mmoja, bali katika nyaraka mbili. Sheria ya Muungano, Sura ya 557 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania... Vivyo hivyo, Katiba ya Zanzibar inapatikana katika (1) Sheria ya Muungano na (2) Katiba ya Zanzibar, 1984." Katika masuala yanayohusu Muungano, kwa mujibu wa Profesa Shivji, Waraka unaotawala ni Sheria ya Muungano.

Hii ndiyo kusema kwamba, panapotokea mgongano kati ya Katiba au Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Muungano, ni Sheria ya Muungano ndiyo inayokuwa na Katiba au Katiba ya Zanzibar inakuwa batili kwa kiasi cha ukiukaji wake wa Sheria ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5 cha Sheria ya Muungano, ambacho ndicho chenye Misingi Mikuu ya Muungano, hakijawahi kurekebishwa tangu Sheria yenyewe ilipotungwa mwaka 1964. Badala yake, Bunge limekuwa na tabia ya kukwepa kuigusa kabisa Sheria ya Muungano na badala yake limekuwa likifanya marekebisho ya orodha ya Mambo ya Muungano iliyowekwa kwa mara ya kwanza katika Katiba za Muda za mwaka 1964 na 1965 kwa kuongeza vipengele katika orodha hiyo.

Lengo la marekebisho haya, limekuwa mara zote ni kuinyang'anya Zanzibar mamlaka yake chini ya Sheria ya Muungano. Ndiyo maana katika Mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya CCM kuhusu Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yaliyotolewa tarehe 27 Januari, 1983, CCM ilitamka kwamba "...msingi wa kuwa na Orodha ya mambo ya Muungano katika Katiba ni kuonesha mamlaka ya Serikali ya Zanzibar ambayo yalikabidhiwa kwa Serikali ya Muungano; na msingi wa kuongeza mambo zaidi katika orodha ya mambo ya Muungano, kama ambavyo imefanyika mara kwa mara, ni kuhamisha mamlaka zaidi ya Serikali ya Zanzibar kwenda kwa Serikali ya Muungano."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Shivji anasema katika *The Legal Foundations of the Union* kwamba; Bunge la Jamhuri ya Muungano halikupewa mamlaka ya kuongeza Mambo ya Muungano bali lilipewa mamlaka ya kutunga sheria zinazohusu Mambo ya Muungano kama yalivyofafanuliwa katika Sheria ya Muungano.

Kwa maana hiyo, nyongeza zote zilizofanyika katika orodha ya Mambo ya Muungano tangu mwaka 1964 zilikiuka Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano na ni batili. Ndiyo maana, kwa muda mrefu sana, Wazanzibari wamelalamikia masuala haya, hasa masuala ya fedha, sarafu na mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya kupuuza Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano iliyoridhia Makubaliano, vilifikia kilele chake tarehe 21 Novemba, 2000 pale Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilipotamka katika kesi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar dhidi ya Machano Khamis Ali na Wenzake 17 kwamba, Zanzibar siyo nchi na wala siyo dola. Bali, kwa mujibu wa Mahakama ya Rufani, hakuna ubishi wa aina yoyote kwamba Jamhuri ya Muungano ni nchi moja na dola moja.

Kama tulivyokwisha kuonesha, suala la Mahakama ya Rufani ya Tanzania yenyewe kuwa suala la Muungano liliingizwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano kinyemela na kinyume na Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano. Jibu la Wazanzibari juu ya ukiukwaji wa muda mrefu wa Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano iliyoridhia Makubaliano hayo lilikuwa ni kupitisha Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misukosuko ambayo imeukumba Muungano wetu tangu mwaka 1964 hailingani na hatari kubwa inayoukabili hivi sasa. Kama tulivyomweleza Rais Kikwete katika Waraka wetu wa tarehe 27 Novemba, 2011, “Muungano wetu upo katika hatari kubwa ya kuvunjika kwa sababu ya mabadiliko makubwa ya kikatiba ambayo yamefanyika katika Katiba ya Zanzibar, 1984 na kutokana na Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Hii ni kwa sababu Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba, 2010, inaashiria tafsiri mpya ya Makubaliano

ya Muungano na ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inahoji misingi ya Jamhuri ya Muungano kama nchi moja, mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, na mambo muhimu ya Muungano."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufahamu jambo hili vizuri, ni muhimu kuelewa kwa undani yaliyomo katika Sheria hiyo ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 13 Agosti, 2010, wakati Bunge la Jamhuri ya Muungano likiwa limevunjwa kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2010, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, 1984. Mabadiliko haya yaliweka msingi wa kikatiba wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar inayoshirikisha CCM na Chama cha Wananchi *(CUF).* Kwa sababu hiyo, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba imepigiwa upatu kama Katiba ya Muafaka, na kwa kiasi fulani, hii ni kweli.

Hata hivyo, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba imekwenda mbali zaidi. Sheria hii siyo tu imehoji uhalali wa orodha ya Mambo ya Muungano ya tangu mwaka 1964 na nyongeza zake zilizofuata, bali pia imehoji misingi muhimu ya Sheria ya Muungano iliyoridhia Makubaliano ya Muungano. Kwa mtazamo huu, Katiba ya sasa ya Zanzibar inaelekea kuwa ni tangazo la uhuru wa Zanzibar zaidi kuliko waraka wa muafaka kati ya vyama viwili vilivyokuwa mahasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aya ya (i) ya Makubaliano ya Muungano na kifungu cha (4) cha Sheria ya Muungano vilitangaza Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na kuundwa kwa Jamhuri moja huru itakayoitwa "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar." Huu ndiyo msingi wa maneno ya ibara ya (1) ya Katiba ya Muungano kwamba, Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano. Vilevile huu ndiyo ulikuwa msingi wa maneno ya ibara ya (1) ya Katiba ya Zanzibar ya kabla ya mabadiliko ya mwaka 2010 kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Sasa msingi huu wa Muungano umehojiwa na maneno ya ibara ya (2) ya Katiba mpya ya Zanzibar yanayotamka kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2(2) ya Katiba ya Muungano inampa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kushauriana kwanza na Rais wa Zanzibar, mamlaka ya kuigawa Tanzania Zanzibar katika Mikoa, Wilaya au maeneo mengineyo. Vile vile, ibara ya 61(3) ya Katiba ya Muungano inampa Rais wa Zanzibar mamlaka ya kuteua Wakuu wa Mikoa katika Tanzania Zanzibar, baada ya kushauriana na Rais. Masuala ya mgawanyo wa nchi katika Mikoa na Mamlaka za Mikoa hiyo siyo, na hayajawahi kuwa, Mambo ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Muungano. Vile vile hayapo katika orodha ya Mambo ya Muungano.

Kwa hiyo, ni wazi kwamba ibara za 2(2) na 61(3) za Katiba ya Muungano zilikuwa zinakiuka matakwa ya Sheria ya Muungano, na kwa hiyo, ni batili. Sasa

wazanzibari wamejitangazia uhuru kwa kutangaza katika ibara ya 2A ya Katiba mpya ya Zanzibar kwamba “Rais (wa Zanzibar) aweza kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.” Aidha, kwa ibara ya 61(1), Rais wa Zanzibar hawajibiki tena kushauriana na Rais wa Muungano pale anapofanya uteuzi wa Wakuu wa Mikoa ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo Sheria ya Muungano ilikuwa imetambua na kuhifadhi mamlaka ya Rais wa Zanzibar kama Mkuu wa dola ya Zanzibar, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, katika Kesi ya Machano Khamis Ali na Wenzake, ilitishia moja kwa moja msingi huo kwa kutamka kwamba Zanzibar siyo nchi na wala siyo dola. Kwa hiyo, haiwezi kutishiwa na kosa la uhaini. Sasa ibara ya 26(1) ya Katiba mpya Zanzibar imerudisha dola ya Zanzibar kwa kutamka kwamba, kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mkuu wa Nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, kwa kutambua kwamba Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano siyo moja ya Mambo ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Muungano, Katiba ya sasa ya Zanzibar imetamka kwamba katika kesi zinazohusu kinga za haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi, uamuzi wa Majaji watatu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar utakuwa ni wa mwisho na hautakatiwa rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(1)(a)(iii) na (iv) cha Sheria ya Muungano kinataja ‘ulinzi’ na ‘Polisi’ kama sehemu ya mambo kumi na moja ya Muungano. Hivyo ndivyo inavyosema aya ya (iv)(c) na (d) ya Makubaliano ya Muungano. Ijapokuwa ulinzi ulichakachuliwa baadaye kwa kuongezwa maneno ‘na usalama’, bado ni sahihi kusema kwamba masuala ya ulinzi na Polisi ni masuala halali ambayo Sheria ya Muungano iliyakasimu kwa Serikali ya Muungano. Kwa sababu hiyo, ni sahihi kwa Katiba ya Muungano kutamka kama inavyofanya katika ibara ya 33(2) kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.’

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika kile kinachoonekana kama hojaji kubwa ya msingi huu wa Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano, ibara ya 121 ya Katiba ya sasa ya Zanzibar imeunda majeshi ya Zanzibar inayoyaita ‘Idara Maalum.’ Majeshi haya, kwa mujibu wa ibara ya 121(2) ni Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU); Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM); Chuo cha Mafunzo (cha wahalifu); na Idara Maalum nyingine yoyote ambayo Rais wa Zanzibar anaweza kuianzisha ikiwa ataona inafaa; Kuthibitisha kwamba Idara Maalum ni majeshi; ibara ya 121(4) inakataza watumishi wa Idara Maalum kujishughulisha na mambo ya siasa. Makatazo haya hayatofautiani na makatazo ya wanajeshi kujiunga na Vyama vya Siasa yaliyoko katika ibara ya 147(3) ya Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba Katiba mpya ya Zanzibar inaanzisha majeshi, bali pia inamfanya Rais wa Zanzibar kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi hayo. Kwa mujibu wa ibara ya 123(1) ya Katiba hiyo: “Rais atakuwa Kamanda Mkuu wa Idara Maalum na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachohisi kwa maslahi ya Taifa (la Zanzibar), kinafaa.” Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 123(2), mamlaka ya Rais wa Zanzibar chini ya ibara ndogo ya (1) yanaingiza: “uwezo wa kutoa amri ya kufanya shughuli yoyote inayohusiana na Idara hiyo kwa manufaa ya Taifa.”

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haya ni mamlaka ya kutangaza au kuendesha vita ambayo kwa mujibu wa ibara ya 44(1) ya Katiba ya Muungano, ni mamlaka pekee ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama tafsiri hii ya ibara ya 123 ya Katiba mpya ya Zanzibar ni sahihi. Kama ni sahihi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko Bungeni, ni kwa nini imeiruhusu Zanzibar kujinyakulia mamlaka juu ya mambo ya ulinzi na usalama ambayo kwa historia yote ya Muungano, yamekuwa ni mamlaka pekee ya Serikali ya Muungano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(1)(b) cha Sheria ya Muungano kilitamka kwamba muundo wa Serikali ya Zanzibar utakuwa kama utakavyoamuliwa na sheria za Zanzibar pekee. Hivyo ndivyo ilivyokubaliwa katika aya ya (iii)(a) ya Makubaliano ya Muungano. Hata hivyo, licha ya muundo wa Serikali ya

Zanzibar kutokuwepo katika orodha ya Mambo ya Muungano, Katiba ya Muungano imetenga Sura ya Nne nzima kuzungumzia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa mujibu wa Profesa Shivji katika *The Legal Foundations of the Union*, Sura ya Nne ya Katiba ya Muungano inasema: " Haina ulazima wowote na ni kuingilia, bila kualikwa, kwenye mambo ambayo yako ndani ya mamlaka pekee ya Zanzibar." Ndio maana Katiba mpya ya Zanzibar, kwa usahihi kabisa imefanya mabadiliko katika muundo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar bila ya kuzingatia matakwa ya Sura ya Nne ya Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba mpya ya Zanzibar siyo tu kwamba imetangaza uhuru wa Zanzibar kwa kuhoji misingi muhimu ya Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba ya Muungano, bali pia imehakikisha kwamba uhuru huo utalindwa dhidi ya tishio lolote la Serikali ya Muungano. Hii imefanywa kwa kuweka utaratibu wa kuwepo kura ya maoni ya wananchi wa Zanzibar kuhusu mabadiliko ya vifungu kadhaa vya Katiba ya Zanzibar. Kwa mujibu wa ibara ya 80A (1) ya Katiba hiyo: "Baraza la Wawakilishi halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusiana na sharti lolote lililomo katika kifungu chochote kilichoainishwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mpaka kwanza mabadiliko hayo yakubaliwe na wananchi kwa kura ya maoni."

Vifungu vinavyohitaji kura ya maoni ni vifungu vyote vya Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Kwanza inayohusu Zanzibar kama nchi na/au dola; kifungu cha

(9) kinachohusu Serikali na watu wa Zanzibar; vifungu vyote vya Sura ya tatu inayohusu kinga ya haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi; na kifungu cha 26 kinachohusu Rais wa Zanzibar na mamlaka yake. Vifungu vingine ni pamoja na kifungu cha 28 kinachohusu muda wa Urais; Sehemu ya pili na ya tatu ya Sura ya nne zinazohusu Makamu Wawili wa Rais, Baraza la Mawaziri na Baraza la Mapinduzi; kifungu cha 80A kinachohifadhi haki ya kura ya maoni; na vifungu vya 121 na 123 vinavyohusu Idara Maalum na mambo yanayohusiana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka masharti ya kura ya maoni kuhusu mabadiliko ya vifungu tajwa vya Katiba mpya ya Zanzibar, kuna athari ya moja kwa moja kwa uhai wa Muungano wetu. Hii ni kwa sababu hata vifungu ambavyo tumeonyesha kwamba vinakiuka misingi mikuu ya Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano haviwezi kubadilishwa bila kura ya maoni ya Wazanzibari. Kwa maneno mengine, kwa mujibu wa Katiba ya sasa ya Zanzibar, masuala ya kama Tanzania ni nchi moja au la, majeshi ya ulinzi, Polisi, na kadhalika ambayo yamekuwa Mambo ya Muungano kwa mujibu wa Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano siyo mambo ya Muungano tena, hadi hapo wananchi wa Zanzibar watakapoamua kwa kura ya maoni kuyarudisha kwa mamlaka ya Muungano. Huku ni kutangaza uhuru wa Zanzibar bila kutaja neno uhuru. Huku ni kuua Muungano bila kukiri hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wa Katiba ya sasa ya Zanzibar, hatuna tena nchi moja

inayozungumzwa katika Katiba ya Muungano, bali tuna nchi mbili. Kwa mtazamo huo huo, masuala ya ulinzi na usalama, Polisi, na kadhalika, siyo tena mambo ya Muungano kwa sababu sasa kila nchi ina majeshi yake na kila moja ina Amiri Jeshi Mkuu wake. Aidha, tuna marais wawili, Wakuu wa Nchi wawili, Viongozi wa Serikali wawili. Haya yote yanakiuka moja kwa moja Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba ya Muungano.

Kwa upande mwingine, kwa mtazamo wa Katiba ya sasa ya Zanzibar, Rais wa Muungano hana tena mamlaka ya kugawa Mikoa na Wilaya kwa upande wa Zanzibar, na wala hawezi kumshauri tena Rais wa Zanzibar anapoteua Wakuu wa Mikoa wa Tanzania Zanzibar. Aidha, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, licha ya kuwa moja ya mambo ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Muungano, haina tena mamlaka ya kusikiliza na kuamua rufaa zinazohusu haki za msingi na uhuru wa mtu binafsi zinazotoka Zanzibar. Yote haya hayapo katika makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano, lakini yapo katika Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilionyesha jinsi ambavyo tafsiri hii mpya ya Makubaliano ya Muungano na Katiba ya Jamhuri ya Muungano imetiliwa nguvu kubwa na Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo imeipa Zanzibar nafasi na ushawishi mkubwa katika utungaji wa Katiba Mpya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilionyesha kwamba, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Rais wa Zanzibar siyo tu kwamba ana

mamlaka karibu sawa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, bali pia ana kura ya turufu katika mchakato mzima wa Katiba Mpya.

Aidha, tulithibitisha jinsi ambavyo ushawishi mkubwa wa Zanzibar hauishii katika kura ya turufu aliyonayo Rais wa Zanzibar pekee yake, bali Zanzibar ina ushawishi mkubwa vile vile kutokana na nafasi kubwa iliyonayo katika vyombo vingine vinavyoundwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia tena tahadhari iliyoitoa wakati huo kwamba, masharti haya ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yana athari kubwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu yanakiuka Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano na hata Katiba ya sasa ya Zanzibar, na kama tulivyosema wakati huo, tafsiri hii mpya ya Makubaliano ya Muungano na ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inarudisha mezani mjadala juu ya muundo wa Muungano wetu na nafasi ya iliyokuwa Tanganyika katika Muungano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ilivyo kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, katika mazingira ambayo upande mmoja wa Muungano umejitangazia uhuru kama ambavyo tumeonyesha hapa, huu ni wakati muafaka kuanzishwa tena kwa Serikali ya Tanganyika. Katika mazingira ambayo upande mmoja wa Muungano siyo tu una Serikali kamili, Bunge kamili, Mahakama kamili, Wimbo wa

Taifa, Bendera ya Taifa, na sasa una nchi kamili yenye mipaka na eneo la bahari linalojulikana, una majeshi yake na Amiri Jeshi Mkuu wake, huu ni muda mzuri kwa Serikali ya Tanganyika kuzaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama haya, upande wa pili wa Muungano unatakiwa kuwa na vitu vyote hivyo pia, ili uweze kujadiliana na upande wa kwanza katika hali ya usawa. Huu ni wakati wa kurudishwa tena kwa Serikali ya Tanganyika kama ilivyopendekezwa na Tume ya Rais ya Chama Kimoja au Vyama vingi mwaka 1991 na Tume ya Kissanga mwaka 1998, na kama ilivyopendekezwa na Kundi la Wabunge 55 wa Bunge hili Tukufu na kuungwa mkono na Serikali ya Rais Ali Hassan Mwinyi kabla ya hoja hiyo kutunguliwa na Baba wa Taifa mwaka 1993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kura ya Maoni Juu ya Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inaielekeza Tume ya Katiba kuongozwa na misingi mikuu ya kitaifa ya kuhifadhi na kudumisha kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo, baada ya kujitokeza kwa wananchi wanaopinga kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano, Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba – Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba amesema kwamba wale wanaopinga Muungano nao wajitokeze kutoa maoni yao kwa Tume.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu, ni namna gani maoni ya wale wanaotaka kiini macho hiki cha Muungano kiishe yatashughulikiwa na Tume ambayo

imepewa jukumu kisheria la kukihifadhi na kukidumisha kiini macho hicho? Ni kipi kitakachoizuia Tume ya Warioba kupuuza maoni ya watu hao kwa hoja kwamba Sheria inaielekeza Tume kuratibu na kukusanya maoni na kutoa mapendekezo ya kuhifadhi na kudumisha Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miezi ya karibuni, kumejitokeza makundi ya wananchi, hasa kwa upande wa Zanzibar, ambayo yamedai kwamba iitishwe kura ya maoni ya wananchi ili kuamua kama bado kuna haja ya kuendelea na Muungano. Makundi haya, yakiongozwa na kundi la Uamsho, yameshambuliwa sana hadharani kwa kudaiwa kwamba yanataka kuvunja Muungano. Watu ambao wameongoza mashambulizi dhidi ya wana-Uamsho ni viongozi waandamizi wa CCM, wakiwemo Viongozi Wakuu Wastaafu wa Chama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, tulisema kwamba, hofu ya kuwaudhi Wazanzibari ndiyo imepelekea kimya kikuu ndani ya CCM na ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya ukiukwaji mkubwa wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano uliofanywa na Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, 2010.

Naomba nikiri kwamba tulikosea kusema hivyo. Tulichotakiwa kusema wakati ule, na tunachokisema sasa ni kwamba, kimya kikuu ndani ya CCM na ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya ukiukwaji mkubwa wa Makubaliano ya Muungano na Sheria ya

Muungano, pamoja na Katiba, kinatokana siyo tu na hofu ya kuwaudhi Wazanzibari, bali pia kinatokana na ukweli kwamba viongozi waandamizi wa CCM pamoja na wa Serikali yake walishiriki katika ukiukwaji huo. Wao ndio wanaoongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndio waliondaa Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, na wao ndio wanaoongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano waliokula kiapo cha kuihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, wao ndio walioiruhusu Zanzibar kutangaza uhuru kwa mabadiliko haya ya Katiba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa viongozi hawa na Chama chao kuibuka sasa na kuwatuhumu wana-Uamsho na makundi mengine kwamba wanataka kuvunja Muungano kwa kudai kura ya maoni ya wananchi wakati wao wenyewe wamekaa na kupitisha marekebisho ya Katiba ambayo tayari yamevunja Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba ya Muungano ni kilele cha juu cha unafiki wa kisiasa. Mashabiki hawa wa Muungano waeleze walikuwa wapi wakati Zanzibar inatangaza uhuru wake kwa kuchanachana Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba ya Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaodai kwamba wana-Uamsho wanataka kuvunja Muungano kwa sababu tu ya kudai kura ya maoni, tunaomba tuwakumbushe yafuatayo:-

Kwanza, kwa mujibu wa Baba wa Taifa katika kitabu chake cha "Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania" kinasema: "Huko nyuma baadhi ya viongozi wa Zanzibar Wapinzani wa Muungano wamewahi kudai tufanye *referendum* kwa Zanzibar kuhusu Muungano. Tukakataa kwa sababu safi kabisa." Hapa Mwalimu alikuwa anamzungumzia aliyekuwa Rais wa Zanzibar – Mheshimiwa Alhaj Aboud Jumbe, Waziri Kiongozi – Mheshimiwa Ramadhani Haji Faki na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar – Mheshimiwa Bashir Ebassuah Kwaw Swanzy waliong'olewa madarakani mwaka 1984 baada ya kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kitabu hicho hicho Mwalimu Nyerere anasema yafuatayo juu ya kilichotokea kwenye Bunge hili hili wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka 1993: "Tarehe 30 Julai, 1993 wakati wa Mkutano wa Bunge la Bajeti ukiendelea, zaidi ya Wabunge 50 kwa pamoja walitoa taarifa ya kusudio la kuwasilisha hoja Bungeni ambayo inadai (kwamba) kuendelea na mfumo huu wa Muungano usiowaridhisha wananchi wengi wa upande mmoja ni kuhatarisha kuendelea kudumu kwa Muungano. Hivyo basi, Wabunge hawa wanaliomba Bunge liazimie kwamba Serikali ilete Muswada Bungeni kabla ya Februari, 1994, kurekebisha katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kuwezesha uundaji wa 'Serikali ya Tanganyika' ndani ya Muungano. Tarehe 20 Agosti, 1993 wabunge wahusika waliwasilisha taarifa nyingine iliyokuwa inalitaka Bunge liazimie kwamba Serikali iandae kura ya maoni ambayo itafanyika kabla ya 31 Desemba, 1994 ili kupata maoni ya wananchi wa

Tanzania juu ya kuundwa kwa Serikali ya Tanganyika ndani ya Muundo wa Muungano.”

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya sasa ya Zanzibar ambayo mashabiki wa Muungano wameileta kwa kupitia Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba, tayari imewapa wananchi wa Zanzibar haki ya kuamua, kwa kura ya maoni, mambo mbalimbali yanayoihusu nchi hiyo na namna itakavyoongozwa. Mashabiki hawa wa Muungano wakubali kuvuna walichopanda, wasibeze wale wote wanaotaka kutumia haki ya kura ya maoni kuamua hatma ya Muungano na nafasi ya Zanzibar ndani au nje yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwa kuzingatia ushahidi huu kwamba, madai ya kuwa na kura ya maoni ya wananchi ili kuamua masuala makubwa yanayohusu Muungano wetu ni ya siku nyingi na yametolewa na watu na Taasisi mbalimbali. Madai haya hayajaanzishwa na wana-Uamsho wala CHADEMA. Ni wazi vilevile kwamba kura ya maoni inaruhusiwa kwa mujibu wa Katiba ya sasa ya Zanzibar. Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wale wote ambao wamedai, na wanaendelea kudai kuitishwa kura ya maoni ya wananchi ili waweze kuamua mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea na kiini macho cha Muungano wakati Serikali zote mbili na Chama Tawala cha CCM wanauvunja kivitendo, kutaipelekea nchi yetu kwenye njia ya Ethiopia na

Eritrea, au Sudan na Sudan Kusini au Yugoslavia ya zamani.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Watanzania waamue kwa kura ya maoni, kama bado wanataka kuendelea na Muungano na kama jibu lao ni ndiyo, ni muundo gani wa Muungano wanautaka? Kama, kwa busara zao wataamua kwamba nusu karne ya Muungano inatosha, basi itakuwa afadhali kwenda njia ya *Czechoslovakia* ya zamani kuliko kwenda njia ya Yugoslavia ya zamani, au Ethiopia na Eritrea au Sudan na Sudan Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania juu ya hatua, kama zipo, ilizozichukua kuzuia ukiukwaji huu wa Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba. Mwisho, Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kama kwa ukiukwaji huu wa Makubaliano ya Muungano, Sheria ya Muungano na Katiba ya Muungano, Bunge hili Tukufu litakuwa ndani ya mamlaka yake kuchukua hatua za kumshtaki Rais kwa mujibu wa ibara ya 46A ya Katiba kwa kushindwa kuihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba ya Muungano kama kiapo cha kazi yake kinavyomtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya Uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya maoni haya. Aidha, niwashukuru familia yangu, mke wangu mpenzi Alicia

Bosensera na mapacha wetu Agostino Lissu na Edward Bulali, kwa kuendelea kuvumilia upweke unaotokana na *Daddy* kuwa mbali muda mwingi kwa sababu ya majukumu mazito ya kibunge. Aidha, nawashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Singida Mashariki kwa imani na nguvu wanayonipa kila siku kwa kuendeleza msimamo wetu thabiti wa kukataa kunyanyaswa, kunyonywa na kupuuzwa na 'Ndaa ya *Njou'!*

Mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Ninawaomba waendelee kutuunga mkono na kututia nguvu katika siku ngumu na za majaribu makubwa zinazokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru wewe binafsi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## HOJA YA KUONGEZA MUDA

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lissu. Kwa mujibu wa Kanuni namba 28 (2) na Kanuni namba 62(a)(d) Bunge linapaswa kusitishwa katika muda wake wa saa 7.00 mchana, lakini tuna taarifa ya Msemaji wa Upinzani ambaye anapaswa kutumia dakika 30. Sasa namwomba Waziri wa Nchi atoe hoja ya kuongeza muda huo.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muungano, sasa tunatarajia kusikia hotuba nyingine ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Mazingira na kwa kuwa muda aliopewa ni dakika 30 na hautoshi, naomba Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Kanuni ya 28 ikubali hotuba ya Msemaji wa Upinzani mazingira, muda uongezwe hadi hotuba hiyo itakapokamilika. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuwa na Kuafikiwa*)

*(Hoja ya Kuongeza Muda kumruhusu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Makau wa Rais (Mazingira)*
*Kusoma Hotuba yake, ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kambi yetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka

wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(3) na (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumsifu, kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu na hekima tele kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania siku hadi siku. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Watumishi wa Mungu popote pale walipo ndani na nje ya nchi, kwa maombi yao yanayonifanya niendelee kuchapa kazi ya kulijenga Taifa. Naomba wasichoke kuniombea mtumishi mwenzao na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu mpenzi Victoria, kwa upendo na sala zao kwangu. Huko waliko naomba niwakumbushe tena kuwa thamani ya utu wetu hapa duniani haitatokana na kile tunachokichuma katika jamii, bali itatokana na kile tunachokitoa kwa jamii. Naisihi familia yangu iendelee kuniunga mkono wakati wote ninapokuwa mbali, nikishughulikia kero na matatizo ya wananchi wa Iringa Mjini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati na kwa unyenyekevu mkubwa, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kunielewa, kushirikiana nami na kuendelea kuniamini na hatimaye kuendelea kulijenga Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Niwashukuru sana kwa kunitia moyo, na hasa ninapokuwa nafanya ziara hapo Jimboni. Niwaombe wananchi wa Iringa kamwe tusiruhusu akili ndogo

kutawala akili kubwa katika Jimbo letu. Mungu awabariki, sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na pongezi zangu za dhati pia nazielekeza kwa viongozi wakuu wa CHADEMA kwa kukiongoza vyema chama chetu na kuwa tumaini pekee na la uhakika la Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kueleza yale yote ambayo Kambi ya Upinzani inaona ni muhimu kuyatoa, nitoe dira ya Taifa ya sekta nzima ya mazingira inayosema kuwa *"Tanzania yenye mazingira salama, yenye afya na endelevu."* Jambo muhimu la kujiuliza ni: Je, Serikali inaendana kivitendo na dira hii ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu na uchafuzi wa mazingira umesababisha mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa jumla huathiri mfumo mzima wa hali ya hewa. Matokeo ya kuathirika kwa mfumo wa hali ya hewa ni kuongezeka kwa joto duniani, viwango vya mvua kutokuwa na mpangilio jambo ambalo husababisha ukame na mafuriko na hivyo kuathiri maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu duniani na kwa maana hiyo kuongezeka kwa shughuli za binadamu na hivyo kusababisha uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa. Mabadiliko ya tabianchi duniani, ambayo kwa ujumla yamesababisha ongezeko la joto, kupungua kwa viwango vya mvua, yameathiri sana ubora wa ardhi, upatikanaji wa maji safi na salama, upatikanaji wa

chakula kwa wanyama na binadamu na hivyo kusababisha vifo kwa viumbe hai ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko hayo ya tabianchi yamesababisha kina cha bahari kupanda kwa sentimeta 17 juu ya usawa wa bahari kwa kipindi cha miaka 100 iliyopita, joto la dunia kuongezeka kwa nyuzi joto 0.74 *centigrade* kwa kipindi cha miaka 50 iliyopita, pia gesi ya joto aina ya *carbon dioxide* limeongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 katika kukabiliana na tabianchi, Serikali iliandaa mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na miradi miwili iliyotekelezwa ni mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta za kilimo, maji, afya, wanyamapori, misitu, mifugo, ardhi na mpango wa kupunguza uzalishaji wa ukaa itokanayo na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunataka kupata taarifa za kina kuhusiana na utekelezaji wa miradi hii na hatua ambazo zimeweza kufikiwa mpaka sasa katika kukabiliana na hali hii nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba bila mazingira rafiki, maisha ya binadamu hayana nafasi hapa duniani. Mazingira ndiyo msingi wa shughuli zote anazofanya binadamu katika kutegemeza maisha yake. Hali kadhalika, mazingira ni nyenzo ya msingi kabisa katika kujenga uchumi wa Taifa. Hivyo, ili binadamu aweze kuishi duniani na kujishughulisha na

kazi mbalimbali za kutegemeza maisha yake na kujenga uchumi wa Taifa lake, ni lazima mazingira yalindwe ili yaweze kukidhi mahitaji ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi majuzi tu ulimwengu mzima ulikuwa kwenye Mkutano ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa uliokuwa ukijadili masuala mbalimbali kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi ambao ulifanyika nchini Brazili na kupewa jina la *RIO +20.* Mkutano huu ulikuwa na maazimio mbalimbali juu ya mbinu na mikakati ya kukabiliana na hali hii na Serikali yetu iliweza kuwakilishwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mawaziri wa Mazingira Muungano na kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa mwaka huu ulijadili kuhusu maazimio ya mwaka 1992 na namna yalivyotekelezwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa wapatao 182. Sambamba na hilo, Mkutano huu ulipitisha maamuzi mapya kuhusu kuiweka dunia na mazingira yake katika hali ya usalama ili yaweze kusaidia vizazi vya sasa bila kuathiri haki ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mkutano huu lilikuwa ni pamoja na ufanisi wa nishati na mchango maradufu wa nishati mbadala kwa wote ifikapo mwaka 2030. Zaidi ya mashirika 50 ya Serikali kutoka Afrika, Asia, Amerika Kusini na mataifa ya visiwa vidogo yalikubaliana kutilia mkazo jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya azimio kuu la Mkutano huo, lilikuwa ni kuanzishwa kwa mfuko

utakaowezesha kuharakisha upatikanaji wa nishati, usalama wa chakula, maji na usafiri endelevu kwa nchi mbalimbali hususan zile maskini. Katika Mkutano huo, zilitolewa taarifa kuwa kiasi cha Dola bilioni tano na ahadi ya dola zaidi ya bilioni 700 zilitolewa kwa ajili ya kuufadhili mfuko huu.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuhusiana na mambo yafuatayo ili kuondokana na tabia ya nchi yetu ya muda mrefu ya kuhudhuria Mikutano na Makongamano mbalimbali, lakini hakuna utekelezaji wa maazimio husika:-

(i) Je, tumejiandaa vipi kama Taifa ili kuweza kunufaika na fedha za mfuko huu? Tumeweka mpangomkakati gani?

(ii) Je, tunajiandaa vipi kuweza kulitekeleza kwa vitendo azimio la kupata na kutumia nishati mbadala, upatikanaji na usalama wa chakula, maji na usafiri endelevu nchini mwetu?

(iii) Je, bajeti yetu ya mwaka huu wa 2012/2013 imezingatia azimio hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mabadiliko haya ya tabianchi yanasababishwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira unaosababishwa na uzalishaji mkubwa wa gesi ukaa kutoka katika viwanda vikubwa katika nchi zilizoendelea kiviwanda, na uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira unaofanywa katika nchi zinazoendelea kwa kukata miti hovyo, uchimbaji

wa madini usiojali mazingira, utupaji wa taka hovyo hasa katika Miji na kadhalika, na kwa kuwa athari za uharibifu na uchafuzi huu wa mazingira unaifanya dunia isiwe mahali pazuri pa kuishi, ni dhahiri kwamba kunahitajika jitihada za kitaifa na kimataifa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nchi yetu kutambua umuhimu wa mazingira na hivyo kuunda Wizara mahsusi ya Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, na kutunga Sera ya Mazingira ya Mwaka 1998 na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu utunzaji wa Mazingira, mfano Agenda 21, bado nchi yetu ina tatizo kubwa la uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaelekea kuwa jangwa kutokana na ukataji miti hovyo bila kupanda mingine, miji yetu imezidi kuwa michafu jambo ambalo ni hatarishi kwa afya za wananchi wetu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini tuipatie fedha Wizara hii ya Mazingira wakati mazingira yanaendelea kuharibiwa na kuchafuliwa kila kukicha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji miti na uchomaji wa misitu Tanzania umeendelea kwa kiwango kikubwa sana. Maeneo yaliyoathirika kwa kiwango kikubwa ni yaliyoko katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Pwani, Mwanza, Mara na Tabora. Sababu kubwa za uchomaji huu wa misitu ni kwa ajili ya shughuli za kilimo, kutafuta nishati hasa mkaa na kuni kwa matumizi ya kupikia na upasuaji wa mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi uliofanyika kuhusiana na utendaji wa kifedha na matumizi ya fedha za Usimamizi wa Misitu *(PFM)* kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 umebaini kuwa kulikuwa na fedha za mradi kiasi cha Sh. 178,826,876 katika Halmashauri 11 ambazo hazikutumika hadi mwisho wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kama fedha za usimamizi hazikutumika, ni kwa vipi Wilaya tajwa zilifanya kazi ya usimamizi wa misitu wakati fedha hazikutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana au kutokutolewa kwa fedha za usimamizi, ndiyo sababu kubwa ya kuongezeka kwa ukataji wa misitu na uchomaji mkaa. Aidha, umekuwa ni muda mrefu sana kwa uharibifu wa mazingira katika msitu wa Shengena uliopo Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro ambapo yupo mwekezaji ambaye ameingia kwenye makubaliano na Halmashauri ya Kijiji cha Marieni, Kata ya Chome kuhusu uchimbaji wa udongo wa *Bauxite* ambao umekuwa ukisafirishwa kwenda nchi ya jirani ya Kenya. Suala hili bado lipo na linaendelea na limesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kusababisha ukame katika vijiji vya jirani vya Bwambo, Tae, Malindi, Gonjanza na Kata ya Chome kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dalili zote za nchi hii kugeuka kuwa jangwa hasa baada ya Serikali hii ya CCM kupandisha ushuru wa mafuta ya taa ili kukabiliana na tatizo la uchakachuaji wa mafuta ya dizeli. Hii ina maana wananchi watashindwa kumudu

bei ya mafuta ya taa kama nishati mbadala na hivyo watageukia miti na misitu kujipatia nishati hiyo. Hii ina maana Serikali ya CCM inavyoendelea kututawala, ndiyo jinsi ambavyo nchi yetu inaendelea kuwa jangwa. Kambi ya Upinzani inapinga utawala wa namna hii na tunatoa wito kwa wananchi pia kukataa kuongozwa na Serikali inayowaelekeza jangwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli uliowazi kuwa kutokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya aina mbalimbali hapa nchini...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa Samahani kaa kwanza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya anayoyasema Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa anajua nilishamwandikia kwamba, akisema nitampinga. Serikali ya CCM haitungi kodi, Serikali ya CCM haitengenezi *Finance Bill,* kodi ya mafuta na kodi zote zinatungwa na Bunge hili kupitia *Finance Bill.* Kwa hiyo, nilitaka tu arekebishe hapo, na akiri kwamba jambo hili limefanywa ndani ya Bunge kwa kupitisha *Finance Bill* na siyo Serikali ya CCM ndiyo imepandisha bei ya mafuta na yeye akiwepo. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni za Bunge ninazozifahamu kama kuna kosa limefanyika, Mbunge aliyeona anatakiwa aseme

utaratibu na aseme ni Kanuni ipi imekiukwa. Haya mambo ya kienyeji hayafai.

**MWENYEKITI:** Nimewasikia wote wawili, ninaomba Mheshimiwa Msigwa uendelee.

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, lakini kwa kifupi *Bill* hii imeletwa na Serikali ya CCM. Ni ukweli uliowazi kuwa kutokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya aina mbalimbali hapa nchini mwetu zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazingira yetu na hii imethibitishwa na ripoti mbalimbali za kiutafiti zilizotolewa kuhusiana na mahusiano yaliyopo baina ya uchimbaji wa madini na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sana madhara makubwa zaidi husababishwa na shughuli za uchimbaji unaofanywa na makampuni makubwa na yenye zana za kisasa, ikilinganishwa na kiwango kinachofanywa na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti mbalimbali zimeonyesha kuwa wananchi pamoja na viumbe mbalimbali waishio karibu na migodi mikubwa ya uchimbaji wa madini nchini mwetu zimeonyesha kuwa wananchi na viumbe wamekuwa wakiathirika sana, mathalan mgodi wa *Barrick North* Mara, *Geita Gold Mine* na migodi mingine mikubwa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya athari ya mazingira katika migodi mikubwa imekuwa ikifanywa baada ya miradi kuidhinishwa badala ya miradi kufanywa kabla. Hivyo tathmini hizi hazisaidii kudhibiti athari za mazingira kwa kuwa tathmini haziathiri usanifu miradi. Miradi kama Geita Mine na *North Mara* imegeuka kuwa majanga ya kimazingira kwa sababu hii. Kambi ya Upinzani inasikitishwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira uliofanyika katika Migodi ya Dhahabu ya Geita na *North-Mara* ambao umeleta athari kubwa sana za kiafya kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti wa *Manfred Felician Bitala (2008)* na tafiti zilizofanywa chini ya ufadhili wa *Norwegian University of Life Scieces* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2009) na Utafiti uliofanywa na Idara ya Biolojia, Chuo Kikuu cha *Oslo (2011)* kuhusu Uchafuzi wa Mazingira Geita na *North Mara* ni kwamba kuna kiasi kikubwa sana cha kemikali-sumu (kwa mfano *"cyanide"*) madini ya zebaki *(Mercury)* na madini chuma yenye sumu *(heavy metals)* katika maji na udongo katika maeneo ya makazi ya wananchi wa maeneo yaliyozungukwa na migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa matokeo ya tafiti hizi ni kwamba wananchi wa maeneo hayo wameathirika vibaya na kemikali hizi zenye sumu kwa viwango vya juu sana kuliko athari za wastani za waathirika katika nchi nyingine zenye tatizo kama hilo. Aidha, hata mifugo ya wananchi hawa imeathirika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iingilie kati na kunusuru maisha ya wananchi wa maeneo hayo ya migodi. Aidha Kambi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali ina taarifa ya tafiti hizi na imechukua hatua gani hadi sasa kudhibiti uchimbaji wa madini ambao siyo rafiki kwa mazingira? Kadhalika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa fidia kwa watu wote walioathirika na uchafuzi huo wa vyanzo vya maji wanayotumia utafanyika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na hali hii ndiyo maana tunakubaliana na tamko la Kamati ya Viongozi wa Dini na Asasi za Kiraia lijulikanalo kama tamko la Ngurdoto la tarehe 20 Oktoba, 2011 na tunaitaka Serikali kuwa tayari kufanya haya yafuatayo:-

(i) Ni muhimu utafiti na taarifa za madhara kwa mazingira na jamii kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini ziwe zinaandaliwa na taasisi au wataalamu wanaoaminika na kuheshimika ambao wako huru kufanya kazi zao bila kuingiliwa na Serikali na wawekezaji binafsi. Utafiti huo ufanywe mara kwa mara wakati shughuli za uchimbaji zinaendelea na baada ya shughuli hizo kusitishwa;

(ii) Ni dhahiri kuwa uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji wa madini utaathiri pia vizazi vijavyo, na unaweza kuzisababishia jamii hizo kuishi maisha ya dhiki na mashaka. Kutokana na hilo, ni lazima kufanya utafiti kuhusu madhara yote ambayo yanaweza kutokea siku zijazo kutokana na shughuli za

uchimbaji wa madini na kuhakikisha kunakuwa na njia za kuwafidia ipasavyo watu wote watakaoathirika;

(iii) Jamii zinazoishi karibu na migodi ya madini, pamoja na wale ambao wameondolewa kwenye maeneo yao ya asili kupisha uchimbaji madini, mara nyingi wamekuwa wakisahaulika na kuna haja ya kuhakikisha kuwa nao wanafaidika na shughuli hizi kwa kuwezeshwa katika kujenga maisha yao na hasa kutokana na uharibifu wa mazingira uliofanywa;

(iv) Uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za uchimbaji madini, unaathiri sana jamii katika maeneo ya uchimbaji na nchi nzima kwa jumla, lakini jukumu la kurekebisha mazingira haya linaachwa kwa Serikali na siyo kwa wachimbaji. Kampuni za Uchimbaji Madini zinapaswa kuwa na jukumu la kurekebisha na kutengeneza mazingira bora baada ya kukamilika kwa shughuli zao;

(v) Serikali itoe ufafanuzi wa kina na wa kueleweka katika suala la fidia, kwa kuainisha kiwango mahsusi cha fidia kwa watu na jamii ambazo zimeathirika na sumu zinazotokana na shughuli za uchimbaji wa madini na uharibifu wa mazingira yao; na

(vi) Serikali ihakikishe kuwa ni lazima jamii zipewe taarifa muhimu na kuwezeshwa kushiriki kwenye shughuli za uchimbaji wa madini na kuwa suala hilo liwekwe kwenye sheria na siyo hiari kutokana na matakwa ya makampuni au Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kugunduliwa kwa madini ya *urani* katika nchi yetu ni habari njema kwa kuwa madini haya yatakuwa na mchango mkubwa katika uchumi wetu. Kwa kuwa madini haya yanahitaji uangalifu mkubwa, kwa sababu ya kuwa na asili ya sumu, Serikali imejiandaa vipi kisera, kisheria na kiutaratibu kuhakikisha kuwa uchimbaji wa madini hayo hauathiri mazingira na afya za wananchi na wanyama katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kujiandaa vyema katika suala hili la madini ya urani na gesi mapema kabla ya kuingia mikataba na wachimbaji ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima hasa pale wananchi na mazingira kwa ujumla watakapoathirika na uchimbaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, pamoja na mikakati mingine, una mkakati mahsusi wa kuboresha muindombinu ya usafi katika maeneo ya Mijini na Vijijini. Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo mwaka huu wa fedha zilipaswa kutengwa kiasi cha Shilingi billioni 7.620 kwa ajili ya Kampeni ya Taifa ya Mazingira safi na kusafisha shule. Cha kushangaza ni kuwa, ukisoma taarifa ya Waziri kuhusiana na Idara ya Mazingira, malengo ya mwaka 2012/2013 (ukurasa wa 41) hakuna kipengele hata kimoja ambacho kimelenga kutekeleza malengo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kuwa hakuna fedha iliyoombwa kutekeleza Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo. Kama Serikali inajiwekea Mpango wake wa Maendeleo, halafu Serikali hiyo hiyo inashindwa kutekeleza Mpango wake yenyewe, Kambi ya Upinzani na wananchi wenye kupenda maendeleo, tunapata wasiwasi na uwezo wa Serikali hii ya CCM kuendelea kuongoza nchi yetu, kwani hata mipango inayojiwekea yenyewe inashindikana kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha ni Shilingi bilioni 7.07, na kati ya hizo, fedha za ndani ni kiasi cha Shilingi bilioni 1.3 tu (randama – ukurasa wa 46) na nyingine tunategemea kuzipata kutoka nje, na miradi ambayo inakwenda kutekelezwa ni miradi namba 5306, 6569, 6571, 5301, 5302, 5305 na 6504. Kati ya miradi yote hii, hakuna hata mmoja unaohusiana na kuboresha miundombinu ya usafi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaiasa Serikali kutofanya mzaha na Mpango wa Maendeleo ambao una maslahi kwa wananchi. Kitendo cha kutotenga fedha kuboresha miundombinu ya usafi Mijini na Vijijini kama Mpango ulivyoelekeza na kutozingatia vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo, ni dharau na dhihaka kwa wananchi, kwani suala la mazingira ni suala la afya. Mtu anayekaa katika mazingira machafu anawezaje kuwa na afya bora na kufanya kazi ili alipe kodi kwa Serikali? Serikali sasa iwekeze katika usafi wa mazingira ili

ikusanye kodi katika mazingira safi vilevile. Serikali isilenge tu kukusanya isikowekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Bajeti lililopita, Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira ilitoa maagizo mbalimbali na kati ya maagizo hayo, yapo ambayo hayajatekelezwa na Serikali mpaka wakati huu. Mojawapo ya maagizo hayo ni *Agizo Na. 4 ambalo linasema:* "Serikali itenge fedha za kutosha Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ili kuwezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira." lla uhalisia ni kuwa fedha zilizotengwa ni kidogo sana na hii inaonyesha kuwa pamoja na Serikali kutokuthamini mazingira, pia haitekelezi maagizo na maazimio mbalimbali ya Bunge. (Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais – ukurasa wa 26)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine ni Agizo Na. 5 ambalo lilisema: "Serikali ihakikishe kwamba fidia zote stahiki kwa wananchi wanaozunguka mgodi wa dhahabu wa *North Mara* zinalipwa na ahadi zilizotolewa na mwekezaji wa mgodi kwa jamii ya eneo husika zinatekelezwa." Taarifa ya Serikali ya Januari – Mei, 2012 inasema kuwa, jumla ya wananchi 474 wamelipwa jumla ya Sh. 22,387,234,156/= ikiwa ni fidia zao kwa maeneo yaliyopo ndani ya mita 200 kutoka kwenye mgodi. Hii ni kwa mujibu wa taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 (Randama – ukurasa wa 26).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi za Serikali siyo sahihi, kwani kwa wastani ni kuwa kila mwananchi

amelipwa kiasi cha Sh. 47,230,451/=. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kwa kina, ni lini fedha hizi zililipwa na zililipwa kwa kutumia utaratibu gani? Ni vigezo gani vilitumika katika kuwateua wananchi waliopaswa kulipwa fidia hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la mwezi Februari, 2012 siku ya tarehe 03/02/2012 wakati Naibu Waziri wa Nishati na Madini – Mheshimia Adam Malima akijibu swali Na. 48 la Mheshimiwa Esther Matiko kuhusiana na fidia kwa wananchi hawa, alisema: naomba kunukuu *Hansard;* "Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanyika tathmini kwa kaya zinazozunguka mgodi, kumejitokeza matatizo mbalimbali; mfano, kaya tano hazijaridhia kufanyika kwa tathmini hiyo ya fidia. Majadiliano yanaendelea kwa kushirikisha Kijiji cha Nyangoto. Familia 40 ziliamua kurudi katika maeneo waliyokwishalipwa na kwa sasa wanadai fidia upya. Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kulipa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha shughuli za mgodi wa North Mara linasimamiwa na Serikali katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, tunataka maelezo ya kina juu ya taarifa hizi, na kukinzana kwa taarifa za Serikali na zile za wananchi kuhusiana na ulipaji wa fidia kwa wananchi. Tuchukue jibu lipi? Lililopo kwenye *Hansard,* la wananchi, au la Waziri mwenye dhamana ya Mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia hizi zililipwa kwa ajili ya uchafuzi wa mazingira uliofanywa na mgodi wa

*North Mara* kwa wananchi hawa au ni fidia ya aina gani hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo hiyo ya Serikali inasema kuwa visima vya maji 16 vimechimbwa katika vijiji vya Kewanja, Nyamwaga, Nyakunguru, Genkuru, Kerende, Matongo na Nyangoto na kuwa kati ya visima hivyo ni visima 14 ndiyo vinatoa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni kuwa, mwekezaji kwenye mgodi wa *North* Mara ameweka utaratibu wa kusambaza maji kwa wananchi kwa kutumia magari. Kambi ya Upinzani inajiuliza, kama visima vimechimbwa na vinatoa maji, ni kwa nini magari yatumike kusambaza maji, tena kwa ratiba maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutunza na kulinda mazingira yetu, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali haijaweka suala la kutunza na kulinda mazingira katika vipaumbele vyake, jambo ambalo ni hatari kwa mifumo ya ikologia na maisha ya binadamu na viumbe hai vingine kwa ujumla. Hili ni janga kubwa na Serikali inapaswa kuzinduka sasa na kuchukua hatua za kukabiliana na janga hili. Kama kawaida, Kambi ya Upinzani tunawapa Serikali bila choyo mbinu za kufanya kukabiliana na tatizo kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihimize na ijenge mazingira wezeshi ya kutumia nishati mbadala na hasa kwa kutumia vyanzo vya upepo, jua na umeme vijijini na hii itasaidia kuokoa miti mingi ambayo hutumika kwa ajili ya nishati, na Serikali igharimie uwepo na upatikanaji wa nishati

hizo. Hii inatokana na ukweli kuwa ni asilimia 14 tu ya Watanzania ndio wameunganishwa kwenye umeme wa gridi ya Taifa;

(ii) Gharama za vifaa vya ujenzi ipunguzwe, na hii ni kwa vifaa kama sementi ili wananchi waweze kujenga nyumba kwa kutumia tofali badala ya kutumia miti. Hii itaokoa asilimia kubwa ya miti ambayo hutumika kwa ajili ya ujenzi;

(iii) Itolewe elimu ya kina katika kupanda miti na kutunza miti pamoja na misitu iliyopo, kwani hali hii isipochukuliwa hatua madhubuti sehemu kubwa ya Taifa itageuka jangwa. Ukame uliokithiri maeneo mbalimbali ya nchi ni kiashiria cha unyemelezi wa jangwa;

(iv) Mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari ibadilishwe na iweke msisitizo katika umuhimu wa kupanda miti na kutunza miti. Hili litasaidia katika kizazi kinachokuja kujua umuhimu huu wa miti katika maisha yao na maisha ya vizazi vijavyo;....

*(Hapa Kengele ya Kwanza ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji umekaribia kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda umekwisha, ninakushukuru.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Ni kengele ya kwanza hii!

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** *No*, kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Nakuomba radhi, endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Ni ya kwanza, tena umenipotezea dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Endelea tafadhali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante**

(v) Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata kote nchini, moja ya majukumu yao liwe ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapanda miti na hiki kiwe ni kipimo kimojawapo katika kupima utendaji kazi wa viongozi hawa;

(vi) Kila Halmashauri nchini itenge fedha kwa ajili ya kununua miche ya miti na kuigawa bure kwa wananchi kila kipindi cha masika kwenye maeneo husika na Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata wagawe miche hiyo kwa kila kaya na kila mwananchi apande miche hiyo; na

(vii) Usafi mijini uwe ndio kipimo cha utendaji wa Mameya wa Miji na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa na kwa umuhimu, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa James Lembeli pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano katika kutetea maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuru Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji ninakushukuru sana kwa taarifa yako. Tumeamaliza shughuli za muda huu, na kabla ya kusitisha shughuli za Bunge, naomba nizungumzie miongozo miwili niliyoombwa na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola kuhusu Bunge kujadili Mgomo wa Madaktari, lakini kama maelezo yaliyotolewa jana na Mheshimiwa Mhagama (Mwenyekiti) ni kwamba suala hili lilishatolewa maelezo na Mheshimiwa Spika. Sasa mimi kama Mwenyekiti, kwenda kinyume na maagizo ya Bosi wangu na kwa kuzingatia mihimili hii mitatu, ninaomba tukubaliane kuwa suala hili tuliache kwa kuzingatia kwamba Mahakama bado haijatoa *rulling* na tutalizungumza baada ya Mahakama kutoa *Rulling* yake.

Waheshimiwa Wabunge, lakini mwongozo wa pili niliombwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, mwongozo wangu ni kwamba *programme* ya kuleta mabadiliko katika Utumishi wa Umma, *programme* ya pili, mfumo wa kutekeleza mradi huu ni ule wa *supply driven* ambapo fedha zote hutengwa chini ya Fungu 32 ambapo kila eneo la utekelezaji, yaani *key remark areas* hutengewa fedha za maendeleo. Kutokana na hali hii, mafunzo ya kujenga uwezo kwa kila eneo hutengwa chini ya Idara husika, hivyo Watendaji wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma watapatiwa mafunzo chini ya *sub vote* (Fungu) 3001 kasma D12S01.

Baada ya kuelezea hili, naomba niwataje ambao watachangia tutaporejea saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu na wengine watatajwa kadri tutakavyokuwa tunaendelea.

Sasa nasitisha shughuli hizi mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.10 Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji wa leo jioni, na kama Mheshimiwa Sylivester Masele Mabumba alivyosema, kabla hajasitisha shughuli za Bunge, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na wengine watafuatia. Naomba niseme tutakuwa na wachangiaji wachache sana kwa sababu hoja hii itabidi tuihitimishe leo.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii leo katika Wizara hii, Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwanza kwa kuwapongeza sana wanawake na watoto wa kike wa Tanzania, kwa sababu tunapozungumza masuala ya mazingira akina mama wamekuwa ni wahanga. Hivyo, nawapongeza kwa sababu wamejitahidi sana kutunza mazingira yetu nchini na hata leo tunaweza tukazungumza wakati mazingira bado yanatia moyo. Kwa hiyo, nawapongeza wanawake wote nchini nikiwa kama Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Njombe, lakini pia nawapongeza sana akina mama wa Wilaya ya Makete Njombe na Ludewa kwa kazi nzuri ya kutunza mazingira pamoja na changamoto zilizopo.

Vile vile nawapongeza dada zangu wote wawili, Mheshimiwa Samia na Mheshimiwa Huvisa na Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Lakini leo naomba ni-*declare* kwamba leo nitakuwa *critic* kwa maslahi ya

Watanzania. Lakini na-*criticise* mfumo, wawe wanachapa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutunza mazingira ni jambo muhimu, tusipoyatunza mazingira, mazingira hayatatutunza. Lakini suala hili tumekuwa tukilipigia kelele na sheria nyingi za kimataifa tumezisaini, *Kyoto Convention* na nyingine nyingi, lakini bado baada ya kuridhia katika Bunge lako Tukufu, hatujazifanya kuwa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu, ukisharidhia mikataba ya kimataifa, haziwi sheria *automatically*, ni lazima tufanye kitu kinaitwa ku-*domesticate*. Kwa hiyo, wakati wa kujibu ningependa kujua ni mikataba mingapi ya kimataifa ambayo tumeiridhia katika nchi yetu. Lakini vile vile suala hili la mazingira bado halimo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakwenda kujadili juu ya Katiba mpya, naomba sana suala la mazingira liingie, liwe ni moja ya *articles* kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba za nchi nyingine mfano Ethipia na India masuala ya mazingira yamo. Unaposema haki za binadamu, lakini mazingira yenyewe hayamlindi na kumtunza huyu mwanadamu, inakuwa ni changamoto. Pia naomba kieleweke kwamba liwe ni jambo ambalo ni la mtambuka *(cross cutting)*, maana ndani ya mazingira kuna maji, kuna ardhi, kuna kilimo na miundombinu; tusipoyatunza haya mazingira changamoto zote hizo zitakuja kwetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa mfano imefika wakati maji yanauzwa. Lakini kuna nchi nyingine maji yanakuwa salama watu wanaweza kunywa, watoto wetu waliopo mashuleni *boarding school* na vyuoni wataweza kununua maji? Nimeshuhudia wanafunzi kwa mfano wa Mzumbe na vyuo vingine wananunua maji chupa moja Sh. 700/= hadi Sh. 1,000/= kwa sababu siyo salama, wakinywa maji ya kawaida wanaweza wakapata magonjwa.

Nimeangalia takwimu kwenye mtandao, zaidi ya watu milioni 12 wanakufa duniani kutokana na kutumia maji yasiyo salama na wengi wao wapo nchi zinazoendelea. Lakini changamoto ya maji imekuwa ni kubwa sana, hata vijijini, Shule ya Sekondari kwa mfano, Sekondari ya Manda haina maji; hivi hao watoto wanaishije? Haya mazingira tunayosema, ni mazingira bila maji salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine, ukienda hata *Airport* unakunywa tu maji ukiwa na kiu. Lakini leo Shule za Misingi hazina maji, watoto wanatembea kwenda shuleni, *no water,* wanarudi Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapojenga shule tukubaliane kwamba ramani za shule ziwe na ramani ya *solar* na visima vya maji, maji taka ya kumwagilia, na pia maji ya kunywa. Ni lazima tuwe na mifumo hata haya maji ya kawaida itengenezwe, wanafunzi wanywe maji.

Juzi tulikuwa tuna semina, wanasema hata kutokuelewa kwa wanafunzi, tunasema watoto wanamaliza Darasa la Saba wengine hawajui kusoma na kuandika, lishe nayo inachangia. Hasa mtoto anatembea kilomita, hajanywa maji, hajala kitu, jamani sasa hata huo uelewa unakuwaje? Ndiyo maana leo nimesema nitakuwa *critic* najadili mfumo. Miaka 50 baada ya uhuru ni lazima turekebishe mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kwa Shule za Sekondari ziwe na michoro ya maji. Watoto watakunywa wapi maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyoo imekuwa ni jambo ambalo tunaliacha tu, zaidi ya mara tatu nimezungumza kwenye bajeti humu ndani, mabasi tunakwenda kuchimba dawa rasmi kabisa, basi linasimama tukachimbe dawa barabarani; kweli Watanzania miaka 50 baadaye! Tunasema kuna *Public Private Partinaship (PPP),* si tutangaze watu wapewe tu eneo wajenge ndiyo *PPP* tuweke mazingira? Kwa kweli hii Wizara ina mambo mazito sana Dada yangu Dkt. Terezya anafanya kazi halali, ningeomba, maana Kamati yangu ya Katiba na Sheria ndiyo inayoshauri Ofisi ya Rais, Naibu Waziri tuliyekuwanaye, Muungano apewe *extended Jurisdiction* ili afanye na kazi za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Naibu Waziri mmoja chini ya Muungano apewe *Extended Jurisdiction,* hii Wizara ni kubwa na nyeti. Ikinyesha mvua Dar es Salaam kutokana na mazingira ya miundombinu ni

maafa. Kweli Watanzania, *are we serious*? Ni lazima ifike wakati tubadilike. Watu tunawahamisha mpaka Mabwepande, yanakuja masuala ya fidia, yote haya ni mazingira. Tunawaambia Watanzania msikate miti kwa ajili ya mkaa, lakini sisi ndiyo tunaotumia. Miti tunatumia wenyewe, madawati hakuna, mkaa tunatumia wenyewe majumbani, mbao tunahitaji za kuezekea, lakini tunasema usikate miti. Wapi tumeweka eneo mbadala kwenye Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika majibu, ningependa kujua mkakati wa kutunza eneo la Mtera. Umeme tunategemea *hydroelectric*, lakini tumeacha vyanzo vinaharibiwa, kule kwetu wanaambiwa wasilime maeneo ya vinyungu, kilimo cha *irrigation* hakionekani, inafika wakati tunaagiza sukari na mchele Watanzania, kweli! Mwisho tutaagiza na mahindi!

*(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji unakaribia kwisha)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba maeneo hayo yazingatiwe. ni kengele ya pili au ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya kwanza.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Kama ni kengele ya kwanza, bado nilikuwa na *point* nyingi tu. Kama ya kwanza, basi naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana miundombinu hiyo izingatiwe suala la mazingira ni

nyeti sana, kama nilivyosema liwe ni suala *cross cutting,* kila eneo tukizungumza kilimo, mazingira, ardhi, ujenzi, vyote ni mazingira. Kuna Wakandarasi wanajenga barabara maeneo mengi tu, eneo la Mtera hapo wanajenga, wakiondoka ni uharibifu wa mazingira kwenda mbele. Hawachangii kwenye Kijiji miti waliyoikata, maji waliyotumia, uharibifu wa mazingira hawachangii hata senti! Serikali ya Kijiji leo zinalalamika hakuna michango.

Kwa hiyo, wale Wakandarasi wote ni lazima wakajitambulishe, Serikali ya Kijiji ni lazima wawashirikishe wananchi wapewe maeneo kwamba ninyi mkitaka miti, mkate eneo hili, *recycling policy* iko wapi mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Maafisa, safari za Mikoani ziongezeke na Vijijini kama zile za *Rio*. Mwende vijijini, tusipande miti kwa mwaka mara moja, tarehe 1 Desemba, tupande miti ya kutosha, mikakati *Carbon Credit*. Mimi sijawaona watu wa *Carbon Credit* Wilaya ya Ludewa, Makete na Njombe. Tunaambiwa kuna mradi wa *Carbon Credit,* hebu hivi vitu viwe *transparent*. Hii mifumo, Mawaziri wanafanya kazi kubwa sana, lakini mimi najadili mfumo, utaratibu wa *PPP* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Halmashauri pia naomba sana iwe ni maelekezo ya Wizara, watenge maeneo wapi wananchi watakata kuni na mkaa. Lakini tunawaambia watu msichimbe kokoto, mchanga, eneo fulani wakati *construction industry* inaendelea kila siku. Jamani, hawa watakwenda usiku

wa manane wakachukue michanga na kokoto, mkija asubuhi tutaachwa mabonde. Kwa hiyo, tutenge eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii. Nawapongeza Mawaziri wote wawili wanamama. Lakini niseme awali kwamba sitaunga mkono hotuba hii kwa sababu ambazo nitazieleza baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kusema kwamba matatizo ya Muungano ni mengi sana. Tangu naingia katika Bunge hili tumekuwa tukiwaelekeza Mawaziri na Serikali hii namna ya kuondoa tatizo la Muungano, hata baadhi ya Tume zimeundwa kama Tume ya Shellukindo, lakini cha kushangaza ni kwamba hadi leo zile keo za msingi bado zipo pale pale, na ndiyo maana yanazuka makundi ya kijamii ambayo yanadai haki na wengine wanafikia hadi kusema hawataki Muungano. Lakini wa kulaumiwa ni ninyi viongozi wa Chama na Serikali, kwa sababu itakuwaje Serikali ya Zanzibar inayoongozwa na CCM na Serikali ya Muungano inaongozwa na CCM lakini miaka 48 hakuna utatuzi wa matatizo ya msingi. Kwa hiyo, hili

jambo lipo katika mikono yenu na mmeliachia limefika hapa na wengine wanayo haki ya kudai haki zao kwa sababu Serikali inaonyesha haina nia ya kutatua matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea suala la Muungano kwanza, nikipata muda nitakuja kwenye suala la Mazingira. Nianze na chenji ya Rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitofautiane na rafiki yangu Mheshimiwa Pinda kwamba Zanzibar hawana haki ya kudai chenji ya rada kwa sababu rada imenunuliwa na Serikali na Wizara ya Mawasiliano. Hapa ndipo ninapotofautiana na rafiki yangu Mheshimiwa Wasira. Katika mambo ya neema, mambo ya manufaa mbona mnatuweka kando?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano huu wa gesi asilia ambao ni wa Muungano, hivi karibuni nimesikia kwamba Serikali imegundua gesi nyingi sana ambayo inafikia *trillion cubic feet* 25 hadi 28. Nimeanza kusikia kwamba wanaanza kuzungumzia suala la kuboresha kilimo Tanzania Bara kujenga miundombinu, sijasikia watafanyeje kwa Zanzibar ambayo ina matatizo makubwa ya umeme. Sasa haya mambo ni kero, kwa sababu mkipata jambo zuri, ni lazima mfikirie wenzenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba, nyongeza ya kwanza ibara ya 11 na Ibara ya 17 inaeleza wazi wazi kwamba rada ni jambo la Muungano. Lakini kama hiyo haitoshi, ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 135 (1)

inasema, fedha zote zitokanazo kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Muungano ni za Muungano. Sasa mtasemaje kwamba rada haituhusu na hii Katiba mnataka kuivunja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimefarijika sana na Waziri wa Fedha wa Zanzibar wakati akitoa majumuisho ya Wizara yake kule Zanzibar alisema kwamba ataidai fedha ya rada kwa hoja. Namwambia Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee kwamba sisi tuko nyuma yake, adai pesa ya rada na Wazanbari wote bila kujali itikadi, nafikiri tutamuunga mkono kwa hili*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mafuta, imeonekana kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Pinda wakati anajibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba haina tatizo na mafuta ya Zanzibar, lakini wakati huo huo Serikali ya Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi limesema kwamba linahitaji kuchimba mafuta yake. Sasa inaonekana hapa kuna mwono wa pamoja katika Serikali hizi mbili, hakuna matatizo.

Sasa kama hiyo ndivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais itueleze: Je, ni hatua gani zitafuata baada ya hii maana kila upande uko tayari? Bara iko tayari na Zanzibar iko tayari, sasa tuendelee. Kama alivyosema Waziri Mkuu – Mheshimiwa Pinda kwamba kuna taratibu nyingi za kufanya, kwa hiyo, naomba hili lifanyiwe kazi haraka ili mafuta haya yachimbwe kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo lingine ni uanzishwaji wa Mfuko wa pamoja wa Fedha. Ni aibu kubwa kwamba tangu Katiba ilipotutaka tuanzishe Mfuko wa pamoja wa Fedha hadi leo hakuna utekelezaji wowote. Hii ni katika Ibara ya 133. Tume imeundwa, lakini bado kuna danadana kwamba Mfuko huu haujaanzishwa. Mimi sijui ni kwa nini kwa sababu kama nilivyosema mwanzo Serikali zote mbili za CCM, kwa nini hamkai mkaelewana? Mnaendelea kuvunja Katiba karibu miaka 38! Nasema hili jambo limetosha, na sitaunga mkono hotuba ya Wizara hii mpaka tupate maelezo ya kweli kwamba mara hii mfuko huu utaundwa kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalofuata ni suala la utafiti wa mahindi na muhogo. Kamati yangu ya Kilimo, Mifugo na maji ilitembelea Makutupora hapa Dodoma na Mikocheni Dar es Salaam kuangalia utafiti wa mahindi ambayo yanastahimili ukame kwa kutumia teknolojia ya *GMO*.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, nilichokikuta kule ni kwamba katika sehemu zote mbili kuna matatizo ya mradi huu. Mradi huu umefadhiliwa kwa Dola za Kimarekani karibu milioni 20, lakini umekwama kwa sababu kuna kanuni ambayo mazingira imeandika kwa makusudi; ile kanuni ilivyoandikwa ni kwamba haitawezekana kwa watu kuja kufanya mradi huo wa utafiti. Lakini cha msingi ni kwamba mradi huo ambao upo kwa nchi tano za Afrika ikiwemo Afrika Kusini, Msumbiji, Kenya na Uganda unakwenda kwa pamoja,

na kwamba hii kanuni inasema, mtu yeyote ambaye atafanya makosa katika hili, basi wale wafadhili mpaka mtu wa chini ataadhibiwa. Sasa wafadhili wamevunjika moyo kwa hili. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Mazingira, suala hili ilifanyie marekebisho ya kanuni kwa sababu malengo ni kwamba baadaye ni kuzalisha mahindi kwa wingi kwa mpango huu wa *GMO* hali kadhalika na muhogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la sheria halipo, kwa sababu tayari tumekubali kwamba Tanzania itumie teknolojia hii, lakini tatizo kubwa ni kwamba Kanuni hii inawakatisha tamaa wafadhili. Naiomba Serikali kwa sababu mradi huu ni wa kuondoa njaa katika nchi hii ambapo kila mwaka tunaagiza chakula, basi ikipatikana itakuwa ni manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya watu hawafahamu malengo ya *GMO*. *GMO* ni teknolojia mpya ambayo nchi nyingi hasa za Marekani wanatumia kuzalisha chakula kwa wingi, na hata nguo tunazovaa hizi ni za *GMO.* Kwa hiyo, hatuna namna ya kukwepa teknolojia hii kwa sababu tayari dunia inaitumia. Kwa wale ambao wana ukiritimba, naomba waiache ili tuweze kupata maslahi ya teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SHAWANA BUKHETI HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uwezo kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii niweze

kuchangia hotuba hii ya Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake leo asubuhi ambapo amewasilisha hotuba mbili kwa pamoja. Nampongeza sana, tunamtakia kila na kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi hii pia kutamka kwamba kabla sijaendelea na mchango wangu, kwamba hotuba hii naikubali kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitakwenda moja kwa moja kwenye Muungano kwa vile muda ni mchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano sote tunalielewa, ni swali zuri. Watu wanasema umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Nataka kusema Wazanzibar walio wengi siwezi nikasema kwa kuwa wapo wachache, lakini walio wengi wanaukubali Muungano. Labda kuna tofauti katika suala zima la kuona muundo uwe upi. Hii inakuja kwa kila mmoja kuona labda katika sera za Chama chake zinasema nini, lakini pia na mtu mwenyewe anaweza akazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano ni suala la muda mrefu, wengi walishasema, sasa hivi karibuni tutaingia miaka 50 na kwa kweli mengi

tumeyapata mazuri. Wazanzibar tumefaidika, wa Bara wamefaidika katika Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupongeza sana Ofisi hii ya Makamu wa Rais kwa jitihada nilizofanya kutatua matatizo mbalimbali ambayo tunayaita kero katika upande wa Zanzibar. Makamu wa Rais aliyeko sasa hivi, Makamu wa Rais aliyemaliza muda wake ambaye sasa hivi ni Rais wa Zanzibar wamefanya kazi kubwa na nzuri. Wametatua kero walizotatua na bado wanaendelea. Hata kero zote hizi zimalizike, bado kero zitakuwepo kwa sababu kila tukienda upeo unakua, watu wanaelewa nini kinachofanyika na watu wanajua nini kinachoendelea huko usoni. Kwa hiyo, kero hazitakwisha. Lakini tunaupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu nilikuwa sikiielewi, lakini nashukuru sana juzi Mheshimiwa Samia alipokuwa akitoa majumuisho kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu alielezea zile kero ambazo zilikuwa zimetatuliwa, tulikuwa hatuelewi. Ametuambia, kati ya kero ya 13 kero saba zimetatuliwa. Hata hivyo, zimeongezeka tena mbili zimekuwa 15. Sasa hivi zimeshatatuliwa tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, kwa kuwa matatizo yaliyopo hakuna mawasiliano na hakuna hata anayesema *information is power*, sasa mawasiliano haya sisi hatuna na ndiyo maana sisi masuala mengi haya tunaendelea kuyanung'unikia na kuona hakuna chochote kilichofanyika. Kumbe yako mambo ambayo tayari yametatuliwa. Kwa hiyo, tunachoomba, kila kinachotatuliwa sasa hivi kidogo ndani ya kero za Muungano ni vizuri tuambiwe. Hii ya

kero kutatuliwa lakini hayawekwi wazi, Baraza la Wawakilishi halijui, Bunge halitambui, ndiyo tunapoendelea kulalamika. Lakini tukijua nini na nini kimefanyika, na nini na nini kinabakia, kwa hiyo, na sisi tunapata moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la Muungano, sisi tunasema, siyo rahisi kuvunja Muungano. Muungano huu usife umetokea baada ya Mapinduzi. Yeyote anayethamini Mapinduzi, hawezi akasema Muungano uvunjike. Kama kuna upungufu walioanzisha Muungano huu, wazee wetu ,basi sasa tuna wakati mzuri na huru wa kuweza kutoa maoni yetu. Ndiyo maana Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ametuletea utaratibu wa kuweza kutoa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na huko tunakokwenda, haya tunayaona kero nzito, tunaomba Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri yupo hapa, ayachukue yaende yakafanyiwe kazi ili bugudha na yote tuliyokuwanayo yaweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti aliyesoma hotuba ya Kamati ya Bunge ya Kamati na Sheria. Mengi ameelezea humu ambayo yanasababisha sisi kwa upande wetu tuone kuwa kero. Siyo huu Muungano unaotukera, isipokuwa kuna mambo ambayo yanatupunguzia maslahi yetu Zanzibar, yanapunguza katika Bajeti yetu, yanapunguza katika uchumi wetu hayo ndio tunaita kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kero kubwa inayozungumziwa, Mjumbe aliyekaa amezungumza suala la mafuta na gesi. Wenzetu huku mmeshaanza kuchimba gesi, tunashukuru na sisi taratibu tumeambiwa zitafanywa ili tuanze kabla ya haya marekebisho ya Katiba. Lakini tunachoomba, basi tupate hati, hasa maandishi ya kuanza jambo hilo la kuonekana kwa kweli tumekubaliana katika kero zetu za Muungano. Suala la mafuta limefikia kupata hati maalum ya kuanza suala hilo ambalo tumelikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika suala zima la kero, tunaomba lifanyiwe uchambuzi haraka haraka; Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli miezi sita iliyopita kwamba kuna Shilingi bilioni 18 za wafanyakazi ambazo wanaishi Zanzibar, wale wanaotoa kodi kule. Kwa hiyo, fedha tuweze kupatiwa. Hili limeshafanyiwa kazi tayari, hizo fedha zitolewe. Waziri Mkuu ameshatoa kauli, kinachokwamisha nini? Tunaomba hili nalo lipatiwe ufumbuzi wa haraka kwa sababu linatuongezea kuonekana kama kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Tume ya Pamoja ya Fedha kwa sababu tutaelezea, kweli inasema kwa utata. Tume ya Pamoja ya Fedha tayari imeshaandaliwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

**MHE. SHAWANA BUKHETI HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba hili suala nalo litafutiwe ufumbuzi. Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo hotuba hizi. Nawapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuwasilisha Hotuba hizi hapa. Naomba kabla ya kuchangia, niseme mambo matatu ya jumla kwamba nawashukuru wananchi wa Igunga kwa kushirikiana na mimi sasa bila kujali vyama vyao, tunashirikiana kujenga Igunga yetu. Lakini jambo la pili namshukuru Mke wangu na familia yangu kwa kuendelea kunihamasisha niweze kuwa mwanasiasa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naomba niseme kwamba amani katika nchi yetu ni tunu kubwa na tunatakiwa kuitunza. Mambo yanayofanyika sasa, malumbano na kashfa nyingi zinazotokea zikihamasishwa na mfumo wa Vyama vingi siyo kitu chema sana kwa amani yetu. Zinaendelea kujaribu kutugawa kidini, kimakundi, kikanda, siyo jambo zuri. Naomba Wabunge na wananchi wote kwa pamoja tuhakikishe kwamba tunatunza amani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie kidogo hoja ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni agenda kubwa ya Kimataifa sasa. Sisi Watanzania tunahitaji kushiriki katika agenda hii. Lakini tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi ni kuongezeka sisi

wanadamu katika uso wa dunia. Tumeongezeka sana, miji inakua, watu ni wengi, lakini rasilimali zetu zimebaki kuwa zile zile, maji yale yale yako kwenye *hydrological cycle* wanasema Waingereza, miti ile ile, ukubwa wa dunia uko vile vile. Tuko wengi sana. Watanzania miaka ya 1970 tulikuwa kama milioni nane, hivi sasa hivi tuko milioni zaidi ya 40, lakini maji ni yale yale, eneo ni lile lile. Kwa hiyo, tuna changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu dunia wakati mwingine inasahau hili jambo, inatusaidia sisi nchi za dunia ya tatu katika masuala ya kupunguza hewa ya ukaa, wanasahau kwamba tatizo kubwa ni wananchi wamekuwa wengi. Miradi tuliyonayo ambayo tunafadhiliwa na wenzetu kwa mfano mradi wa (MKUHUMI) Mkakati wa Kupunguza Hewa ya Ukaa kwa Kutunza Misitu, *REDs* pia ni *strategy* nyingine ya kuhakikisha kwamba hewa ya ukaa katika ukanda wa juu wa dunia haibaki. Ni miradi ambayo iko sawa, lakini sasa tuongeze bidii zaidi katika kuhakikisha kwamba jamii yetu, watu wetu ambao wameongezeka waweze kuishi maisha ambayo yanatumia rasilimali kidogo lakini maisha yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema rasilimali kidogo nina maana kwamba, ukiangalia kwa mfano jamii ya Kisukuma na sisi Wasukuma na jamii ya Kimasai tumeongezeka sana tunaondoka, tunasafiri, tunakwenda Tanzania nzima. Jibu la jamii hizi siyo kuwafukuza kwenye misitu, jibu ni kuhakikisha tunawafundisha namna ya kuishi kwa kutumia rasilimali ile ile na maeneo yale yale bila kuhamahama, lakini tukitunza mila na desturi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba tutenge fedha kutoka kwenye kodi, tuwaombe na wafadhili watupe fedha, lakini pia tunaweza kukopa tupate fedha kwa ajili ya kushughulikia ongezeko la watu. Miji yetu imepanuka sana, tufanye namna ambavyo watu waweze kuishi sehemu ndogo, watu waweze kutumia rasilimali kidogo, lakini maisha yakiwa bora. *(Makofi)*

Nikitoa mfano wa jamii za wafugaji na wakulima, tunatakiwa tuweke miradi ya kupanga matumizi ya ardhi, tutumie hela nyingi zaidi huko tuwagawie watu hawa, ndugu zetu, maeneo makubwa kidogo lakini tuwafundishe stadi mpya za ufugaji na ukulima wenye tija badala ya kuwaacha wanahamahama.

Namna nyingine tunatakiwa tuwafundishe kuotesha majani kwenye maeneo yao, kutunza maeneo na kuchunga kwa kuzunguka. Miradi hii iko kule Shinyanga, Wasukuma tunasema Ngitele unagitila, au unazuia sehemu na unachunga upande mwingine baadaye unahamia huko. Sasa kama una Ngitele nne, tano hivi, utaweza kuchunga bila kuhama mradi una eneo la kutosha. Ni wajibu wa Serikali sasa kutenga maeneo haya na kuwafundisha watu wetu kufanya hivyo. Lazima tuwafundishe kuvuna maji, wao wenyewe tuwafundishe kutumia fedha zao na ng'ombe zao kutengeneza mabwawa, kuvuna maji, kuchimba visima ili wasihame, maji yawepo kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, ni lazima Serikali sasa tukubali kuelekeza fedha kwenye jambo hilo la kushughulikia ongezeko la watu. Sasa hivi tunafukuza watu kwenye maeneo ya hifadhi, lakini baada ya miaka 50 kama tusipofanya utaratibu wa kuishi mahali padogo kwa tija, litakuwa ni tatizo kubwa na hatutaweza kuwazuia Wasukuma kuingia kwenye hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itenge fedha hizo kama nilivyosema na kwenye bajeti hii nitaomba basi tuangalie kama kuna fedha za kushughulikia jambo hilo, badala ya kutunza tu misitu na kuacha watu wanazunguka. Miradi yote tunayofanya bila kushughulikia suala la ongezeko la watu, tunafanya makosa kidogo. Dunia itaendelea kukauka, wanasayansi tunasema dunia itakauka hata kama tusingekuwepo sisi, dunia itazeeka na itakwisha. Lazima tujifunze kuishi katika mazingira hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja katika makadirio na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Nitajikita katika maeneo mawili tu kwa kifupi. Jambo la kwanza ni mazingira kama ambavyo imezungumza nafasi ya nchi katika kutunza mazingira; uumbaji wa Mungu ambao kwa kweli wanadamu wameuharibu. Hii ni kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Matokeo yake ndiyo kuharibika kwa uumbaji huu. Tunazungumza juu ya uharibifu kwenye vyanzo vya maji, ukataji wa miti ovyo na suala zima la mazingira kama ambavyo wengine wamesema ni suala mtambuka. Wizara nyingi pia zinahusika ili kuhakikisha kuwa mazingira yanatunzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuihoji Serikali. Tunapozungumza juu ya Sheria ya Mazingira na hata *by laws* ambazo zimetengenezwa katika Halmashauri zetu, sheria siku zote huua, wala haihuishi. Maana Serikali imetumia nguvu kubwa katika maeneo mengi kulazimisha wananchi watende, lakini wananchi hawa wameendelea kutenda uovu huo wa kuharibu mazingira bila mafanikio. Sasa nafikiri Serikali iangalie *approach* mbadala ya kuhakikisha kwamba wananchi waelewe kwamba mazingira ni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano michache, tunazo sheria, tunazo *by laws*, kule kwangu Karatu kwenye vyanzo vya maji vya Qanded ambako kwa kweli ni chimbuko la umwagiliaji kwa wakazi wote wa Bonde la Eyasi wanaolima vitunguu, mahindi, mpunga; bonde lile linaangaliwa na watu wa bonde la maji kati Singida. Sheria ipo, watu wachache wameendelea kuharibu vyanzo vile, sheria zipo, wanaonewa haya. Kwa hiyo, naomba Waziri wakati akihimitisha hoja yake, aniambie sheria *by laws* ambazo zipo, ni kwa nini haiwezi kutenda sawa sawa? Kuna wengine wanaogopwa kuchukuliwa hatua, wakati wananchi wanahangaika kule Qanded. Naomba sana Waziri anipe maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalohusu vyanzo hivi vya maji, pia ni kweli tunahitaji kuangalia vyanzo vya maji ili vitutunze. Naomba Sheria ifanye kazi iwe na meno. Nataka kusema pia juu ya ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya nishati ya kupikia kuni, mkaa na kila kitu. Naomba Serikali iweze kuweka wazi, huwezi kumlazimisha huyu mwananchi asitumie kuni, asitumie mkaa pasipo kumwekea nishati mbadala. Sasa kwa sababu tuna gesi, naomba Serikali ifanye haraka kuhakikisha upatikanaji wa gesi hii na iweze kupatikana kwa bei nafuu na wananchi waachane na kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume cha kutokuwa na nishati mbadala, hawa wananchi tunaowakimbiza, tutawakimbiza na itakuwa hatari. Mfano mdogo, kule kwangu wananchi wanaochukua mkaa askari *TANAPA* wao wanawakimbiza, wanawakamata, wananchi wanatupa mikaa huko, askari wa *TANAPA* wanakusanya mkaa na hujui hata wanapeleka wapi. Haya ndio matatizo ambayo yapo.

Kwa hiyo, suala la mazingira ni la msingi sana kwa nchi yetu kuhakikisha kwamba Serikali ichukue hatua za dhati kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzika. Naomba kuuliza, Serikali kule Karatu tumepata baraka kama ambavyo baraka ziko katika nchi yetu, maeneo mengi hasa katika migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mgodi wa dhahabu ambao umegundulika hivi karibuni wa *Murus-Endabash Oorseenvenrash Gold Mining*, wamekuja watu kutoka kila eneo kuchimba dhahabu pale,

mazingira yamechafuliwa vibaya sana, miti imekatwa hovyo, mashimo kila mahali, uchafu, kujisaidia hovyo. Je, Serikali inafahamu hali hiyo na imechukua hatua gani ku-*rescue* maisha ya wananchi wale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la Muungano. Ni kweli umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Usemi huu hauna kipingamizi kwa mtu wa aina yeyote. Sasa mimi, nataka Watanzania waelewe, hakuna mtu hata mmoja anayekataa suala la Muungano, na tafsiri inayochukuliwa, watu wakizungumza utasikia yule anapinga Muungano. Kinachogomba hapa ni aina ya Muungano tunaoutaka. Mimi nafikiri wale waasisi wawili, *the late father's are founders* wa Muungano; Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Karume. *It was just a good will between the two*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *good will between the two* kama ina nia nzuri, basi italeta maendeleo. Sasa watu wanasema, mkiuvunja Muungano hakutakuwa na maendeleo. Hii siyo kweli, haya ni mawazo finyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayetaka kuvunja Muungano, lakini kwamba kama Muungano unaleta matatizo, unadhohofisha maendeleo, kuna sababu gani ya kuendelea nao? Kwa miaka 50 unapokataa kujadili suala la Muungano, hapana. Kwa nini tusijadili? Mimi nataka kuiambia Serikali, kama hatutakubali kujadili Muungano huu sawasawa, tunajichimbia kaburi na Muungano huu, sitoi unabii na utabiri, Muungano huu unawezekana tu kama CCM

wataendelea kutalawala nchi hii. Kinyume, kama CCM kesho wataondoka madarakani, mtaiweka nchi hii mahali pabaya. Tujadili huu Muungano, ni aina gani ya Muungano tunaoutaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Kambi ya Upinzani imeeleza mambo bayana, wazi! Watu wawili wakiungana, ni lazima wakubaliane aina gani ya Muungano wanaotaka, na nini hawataki. Zanzibar, ina Serikali yake *full*, Bara hakuna kitu. Kwa hiyo, naiomba Serikali tuangalie aina ya Muungano tunaoutaka na watu wapewe uhuru wa kutoa maoni yao na kuamua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Natse, ni kengele ya pili.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nami natoa shukurani zangu kwako kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Mchango wangu na mimi nauelekeza katika upande wa Muungano. Zaidi, ambacho nataka kukichangia ni kuhusiana na uwepo wa *account* ya pamoja. Nasema hili kwa sababu, kuwepo na *account* ya pamoja, Muungano ndiyo njia pekee ambayo inaweza kutatua mgogoro wa kutambua ni yapi matumizi ya Muungano na yapi siyo ya Muungano. Kwa nini niseme hili? Juzi

wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwasilisha hotuba yake, ilizungumziwa suala la chenji ya rada. Kwa kweli, Mheshimwa Mwanasheria Mkuu wakati anakuja kufanya majumuisho katika namna ya kusaidia hii ofisi, alituacha hoi Wazanzibari, kwanza alipokuja kusema kwamba chenji ya rada haihusiani na Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu wa kawaida, ukimwambia neno rada, linampelekea moja kwa moja kwamba kwa Zanzibar ni masuala ambayo kwanza yanahusiana na Jeshi hasa masuala ya anga. Katika masuala ya Muungano, tunasema suala la usalama, kwa maana ya ulinzi na usalama. Sasa tunasema masuala ya ulinzi na usalama ni ya Muungano. Kama inanunuliwa rada kwa fedha ambayo hatujui imetoka katika mfuko gani, lakini katika mazingira kwamba kinanunuliwa kifaa cha usalama wa nchi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali sisemi amepotoka, lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali afanye utaratibu wa kuja kutupa maelezo yatakayokuwa ni rahisi kufahamika kwa wananchi, hasa Wazanzibari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka kauli ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tulitumiwa *message* tukiulizwa, huyu Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazungumza vitu gani kuhusiana na rada? Hatukuwa na jawabu, kwa sababu tuliona kwamba siyo vizuri kulitamka hili neon, tunajua tutakavyolitoa, lakini tumepigwa changa la macho, hatukujua maana yake alivyokusudia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu unalingana kabisa na Muungano wa iliyokuwa Urusi ya zamani. Watu wanatoa hoja kuhusiana na Muungano, kauli mbalimbali zinatolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Muungano. Siku zote katika Bunge letu kabla hatujaanza shughuli za Bunge, tunasoma Dua hapa. “Ee, Mwenyezi Mungu tujalie sisi Wabunge hekima na busara ili tuweze kujadili kwa dhati mambo yatakayoletwa mbele yetu leo.” Lakini hekima na busara katika kujadili haya mambo, humu ndani tunakuwa nafikiri hekima na busara inapotea. Sisi Waislamu tunaamini kabisa kwamba Mungu ndiye apangaye kila jambo. Tunaomba Muungano usife, lakini kwa sababu baadhi yetu ni Mungu anayeleta kila jambo, anawezesha kila jambo, kwa kauli kama hizi na chokochoko za namna hii, tutafika pahala ambapo hatutofahamiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wa Urusi ulishamalizika, ulishakufa. Warusi waliibua hisia zao kama ambavyo leo Watanzania wanaibua hisia zao. Warusi walisema vile vile kama wanavyosema Wazanzibari, wanasema kwamba Bara wanatunyonya, Warusi walisema *Moscow* inawanyonya. Kwa sababu wakati ule *Moscow* ilikuwa ndiyo kitovu cha Muungano wa Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila aliyesimama alisema Moscow inatunyonya, hatutaki Muungano. Matokeo yake Muungano wa Urusi ukamalizika, hivi sasa kila mtu anakwenda kivyake na sisi sasa Watanzania tumeanza kuujadili Muungano. Tuombe Mungu kama ambavyo siku zote tunaomba, ajalie Muungano wetu usife. Kwa

sababu ndiyo kusudio letu sisi kuwemo ndani ya Muungano.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba aje amsaidie Waziri wetu wa Muungano, inawezekana kwa sababu yeye asijibu hiyo hoja, atupe ufafanuzi wa kauli ambayo ametoa wakati ukifanya majumuisho ya hotuba ya Waziri Mkuu ili wananchi waweze kuitambua na sisi tuchoke kuulizwa maswali ambayo majawabu yake hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la Mahakama ya Rufaa. Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii, alisimama na kulizungumza suala la Mahakama ya Rufaa; alisema kwamba Mahakama ya Rufaa siyo chombo cha Muungano kuanzia sasa. Mimi sikubaliani naye, kwa sababu Mahakama ya Rufaa bado ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Jambo moja ambalo nalikubali ni kwamba Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa Katiba yenyewe ya nchi, haina uwezo wa kusikiliza maswali ambayo yatakuwa yanatoka Zanzibar yenye kuhusiana na dini ya Kiislamu. Hilo ndiyo jambo pekee ambalo limeelezwa katika Katiba, kwamba limewekewa *exception* hiyo kwamba Mahakama ya Rufaa haiwezi kulishika swali hilo. Kwa hiyo, Mahakama ya Rufaa bado ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bado kinasikiliza kesi za Rufaa kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, hili siungani na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa endelea, mtoa taarifa amevunja utaratibu alitakiwa kusimama na jicho langu limwone. Endelea Mheshimiwa.

**MHE.JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena hapo hapo kwa mtaka kutoa taarifa. Alizungumza suala la Zanzibar kutaka kwamba kwa mujibu wa kuanzisha vikosi maalum vya SMZ Zanzibar, kwamba Zanzibar sasa inajitangazia uhuru na kwamba ipewe mamlaka na itakuwa na uwezo wa kutangaza vita, siyo kweli. *(Makofi)*

Mipaka yote ya Tanzania ikiwemo ya Zanzibar inalindwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Zanzibar haina mamlaka ya kutangaza vita wakati wowote. Kwa hiyo, niseme tu, Zanzibar kwanza haina mamlaka ya kuagiza silaha popote, silaha ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa suala la kutangaza vita, Zanzibar hili siungani mkono na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, amepotosha wananchi. Zanzibar kuwa na vikosi vya SMZ, kwanza ningemwomba Msemaji wa Kambi ya Upinzani afanye utafiti, vile vikosi kazi zake ni nini ndipo aje hapa Bungeni aseme kwamba Zanzibar kuanzisha vikosi vile inataka kujiamulia uhuru wa kuanzisha vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar haiwezi kuanzisha vita, itaanzisha vita na nchi gani wakati yenyewe haina silaha? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, nilisema anayefuata ni Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, na ninaendelea kusisistiza kwamba mtu yeyote mwenye mwongozo au taarifa, atasimama mahali pake kwa mujibu wa Kanuni na jicho langu likishamwona, nitampa tu ruhusa ya kusema anachotaka kusema. Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, karibu.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumshukuru Mungu sana kwa neema zake nyingi. La pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii jioni hii leo ingawa nafikiri jina langu lilikuwa nafasi ya tano limeshuka kuwa nafasi ya saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini kwa kunichangua kwa kura nyingi, na la tatu, niwapongeze Mawaziri wawili hawa wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuleta bajeti yao nzuri na yenye fasaha nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Waziri Mkuu, bajeti ya Waziri wa Fedha na bajeti ya hii leo zote zimelenga kunyanyua maisha ya Mtanzania. Wananchi wale waliokuwa wana maisha duni kabisa ambayo hali zao ni mbaya. Hii ni kutekeleza msemo wa CCM, “Maisha Bora kwa Watanzania.” Kwa hiyo, kwa hali hii nawajibika kui-*support* bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, niende katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Samia. Bajeti hii imeanza ukurasa wa tano na kumalizikia ukurasa wa 23. Ina maana kwamba mambo ya Muungano katika buku hili ni asilimia 16 tu, inasikitisha. Kwa sababu inaonesha Muungano haukupewa umuhimu. Kuna mambo mengi yalikuwa yazungumzwe, mathalan kero za Muungano zitajwe zipi, na zipi zimezungumzwa na nini tatizo na mambo kama hayo. Lakini bahati mbaya sana, zimegusiwa juu juu tu na kwenda mbele. Sasa nafikiri hili suala limetuvunja moyo mno Wanzazibari na Watanzania kwa ujumla kwa sababu buku hili kwa kweli hasa linazungumza mazingira badala ya kuzungumza bajeti ya Mazingira na Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Muungano huu umeasisiwa na Sheikh Abeid Karume na Mwalimu Nyerere. Lakini kwa taarifa yako humu katika buku hili, taarifa ya Waheshimiwa hawakutajwa kabisa wala Muungano haukutajwa. Jamani lazima tuwaenzi Viongozi wetu hawa. Hawa ndio walioleta Muungano, itakuaje kwamba katika buku hili zima hata mahali pamoja hawakutajwa? Mahali gani katika bajeti, watu hawa wawili wametajwa? Kwa hiyo, nafikiri *omission* hiyo ningemwomba Mheshimiwa Waziri a-*take note* na baadaye *at least* awaingize ili tuone kwamba Viongozi hawa tunawaenzi na hii ndiyo Wizara amabyo inashughulika na Waheshimiwa hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, labda nigusie kidogo suala moja ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu aliligusia, na mimi ningependa vile vile kulieleza.

Nalo mara nyingi hata katika bajeti ya mwaka 2011 amewazungumzia Marehemu ambao ni Mheshimiwa Hanga na Waheshimiwa wengine. Utaona kwamba hizi ni kovu ambazo zilishapona, kwa nini unazitonesha mara kwa mara? Unayajua maumivu ambayo wewe unawapa watu ambao wako karibu nao? Jamani msijaribu kupata umaarufu kwa kutaja majina kama haya, hayasaidii kitu kwa sababu mambo haya yamepita, imeshakuwa katika historia. Wewe kila mwaka unayaleta katika Bunge hili na unawapa taabu hawa wananchi masikini bure, *just* kwa kutegemea labda pengine utaweza kuwavutia watu. Siyo rahisi kumvutia mtu kwa suala hili*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nitazungumzia ghasia ambazo zimetokea hivi karibuni Zanzibar.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Nassib subiri.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo kuhusu utaratibu. Kanuni ya 64(1) (a) na vile vile Kanuni ya 64(1) (f) na (g), lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

**MWENYEKITI:** *Order*. Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika hotuba yangu kwamba tunahitaji

kuelewa historia ya Muungano, ya mambo yaliyotokea na historia ya Muungano wetu inatuambia kuna watu walikuwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi na Viongozi wa Muungano hawatajwi kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu hebu nisaidie kitu kimoja...

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema, naposema kwamba tu...

**MWENYEKITI:** Naomba ukae kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Nani akae chini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, hebu ongea na Kiti. Sasa ukitaka tena uongee na watu wengine, itakupa taabu bure bila sababu. Sasa nisikilize basi kama unataka kuendelea na mwongozo. Umeomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni Na. 64(a), (f), (g), sasa naomba unisaidie ili niweze kutoa huo mwongozo. Hebu nenda ile (a) moja kwa moja na unifafanulie. "Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli" uniambie ukweli huo, na hebu subiri usiwe na haraka Mheshimiwa Tundu Lissu, uwe mpole, fuata taratibu na Kanuni na sikiliza mwongozo wa Kiti. *(Makofi)*

Sasa naomba unipeleke kwenye ile (f) iliyovunjwa kwamba, hatasema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge, au mtu mwingine yeyote. Sasa pale, naomba uende *straight,* uniambie Kanuni iliyovunjwa na lugha hiyo, na umalize na ile (g).

Sasa, nisingependa upoteze muda wa kuchangia kwa kuhutubia. Naomba nenda, umeshataja maeneo ambayo yamekiukwa, kwa hiyo, sasa wewe nenda moja kwa moja. Ile (a) iliyovunjwa, imevunjwa kwa utaratibu huu, (f) imevunjwa kwa neno hili na (g) imevunjwa kwa neno hili. Vinginevyo ukianza tena hadithi nyingine, utanifanya na mimi nishindwe kukuvumilia. Nataka unisaidie kanuni hizi, ili nitoe Muongozo. Mheshimiwa Tundu Lissu, karibu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza (a), Kauli isiyokuwa na Ukweli; Hotuba yangu imeandikwa, inasema hivi: "Mahakama ya Rufani, haikuwa jambo la Muungano kwa mujibu wa makubaliano ya Muungano na kwa mujibu wa Sheria ya Muungano ya mwaka 1964." Nimesema kwamba, Mahakama ya Muungano, iliingizwa kwenye orodha tu, mwaka 1984.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu Mheshimiwa aliyesema kwamba, nimedanganya Mahakama ya Muungano, siyo jambo la Muungano, hajasoma hotuba yangu. Kwa hiyo, alichosema siyo kweli. *(Makofi).*

**MWENYEKITI:** Sawa, nenda kwenye ile ya (f).

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (f). Lugha ya Matusi. Kuna kauli imetolewa hapa na huyu Mheshimiwa anaitwa nani sijui, kwamba, huyu Lissu, anajitafutia umaarufu. Umaarufu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, najitafutia umaarufu kwa kitu gani? Ni umaarufu gani ninaoutafuta kwa kusema kwamba wale waliokuwa Viongozi wa Serikali wa Baraza la Mapinduzi, walioulizwa, waliuliwa kweli na ninasema watambuliwe na historia, huko ni kutafuta umaarufu? Hiyo siyo lugha ya kuudhi?

**MWENYEKITI:** Haya, tuendelee na (g).

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa (g) ni lugha ya kuudhi na ya kudhalilisha. Kusema kwamba, kwa mimi kutoa hoja kwamba, wale ambao waliuliwa watambuliwe na historia yetu, ni kujitafutia umaarufu? Ni kunidhalilisha. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa, endelea. Nitatoa maamuzi baadaye.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniruhusu. Ghasia ambazo zimetokea karibuni Zanzibar, zimesababisha maharibiko ya majengo na nyumba za ibada. lnasemekana kikundi hiki cha Uamsho, ndiyo kilisababisha maafa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni zito na kwa kweli, kampeni kubwa zinakwenda chini kwa chini katika redio, katika *message* za watu na katika mambo mengi zinakwenda. Hivi ninavyokwambia hapa sasa hivi, Wabunge wengi wa Zanzibar, kila siku wanapata *message* kutoka katika Kikundi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikusomee *message* moja katika *message* tano ambazo nilipewa, nimeletewa mimi binafsi. Inasema kama hivi...

**MWENYEKITI:** Haya, kwa ruhusa ya Kiti.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Hebu angalia dhuluma za Muungano ni hizi, Rais wa Muungano kutoka Tanzania Bara, Jaji Mkuu kutoka Tanzania Bara, Spika wa Bunge kutoka Tanzania Bara, Naibu Spika kutoka Tanzania Bara, Waziri wa Mambo ya Nje kutoka Tanzania Bara, Waziri wa Fedha kutoka Tanzania Bara, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi anatoka Tanzania Bara, Msajili wa Vyama anatoka Tanzania Bara, Mkuu wa Polisi anatoka Tanzania Bara, Mkuu wa Jeshi, Mkuu wa Usalama, Uhamiaji, *NECTA*, Gavana wa Benki, Katibu wa CCM, Waziri wa Afrika Mashariki, Balozi wa Umoja wa Mataifa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa." *Message* kama hizi zinapopelekwa kwa watu ambao hawajui hali halisi, zinasababisha matatizo makubwa. Kwa kweli, Serikali ya Muungano ni lazima isaidie katika kuondoa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempigia simu nikamweleza kwamba, sikubaliani na mambo haya. Lakini kuna wengine ambao hawaelewi kabisa habari hii. Inaleta matatizo, inaleta chuki na baadaye hali hii inaweza ikaharibika na tukashindwa kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo Serikali ya Muungano ninapenda iliangalie, wengi hawa ni vijana wadogo wadogo kule Zanzibar, na

wengi hawana kazi. Nafikiri moja katika nyanja ambayo Serikali ya Muungano inaweza kusaidiana na Serikali ya Zanzibar ni kuangalia uwezekano wa kusaidia kupata kazi kwa vijana hawa, kama kupatiwa *training* na mambo mengine kama hayo. Lakini hali ikiachiwa kama hivi ilivyo sasa hivi, tumekaa kimya, hatuchukui hatua zozote, tutegemee huko tunakokwenda baada ya hili, kutatokea suala lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nitalizungumzia ni mchakato wa Katiba Mpya. Kwanza, tumshukuru Rais Jakaya Kikwete, kwa kuridhia mchakato huu wa Katiba Mpya. Katiba Mpya, itaweza kuondoa maovu yote yaliyokuwemo katika Katiba kongwe na kuingiza mambo ambayo yataweza kusaidia nchi hii. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwa wananchi wote kushiriki katika Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mchakato huo umeanza Mkoa wa Kusini Zanzibar. Nina furaha kukueleza kwamba, wananchi wengi wamejitokeza, na wote wamesema wanautaka Muungano wa Serikali mbili, hongera sana. Mimi binafsi natoa wito kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini...

*(Hapa, Kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga Mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nassib. Waheshimiwa Wabunge, naomba nimalize kabisa huu Mwongozo, tuendelee na vitu vingine.

Mheshimiwa Nassib, kwa mujibu wa Kanuni 64 (f) na (g), hii lugha uliyoitumia ya umaarufu, nafikiri ni lugha ambayo Mbunge mwingine anaweza kuwa hajavutiwa nayo. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba usimame uifute, ili nimalize kutoa Mwongozo kwa Kanuni ile (a), iliyobakia. Mheshimiwa Nassib.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaifuta Kauli yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, katika lile la (a), hatatoa ndani ya Bunge, taarifa ambazo hazina ukweli.

Waheshimiwa, mimi hapa naona tunafanya tu mabishano ya lugha na ya uelewa. Mwongozo wangu nafikiri kila mtu anachokisema, anakiamini kwa namna ile alivyokisoma na kukiona. Kwa hiyo, nadhani taarifa hiyo tuiache kama ilivyosomwa na Upinzani na Mheshimiwa Mbunge, jinsi alivyoilewa. Tukianza kubishana kuhusu taarifa hiyo, tutakuwa tunapoteza muda tu ndani ya Bunge, bila sababu ya msingi.

Naomba tuendelee na mchangiaji anayefuta. Nadhani atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho; labda tunaweza kuongeza mmoja, tutaangalia kwa sababu, muda wetu ni mfupi sana.

Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Cap. John Zephania Chiligati. Kama muda utatosha, Rashid Ali Omar, nimpe nafasi. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika mjadala huu. Kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili na Manaibu Waziri kwa hoja nzuri na kazi nzuri wanayoifanya katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mungu awabariki waendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja hii. Lakini pia ningependa nitofautiane kwa maneno mengi tu, mambo mengi ambayo yalisemwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani – Muungano. Kwa sababu ya muda, nitasema machache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ambalo sikubaliani na yeye, ni yale maneno ameandika ukurasa wa 17, akiuelezea Muungano kama ni kiini macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiini macho ni kitu ambacho siyo halisi. Ni kitu kinaonekana kama kipo, lakini hakipo. Ndiyo maana ya kiini macho. Haiwezekani kitu ambacho tumekuwanacho kwa miaka 48, leo mwenzetu mmoja tu anasimama, tena anasema kwa niaba ya wenzake wote na Kambi ya Upinzani kwamba eti ni kiinimacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatujitendei haki sisi wenyewe. Muungano huu ndiyo muungano peke

yake katika Bara la Afrika. Ndiyo mfano wa Umoja katika Afrika na Waafrika wanajivunia. Sasa sisi wenyewe, tunaukejeli; kwa kweli, siyo sawasawa. Wala hatupeleki ujumbe sawasawa kwa vijana ambao wanataka warithi Muungano, tunasema eti ni kiinimacho. Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani labda tu mdomo umeteleza. Kama ni muungwana, basi aombe radhi kwa sababu, miungano mingi imeshindwa, lakini wakwetu unaendelea. Tutoe mawaidha kuimarisha Muungano, siyo mawaidha ya kuukejeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo sikubalini nalo ni pale alipopendekeza kwamba, sasa Tanganyika ifufuliwe ili ipambane katika hali ya usawa na Zanzibar, kwa sababu Zanzibar inaionea Tanzania Bara. Kwa hiyo, nayo Tanzania Bara, ili sasa ipambane sawasawa, basi Tanganyika nayo ifufuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli, huyu anayesema anaonewa, ana watu milioni 44, huyu mwingine ana watu milioni moja, sasa wa milioni moja anamwonea wa milioni 44; hata haiingii akilini. Huyo anayeonea mwenzake, ukubwa wake ni kilometa za mrada 2,000. Anayeonewa huyu, ni *giant* wa kilometa za mraba 950,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haiingii akilini. Anasema, huyu Zanzibar ana Majeshi. Hivi Zanzibar wana Majeshi gani ambayo yana vifaru au ndege za vita au meli za vita, viko wapi? Wametengeneza utaratibu wa kujilinda tu, ulinzi wa kawaida tu. Wana

Kikosi cha Kuzuwia Magendo, huko ndiyo kuvunja Muungano? Kikosi cha Kuzuwia Magendo, ni jeshi? Wana Askari wa kulinda wafungwa, ndiyo Majeshi hayo? Ndio uonezi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwamba, kufufua Tanganyika na wale wote ambao wana mawazo ya kufufua Tanganyika; ni wa makundi mawili, kuna wengine ni shamra shamra tu kwamba, na sisi tuwe na Serikali, lakini kuna wengine wanajua, ukimfufua Tanganyika na utanganyika wenyewe, unavunja Muungano. Ndiyo ukweli wenyewe kwa sababu, huyu Tanganyika, akishafufuka na kutetea maslahi ya utanganyika, kwa uchumi wa Tanganyika na uchumi wa Zanzibar, atakayebeba mzigo mkubwa wa kuendesha hii Serikali nyingine ya tatu, ni Tanganyika. Tanganyika atabeba mzigo wa Serikali ya Tanganyika, atabeba na mzigo mkubwa karibu ya 95% ya mzigo wa kuendesha Serikali ya Muungano, ni mizigo haibebeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lundo na utitiri wa Serikali, uchumi wa kubeba Serikali hizo, uko wapi? Hizi pesa badala ya kwenda kwenye barabara, kujenga barabara, ziende kwenye reli, ziende kwenye bandari; sisi tunakwenda kuendesha Serikali matatu? Za nini? Mwingine, anataka mpaka Serikali nne, eeh! Wanataka Jamhuri ya Watu wa Pemba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufufua Tanganyika na Utanganyika, ni kurudi nyuma. Tukivunja Muungano na Watanzania wenye nia njema, hili ni wazo ambalo ni

lazima tulikatae. Muungano wa Serikali mbili, ndiyo Muungano ambao umetufikisha miaka 48. Ndiyo Muungano ambao historia imeonyesha kwamba, inawezekana. Kuna nchi nyingi zimejaribu Serikali tatu, zimeshindwa. Kulikuwa na Muungano wa *Senegal* na Gambia, ukafa; Libya na Misri, ukafa. *Egypt* na Syria, ukafa. Huu Muungano wa Serikali tatu, hakuna mahali zimefanikiwa. Sasa hawa wanaosema Serikali tatu, wanatupeleka kuzimu na tukatae kwenda kuzimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kero au changamoto, na hakuna Muungano duniani, hauna kero, hauna changamoto, zipo na pengine katika Katiba inayokuja pengine, tupendekeze mbele ya ile Tume kwamba, pengine tuwe sasa na Tume Maalum, itakayokuwa inashughulikia hizi kero ambazo hazitakwisha, lakini kuweko na chombo maalum cha kushughulikia. Kwa sababu, kuwaachia tu Mawaziri, chini ya Makamu wa Rais, wana kazi nyingi sana. Kwa hiyo, wakati mwingine kushughulikia hizi kero wanachelewa. Kwa hiyo, pengine tungependekeza kuwe kuna chombo maalum (Tume Maalum) ambacho hivi sasa kitakuwa kinashughulikia hizi kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kero zenyewe, zinazungumzika tu. Orodha ya Mambo ya Muungano, inazungumzika. Kama kuna mambo ambayo wenzetu, upande wa pili wa Muungano wanaona yaondoke, tutazungumza, inazungumzika tu. Kama wanataka Bandari...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya kwanza.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama wanataka Bandari iondoke, inazungumzika. Wanataka sijui reli, Posta ziondoke, inazungumzika. Wanataka mafuta na gesi na nini viondoke, yanazungumzika. Pia iko kero kwamba, Makamu wa Rais, aah hapana; kwamba, Rais wa Zanzibar awe ndio Makamu wa Rais wa Muungano, iko hoja. Jambo hili tuliwahi kuwanalo huko nyuma wakati wa Chama Kimoja. Tulikuwa na Rais wa Zanzibar, alikuwa ndiye Makamu wa Rais, halafu huku kwa upande wa Bara, tulikuwa na Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuingia Vyama Vingi kwa sababu ya hofu: Je, kama Rais wa Muungano akitoka Chama kingine tofauti na Rais wa Zanzibar, itatokea fujo? Vurugu! Kwa hofu hiyo, ndiyo ukaanzishwa utaratibu wa Mgombea Mwenza. Miaka 20 baada ya Vyama Vingi, hiyo hofu haipo. Tunaweza tukarudia tena katika utaratibu wa mwanzo. Haya mambo tukiyatolea majibu, hata lile la mgawanyo wa mapato, ile Tume ya Pamoja, mapendekezo yake yale, yakifanyiwa kazi na mgawanyo wa mapato ukipata muafaka, hizi kero zitapungua. Hivyo, ndani ya Serikali mbili, Muungano wetu utaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nataka niwashawishi Watanzania wenzangu kwamba, tukubali uendelee mfumo huu wa sasa. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuwasilisha Bungeni hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano, Wazanzibar tunaupenda, tunautaka na tunauthamini, isipokuwa changamoto zifanyiwe kazi kwa haraka kwa faida ya Mtanzania na ustawi wa watu wake kwenye uchumi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, mikataba yote ya makubaliano, na itifaki zinazotiwa saini kwenye makubalianio ya mazingira kama mkataba wa makubaliano ya tabianchi; makubaliano ya *Rio*; na makubaliano ya ardhi oevu *(wet land);* Makubaliano ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na mikataba mingineyo mingi ya mazingira ambayo kwenye makubalinao yatakiwa kuwepo na *focal person* na pia nchi maskini zilizotia mkataba au makubaliano hayo *(least development country)* zinapata msaada wa kuhudhuria mikutano. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamewapatia wafanyakazi wangapi wa Zanzibar nafasi za kushiriki Mikutano hiyo au wangapi wamepata nafasi ya kuwa *focal persons*.

Mheshimwa Mwenyekiti, vifaa chakavu vya umeme na *electronic* vina madhara makubwa kwa mazingra na jamii (maisha ya watu) na kumekuwa na uingizaji mkubwa wa vifaa hivi. Je, Serikali imejiandaaje kudhibiti uingizaji wa bidhaa hizi? Je, Serikali imejipangaje kuthibiti au kuangamiza bidhaa zitokanazo na *analogy* zisije kutupwa ovyo na kuharibu mazingira wakati muda wake ukimalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar imefanikiwa kuondoa na kuthibiti mazingira kwa kuweka na kusimamia uingizaji wa mifuko ya *plastic* isitumike. Changamoto ni mifuko inayotoka Dar es Salaam. Je, kwanini tatizo hili limechukua muda kwa Tanzania Bara kurekebisha kanuni hizi ambapo bado utekelezaji wake ni mdogo na mifuko ya plastiki inazidi kuwa mingi na inachafua mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni za kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia, yaani *environmental Management (Bio safety Regulations, 2009)* bado inaonyesha kurudisha nyuma baadhi ya aina ya mazao ambayo tafiti nyingi duniani zinaonyesha bioteknolojia inaweza kutumia na kuongeza uchumi katika kilimo, mazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali iangalie tena kanuni hii ili pale inapowezekana iruhusu tafiti zifanyike ili Tanzania nayo ifaidike kwa teknolojia ya bioteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna kero nyingi za Muungano zinahitaji ufafanuzi, nashauri hatua za haraka zichukuliwe ili kuweza kuleta uwelewano wa pande zote mbili.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii pande mbili hizi, kila mmoja analalamika. Zanzibar wanalalamika na Tanzania Bara pia wanalalamika, kila mmoja anaona ni mzigo kwa mwenzake. Hata baadhi ya Wabunge wanadiriki kusema Majimbo ya Zanzibar ni kama Kata. Baadhi ya Viongozi wamekuwa wakilalamika idadi ya Wabunge wanaotoka Zanzibar ni wengi. Ni kwanini Wabunge wa Jamhuri ya Muungano hawashirikishwi katika Baraza la Wawakilishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi limekuwa ni mfumo wa Vyama viwili CCM na CUF na hii imepelekea kuwa na migogoro isiyokwisha kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wangu, ni kwanini mfumo huo wa Baraza la Wawakilishi

ubadilishwe uwe na sura ya Vyama vingi ili kuondoa malumbano ya kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, ni kwanini ilivyobadilishwa katiba ya Zanzibar wananchi hawakushirikishwa wakatoa maoni yao kuhusu katiba Zanzibar? Lakini wananchi hao hao walishirikishwa kupiga kura ya maoni ya ndiyo au hapana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, ni Mabalozi wangapi Wazanzibar wapo Bara la Ulaya? Ukitazama Mabalozi wengi wa Kizanzibar wamekuwa wakipelekwa nchi za Kiarabu na hata hizo nafasi zenyewe ni chache wanazopewa Mabalozi wa Kizanzibar. Kwa hiyo, naomba unipe idadi ya Mabalozi wetu wa Kizanzibar ambao wapo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Elimu ya Vyuo Vikuu, kumekuwa na baadhi ya nafasi zikitolewa za kwenda kusoma nje ya nchi, vijana wengi Wazanzibar ambao wanasoma Vyuo Vikuu wamekuwa wakilalamika kuwa nafasi hizo haziwafikii. Hata nafasi za ajira katika Sekta ya Muungano imekuwa ni shughuli kuzipata. Vile vile mikopo wanayokopeshwa na Serikali, wanafunzi wa Vyuo Vikuu imekuwa na usumbufu mkubwa, hawaipati kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mazingira, kumekuwa na uharibifu mkubwa sana baharini, kama vile kutupa mifuko, na mitaro ya maji machafu yote imeelekezwa baharini na hata ardhi ya wakazi ambao wanaishi kando kando ya bahari

wamekuwa hawajengi vyoo, wamekuwa wakijisaidia baharini haja kubwa na haja ndogo na wengine wamekuwa wakitumia uvuvi haramu na kuharibu mazalio ya samaki (matumbawe). Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwafikia wananchi na kutoa Elimu ya Mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la magari ambayo yanaharibika barabarani na kupata ajali, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hao wanaotumia alama za kukata miti na kuweka barabarani, ni kwanini wanapomaliza hawayaondoi? Huu ni uharibifu wa mazingira kwa sababu Dar es Salaam mpaka Mikoani unakuta miti imekatwa kwa alama za barabarani. Huoni huu ni uharibifu wa mazingira. Kwani hawa Trafiki wetu hawana alama nyingine za kuweka mpaka watumie alama za miti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Waziri kwamba, mabasi mengi yanayokwenda Mikoani, abiria wengi wamekuwa wakiteseka kwa kujisaidia maporini (wenyewe wanaita kuchimba dawa) huu pia ni uharibifu wa mazingira. Ni lini Serikali itajenga vyoo kwa abiria wanaosafiri Mikoani na kuondoa usumbufu huu wanaoupata wa kuchimba dawa vichakani?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ni wa miaka 48 sasa. Hili ni jambo la kutia faraja, lakini ni bahati mbaya sana kwamba Muungano huu ulianza

kwa usiri mkubwa. Maandishi mbalimbali yanaonesha kuwa Hati ya Muungano ziliandaliwa na upande mmoja hasa wataalam na washauri wa Mwalimu Nyerere bila kuwepo wataalam wa upande wa pili. Usiri huu umedumu kwa miaka yote hii bila kutolewa ufafanuzi na kuleta wasiwasi kwa upande ambao haukushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa, hakuna anayepinga uwepo wa Muungano, ila kwanini historia ya kuanza kwake isiwekwe wazi ili watu wote waridhike na kutoa maoni ya kuboresha? Tunachoshuhudia kila mwaka ni mwasisi mmoja akichanganya udongo. Kwa nini isifike mahali mambo haya yakawekwa wazi? Kuna dhambi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mapato/mgao wa pesa za mapato ya misaada ya nje ni kero mojawapo kubwa kwa upande wa Zanzibar. Serikali iweke wazi vigezo vinavyotumika katika kugawa pato hili.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira, ndiyo maisha ya kila mtu popote duniani. Serikali ina mikakati mbalimbali ya kuinusuru nchi kutokana na uharibifu wa mazingira na hivyo kuokoa maisha ya watu pamoja na mikakati yote iliyowekwa, bado kuna mambo kadhaa ya kutazamwa kwa kina ili kutimiza azma hii ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za vifaa vya ujenzi ni kubwa mno. Ni ukweli usiopingika kuwa asilimia 80 ya Watanzania wote huishi vijijini. Asilimia hii

ni kubwa sana na wote hutegemea mazingira moja kwa moja kwa maisha yao ikiwemo ujenzi wa makazi. Kwa sababu watu hawamudu gharama za vifaa vya ujenzi, hugeukia kukata miti ili kuweza kujenga. Hii hupelekea mazingira kuharibika sana na kufifisha lengo la kunusuru nchi kutokana na jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumetokea mfumuko wa ajabu wa nishati za mafuta ya taa, umeme na gesi. Kupanda kwa bei ya nishati hizi kumepelekea watu walio wengi hasa Mijini na maeneo mengine yafananayo kuacha matumizi yake. Kwa sasa watu walio wengi hupendelea kutumia mkaa badala ya nishati hizo tajwa. Hatua hii inasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kuzuia azma iliyokusudiwa kutotimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kusema kwamba, wakati muafaka Serikali kuweka wazi masuala ya Muungano, kwani italeta afya na uhai endelevu. Serikali ichukue hatua madhubuti kuangalia upya suala la nishati mbadala, kwani hata kama elimu ya namna gani itatolewa, bila kuchukua hatua, haitasaidia. Hatua mojawapo ni kuangalia upya bei ya mafuta taa, kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi, kuangalia upya bei ya gesi na kupitia upya bei ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni uhai, tusipuuze.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uharibifu wa mazingira katika

Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Pwani, Mwanza, Mara na Tabora, kutokana na ukataji na uchomaji wa misitu katika Mikoa hii, napendekeza Serikali itangaze kuwa Mikoa hiyo saba, itangazwe kuwa ni janga la kitaifa. Napendekeza kuwa mipango kabambe ifanyike ili kuinusuru Mikoa hiyo isigeuke na kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mazingira ipewe fedha nyingi kwa mfululizo wa miaka mitano ijayo ili miti mingi iweze kupandwa katika Mikoa yote saba. Serikali pasipo aibu, iombe msaada kutoka nchi za nje, mfano Marekani, China, Uingereza, na nchi za Scandinavia, zinazosaidia katika masuala ya mazingira, ili tuweze kunusuru nchi yetu dhidi ya jangwa nyemelezi linalotukabili sasa hivi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa hii saba, Serikali ichukue hatua za makusudi kusaidia watu wetu kutumia nishati nafuu kwa ajili ya kupikia, mfano majiko ya mafuta ya taa, kujenga gesi ya mbolea ya ng'ombe kwa makabila yanayofuga ili majiko ya kupikia yatumie gesi hiyo badala ya kutumia mkaa au kuni ambazo zitaendeleza uharibifu wa mazingira. Lakini yapo mashirika yanayoweza kusambaza umeme wa jua badala ya mkaa au kuni. Ni vizuri tukashirikiana na mashirika hayo *(NGO's)* ili misaada mingi ya umeme wa jua upate kutolewa kwa Mikoa yote saba ambayo imeathirika sana na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vingi vya maji vichimbwe kwa matumizi ya binadamu, kwenye Mikoa hiyo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa yapanuliwe kwa ajili ya maji ya mifugo na kilimo cha mboga mboga. Yote haya yatawezekana kwa kutenga bajeti kubwa kuomba misaada (tuone haya, maana mazingira yameharibika), pia kuwa na uwakili *(stewardship)* mzuri katika matumizi ya fedha yetu na misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa hotuba nzuri sana. Vile vile nampa pongezi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie utekelezaji wa *Environmental Management Act (EMA)* ili kunusuru mazingira yetu na kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo vitakuwa na stahili zao za maisha kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *shifting cultivation* idhibitiwe vizuri, ufyekaji wa kufungua mashamba uruhusiwe tu kwa vibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mikubwa ifanyiwe *Environmental Impact Assement (EIA),* isimamiwe kwa karibu sana na kupewa *Certificate* maalum kwa kutimiza masharti ya *EAI*. Elimu ya *(climate change)*

mabadiliko ya tabianchi itolewe ili watu wajue athari zake na jinsi ya kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya nishati mbadala vibuniwe ili kupunguza na hatimaye kumaliza matumizi ya mkaa na ukataji miti.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu na viumbe wengine tunaishi katika dunia hii tukiwa pamoja na ardhi, misitu, maji, hewa, bahari na kadhalika. Kwa umoja wake, mambo hayo yanayomzunguka binadamu ndiyo tunayaita Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mkusanyiko wa mambo hayo, ni dhahiri mazingira yana umuhimu wa pekee kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wowote wa mazingira ni sawa sawa na kuyaharibu maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni sehemu muhimu ya mazingira, kwa hiyo, inahitaji kutunzwa na isiharibiwe. Bahati mbaya ardhi yetu hivi sasa inakabiliwa na uchafuzi kwa kupitia kilimo. Kilimo kinachofanywa na wakulima wadogo wadogo hapa nchini wapatao milioni tano hutumia mbolea za chumvi chumvi. Hivi sasa kuna maeneo katika nchi hii wakulima hawawezi kupata mazao bila kutumia mbolea. Kwa hiyo, ni dhahiri ardhi hiyo tayari imeshaanza kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matumizi makubwa ya misitu ambayo pia ni sehemu moja au nyingine ya mazingira. Hivi sasa asilimia 92 ya nishati ya kupikia inatokana na mkaa na kuni. Ni dhahiri kwa hali hiyo na kwa vile hakuna nishati mbadala ya kupika, misitu yetu itaendelea kuteketea na nchi kukabiliwa na jangwa. Bahati mbaya miti inayokatwa hailingani hata kidogo na inayopandwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga vipi na suala la nishati mbadala ya kupikia? Kwani kila bajeti ahadi inabakia kuwa, Serikali iko mbioni katika kupata nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hewa ina umuhimu wa pekee katika maisha ya binadamu na viumbe wengine. Hivi sasa kwa kupitia uzalishaji mkubwa wa gesi joto kutoka viwandani kwenye nchi zilizoendelea, kuna uchafuzi mkubwa wa hewa. Kutokana na uchafuzi huo wa hewa, hivi sasa dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi *(MTN).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabadiliko ya tabianchi kutokana kuongozeka joto la dunia kumeleta athari kubwa duniani. Hivi sasa kina cha bahari kimeongezeka na kusababisha visiwa vingine kuzama. Maeneo ambayo kiasi hakukuwa na homa ya Malaria, hivi sasa maeneo hayo malaria ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko na ukame, pia ni athari nyingine inayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kinachopaswa kuhifadhi na kusimamia mazingira hapa nchini ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya jukumu kubwa walilonalo Baraza, bado lina upungufu wa Wataalamu wa mazingira. Hivi sasa Baraza lina wataalamu 89 wa mazingira ambao hawakidhi mahitaji kwa nchi nzima. Pia Baraza mwaka huu 2012/2013 wa bajeti ilimepewa fedha pungufu ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2011/2012. Mwaka huu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingara limepewa Shilingi bilioni 3.71 wakati mwaka uliopita Baraza lilipewa Shilingi bilioni 4.09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ingekuwa makini kwa suala la mazingira, ingewezekana mwaka huu Baraza kupata fedha kidogo kuliko mwaka jana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi ya maendeleo, fedha iliyotengwa ni Shilingi bilioni 7.07. Katika fedha hizo, Shilingi milioni 5.77 kutoka nje na Shilingi bilioni 1.30 ni za ndani. Tatizo ni la kawaida, fedha za kigeni kupatikana huwa ni tatizo. Hivyo uwezekano wa miradi ya maendeleo kutekelezwa kwa kutumia fedha za kutoka nje ni mdogo mno. Kwa nini Serikali isitegemee fedha zake wenyewe kwa maendeleo? Ahsante.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa napenda kuunga

mkono hoja ya bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mgawanyo wa Mapato;
(ii) Mafuta na Gesi; na
(iii) Kulipishwa ushuru wa forodha mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgawanyo wa mapato, kumekuwa na masikitiko mengi katika eneo hili kwa upande wa Zanzibar. Toka hapo awali, mgawo wa mapato kwa Zanzibar ni asilimia 4.5. Hii imedumu kipindi kirefu toka hapo watu wa visiwa hivi kiasi cha 50,000, lakini sasa wanafikia 1,200,000, karibu ongezeko la asilimia 100 mpaka sasa. Kwa hiyo, iko haja ya kuongeza mgawo huu kutoka asilimia 4.5. mpaka 5%kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia mafuta na gesi. Kwa vile kwa upande wa Bara tayari kumekuwa tayari kwa upatikanaji wa gesi, sasa kwa maoni yangu, iwapo watu wa Zanzibar wakaachiwa na wao ili ikiwa hayo mafuta na gesi vitapatikana kwa Zanzibar, naona hakuna tatizo, maana na wao pia watakuwa na nguvu ya kuchangia katika kuimarisha Muungano wetu, maana wenzetu wa Visiwani hawana mapato mengine baada ya karafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala kulipia ushuru mara mbili. Hili ni tatizo kubwa kwa watu wa Zanzibar, kwani *TRA* ni moja kwa Tanzania

nzima, sasa sioni haja kwa mtu kulipia Bandari ya Zanzibar halafu akiamua kwenda Bara, aongezewe ushuru. Hili linaleta kutoelewana kwa watu wa nchi hizo. Kwa nini Afrika Mashariki wanafanya ushuru mmoja tu kwa nchi zote za Afrika Mashariki? Je, kumetokea nini kwa nchi moja kukawa na ushuru tofauti? Naomba Serikali ya Muungano kulirekebisha hili mara moja ili watu wawe na imani na nchi yao ya kuamini kuwa kero za Muungano zinatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya pili tena, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba kero za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi, ziarifiwe Taasisi pamoja na wananchi ili wapate kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kero ambazo hazijapatiwa ufumbuzi pia ziarifiwe Taasisi pamoja na wananchi ili wazielewe na wataweza kupunguza manung'uniko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, hususan kwenye eneo la Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya migodi kama *GGM* na ule wa *North Mara*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kwa masikitiko juu ya athari za uchafuzi wa mazingira ambao umepelekea wananchi waishio maeneo yale kuathirika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uchafuzi wa hali ya hewa *(Air pollution)* kwenye maeneo ya mgodi ambao unakaliwa na wakazi wengi ambao ni makundi ya akina mama wajawazito, wazee ambao wapo katika hatari kubwa ya magonjwa yatokanayo na vumbi linalomwagwa kwenye mkusanyiko wa kemikali zinazotumika katika uchimbaji, vile vile vumbi la vile vifusi ambavyo vinamwagwa karibu au pembezoni kabisa na makazi ya watu. Nataka Serikali iniambie, ni juhudi gani zimechukuliwa hadi leo licha ya kelele nyingi ambazo tumekuwa tunazipiga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kumekuwepo na uchafuzi wa mazingira kwa maana ya kelele *(noise pollution).*Hili nalo ni tatizo kubwa sana, kwani shughuli zinazofanywa na mgodi hupelekea watu wengi kuumwa na kichwa, masikio kuziba na hata kuwa na magonjwa ya masikio, kwani inapelekea watu kuongea kwa nguvu muda wote kama wendawazimu. Nimekuwa nikishauri siku zote kuwa yapasa wananchi wa karibu kabisa na maeneo wahamishwe kabla ya shughuli za uchimbaji kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kumekuwepo na madhara ambayo hutupelekea *physical injury* kwa wananchi na hasa wanafunzi, mfano, tukio la mwaka

2011 ambapo Polisi walipiga mabomu kwenye eneo la Shule ya Msingi Nyabigena ambapo pia lina changamoto ya uchafuzi wa kelele, uchafuzi wa hewa na kupigwa mabomu na Polisi na kuwajeruhi wanafunzi wawili macho na meno kutoka; vile vile wajawazito kuzirai na hata wengine kupelekwa kulazwa na kuharibu mimba. Naomba kujua kwa kina, Serikali imechukua hatua gani katika uchafuzi wa mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa sana na taarifa iliyotolewa kwenye hotuba ya Wizara ya mwaka 2012/2013, ambayo inadiriki kusema kuwa uchafuzi wa maji katika mgodi wa North Mara haukutokana na kuvuja kwa kemikali za mgodi wa *North Mara* kwenye ukurasa wa 90 mpaka 92, kuwa madhara ya wananchi wale, mifugo na mimea haikutokana na kuvuja kwa ile tindikali, bali ni matumizi ya madini tembo, na kuwa hamna ushahidi wowote wa kisayansi unaoonesha mahusiano kati ya athari za kiafya zilizojitokeza. Hii ni fedheha kubwa sana kwa Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tafiti za kisayansi zimefanyika na zinaonyesha ni jinsi gani ule uchafuzi wa maji ulivyopelekea madhara kwa viumbe hai kama mimea, wanyama, na binadamu. Tafiti hizi za kisayansi zimeainishwa vyema kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani, hata mwaka 2011 nilitaja baadhi ya tafiti hizi. Ukweli ni kwamba, kwanini haya madhara yajitokeze baada ya tindikali/kemikali ile kuvuja na kutiritika kwenye vyanzo vyetu vya maji na maeneo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishauri Serikali kwamba ijaribu kusoma tafiti nyingine ambazo

zimeainisha ni kwa kiwango gani kemikali mbalimbali zinazo/zilizokuwa zinatumiwa na mgodi zinaweza kusababisha madhara mbalimbali kwa viumbe hai wale kama vile madhara ya nywele, maini, ngozi, macho na sehemu mbalimbali, vilevile kwenye viumbe hai vingine kama mimea yote kukauka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu suala zima la Muungano. Maoni yangu ni kwamba, ili usawa uwepo, tuwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Tanganyika. Hii kwa maoni yangu itakuwa imeondoa manung'uniko yaliyopo sasa, itapunguzaa matumizi ya Serikali, na kila nchi itatakiwa kuchangia kwenye Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Mchango wangu utajikita sana katika usimamizi wa Mazingira. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, shughuli za kilimo, shughuli za kukata mkaa zimesababisha kwa kiasi kikubwa sana uharibifu wa mazingira. Nikitoa mfano, Wilaya ya Geita kwa sasa imeathirika sana kutokana na ongezeko la watu, shughuli mbalimbali za kukata mkaa ili kukidhi upatikanji wa nishati kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa wananchi wa Mijini na Vijijini. Nikirudi nyuma miaka 15 iliyopita, ukilinganisha na leo, athari za uharibifu wa mazingira zipo dhahiri sasa. Hali ya ukame kwa baadhi ya maeneo mfano Kata ya Bukoli, Nyamalimbe na sehemu nyingine katika Wilaya ya

Geita, zimeanza kuathirika. Kukauka kwa vyanzo vya maji ambapo miaka 15 iliyopita maji yalikuwa yakitiririka; na kwa hali ninavyoiona, kasi ya ukataji miti inaongezeka siku hadi siku. Hali hii inatishia usalama kwa kuwa mazingira yanapoharibiwa, mwisho wake ni ukame na matokeo yake ni njaa isiyokoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ina dhamira ya dhati ya kusimamia hifadhi ya mazingira, nashauri Wizara ya Nishati na Madini ibuni mbinu mbadala wa upatikanaji wa nishati vijijini kwa ajili ya kupikia. Mfano, matumizi ya *biogas* na matumizi ya nishati ya jua. Serikali iweke mkakati wa kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya nishati mbadala, sambamba na elimu, pia waletwe wataalam watakaoelimisha namna ya ya kutengeneza teknolojia ya *biogas* na *solar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kusimamia utekelezaji wa kutunza mazingira kupitia Halmashauri zetu. Naomba katika mwaka huu wa fedha tuweke msisitizo sana katika Halmashauri ili ziweze kutekeleza sheria hii. Bila kusahau katika Serikali za Vijiji, uwekwe msukumo mkubwa wa kuhakikisha kuwa sheria ndogo ndogo zinatungwa na kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mungano) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano tulionao ni muhimu, umeanzishwa kwa makusudi na waasisi wetu Mwalimu J. K. Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume. Lazima tuyaenzi mawazo yao, Muungano tumeziona faida zake nyingi, kama ni kero hizo chache, ni suala la pande zote mbili Bara na Visiwani kukaa na kuzijadili na hatimaye kuja kwenye makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile mawazo na michango ya Wabunge hapa Bungeni walivyochangia, michango ambayo hatimaye tunafikia muafaka na utekelezaji unaendelea: Swali ni Je, miaka ijayo watoto wetu waje watuweke kasoro na kutulaumu kwanini tulifikia makubaliano juu ya hoja hiyo na kufika utekelezaji?

Jibu ni hapana, watoto wetu wanatakiwa waje waondoe kero/kasoro ambao zitakuwa zimejitokeza wakati wa utekelezaji wa hoja za sisi wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, napenda kusemakwamba mazingira ni muhimu yatunzwe. Mkoa wa Rukwa hivi sasa unapoteza misitu kutokana na ufugaji holela unaofanywa na wafugaji wahamiaji hasa Wasukuma. Wasukuma wana makundi makubwa sana ya ng'ombe na kwa makusudi hukata miti/misitu ukiwauliza, eti wanasema, ni ili waweze kuwaona ng'ombe ni wapi wanakula, hasa wakiwa mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uharibifu wa hali ya juu. Natoa rai kwamba Kamati za Usalama na Ulinzi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zisimamie suala hili ili

kunusuru kuingiza nchi katika jangwa litakalotupelekea kufa kwa njaa kama Ethiopia, Somalia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa ufupi sana kuhusu Muungano unaoonekana kuwakera baadhi ya Watanzania ambao wana maono ya kutoitakia nchi hii mema.

Mheshimiwa Spika, Muungano ni ndoa. Ndoa ni kuvumiliana kwenye nyumba. Haiwezekani kukawa hakuna changamoto! Ni lazima tuvumiliane, tushughulikie changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuupime Muungano kwa mema yake na shida zake. Shida za Muungano zinazungumzika na ufumbuzi wake upo, ila ni *timing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na Muungano ni maangamizi yasiyokuwa na maelezo. Muungano ukivunjika ni mpambano kati ya Zanzibar na Pemba, patakuwa hapatoshi. Mtakimbilia wapi, huku hamkutaki, upande wa pili ni bahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba inakuja, tusubiri ili tuuboreshe Muungano wetu.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika suala la akaunti ya pamoja ya fedha, kwani ni miongoni mwa kero za Muungano ambalo linapelekea kwa upande wa Zanzibar kutopata gawio sahihi. Suala hili liliundiwa Tume, na Tume hiyo ilianza kazi mwaka 2004 na katika kazi za Tume hiyo ni kuhusiana na kuchambua mapato ya Muungano na matumizi ya Muungano. Kutokana na kazi hizo za Tume katika mapato pia kuna kiasi ambacho kinabaki na kwenda Hazina kwa upande wa Tanzania Bara pekee, wakati Zanzibar haipati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Wizara sasa ione kuwa ipo haja ya fedha zinazobaki na Zanzibar nayo ipate mgao/gawio katika pande zote za Muungano. Angalau kupata japo kiasi cha *share* yake ya asilimia 4.5 kwa kila mwaka wakati tunasubiri maamuzi sahihi kuhusiana na mgao huo. Pesa zinazobaki zitakapogawiwa, na Zanzibar nayo kupata mgao huo, kutapelekea kuondoa *deficit* katika bajeti ya Zanzibar. Kwani kwa bajeti ya sasa Zanzibar, ukiongeza na gawio la pesa zinabaki ambazo kwa sasa Zanzibar haipati kitu, itasaidia kuondoa tatizo la kutokuwa na pesa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, kutakuwa hakuna haja ya *budget support* kwa upande wa Zanzibar. Pia kutapelekea kuwa na pesa

za kutosha kwa Zanzibar na kusaidia kuinua uchumi wa Zanzibar na pia kupanda na kuongezeka kwa *GDP* ya Zanzibar ambayo itaiwezesha Zanzibar kuwa na hali nzuri kiuchumi, vile vile Zanzibar kuwa na uwezo wa kukopa pesa zaidi ya 4% katika Benki ya Dunia, kwani kwa sasa imeshindikana, kwa kuwa na hali ndogo kifedha/kiuchumi. Pia itasaidia kuondoa tatizo la *Deficit* ya bajeti kwa upande wa Zanzibar na pia uchumi wa Zanzibar nao kuwa katika nafasi nzuri, yaani kupiga hatua mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Tume iliyoundwa yafanyiwe kazi ili kufikia matakwa ya Muungano na pia matakwa ya Katiba kama ambavyo inaoneshwa katika Katiba Ibara ya 133 na ibara ya 134 ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo basi, Serikali kufanyia kazi kwa haraka mapendekezo ya Tume ya pamoja ya fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yameshafikishwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kuifanyia marekebisho sheria ya pamoja ya fedha ya mwaka 1996 ili kuondoa vifungu vinavyosababisha ongezeko la kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mafuta *(TPDC)* hutoa leseni za uchimbaji na utafiti wa mafuta pamoja na malipo madogo madogo yanayohusiana na *TPDC*, kwani inaonekana wazi kuwa *TPDC* haina sura ya Muungano na kuifanya kutokuwa na mamlaka yoyote kwa upande wa Zanzibar. Hivyo basi, napendekeza Zanzibar nayo iwe na shirika lake la kufanya utafiti wa mafuta na ambalo litakusanya mapato ya Zanzibar

peke yake bila kuihusisha *TPDC* kwa upande wa Bara. Kwani, haina mamlaka ya kusimamia vitalu vilivyopo Zanzibar. Kwa nini mafuta kuwa jambo la Muungano wakati Wizara inayosimamia ni ya upande mmoja wa Muungano? Ndiyo chanzo cha mgogoro!

**MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na nichukue fursa hii kuwasilisha maoni na ushauri wangu na hasa eneo la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni nyeti na ni muhimu kwa maisha yetu kama Watanzania na ikiwa ni sehemu ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa miti ni wa kasi kubwa sana na kwa hakika ni maeneo ambayo hata ya mabonde, bado miti katika vyanzo vya maji inakatwa, shughuli nyingine za kibinadamu zinaendelea na udhibiti wa maeneo, hata yale yaliyoainishwa kisheria, bado udhibiti na ulinzi wake unakiukwa au kuvunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria kufuata mkondo wake na ni muhimu kusimamiwa kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mchakato wa kujadili Muungano uangaliwe kwa makini wakati wa kujadili katiba yetu sanjali na yaliyomo kwenye katiba mpya ya Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuunga mkono hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi za mazingira ambazo zinamgusa kila mwananchi hapa Tanzania. Cha msingi ni kuelimisha jamii yote kuhusu utunzaji wa mazingira, wananchi au jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri tujikite katika kilimo cha umwagiliaji ili tuzalishe chakula cha kutosha, wananchi wasishawishike kukata miti kama chanzo cha kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wapewe elimu kutumia nishati mbadala kama mapumba ya mpunga kwa kuchoma tofali, waelimishwe kuwa na mashamba ya miti. Lakini yote haya, yanahitaji kuwezeshwa, kwani elimu inahitajika. Bajeti iongezwe kwenye utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchafuzi wa mazingira maeneo ya migodi ya Geita na *North Mara* linaelezwa kwa kupotoshwa kidogo hasa kuhusu vyanzo vya uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtaalam wa madini mwenye uzoefu wa kusimamia Sekta ya Madini, vyanzo vya uchafuzi wa mazingira vinatokana na uwepo wa elementi nzito *(heavy elements)* kama *Fe* (Chuma), *Ni* (Nikeli), *Mg (Manganese)* na nyingine. Hizi zinatokana na uwepo wake kwenye mawe nyenye dhahabu ambayo yapo kwenye maeneo hayo. Hata kabla ya kuanzishwa migodi kwenye maeneo hayo, *elements* hizo zilikuwa juu na maji ya maeneo hayo yalikuwa na *heavy elements.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zebaki *(Mercury),* uchafusi huu unatokana na uchimbaji mdogo wa maeneo hayo, kwa sababu migodi mikubwa haitumii zebaki kuchejua dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kemikali nyingine inayochafua mazingira isipotunzwa mahali pake ni *cyanide*. Kemikali hii ni hatari sana, na huhitajika kutokuruhusika kuingia kwenye mazingira kwa kuwa huwa pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kemikali hii ndiyo inayotumika na migodi mikubwa kuchujua madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana migodi kuhakikisha mazingira hayachafuliwi kwa kusimamia vyema ili mazingira yawe salama. Kusema uchafuzi wa mazingira wote unatokana na kemikali zinazotumika migodini, siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa maelezo hayo ili Serikali itoe elimu hii kwa Waheshimwa Wabunge ili sote tusaidie kusimamia usalama na usafi wa mazingira.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania sasa imekuwa damu moja tangu tulipoungana tarehe 26 Aprili, 1964 ambapo Mwalimu J. K. Nyerere na Mheshimiwa Karume alipoketi na kuunganisha Tanganyika na Zanzibar, kwa umoja wetu sasa Tanzania Bara na Zanzibar watu wake imekuwa ni kitu kimoja. Pia watu wameunganisha familia, maana yake Tanzania Bara watu wake wameoa na kuolewa Zanzibar. Pia Zanzibar watu wake wameoa/kuolewa Tanzania Bara, kwa hiyo basi, tumekuwa damu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nashangaa kusikia kuna watu wanataka Muungano kuvunjwa. Hili ni wazo ambalo ni gumu sana kwa Watanzania wa sasa, kwa sababu ya kuungana kifamilia ingawa tunasema kuna mambo ambayo tumeungana kama vile Jeshi, Elimu ya juu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Muungano usivunjike isipokuwa kuna mambo ambayo yanatakiwa kubadilishwa katika Muungano wetu ili kuwa imara, kwa mfano kutoa ushuru wa bidhaa ambazo zinatoka Zanzibar na kuingia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuingiza mambo mapya katika Katiba ya Jamhuri ya Muugano ambayo yanaweza kuimarisha Muungano wetu.

Serikali isijihusishe na masuala ya udini, kwa sababu Serikali yetu haina dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuchangia kuhusu mazingira. Katika nchi yetu bado mazingira hayaridhishi, bado watu hawajitumi katika kulinda mazingira yetu wala hawathamini. Kwa mfano, Mji wa Dar es Salaam bado ni Mji ambao ni mchafu mno/sana. Mifereji ya maji machafu bado haijaimarishwa, nyumba hazijajengwa kwa kufuata *plan* ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa ya Kusini na sehemu nyingine mwa Tanzania, bado wanashindwa kuheshimu mazingira yao. Kwa mfano, ukataji wa miti ovyo, utunzaji wa mito, kulima sehemu ya mabondeni/kwenye vyanzo vya maji, ufugaji holela hasa ufugaji wa ng'ombe hado hauna utaratibu wa utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba watu wafundishwe zaidi kuhusu utunzaji wa mazingira hasa ukataji wa miti ovyo au kukataji miti kwa ajili ya mkaa.

- Kufuga wa kufuata sheria za nchi yetu inayohusiana na ufugaji;

- Kuheshimu vyanzo vya maji;

- Kutunza mazingira ya miji yetu hasa Jiji la Dar es Salaam ni chafu mno;

- Kuwepo na wiki ya usafi kwa kila mwezi; na

- Kutumia gesi kwa matumizi ya nyumbani badala ya kutumia mkaa.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kwa maandishi, kuhusu hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii ili ipate nafasi ya kushughulikia mapendezo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano limekuwa la muda mrefu, lakini inavyoonyesha, aina ya Muungano tulionao haukui. Tunahitaji Muungano unaokua, yaani kisiasa na kiuchumi. Serikali hizi mbili ziwe na dhamira ya dhati katika kuona pande zote mbili zinapata faida ya Muungano katika nyanja za kisiasa na kiuchumi bila kutegemea upande mmoja. Muungano ulianza kwa maeneo machache, basi baada ya miaka 50 tukitaka Muungano uwe imara, ni vizuri tukaongeza maeneo ya ushirikiano hata tufikie nchi moja. Najua tutatoa maoni kwenye Katiba mpya, lakini tuanze kuchukua hatua kwa kutengeneza mazingira yatakayotufikisha kuwa nchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mazingira, tunahitaji kuongeza bajeti ya kupanda miti kuanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, maeneo yote yanayoweza kupandwa miti tufanye hivyo. Miji yetu mingi imeachwa vichaka bila kuwa na miradi endelevu ya kupata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sheria za kutunza miti na vyanzo vya maji zipo, lakini hazisimamiwi kwa sababu siyo rafiki wa wale wanaovunja sheria pamoja na wanasiasa wanaotumia wananchi hao kwa maslahi ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha wananchi wawe wanakata miti ovyo bila udhibiti, nchi yetu itakuwa jangwa baada ya muda siyo mrefu. Tulete sheria kali zaidi na tuzisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, tuongeze bidii ya kuwekeza kwenye nishati mbadala na hii ionekane kwenye bajeti ya Serikali na siyo nadharia tu. Kuwe na mikakati endelevu na wananchi wapewe elimu ya mazingira katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya matumizi bora ya ardhi kwa wakulima na wafugaji, lazima tulipe kipaumbele. Tuzuie kulima, ufugaji wa mifugo ya makundi makubwa kwa kuhamahama, maana yake tunakuwa tunaruhusu uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kiwe cha kisasa zaidi, kinachotumia maji kidogo kuliko cha sasa ambacho maji ya mto yote yanaishia kwenye shamba na hayarudi mtoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pendekezo kwamba wataalam wa mazingira watembelee China

ili kujifunza namna nchi ile inavyolishughulikia suala la mazingira kuanzia ngazi za Vijiji mpaka Mijini.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni nyeti sana. Ingawa hivi sasa Muungano unakaribia kuwa na umri wa miaka 50, lakini kuna mambo ambayo nayaoufanya Muungano huu uwe wa kero badala ya starehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Muungano ndiyo matatizo. Ni vyema ukarekebishwa kwa kuleta unafuu kwa wananchi wa pande zote mbili. Muungano ulikuwa ni wa mambo 12, sasa umekuwa na mambo 32, kwa amri ya nani? Haieleweki! Hivyo, ili kubadilisha mfumo, kila nchi iwe na Serikali yake kwa maana kwamba kuwe na Serikali mbili. Moja ya Zanzibar na ya pili ya Tanganyika.

Tena Serikali hizi ziwe na mamlaka yake na hata kiti chake cha *United Nation*. Serikali ya Zanzibar tunataka Rais wa Zanzibar ajulikane anapotoka nje ya nchi kwamba huyu ni Rais wa Dola ya Zanzibar. Hata hivyo, kuwe na Muungano wa Mkataba ambao huo utakuwa ni wa baadhi ya mambo tu na siyo kuingiliana katika Serikali. Vile vile Serikali hizi mbili zikichokana, ni vyema kuachana kwa uzuri tukiwa kila nchi inaendelea na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Account* ya pamoja, hili ni tatizo kubwa na mpaka leo bado halijatatuliwa. Kwa nini haieleweki? Namwomba Waziri aje atueleze, kwa nini mpaka leo kuna ugumu huo?

Kwa lugha nyingine, Serikali ya Tanganyika bado wanawala kivuli wa Zanzibar; na Wazanzibar wa jana, sio wa leo. Wa leo wanafahamu nini kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Katiba ni Tume inayoangaliwa kwa macho makubwa, ni Tume yenye Wajumbe kutoka sehemu zote mbili, hivyo suala kubwa kwa wananchi wa Wazanzibar ni kutaka kuzungumzia Muungano na jinsi wanavyoutaka. Kutokana na hilo, Tume iwe makini katika maelezo ya wananchi na jinsi ya majumuisho yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero ya wafanyabiashara ya kulipishwa kodi ya magari hasa mara mbili, na tatizo hili ni kati ya kero ambazo zimekwishatatuliwa, lakini bado kero hii inaendelea. Hata hivi juzi Naibu Waziri wa Fedha alipoulizwa suala hili, alikubali kwamba bado kero hii ipo, lakini ni lini Waziri atamaliza? Hebu akifanya majumuisho atueleze ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero kubwa kwa Mabalozi, Serikali ya Zanzibar inakosa kupata Mabalozi katika nchi za nje, hii ni kusema kwamba 95% ya Mabalozi ni kutoka Tanganyika. Je, Serikali ya Zanzibar haina watu wanaofaa? Huku ni kuumizana na kuleta matatizo. Ni vyema Zanzibar iwe na Serikali yake, Mabalozi wake na kiti chake. Hii itasaidia kama nchi za Ulaya, *Emirates* zilivyoungana kwa baadhi ya mambo na huku kila nchi ikiwa na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rada ni suala la Muungano, hivyo Zanzibar ipewe haki yake na fedha

zake watumie kwa shughuli za elimu kama ilivyokubalika huko Uingereza.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kunijalia afya na ufahamu wa kuweza kuandika, kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano maana yake ni udugu, upendo, heshima na huruma. Tukizingatia haya, Muungano utaimarika na utavutia. Hivyo utaonekana na kila upande kuwa ni mzuri. Kuyapuuza haya, ndiyo chanzo cha wasiwasi, hofu na mashaka, kuwa Muugano siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi kabla ya kuwa kiongozi (Mbunge) nilikuwa na imani na Muungano. Hata sasa baada ya kuwa Mbunge nimeona zaidi faida ya kuwepo Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni mwakilishi wa watu, sina budi kueleza maoni kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibar wote takriban wa Visiwa vya Unguja na Pemba wanataka Muungano uwepo, lakini uimarishwe. Sasa ni vipi utaimarisha Muungano?

Kwanza, Kuondoa kero zote ambazo ni sababu ya kukwaza maendeleo ya pande mbili. Kila upande uwe na nia njema na mwenzake; kuoneana huruma na

kusaidiana kwa dhati, kuwa na uwazi *(transparency)* kwa mamlaka ya kila upande; nafasi ya Zanzibar kutambulika Kimataifa; mafuta na gesi isiwe suala la Muungano; Mgawanyo wa mapato, asilimia 4.5 haikidhi haja ya Muungano; kuwepo na *account* ya pamoja; bidhaa zitokazo Zanzibar kulipishwa kodi mara mbili zinapoingia Tanzania Bara; Kuwepo na usawa (uwiano unaolingana) kwa watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, ni lazima tuwe na nia safi katika Muungano wetu kurekebisha kasoro zote zilizopo na zinazoendelea kujitokeza ili kunusuru maadui kujipenyeza na kuleta chokochoko zisizo na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia mchango wangu kwa kusisitiza kuwa kero za Muungano zisiachwe bila ya kutatuliwa mpaka zikapata watoto na wajukuu. Kila kero ikijitokeza, itatuliwe haraka ili kuudumisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. SHAWANA BUKHET HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongezea mchango wa maandishi baada ya kuwa sikumaliza hoja zangu wakati nachangia kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya *TRA* kutoza kodi mara mbili ni kweli suala hili ni kero inayoendelea, bidhaa zinazotoka Zanzibar watu wanatozwa mara

mbili mbili suala la magari. Wiki mbili zilizopita kuna mtu kaja Dar es Salaam harusini, kachukua perfume tisa, katakiwa atoe ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika Baraza la Wawakilishi kumejitokeza tena tatizo la *OIC* kuwa Zanzibar ilitaka kujiunga ikakataliwa, lakini Tanzania Bara walisema watajiunga wao. Kinacholeta tatizo ya kuwa mpaka hii leo Tanzania Bara haijajiunga, kwa nini basi, kama hawataki kujiunga, ziandaliwe taratibu ili Zanzibar ijiunge? Hali ya uchumi ya Zanzibar siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu Zanzibar hivi sasa tunategemea utalii na Karafuu. Leo Karafuu ikiisha nchini, uchumi umeanguka, na utalii, watalii wakiamua wasije, uchumi umeanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi sasa takriban miaka 47 nchi yetu imeendelea kufurahia uwepo wa Muungano ambao ni wa pekee kabisa duniani kote. Pamoja na uwepo wa huu Muungano, lazima tujaribu kuangalia kwa makini yale masuala yanayoweza kutuyumbisha au kuleta nyufa miongoni mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kero za Muungano zimekuwa wimbo maarufu kwa pande zote mbili za Muungano. Suala hili limeshazungumzwa mara nyingi, tena kwa kurudiwa rudiwa. Lakini cha kustaajabisha ni suala hili kuendelea muda wote huo bila kwisha. Swali linaloweza kujitokeza ni: Je, kitu gani

kinakwamisha jambo hili kufikia tamati? Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete wakati akilihutumia Bunge, alionesha dhamira ya dhati kulitatua bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wa Muungano nao umekuwa ni msamiati unaozidi kukolea vichwani mwa watu. Zaidi ni kwamba suala hili linaonekana kana kwamba ni Maandiko ya Biblia/*Quran* hata kujaribu kulitafutia ufumbuzi kwa kulizungumza, halipewi nafasi. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumeibuka mjadala mzito juu ya Muungano hasa kwa upande wa Zanzibar. Inavyoonekana, Serikali bado inajaribu kuzima hizi hoja kwa kisingizio cha kuwa, wale wanaotoa maoni ni wahuni. Kwa kufanya hivyo, ni hakika kuwa suluhisho halitapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupendekeza yafuatayo, kwamba, ni wakati muafaka kuketi kitako na kutatua hizi kero za Muungano ambazo zimedumu karibu nusu karne sasa. Serikali ioneshe nia ya kweli katika hili.

Suala la Muundo wa Muungano ni vyema nalo likatazamwa upya, ikiwezekana kura za maoni zipigwe ili wananchi waamue. Au nafasi ya kubadilisha katiba itumike kwa ukamilifu bila ya Serikali kuwakataza wananchi kuujadili Muungano.

Serikali itege sikio tena kwa umakini na kuchukua hoja zote zinazotolewa na wadau mbalimbali nchini

zikiwemo zile za uamsho. Kwa njia hii, Serikali itakuwa imejenga imani kwa watu na kuleta utulivu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake. Napenda kuchangia katika bajeti hii kwanza katika Sekta ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sekta muhimu inapewa msisitizo mkubwa kinadharia, lakini kwa vitendo tunaelekea pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira kwa ujumla ni sekta pana mno, kuna maeneo katika sekta hii muhimu ambayo inabidi yafanyiwe kazi mapema kabla Taifa halijaingia katika janga kubwa la jangwa; na maradhi yanayotokana na uchafu wa mazingira na kukosa nishati ya matumizi ya nyumbani (kupikia) hasa huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kuwa sheria zote kuhusiana na mazingira zipo, isipokuwa hazitekelezwi. Ni muhimu sana tukaangalia namna ya kutekeleza sheria hizo kwa kushirikisha wadau wote na kuhakikisha Watendaji wote ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vitongoji wanatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunapanda miti, tunatoa taarifa mbalimbali juu ya kuboresha mazingira, lakini mafanikio ni madogo. Viongozi mbalimbali wa Serikali katika eneo husika wapo, na vitendo vya uharibifu wa mazingira vinafanyika mbele ya macho yao na hawachukuliwi hatua. Serikali ifike

mahali iweke kigezo cha mazingira kuwa moja ya sifa ya mafanikio ya kiongozi katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ianze kutumia makaa ya mawe katika Taasisi mbalimbali za Umma. Mfano, Shule zote za Msingi, Sekondari, Vyuoni na pia katika Hospitali zote za Wilaya na Mkoa pamoja na Magereza yote nchini. Ni rasilimali ambayo ipo kwa wingi nchini na inaweza kutumika vyema, kote na itahamasisha wadau wengine kufanya hivyo pia. Taasisi hizo za umma zinachangia kwa sehemu kubwa katika uharibufu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza Serikali iangalie kwa kuhusisha Wizara zote husika kutumia nishati mbadala. Tutumie makaa ya mawe ambayo tunayo kwa wingi sana katika Taasisi zetu, na kwa upande wa Magereza iwe mfano wa kutumia teknolojia ya *(Bio-latrine)* biogesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishati mbadala kwa kutumia jua *(solar power)* na upepo *(wind power)* itumike kuleta mabadiliko ya kiuchumi, lakini pia kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya upandaji miti iongezwe hasa katika maeneo ya milima na vyanzo vya maji, pia maeneo ya kando kando ya mito, maziwa, maeneo ya kuvuna maji *(catchment areas),* tuhimize upandaji wa miti ya matunda ili wananchi wapate kipato na wasiendelee kulima mazao ya msimu na pia ufugaji wa nyuki. Kama mwanadamu

anaweza kupata mapato na kufaidi mazingira bila ya kuyaathiri atatunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopo zitumike na viongozi husika na wakishindwa kutekeleza wachukuliwe hatua wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine na kwa umuhimu wake, tunaishauri Serikali iangalie kanuni za Sheria ya *GMO*, kwani inatunyima fursa ya kufanya tafiti zinazohusisha teknolojia ya *GMO*. Fursa hii tukiikosa, wataalam wetu waliosoma watabaki walivyo na nchi zinazotuzunguka zitaendelea na kutuacha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zimefanikiwa kiuchumi kwa kutumia *GMO,* teknolojia mfano China, India katika pamba, wameweza kuongeza uzalishaji kutoka kilo 400 hadi 600 kwa ekari, hadi tani mbili kwa ekari na kupunguza kutumia viatilifu ambavyo vimeongeza afya ya wakulima wao waliokuwa wanaathirika na viatilifu. Lakini nchi hizo zilizokuwa zinaagiza pamba kutoka nje ya nchi *(import)* leo wanasafirisha *(export)* nje. Nchi nyingi pia Afrika wanatumia teknolojia ya *GMO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *Water Efficient Maize for Africa (WEMA)* pia unaweza kukwama kwetu kama kanuni zetu hazitarekebishwa. Nchi za Kenya, Uganda, Msumbiji na Afrika Kusini tayari wako katika hatua mbalimbali za utafiti, lakini sisi hatujaanza kutokana na kanuni hasa inayohusu *(liability)* madai na fidia katika kipengele hicho. Hata leo, vyakula vingi

mfano ngano, sukari tunayoagiza nje ya nchi ni *(GMO)* iliyotokana na teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kanuni irekebishwe angalau tufanye tafiti na hapo baadaye tukiridhika, ndipo tufanye marekebisho ya sheria kutumia kibishara. Kwa sasa ilenge utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na kutaka mafanikio katika Mazingira na Muungano wetu.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. Pamoja na kuwapongeza Mawaziri wetu kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika Wizara hii na kwa ushirikiano na wataalam na Watendaji wao, napenda kuchangia katika maeneo ya Muungano na Mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza viongozi wetu walio waasisi, Marehemu Mwalimu Julias K. Nyerere na Marehemu Sheikh Abeid A. Karume. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, napenda kusisitiza Serikali zetu zote mbili kuudumisha Muungano wetu pamoja na kurekebisha kero zilizobakia ili wanachi waweze kuupenda na kuuthamini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu juu ya Muungano wetu inatakiwa kwa ukamilifu kwa sababu wananchi wengi hawauelewi Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Muungano udumu milele kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mazingira, naiomba Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wakazi wanaoishi pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro kuendelea kuulinda Mlima wa Kilimanjaro na kuachana na kukata miti ovyo, maana kukata miti kutausababishia mlima huu jangwa, mlima ambao ni kivutio cha watalii ambao wanaiingizia fedha za kigeni nchi yetu kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wanaouzunguka mlima huu wana tabia ya kuchoma moto na ukataji wa miti kwenye kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara kuhusu kulipa kodi mara mbili Mheshimiwa Waziri aliahidi katika bajeti iliyopita kwamba suala la wafanyabiashara kulipa kodi mara mbili atalipatia ufumbuzi. Lakini la kusitikisha, mpaka leo hii mizigo iliyotoka nje kwenda Zanzibar ambayo tayari yashalipiwa kodi kule Zanzibar mizigo hii ikija Bara hulipiwa tena na kama huna pesa, mizigo huwa inabaki Bandarini mpaka ilipiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulitaka upatiwe ushahidi ikiwa jambo hili kweli linatendeka, umepatiwa ushahidi wa kuletewa risiti chungu nzima ambazo mizigo hiyo imelipiwa mara mbili, lakini mpaka hii leo hujachukua hatua yoyote, kwani ungechukua hatua. Hili jambo lisingeendelea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ushahidi wa risiti bado hujauamini: Je, unataka ushahidi wa Mnyamwezi? Kwa kuwa hili ni moja ya kero za Muungano, naomba Waziri hii leo wakati wa majumuisho akemee suala hili au alipatie ufumbuzi kwa kuwaambia wafanyabiashara wote wanaoleta mizigo Bara ambayo tayari mizigo hiyo ishalipiwa ushuru ikija Bara isilipiwe tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ajira katika taasisi za Muungano, bado hazijapatiwa ufumbuzi na ushahidi umepatikana hii leo kwenye kipindi cha maswali wakati Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alipotakiwa kusema askari wangapi wa Jeshi la Polisi walioajiriwa mwaka 2011/2013 na akajibu kuwa ni asilimia tano tu kwa askari wote walioajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *percentage* ndogo sana. Vijana wengi tu wapo Zanzibar, ambao wanataka kuajiriwa. Nikukumbushe tu, wakati wa Zanzibar na Tanganyika tulipoungana, tumeungana nchi ya Zanzibar na nchi ya Tanganyika bila kujali ukubwa na idadi ya watu. Hii asilimia tano ni ndogo mno, angalau ingekuwa asilimia 20. Kwa hiyo, hii ni kero moja ya Muungano wakati hivi sasa tumejipanga kutatua kero za Muungano, lakini bado mnazizimisha

hizi kero. Pale Wazanzibar wakisema hawataki Muungano, ni kwa sababu ya hizi kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili lipatiwe ufumbuzi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Bilal kwa jinsi ambavyo amekuwa akijitoa kwa hali na mali katika kutuelekeza na kutembelea maeneo mbalimbali nchini na hasa katika kuhimiza juu ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga, pamoja na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wangu tu ni juu ya kuimarisha umoja wetu. Ni vyema suala la watu wenye imani tofauti za kidini, tushirikiane na kuheshimiana kuleta vurugu kwa imani nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano bado ni jambo jema hasa ikizingatia kuwa tumeshazoeana na hata shughuli zetu zipo pande zote Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kupitia mchakato wa Katiba, kasoro zilizopo zizingatiwe na kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, *shares* za *carbon credit* ziwe kwa uwepo na namna ya kuzipata iwe wazi ili wengi (Mikoa) mingi inufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia usafi wa mazingira, Wizara isaidie kupata vitendea kazi kama magari maalum ya taka ili kuzisaidia Halmashauri na Manispaa. Mkoa wa Rukwa uliomba kusaidiwa kupata gari katika risala yao wakati amekuja Mheshimiwa Makamu wa Rais, Sumbawanga Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ilikuwa finyu. Tumeweka katika maombi maalum, endapo kutapatikana msaada katika eneo hilo tafadhali tusaidiwe.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Muungano na ile ya Mazingira kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa mazingira ni muhimu kwa ustawi na maendeleo yetu. Mchango wangu unalenga katika hifadhi ya mazingira ambayo yanaharibiwa kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Mazingira ijenge na kuimarisha mfumo wa kiutendaji ambapo katika ngazi za Wilaya, Tarafa, Kata na Kijiji

watakuwepo Watendaji ambao pamoja na majukumu yao mengine, watawajibika na kusimamia udhibiti na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo la uharibifu wa mazingira, Wilaya ya Muleba mwaka huu (2012) imeshuhudia mvua za masika zikikaribia msererekο wa ardhi *(land slide)* hii ni hatari au maafa ambayo tumekuwa tukisikia nchi za Amerika Kusini na jirani zetu Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, undani wa tatizo tajwa hapo juu, ni utamaduni wa binadamu kuharibu mazingira. Kwa Muleba watu wanakata miti hovyo. Baya zaidi, wanakata na kung'oa miti ya asili. Shughuli za binadamu zinazohusisha kung'oa mawe kwenye miteremko kwa ajili ya shughuli za ujenzi na kilimo kisichozingatia mkingamo limekuwa ni chanzo cha tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kuwa, Serikali iandae mpango wa kudhibiti na kuhifadhi mazingira. Zaidi ya mpango ni kuwa na watendaji watakaobeba majukumu haya. Watendaji hawa wawezeshwe ili kumudu majukumu haya. Kinyume cha hapo, tuwajibishane. Suala la mazingira ni muhimu na lipewe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine katika kuboresha mazingira, ni kutumia mtandao wa Shule kuanzia msingi mpaka Vyuo. Taasisi hizi zilenge zaidi katika upandaji wa miti, zaidi miti ya vivuli, matunda, kuni na mbao. Serikali za Vijiji nazo zinayo nafasi kuhami

maeneo ambayo matumizi mabaya yanaweza kuleta madhara. Hii ni pamoja na sehemu za miteremko, vyanzo vya maji na kingo za mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Muungano. Muungano wa Tanzania ni muhimu na ni bora ukaendelea kuwepo. Ushauri wangu ni kuwa kero au changamoto zilizopo na zitakazojitokeza zijengewe utaratibu wa kuzipatia suluhu. Bila kuingia kwa undani wa malalamiko moja baada ya linguine, tatizo kubwa la kero za Muungano ni ubinafsi. Muungano ni umoja na umoja maana yake ni watu mmoja mmoja kujali maslahi ya umoja wao kuliko kujijali.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kutoa hotuba nzuri katika Bunge letu. Ninayo machache ya kuchangia hotuba ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashindwa kuelewa kabisa, ni tatizo gani limeikumba Wizara hii (mazingira) hadi tunashindwa kulinda mazingira yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji miti, kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais ni kupanda miti kama wendawazimu, akimaanisha tupande miti kadiri ya uwezo wetu ili baadaye tufaidike. Wizara hii na Waziri mhusika aje na mpango madhubuti wa kupanda miti nchi nzima kwa kipindi cha kati na kirefu. Kwa kuanzia, Serikali ishirikiane na TAMISEMI na ikibidi ipeleke *desk officer* Halmashauri, ambaye atahakikisha kuwa kila

Mtendaji wa Kata, Kijiji na Kitongoji, anasimamia upandaji miti katika kila kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yoyote mbali na kupanda miti, hayana nafasi tena. Tunataka tuone mkakati mzuri unaotekelezeka haraka iwezekanavyo, kwani hatuna sababu yoyote ya kutopanda miti wakati wenzetu duniani ikiwemo hata nchi jirani ya Rwanda na Kenya wamefaulu katika upandaji miti. Mfano mzuri ni ule anaoutumia Mkuu wa Mkoa wa Kagera - Mheshimiwa Kanali Mstaafu Fabian Masawe. Yeye ameamua kuufanya Mkoa wa Kagera kuwa *green belt*. Mkuu huyu wa Mkoa alipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Karagwe aliotesha miche na kuwagawia wananchi wa Wilaya ya Karagwe, sijui fungu hilo lilitoka wapi. Lakini juhudi zake zimesaidia kuongeza idadi ya miti Wilayani Karagwe. Hivi sasa anao mkakati wa kupanda miti Mkoa wa Kagera kwa *style* hii. Huu ni mfano tu wa kiongozi mmoja mwenye ukereketwa wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa inageuka jangwa, mito inakauka, Mlima Kilimanjaro barafu inayeyuka. Serikali iache visingizio, tupande miti, Wabunge tuhamasishe upandaji miti. Mimi mwaka 2011 nimepanda miti laki moja Jimboni Karagwe.

Waheshimiwa Wabunge, wengine tupande miti, watumishi wa Serikali pia waajiriwe, Maafisa Misitu katika kila Kijiji ili wasimamie upandaji miti na ukataji miti. Maafisa hawa wapewe malengo ya kutimiza na pia wahakikishe miti haikatwi ovyo bila kibali maalum na baada ya kibali maalum na baada ya mhusika kupanda miti kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ulindwe kwa maslahi ya Taifa letu kwa kutatua baadhi ya kero za Muungano ambazo bado hazijatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kujikita zaidi kwenye suala la mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara hii kutoa elimu kuhusu tatizo hili kwa vikundi mbalimbali, bado kuna haja kubwa ya kuwashirikisha wananchi wote wa Tanzania kujihami na tatizo la tabianchi kwa vitendo. Kwa mfano, wananchi wa vijijini wahamasishwe kupanda aina madhubuti ya miti ambayo watatumia kama chanzo cha mkaa. Kuna aina za miti ambayo inafaa kwa mkaa. Ukizingatia kuwa mkaa wake huwa ni imara na kutumika kiasi kidogo ukilinganisha na miti mingine, hivyo naishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kufanya utafiti kuhusu miti itakayoisaidia kupunguza kasi ya tatizo la tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima izingatiwe kuwa wananchi waishio vijijini wataendelea kutumia kuni na mkaa kwa kupika. Hivyo ni vyema ufumbuzi wa kuhifadhi mazingira uzingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la tabianchi husababishwa na mvua, ukame mafuriko, ongezeko la joto, ongezeko la kina cha bahari na

kadhalika, mambo ambayo hayatabiriki. Ni lazima Serikali kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais itenge mfuko maalum kwa ajili ya maafa yanayoweza kutokea wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la Muungano. Suala hili limezidi kuonekana kuwa na utata kila kukicha. Hii ni kwa sababu Serikali zote mbili hazijaamua kuuzungumzia Muungano kwa uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kabisa kwamba Muungano wetu lazima uendelee kuwepo, lakini vilevile ni lazima pande zote mbili ziwe tayari kujadili mafanikio pamoja na matatizo ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuko kwenye mchakato wa Katiba mpya, ni lazima pande zote mbili ziujadili tena Muungano kwa kina ili kuepusha minong'ono ya baadhi ya wadau wa Muungano huu. Endapo tutatekeleza hili, hakika Muungano wetu utadumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban sasa ni zaidi ya miaka 48, bado Tanzania Bara wanalalamikia Muungano. Muungano unaonekana kuwa ni wa Viongozi na siyo wa wananchi. Viongozi ndiyo wamekuwa watetezi wakubwa wa Muungano na siyo wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Jamhuri ya Muungano hujadili hata mambo yasiyo ya Muungano kama afya, kilimo na kadhalika. Lakini Baraza la Wawakilishi wao wanazungumzia na kujadili mambo yanayowahusu Wazanzibar tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa akaunti ya pamoja, mgao wa mapato kwa Wazanzibar, asilimia 45 ni yale yale mapungufu ya muda mrefu ambayo yanalalamikiwa na wananchi wa pande zote, lakini hasa Wazanzibar. Baada ya kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, hadhi na nafasi ya viongozi wa Zanzibar hasa Rais wa Serikali ya Mapinduzi yanayumba, huwa anaangaliwa kama Waziri anapokuwa katika ardhi ya Tanzania Bara, lakini kiitifaki anakuwa ni watatu baada ya Rais wa Muungano na Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano unalalamikiwa pia kwa upande wa rasilimali. Wazanzibar wanataka mafuta na gesi yaondolewe kwenye Muungano. Kuzuiwa kwa Zanzibar kujiunga na *OIC* kunaongeza manung'uniko kwa Wazanzibar na kujihisi kuwa Serikali ya Muungano haiwatendei haki. Suala hili la *OIC* linalalamikiwa pia na Watanzania Bara (Waislam) ambao wanaamini kama Tanzania ingejiunga na *OIC* ingepata mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote kwa pamoja wanahisi kurudishwa nyuma kimaendeleo, Muungano unadumaza michezo hasa mpira wa miguu, mpira wa pete, riadha na kadhalika. Michezo hii mara nyingi

hukumbwa na misukosuko ya malumbano na uteuzi wa upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachangia kwa kiasi kikubwa kwa kuweka kodi kubwa kwenye umeme, mafuta na kusababisha wananchi kukata miti hovyo kwa matumizi ya kuni na mkaa. Hali hiyo husababisha maeneo mengi kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kuhamahama nao husababisha mmomonyoko wa ardhi kutokana na mifugo mingi inayozagaa kwa kutafuta malisho. Viwanda hutiririsha maji yenye kemikali na kuchafua hata maji yanayotumiwa na viumbe hai wakiwemo binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la magari na mitambo nayo husababisha ongezeko la joto na uchafuzi wa mazingira. Serikali na baadhi ya miji, Manispaa na Majiji kutopewa viwanja vya kutosha na kusababisha wananchi kujenga nyumba bila kufuata utaratibu jambo ambalo huchafua mazingira kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhifadhi na kulinda mazingira yetu kwa Serikali kutimiza majukumu yake ya usimamizi na kuwawezesha wananchi kwa kuwapunguzia gharama ya maisha ili wapunguze kama siyo kuacha kabisa kukata miti ovyo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo: gawio la asilimia 4.5 (ukurasa 17).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado zipo fikra hasa miongoni mwa Wazanzibar wengi kwamba gawio hilo ni kiasi kidogo sana. Kwa kuwa zipo fikra hizo, napenda kushauri kama ifuatavyo: Moja, Serikali iwaeleze hao wanaolalamika namna ambavyo *formula* ya mgawanyo ilivyofikiwa. Pili, Serikali itoe elimu zaidi kuhusu msingi wa gawio hilo ili kuondoa dhana mbaya iliyojengeka miongoni mwa baadhi ya Wazanzibar kwamba wanapunjwa na Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo fikra za baadhi ya Vyama vya Siasa na baadhi ya Wazanzibar kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haukuwa na ridhaa ya wananchi wengi kwamba, maamuzi haya makubwa yalifanywa na viongozi wa juu tu. Harakati za maandamano huko Zanzibar zilizoongozwa na wana uamsho hazipaswi kupuuzwa hata kidogo. Kundi hilo linapinga kwa uwazi kabisa aina ya Muungano uliopo. Kwa ujumla, Wazanzibar wengi wanaona nchi yao kunyimwa fursa za kujiunga na Taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa huchangiwa na wao (Wazanzibar) kuwa kwenye Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chokochoko na kelele zilizopo sasa hazipaswi kupuuzwa hata kidogo. Kuendelea kung'ang'nia kwamba Muungano ni wa kihistoria, hakuna wa kuuvunja na wakati hata humu ndani ya Bunge vipo viashiria vya kuukataa Muungano, ni kujidanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, itumike busara kubwa, na kikubwa zaidi ni kuitisha kura

ya maoni kwa Wazanzibar wote, waseme kupitia kura, wanautaka Muungano huu na kwa sura hii au vipi? Kwangu mimi hili ndilo litakuwa suluhisho la kudumu. Aidha, najua kwamba lipo zoezi ambalo linaanza hivi karibuni la kupata maoni kuhusu Katiba ambayo Watanzania wanaitaka, zoezi linaloendeshwa na Tume ya Katiba. Ni kweli baadhi ya Wazanzibar na Watanzania watatoa maoni kuhusu aina ya Muungano. Hata hivyo, naamini watakofikiwa ni wachache sana kwa kuzingatia kwamba muda wa Tume kufanya kazi ni mfupi sana. Kura ya maoni ndiyo suluhisho la kutoa picha/sura halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika sana kama tunafanikiwa sana katika zoezi la utunzaji mazingira. Leo hii nani sio shahidi kwamba misitu yetu hasa ile ya asili inafyekwa sana kwa ajili ya uchomaji mkaa? Kwa mfano, njia nzima kutoka Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Chalinze, Segera na kadhalika, imejaa mikaa! Je, sani amejali? Maana hata Mawaziri ni mashahidi juu ya hali hii. Serikali imechukua hatua gani? Naamini zinahitajika jitihada zaidi ili kuokoa mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua ya kupiga marufuku matumizi ya mfuko ya plastiki. Nashauri mifuko yote ya plastiki hata hiyo ya vifungashio ambayo tunaelezwa kwamba itaruhusiwa, yote ipigwe marufuku. Viwanda vitafute vifungashio vya aina nyingine, siyo mifuko ya plastiki, maana madhara yake kwa mazingira ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuchangia katika Bunge lako Tukufu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nakupa pongezi wewe Mwenyekiti, Spika, Naibu Spika, wote wane kwa jinsi mnavyosimamia na kuendesha Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na Muungano na Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na Mazingira, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote waliokamilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti na mipango yote ni nzuri, na cha msingi, nashauri na ninawasihi kwamba mipango na bajeti vitekelezwe kama ilivyopangwa ili kuwaletea maendeleo Watanzania wanaopenda Muungano pamoja na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Muungano ni mzuri sana. Kutokana na Muungano huu, Watanzania wako huru kuja Tanzania Bara na pia kwenda Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu na maelezo ya mara kwa mara yazidi kutolewa ili wananchi wa pande zote mbili wajue faida za Muungano na hasara za kutokuwa na/au kuvunja Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzidi kuwakumbuka waasisi wetu walioanzisha Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar na ikazaliwa Tanzania; baba zetu, Hayati Mwalimu Nyerere - Baba wa Taifa pamoja na Hayati Karume kwa kazi nzuri ya kuunganisha Tanganyika na Zanzibar. Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda huko walikolala na tunawakumbuka kwa mengi na hasa Muungano wa nchi hizi mbili ikawa nchi moja. Mungu awalaze pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kasoro au mambo ambayo hajaeleweka katika Muungano wetu, yazidi kufanyiwa kazi kwa muda muafaka, watu wazidi kukaa kwa amani na utulivu. Tusiwapatie nafasi wale wote walio na nia mbaya na wanaotaka kuvuruga Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania jamani inapendwa, na ni nchi ya amani na utulivu, kila mmoja nje na ndani ya nchi anafahamu. Tusivuruge Muungano wetu, tuzidi kuulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi nzuri inafanyika ya kuhamasisha wananchi kuhusu kutunza mazingira, lakini kazi ya ziada inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanyika chini ya Mheshimiwa Waziri, nashauri vipindi vya Redio, *TV* kuhusu mazingira ,vizidi kutolewa hasa kuhusu faida na hasara za utunzaji na uharibifu wa mazingira na mambo gani yafanyike ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Mikoa, wakati wa masika uwepo msukumo na uhamasishaji wa upandaji miti. Zoezi kubwa lifanyike hasa kwenye Mikoa iliyoharibu sana mazingira. Bajeti za Mikoa kuhusu upandaji miti na ufuatiliaji, ziwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, Mikoa na hasa baadhi ya Wilaya zinakumbwa na ukame ambao chanzo chake ni kasi kubwa ya ukataji miti. Watanzania tuwe na tabia ya kupanda miti ili kunusuru nchi yetu na Watanzania ambao walizoea amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji miti kutengeneza mkaa (na hasa unaosafirishwa na kutumiwa na wananchi wa Dar es Salaam kwa wingi kunamaliza misitu na kuleta jangwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Nashauri nishati mbadala *(Gas, Biogas)* ihimizwe kwa matumizi tukianzia hapa kwa Wabunge na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moto kila mahali na hasa wakati wa kiangazi, ng'ombe wengi kuzidi kiasi wanaosababisha mmomonyoko wa udongo, yote hayo yanaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Miji, ni michafu sana. Mheshimiwa Waziri anafahamu Miji mingi iliyo michafu. Tafadhali jitihada zozote zile zifanyike tukianza na Wabunge wanaotoka katika Mikoa hiyo, ili wahamasishe usafi wa mazingira katika Miji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji ovyo bila mpangilio; uchimbaji wa madini, mchanga na udongo pia kunaharibu mazingira. Maeneo haya yanayoharibu mazingira yaangaliwe na wananchi/wahusika wazidi kupewa elimu ya utunzaji mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na hasa wanaoshughulikia na misitu, usimamizi mzuri ukitolewa elimu na ufuatiliaji, tunaweza kufanikiwa katika upandaji na kutunza miti na misitu yetu na kulinda misitu ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanaharibu misitu ya asili kwa upanuzi wa kilimo. Elimu izidi kutolewa tulinde mazingira, tuishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Vijiji na Kata za Mazingira hazifanyi kazi kama mwongozo ulivyo. Ni vizuri Kamati hizi ziimarishwe na kupewa uwezo. Je, Serikali ina mpango gani juu ya hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utupaji taka za elektronik *(e-waste),* kwa vile matumizi ya vifaa mbalimbali vya elektronik *(electronic)* kama vile *TV, computer, scanner,* simu za mikononi na kadhalika, yameongezeka sana nchini na utupaji wake siyo salama na taka hiyo ni sumu na hatari kwa maisha ya binadamu. Je, Serikali ina mpango gani juu ya hali hatari nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu mkubwa sana katika bonde la Mto Mara, kwa vile ukataji miti umekithiri katika bonde la Mto Mara na hali hii pia inachangiwa na kilimo hadi kwenye kingo za Mto Mara na hali hii pia inachangiwa na kilimo hadi kwenye kingo za mto imesababisha kutokea kwa mafuriko ya mara kwa mara. Ni vizuri juhudi za makusudi za kuokoa hali hii ambayo inazidi kuchangia uharibifu mkubwa wa mto. Pia uhamiaji haramu katika Bonde la Mto Mara udhibitiwe na wahamiaji hao haramu wahamishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini katika maelezo ya hotuba hapakuwa na sehemu ya kueleza juu ya kuondoa kero za Muungano? Ni vizuri kuwa na maelezo kuwa, kero zilizojitokeza zimetatuliwa ngapi na zipi hazijatatuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, magugu pori kushambulia Wilaya Serengeti hadi hifadhi ya Taifa *(Serengeti National Park).* Magugu pori haya *(chromolaena)* yamevamia Wilaya ya Serengeti hadi Mbuga ya Taifa ya Serengeti na sehemu nyingine za Mkoa wa Mara. Ni vizuri hatua za haraka na za kisayansi zichukuliwe kama nchi za Senegar, Ghana, na Kenya, walivyofanya ili kupambana na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Carbon trading* iimarishwe na kujulikana sehemu zote za nchi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri: Mheshimiwa

Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, kwa hotuba yao nzuri. Hata hivyo napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kuwa Zanzibar na Serikali ya Muungano ni ndugu, hivyo tusitafute visingizio wakati vinapotokea neema ili mmoja amnyime mwenzake. Kikatiba, katika nyongeza ya kwanza kifungu namba 11 na 17 vinadhihirisha kuwa suala la rada ni la Muungano, lakini pia ibara ya 135 (i) ya Katiba ya *SJMT* inadhihirisha kuwa chenji ya rada ni yetu sote (Muungano). Nawasilihi ndugu zetu wa Tanzania Bara muache uchoyo. Tugawane neema hii sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kuratibu Maoni ya Wananchi kuhusu Katiba Mpya, imefurahishwa sana kauli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa tutakuwa na Katiba Mpya ifikapo mwaka 2014. Kwa sababu hili halikuwa ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, naamini chama cha *CUF* na vyama vingine vya upinzani vilifanya kazi ya ziada kufika hapa. Lakini *CUF* ili kwenda mbali zaidi kwa kuandika rasimu ya Katiba *(zero draft)* na kuwasilisha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wananchi wa Jimbo la Chambani, Wazanzibar wote na Watanzania wote kwa jumla kuitumia nafasi hii adimu, ambayo siyo rahisi kuipata tena katika miaka mingi ijayo. Wote wenye mawazo tofauti wasiogope kwenda kutoa mawazo yao. Naishauri Tume ya kuratibu maoni, kutenda haki na kuwa wa kweli na wasijaribu kuchakachua maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imedhihirika katika kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa akitoa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge akihitimisha hotuba yake kuwa, kuna mwono mmoja kati ya SJMT na STZZ juu ya suala la mafuta. Je, Ofisi ya Makamu wa Rais inachukuwa hatua gani za haraka kuona kuwa taratibu zitakazopelekea Zanzibar kuchimba mafuta yale zianze mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Fedha wa Pamoja ni la kikatiba. Inasikitisha kuwa kwa miaka mingi (28), Serikali inaendelea kuvunja Katiba kwa kutoanzisha Mfuko wa Pamoja wa Fedha kwa mujibu wa Katiba ibara ya 133. Inasikitisha kusikia hadi leo hii Serikali inaendelea kukusanya maoni ya jinsi ya kukusanya pesa na kugawa kwa nchi husika. Ni dhahiri kuwa nchi hizi mbili haziko tayari kuanzisha mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba wananchi waelezwe kuwa suala hili haliwezekani.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na jopo zima walioweza kufanikisha bajeti kwa manufaa ya nchi kwa ujumla. Hapa nami nataka nichangie kwa machache juu ya bajeti hii.

Pamoja na Mratibu wa masuala haya ya Muungano kuratibu vizuri, lakini bado kuna upungufu

unaosababisha mambo yasiende vizuri. Upungufu huo ni pamoja ya kutokuwepo ulinganifu katika mambo kadhaa ikiwemo masuala ya ajira, mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada, ushirikishwaji wa Zanzibar Afrika ya Mashariki, Uwanja wa Ndege, Bandari ya Maruhubi na kadhalika. Hapa nitatoa mifano michache tu, kati ya hiyo, ni ajira.

Katika masuala ya ajira, Wizara mbalimbali katika kutoa ajira kwa upande wa Zanzibar huchukuliwa wachache na pengine hakuna wanaochukuliwa kama idadi inayotakiwa ni chache. Kwa mfano, Watumishi Wakuu wa Vitengo kama Jeshi la Polisi, Usalama wa Raia kwa upande wa Muungano, karibu ajira nyingi huangaliwa kwanza Bara kuliko Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migawo ya mapato yatokanayo na misaada, pia Serikali huwa inasahau upande huo wa pili na kutowashirikisha kwa mambo mbalimbali kisingizio kikiwa, siyo vya Muungano; kwa mfano, masuala ya madini, gesi na kadhalika. Wakati huo huo Bara inadai mafuta yaliyopo Zanzibar kuwa yawe ya Muungano wakati masuala haya ya madini yaliyopo Bara siyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya usafiri kule Zanzibar, vyombo vya usafiri ni vichache na Serikali ya Muungano haijalifanyia kazi ili kuwafanya nao wajisikie wanajaliwa badala ya kutumia Serikali yao tu. Upande wa biashara, pia wafanyabishara kutozwa kodi mara mbili iwapo bidhaa zao huletwa Bara, vile vile masuala ya fedha pia hayajakaa sawa kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Ofisi za Zanzibar hazitumiki kwa masuala ya pamoja kama vile Mikutano, kama Kamati za Bunge, badala ya kugharamia kumbi za watu binafsi, zingetumika za Zanzibar. Katika kufanya hivyo, ingeonekana kweli kuna Muungano. Siyo mara zote vikao vikuu vikaliwe Bara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ili kuweka sawa muungano wetu. Serikali iangalie mambo haya na kuyaweka sawa kwa manufaa ya umma.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia Hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Terezya Luoga Huvisa, pamoja na Watendaji wao wote, kwa kuweza kufanikisha Hotuba hii ya Bajeti iliyowasilishwa leo hapa mbele yetu. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo, nitajikita sana kwenye suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na wimbi la baadhi ya watu ambao wanaonesha nia au dhamira ya kutaka kuuvunja Muungano, jambo ambalo kwa mtazamo wa baadhi ya watu inaonekana kana kwamba ni Wazanzibari

wote hawautaki Muungano; kitu ambacho siyo sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi ni muumini mkubwa wa Muungano wetu huu na ninaamini hivyo hivyo na Wazanzibari walio wengi kabisa ni waumini na wanaupenda Muungano huu. Kitu kinachopelekea Wananchi wa Zanzibar waonekane kana kwamba hawaupendi Muungano ni pale wanapoona kuna baadhi ya mambo ya Muungano, hayaendeshwi ama kwa mujibu wa makubaliano ya nchi zetu mbili au vinginevyo, ambayo ndiyo mwisho wa siku yanakuwa Kero za Muungano kama alivyoyaainisha Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake, ukurasa 14, kifungu cha 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwulize Mheshimiwa Waziri ni kitu au jambo gani linalosababisha kukwama kutatuliwa kero hizo hadi leo hii; jambo ambalo linasababisha baadhi ya watu kuutumia mwanya huu wa Kero za Muungano ambao kila siku tunaelezwa zipo kwenye mchakato, kusema Muungano haufai na kutusababishia matatizo makubwa ya vurugu katika Kisiwa chetu cha Unguja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naziomba Serikali zetu zote mbili zifanye haraka iwezekanavyo kumaliza kutatua hizo kero za Muungano zilizobakia na kwa kufanya hivyo, naamini wananchi wetu watarudisha nyoyo zao na kuweza kuwa na imani thabiti na Muungano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuziomba Serikali zetu ziunde Chombo muhimu cha

Kikatiba ambacho ni Tume ya Mambo ya Muungano, ambayo kazi zake zitaainishwa ndani ya Sheria itakayotungwa na Bunge badala ya utaratibu wa sasa wa kuwa na Kamati ya Ufuatiliaji na Kuondoa Kero za Muungano ambayo haipo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini ikiundwa Tume hii Kikatiba, itaweza kufuatilia na kutatua kero zilizopo sasa na zile zitakazojitokeza baadaye kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kuomba kuwasaidia Wahanga waliohamishwa toka Milima ya Vijiji vya Ruaha na Kidodi. Wananchi wamekaa maeneo hayo kwa muda mrefu sana, walikuwa wakilima maeneo hayo pia. Serikali imewaagiza wahame mwaka 2007/2008 na wao wameitikia wamehamia vijiji jirani. Wananchi hawa wanataabika sana hadi leo kwa sababu hawakutengewa maeneo yoyote ya kuhamia na kuanza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa undani kwani wanasema kuwa, waliahidiwa kulipwa fidia na walijiorodhesha na Serikali inayo idadi ya Wahanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Kijiji cha Malolo wameathirika sana na upasukaji wa bomba la mafuta la Kampuni ya *TAZAMA.* Mwaka jana mwezi wa Mei au Juni, bomba ililipasuka na hadi leo harufu ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imegharamia ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji wenye thamani ya shilingi bilioni saba, upasukaji wa bomba hilo umeathiri sana mazingira ya maeneo husika na pia kuathiri mfumo wa maji ya umwagiliaji na mazao na kuwafanya wakulima wapate hasara na umaskini. Mafuta hayo yaliyomwagika yameathiri wananchi kwa kutopata maji safi na salama. Naomba Wizara ifuatilie na kuweza kulipwa fidia wananchi hao pamoja na kupatiwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifuko ya Rambo, naomba Mheshimiwa Waziri aongeze nguvu kuchukua hatua kali dhidi ya wale wanaotengeneza mifuko hiyo ambayo huharibu mazingira na kuchafua sana. Pia husababisha vifo vya wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo na wanyama walioko kwenye hifadhi pia hufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mipaka na kulinda mazingira ya vijiji limeleta malumbano na ugomvi kati ya wananchi na viongozi wa vijiji. Ningeshauri Wizara ifanye tathmini tena katika baadhi ya maeneo. Viongozi wa Wilaya wanatumia nguvu au kulazimisha hiyo mipaka. Walifanya tathmini hiyo zamani sana wakati wananchi walikuwa wachache katika sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya utunzaji mazingira ni tegemezi. Nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa sana la uharibifu wa mazingira hususan ukataji miti hovyo, kulima kwenye vyanzo vya maji, utiririshaji wa maji machafu kutoka viwandani kuelekea baharini au kwenye mito, ambamo hudhuru viumbe wa baharini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Mazingira imekuwa inategemea wahisani wa nje na sisi kama Taifa hatujatilia maanani umuhimu wa utunzaji wa mazingira na hivyo kutenga fedha za ndani kwa ajili ya suala hili. Athari kubwa zinatukumba pindi kunapotokea mdororo wa kiuchumi *(Financial Crisis)* kwa nchi wahisani. Maana yake ni kwamba, shughuli za utunzaji wa mazingira zinasimama pindi wahisani wasipoleta fedha na hili siyo jambo jema kwa Taifa linalojiita huru. Bajeti ya Mazingira ni lazima itengwe na Serikali na siyo kutegemea wahisani kwa kila jambo hata kama tuna uwezo nalo kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa Baraza la Mazingira *(NEMC)* na majukumu yaliyoainishwa, Baraza hili halitimizi majukumu yake ipasavyo. Mfano, kumekuwepo na malalamiko mengi toka kwa wananchi jinsi ambavyo wawekezaji kwenye

Sekta ya Madini wanavyochafua mazingira kwa kuzalisha sumu zinazoingia Mtoni au Ziwani, ambapo wananchi hutumia maji hayo kwa matumizi ya nyumbani hasa huko Mkoani Mara. *NEMC* kabla ya kutoa kibali chochote cha uwekezaji ni lazima iingie mkataba na mwekezaji wa kutunza mazingira na endapo ataharibu alipe fidia au vinginevyo anyang'anywe leseni yake. Kwa nini hili halifanyiki na matokeo yake wananchi wanaendelea kudhurika na kupata magonjwa ya ngozi na hata vifo?

Kwa nini hakuna Sera zinazotekelezeka kuhusu masuala ya utunzaji mazingara? Hapa ni lazima Baraza hilo liwajibike ipasavyo kama kweli linalitakia mema Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *Environmental Audit:* Kumekuwepo na matatizo makubwa ya uharibifu wa mazingira yanayosababishwa na ukataji miti kwa ajili ya shughuli za maendeleo hasa ujenzi wa barabara na viwanda. Pamoja na nia hii njema ya kurahisisha usafiri, hakuna Sera ya kurudisha mazingira yaliyoharibiwa. Sera hii *(Replacement Policy),* ina umuhimu wake kwani ingefanya kazi ya kutunza mazingira na kurudishia mimea ambayo imekatwa na uharibifu mwingine; mfano, kurekebisha au kufukia mashimo makubwa yanayosababishwa na uchimbaji wa kokoto au mchanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua kali zichukuliwe kwa waharibifu wa mazingira. Serikali sasa ichukue hatua kali sana kwa wadau wanaoharibu mazingira

hususan wawekezaji wa Sekta ya Madini wanaoharibu mazingira kwa makusudi huku wakikiuka Mikataba ya Utunzaji wa Mazingira. Pia ichukue hatua kali kwa watu wanaojenga kiholela kwenye vyanzo vya maji, maana ndiyo chanzo kikubwa cha kusababisha ukame na mabadiliko ya tabianchi. Matokeo yake ni njaa inayopelekea afya duni kwa wananchi, maradhi na hivyo kupunguza nguvu kazi ya Taifa. Pia ukame husababisha kupanda kwa bei za vyakula na hivyo maskini kushindwa kumudu kupata milo mitatu na kuzorotesha afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu namna Muungano ulivyopatikana na jinsi ambavyo Hati za Muungano zimekuwa ni siri kubwa, ambayo wananchi wengi hawafahamu historia yake; vurugu na fujo zinazoendelea kutokea hii leo Tanzania Visiwani kuhusu uhalali wa Muungano ni dalili tosha kwamba huko tuendako ni kubaya zaidi kuliko tulikotoka. Ni vyema Serikali ikaingilia kati na kuona ni namna gani Muungano unatakiwa uwe. Hapa nikiri wazi kuwa, kuvunja Muungano ni kuvunja nguvu ya pamoja ya Watanzania, jambo ambalo ni baya na halikubaliki. Muungano uangaliwe upya uwe ni wa namna gani kwa manufaa ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar 2010 yamekuwa kwa kiasi kikubwa makubaliano yaliyokuwa kwenye Hati ya Muungano kwa kuitambua Zanzibar kwamba ni nchi ndani ya nchi mbili (Tanzania na Zanzibar) na pia kumfanya Rais wa Zanzibar kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa

Majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Zanzibar na vile vile kuwa na jukumu la kuteua Wakuu wa Mikoa au Wilaya bila kushauriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hii pekee inatosha kusema wazi kwamba, Muungano huu sasa una matundu na unatakiwa uangaliwe upya.

Naungana na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Muungano huu sasa unapaswa kuwa wa Serikali tatu, yaani Serikali ya Tanganyika, Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii itamaliza malalamiko ya upande mmoja kuonewa na kunyang'anywa mamlaka yake. Masuala ya Muungano yajadiliwe kwenye Serikali ya Muungano, Masuala ya Tanganyika yajadiliwe na Watanganyika wenyewe na ya Wazanzibari yajadiliwe na Wanzanzibari wenyewe ili kumaliza vurugu, chokochoko na fujo kama zinavyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba yake, nami naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono bado ninayo mambo muhimu ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Bado Serikali haijaona umuhimu mkubwa juu ya kutenga fedha za kutosha kuhifadhi mazingira katika Maziwa yetu. Kwa mfano, Ziwa Rukwa; ni wazi kuwa hili

ni Ziwa muhimu sana kwa nchi yetu, kwa jamii na hata kwa viumbe hai vinavyotegemea Ziwa hili. Pamoja na umuhimu wa Ziwa Rukwa, bado Serikali haijachukua hatua thabiti za kulilinda na matokeo yake kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ambao unahatarisha Ziwa hilo kukauka kwa makosa yafuatayo: Wimbi kubwa la mifugo kuchungiwa na kupitishwa, jambo ambalo linasababisha mmomonyoko wa udongo; na baada ya mvua kunyesha udongo wote uliotifuliwa na mifugo huenda Ziwa Rukwa na kujaza tope jingi na hatimaye kusababisha Ziwa kuwa na kina kifupi na baadaye linaweza kukauka.

Sababu nyingine ni kukata miti hovyo kando kando ya Ziwa na kusababisha uhaba wa mvua na kuathiri mazalia ya viumbe hai kama vile samaki. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kulilinda Ziwa hilo na hasa katika Bajeti hii? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kwa nini Serikali imemruhusu mwekezaji afuge na alime katika Shamba la Malonje wakati ni vyanzo muhimu vya mito muhimu inayotiririka kwenda upande wa Ziwa Rukwa. Mito hiyo ni Mto Nzovwe, Mto Kisa, Mto Msanda, Mto Mbulu, Mto Lundi, Mto Songole, Mto Mumba na Mto Momba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi ni jinsi gani Serikali itanusuru vyanzo vya Mito hiyo ili Mito hiyo isikauke na Ziwa Rukwa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kampeni ya Upandaji Miti kila mwaka Serikali inadanganywa na Viongozi wa Wilaya au Mikoa kwa kutoa takwimu kubwa za upandaji miti, jambo ambalo linakuwa ni kuidanganya Serikali. Ninashauri Serikali iunde Tume ya Kufuatilia na Kukagua Taarifa za Upandaji Miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo zinazotungwa na Vijiji au Halmashauri ili kuhifadhi mazingira hazifuatwi, hazisimamiwi na hazipewi nguvu na vyombo vya sheria au dola; elimu bado ni muhimu sana kwa jamii katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi wote waliopewa madaraka wawekewe Mikataba ya Uhifadhi wa Mazingira iwe sehemu ya utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa mchango wangu kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na (Muungano) kama ifuatavyo:-

Mazingira: Ili kuweza kuhifadhi uumbaji wa Mungu kwa kuangalia uharibifu unaotendeka nchini katika maeneo ya vyanzo vya maji, ukataji miti ovyo, matumizi ya nishati ya mkaa, moshi utokao viwandani, magari mabovu, matumizi ya mifuko ya plastiki na ujenzi holela hasa mijini kutokana na *Master Plan* za miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Waziri kuhusu Sheria Ndogo *(By Law)* kwa Halmashauri zetu, bado uharibifu wa vyanzo vya maji umekithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninapenda Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya mgogoro wa siku nyingi kwa chanzo cha Qanded kule Eyasi – Mang'ola. Chanzo hiki ndicho uhai wa Wananchi wote wa Bonde la Eyasi; cha kushangaza huharibiwa sana bila mamlaka husika kuchukua hatua madhubuti (Bonde la Kati). Namwomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati suala hili ili kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba, kwa wananchi wa kawaida ili waweze kumudu maisha yao hasa vijijini, nishati pekee kwa maisha yao ni kuni na mkaa. Hivyo, Serikali inapaswa kuharakisha mpango wa nishati mbadala na ipatikane kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepaswa kuhakikisha kuwa, Sheria ya Mazingira na *By Laws* zinasimamiwa sawa na mamlaka husika na hata wanachama kupata elimu ya kutosha.

Je, Serikali inaufahamu Mradi wa *Murus – Endabash Gold Mining* ulioko Wilayani Karatu? Kama jibu ni ndiyo; imechukua hatua gani kutokana na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo; ukataji wa miti ovyo, uchafu na kutokuwa na vyoo? Nchi yote kuachwa mashimo mashimo? Uchafu wa maji hasa kuelekea Bonde la Eyasi? Hali ya afya ya binadamu katika eneo la Bonde la Eyasi iko mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili ni mtambuka; je, Wizara ya Nishati na Madini na Mazingira wanajipanga vipi katika kuokoa Taifa na janga hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa mchango wangu kwa kifupi sana kuhusu Muungano. Waswahili husema; “Umoja ni nguvu bali utengano ni udhaifu.” Kwa maoni yangu, hakuna mtu anayepinga Muungano. La msingi ni Serikali kuona wananchi wanataka Muungano wa aina gani. Serikali kutoweka wazi mambo yote yahusuyo Muungano na Muungano ambao wananchi wanautaka ndiko kunakozaa matatizo au migogoro. Mfano, rejea vurugu ya Uamsho na Serikali kuchukua hatua ya kutumia nguvu badala ya kutafuta chanzo chake kuvamia wananchi wanaodaiwa kuwa Wanauamsho wakiwa ibadani au hata katika vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali ipate nafasi ya mazungumzo ili kudumisha amani na umoja.

**MHE. ANNA MARYSTELLA MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na usimamizi wa mazingira, ukurasa wa 83. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambalo sasa lina mwaka wa saba tangu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ianze kutekelezwa, bado halijafanikiwa na

utekelezaji wake bado ni mdogo. Nasema hivyo kwa sababu mazingira au utunzaji wa mazingira ni kitu muhimu sana katika maisha na maendeleo kwa jamii, lakini suala hili limekuwa likizungumzwa kama wimbo wa kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yetu itoe kipaumbele kwenye suala hili la utunzaji wa mazingira kwa kutoa elimu hasa kwa wananchi vijijini. Sababu elimu hii ikitolewa vijijini ambako hata vyanzo vya mito na misitu imeanzia, tutaokoa au kuepuka uharibifu wa vyanzo hivyo tayari kwa sababu watakuwa na uelewa. Sasa hivi tunakumbwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na wananchi hasa vijijini kuchoma mapori hovyo, kukata miti hovyo, kuharibu vyanzo vya maji na kadhalika. Hivyo, nasisitiza Serikali itoe elimu vijijini hata kwa kutushirikisha Wabunge kusambaza ujumbe huu tunapowazungukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni mito ambayo inazunguka machimbo ya madini kama mto uliopo Mpanda Mjini uitwao Mto Mpanda. Mto huo unatumiwa na Wakazi wa Mpanda Mjini na Vijijini kwa matumizi ya kunywa na kupikia. Mto huo huo wachimbaji wa madini wanategemea kuchekechea (kusafisha) dhahabu, pia unategemewa na madereva wengi kusafishia magari yao. Je, hali hiyo siyo hatari kwa afya za watumiaji wa maji hayo?

Mpaka sasa sioni hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali kuokoa afya za watumiaji wanaokunywa maji hayo yenye chembechembe za madini na mafuta ya magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naoimba Serikali ihimize suala la upandaji miti kwa kila shule za msingi na sekondari iwe ni lazima ili tuepukane na ukame mkubwa unaokuja. Mpaka sasa kuna shule ambazo hazina ubunifu wa upandaji miti na kufanya wanafunzi kukosa vivuli vya kupumzikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tarehe 5 Juni ni Siku ya Mazingira Duniani. Hivyo, hata shule ziwekwe kwenye mashindano ya kujali mazingira na kupewa tuzo ili wazingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiuliza Serikali inasema nini kwa wakazi waishio pembeni ya mito inayozungukwa na wachimba madini na kusafishia madini na wanaopeleka magari kusafishia mtoni huku wakifahamu kuna wananchi wanakunywa maji hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kuwasilisha.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika Hotuba hii kuhusu mazingira kama ifuatavyo:-

(i) Kumekuwa na tatizo la *overgrazing*; ni vyema Serikali iendelee kuwatawanya wafugaji ili kulinda mazingira.

(ii) Ili kutunza mazingira ni lazima Serikali iendelee kuzuia uingizaji wa magari chakavu ambayo yatatoa moshi utakaoathiri tabia nchi.

(iii) Serikali lazima ifanye *survey* ni sheria ndogo zipi zipo kwenye Halmashauri zetu na kwa kiwango gani zinakuwa *enforced* ili kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira mfano, kujisaidia vichakani, baharini, ziwani au mtoni.

(iv) Kumekuwa na mila na desturi mbaya za uchomaji mioto mapori ili watu waweze kukadiria umri wao wa kuishi, mila hizi zinaathiri mazingira.

(v) Lazima Serikali iwabane watu wa Ardhi kuhusu ugawaji na uuzwaji holela wa viwanja vya makazi katika Mikondo ya Mito. Hii inasababisha kupunguza pesa za maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kutokana na uzembe.

(vi) Kumekuwa na athari kubwa ya mmomonyoko wa udongo kutokana milima na kuathiri Ziwa Tanganyika. Pamoja na reli yetu ni lazima Serikali izuie hali hii na sasa itoe fidia ili waliojenga walipwe na wahame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 39, kunasisitizwa uwepo wa vipeperushi vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira viandaliwe, vichapichwe kwa wingi na vitumike kwenye mafunzo ya elimu yenye manufaa nchini kote. Tukiangalia fedha iliyowekwa kwa ajili ya *Printing Advertising and Information Supplies and Services* katika *Vote 31, Sub vote 5001,* kifungu 221600 ni shilingi 3,000,000 tu na mwaka 2011/12 ilikuwa 12,000,000. Je, kwa nini Waziri au Wizara imetengewa kiasi hiki kidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia masuala ya Muungano kwamba, sasa Serikali ishughulikie Kero za Muungano ili Taifa hili liwe salama na lisitokewe na machafuko.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi zao. Kadhalika, Katibu Mkuu wa Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siridhishwi na uharibifu wa mazingira unaofanywa na wawekezaji katika maeneo ya migodi. *NEMC* wakaangalie Mgodi wa Dhahabu Buhemba wawekezaji walivyoacha mashimo ya kutisha katika eneo la Mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matajiri wanaendelea kujenga majumba makubwa ya kifahari kando ya ufukwe wa bahari na kuzuia bahari kufuata mkondo wake. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), alitoa tamko akishirikiana na Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Anna Tibaijuka, kulielezea Taifa kuwa waliojengwa ndani ya mita 60 kutoka ufukwe wa bahari waanze kubomoa nyuma zao. Naomba kujua hatua waliyochukuliwa waliokaidi agizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyopita Serikali ilipiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki iliyo kati ya kipimo cha kuanzia *micro 1 – 30.* Baadhi ya wafanyabishara walianza kuogopa kutumia mifuko hiyo kwa wateja wao. Baada ya kuona kuwa Serikali haifuatilii agizo lake hilo, biashara hiyo ya mifuko ya *plastick* inaendelea kama kawaida na kila kona mifuko

hiyo imeenea kwa kuchafua mazingira. Serikali inasemaje kuhusu kupuuzia agizo lake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tarehe 1 Aprili, wananchi hupanda miti kwa nia ya kutunza mazingira na kuepusha ukame. Je, Serikali inaweza kutoa tathmini ya ukuaji au utunzaji wa miti hiyo inayopandwa kila mwaka? Kama miti hiyo haitunzwi inapasavyo na baada ya kipindi kifupi miti hiyo hufa; je, kuna faida gani kujidanganya katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ihimize upandaji na utunzaji miti katika shule za msingi na sekondari na matunda yake yataonekana. Serikali pia ihimize uvunaji maji katika shule hizo na matokeo mazuri yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangazwa na Wananchi wa Zanzibar kulalamika kuwa mgao wa fedha za Muungano kwa upande wa Zanzibar ni kiasi kidogo sana. Ni vizuri Wazanzibari wakaelewa kuwa Tanzania Bara kuna watu zaidi ya milioni 47; hivyo, kudai kuwa mgao wa fedha kwa Zanzibar siyo sahihi, siyo kweli na siyo sahihi. Ni vizuri suala hili likashughulikiwa mapema na Kamati inayoshughulikia Kero za Muungano ili pande zote ziridhike na mgao. Watanzania hatupendezwi na malumbano yanayoendelea kuhusu Kero ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji misitu ni tatizo lingine linalosababisha uharibifu wa mazingara. Maeneo mengi katika nchi yetu hakuna usimamizi wa

misitu. Misitu yetu imekuwa shamba la bibi, kila anayetaka hukata atakavyo. Serikali isimamie utunzaji wa misitu, inajua lakini imeshindwa kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoangalia na tusipojali mazingira yetu, nchi hii itakuwa jangwa muda si mrefu na vizazi vijavyo vitatulaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie sheria zake ndogo ndogo zinazohusu utunzaji wa mazingira. Jiji la Dar es Salaam ni chafu, kila eneo ni *parking* ya magari, kila kona kuna gereji, maji machafu yanatitirika ovyo, mifuko ya plastiki na kadhalika. Tuone aibu kwa hali mbaya ya uchafu kwa Jiji letu na tufanye mabadiliko ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mawaziri kwa uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora umeathirika sana na ukataji miti. Wilaya zote zimeathirika sana hasa Wilaya za Urambo na Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtusaidie elimu kwa wananchi ili tuwazungukie na kuwaelimisha umuhimu wa kutunza miti na mazingira kwa ujumla. Hali ni mbaya na niko tayari kusaidiana nanyi.

Ahsante sana, tuokeni Tabora hali mbaya tunahitaji elimu na kuhamasisha.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazingira tuliyonayo kiutendaji na kiutekelezaji wa maagizo mbalimbali yanayotolewa kutotekelezwa sawa sawa, lakini ni matumaini yangu kadiri tunavyoendelea, matatizo hayo yatatekelezwa hatua kwa hatua, kwani naamini kila safari ndefu huanzia na hatua moja. Kwa hilo tu, naunga mkono hoja Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yametajwa na kuwasilishwa na Kamati za Kisekta, naomba kero mbalimbali ambazo Serikali haikuzitekeleza miaka iliyopita, kwa sasa ijipange tena na kuzitatua kwani ni changamoto zilizojitokeza. Mfano, uundwaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wafanyabiashara kutozwa kodi kwa bidhaa kutoka Zanzibar mara mbili wakati *TRA* ni moja na chini ya Uongozi mmoja; na Sheria moja ya Fedha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara za Muungano ziongeze nafasi kwa idadi maalum kwa upande wa Zanzibar kwani siyo halali. Mfano uliojitokeza leo kati ya ajira zilizofanyika za zaidi ya polisi 3,600 na Zanzibar kupata nafasi 160 tu; kwa hiyo basi, tunapendekeza kwa Wizara ya Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani, Uhamiaji, Jeshi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ijitahidi kutoa elimu kwa wananchi na hasa vijana ikiwezekana katika vyuo au mashuleni kuhusu suala la umuhimu wa kuwepo Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile suala hili halishughulikiwi ipasavyo ndiyo tumefika mahali maadui wa Muungano huu wanapenyeza siasa za chuki na Ujimbo; jambo ambalo linaleta mtafaruku mkubwa sana nchini siyo Zanzibar tu bali hata Bara na kupelekea mara nyingi kuvunjika kwa Katiba za Nchi na kwa vile hatua hazikuchuliwi, hupelekea kuvunjika kwa amani na utulivu wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mazingira nchini ni mbaya mno, tunashauri pamoja na elimu ya umma kutolewa, tunaomba maboresho ya sheria iliyopo fayanyike kwa kupunguza matumizi ya mkaa, ukataji wa miti, uchomaji wa miti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, natamka kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala na kwa ajili hiyo naungana na Maoni ya Kamati kuhusu hoja hii. Ili kuokoa muda, naomba nichangie kwa mpangilio ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, mambo yote yanayohusu Muungano yasubiri kukamilika kwa mchakato wa kuandikwa upya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania unaoendelea. Kwa wakati huu kila kitu kiendelee kama kilivyo *(status quo be maintained).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, kama ilivyoelezwa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwamba, mabadiliko ya tabianchi yameleta madhara makubwa kwa sababu ya ukataji ovyo wa miti na uvunaji usio wa mpango. Natoa ushauri ufuatao:-

(i) Ili kuzuia au kupunguza matumizi ya nishati ya mkaa, bei ya gesi ipunguzwe kwa Serikali kutoa ruzuku *(subsidized gas price).*

(ii) Sheria ya kusimamia na utunzaji wa vyanzo vya maji isimamiwe kwa ukamilifu na kila Halmashauri ihakikishe kuwa hakuna ujenzi unaojengwa ndani ya mita 60 kutoka vyanzo vya maji. Kadhalika, hakuna Mradi wowote ulioanza bila *Environmental Impact Assesment* na kupitishwa na *NEMC.* Mwisho, Mamlaka ya Jiji na Manispaa za Wilaya zisimamie usafi wa mazingira. Bajeti ya *NEMC* iongezwe bila kusahau kuongeza elimu ya kukabiliana na hewa ya ozoni na uchimbaji wa madini katika maeneo ya vyanzo vya maji.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna mwitikio mdogo katika Serikali za Mitaa juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao. Sheria Ndogo za Uhifadhi wa Mazingira hazisimamiwi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali au Wizara ihakikishe Serikali za Mitaa zinakuwa na mikakati ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Aidha, Sheria

Ndogo ya Uhifadhi wa Mazingara ziwepo na kusimamiwa ipasavyo ili kuletea ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* linahitajika kuwezeshwa zaidi ili lifanye ukaguzi katika maeneo mengi nchini kuhakikisha Sheria ya Mazingira inazingatiwa na inasimamiwa ipasavyo. Aidha, bado viwanda vingi vinatiririsha maji machafu na uchafu wa hewa *(air pollution);* ni vyema *NEMC* ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali au Wizara ni vyema iweke mkazo katika utunzaji wa mazingira kwenye vyanzo vya maji. Hii ni sambamba na ukataji wa miti katika vyanzo, ujenzi wa hoteli na nyumba za kuishi na shughuli mbalimbali za binadamu katika hifadhi ya vyanzo vya maji. Hata hivyo, mgogoro uliopo Wilaya ya Karatu juu ya uhifadhi wa chanzo cha maji katika Kijiji cha Qanded, Kata ya Baray – Karatu, haujatolewa majibu na *NEMC* na uharibifu wa chanzo cha maji na hifadhi ya eneo hilo unaendelea, huku shughuli za binadamu zinaendelea bila kujali athari ya uharibifu wa mazingira katika chanzo cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Serikali juu ya uharibifu wa mazingira katika chanzo cha maji ya chemchemi katika Wilaya ya Karatu (Kijiji na Kata niliyoitaja hapo juu). Suala hili limekuwa la muda mrefu na hatujaona dhamira ya dhati ya kushughulikia tatizo hilo. Japokuwa *NEMC* walitoa mapendekezo kadhaa, lakini bado Halmashauri ya Karatu na wadau

mbalimbali hawajawa na dhamira ya dhati kuokoa mazingira hayo yanayoharibiwa katika chanzo cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema pia elimu itolewe kwa wananchi ili watambue athari za baadaye kutokana na athari ya uharibifu wa mazingira katika chanzo hicho cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni yangu kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Kero za Muungano bado hazijafanyiwa kazi ipasavyo ili kuzimaliza. Ninashauri Serikali iongeze nguvu katika kushughulikia Kero za Muungano na taarifa rasmi iletwe katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inaonekana kuna mkanganyiko kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na Katiba Mpya ya Zanzibar na Sheria ya Kuthibitisha Mapato ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1964; ni vyema Serikali ione ni wakati mwafaka wa kumaliza mkanganyiko huo. Wakati umefika sasa wa uhitaji wa kuwepo na Serikali tatu, yaani Serikali ya Tanganyika, Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na leo nikaweza kuchangia Hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haijataka kutatua Kero za Muungano na kutokana na sababu hiyo, inachangia sana kukaribisha migongano, vurugu zinazotokea kutokana na ulegevu na kuchelewa kutatua matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipiga kelele sana kuhusu wafanyabiashara wa Zanzibar kulipishwa ushuru mara mbili wanapoingiza bidhaa zao Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaonekana kuudanganya Umma wa Watanzania kwani kinachofanyika ni kutoa ahadi za uongo za kesho, kesho kutwa, lakini hakuna kinachofanyika. Serikali iliahidi kwamba, jambo hili lingekwisha tangu Aprili mwaka jana lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. Kama hiyo haitoshi, Serikali kwa mara nyingine mwaka huu inarudia kutoa ahadi kwamba, hili litaisha ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo na tunashindwa kuelewa Serikali hii ni ya aina gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuchangia.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *GMO* ni njia ya kisayansi inayotumika katika kuzalisha mazao mbalimbali Duniani. Taarifa kutoka Shirika la Afya Duniani *(WHO*) zinaonesha kwamba, vyakula vitokanavyo na mazao ya *GMO* vilivyoko latika soko, havina madhara yoyote kwa watumiaji kwa kuwa

vimethibitishwa na kupasishwa na vyombo vinavyosimamia matumizi salama ya *GMO* katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuandaa mfumo wa kusimamia matumizi salama ya Bioteknolojia (mwaka 2003 – 2005), kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi za Afrika, Tanzania tulijiwekea kwa makusudi mazingira magumu *(Precautionary Principle* na *Strict Liability)* ili kudhibiti uingizaji na matumizi ya bidhaa zinazotokana na bioteknolojia ya uhandisi jeni *(Genetic Engineering).* Kanuni za *strict liability* zinafanya sheria iwabane wahusika katika mlolongo mzima wa kutafiti, kuendeleza, kusafisha na kutumia teknolojia hii, wahusike moja kwa moja na madhara ambayo yanaweza kutokea hata kutokana na makosa ya watu wengine au hata kama hayatakuwa yamesababishwa na teknolojia yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa Kanuni ya Strict *Liability* kumezuia kwa kipindi kirefu maeneo ya kilimo hapa nchini. Tatizo hili limerudisha nyuma sana nchi yetu ikichukulia kwamba nchi mbalimbali zimekuwa zikipinga maendeleo kutokana na matumizi ya *GMO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, naiomba Serikali ifute kipengele hiki cha *strict liability* ili nchi yetu iweze kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo na hivyo kuzalisha kwa wingi na kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania tukiwa tunasuasua, wenzetu wamekuwa wakiitumia teknolojia hii. Kwa sasa nguo nyingi tunazovaa zimetokana na mazao ya pamba yaliyozalishwa kwa teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozidi kuchelewa, Tanzania itajikuta inaagiza bidhaa nyingi hata mbegu za mazao kutoka nchi nyingine zinazotokana na teknolojia ya *GMO.* Sasa naiomba Serikali irekebishe kanuni hii kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa kuzingatia marekebisho ya Kanuni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Bajeti yake hapa Bungeni. Maoni yangu ni kufanyiwa marekebisho ya Kanuni ya Matumizi Salama ya Bioteknolojia *(Environmental Management (Bio Safety) Regulations, 2009).* Naambatisha maoni yangu ya taarifa nzima kuhusu *GMO* na mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bioteknolojia ni taaluma ya kutumia michakato ya ki-baiolojia ya viumbe hai ili kutengeneza bidhaa au kupata huduma kwa matumizi mbalimbali. Bioteknolojia inaweza kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Sekta za Afya, Kilimo, Viwanda na Mazingira hapa nchini. Katika Sekta ya Afya bioteknolojia inatumika kutengeneza dawa na chanjo mbalimbali; kutambua magonjwa mbalimbali na kutengeneza vyakula vyenye virutubisho vya kukabiliana na matatizo ya utapiamlo. Kwa upande wa mazingira, teknolojia hii

inaweza kutumika kusafisha mazingira; kwa mfano, kwa kuondoa mabaki ya sumu zinazotokana na taka za viwandani na majumbani. Aidha, teknolojia hii inaweza kupunguza matumizi ya viuatilifu na hivyo kuchangia katika kutunza na kuhifadhi mazingira na afya za binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya taaluma hii katika Sekta ya Viwanda ni pamoja na kuzalisha bidhaa mbalimbali kama vile nishati mbadala (bio-gesi, biofueli), vyakula vya wanyama, madawa ya kusafishia *(detergents),* plastiki zinazoweza kuoza na vipodozi mbalimbali. Katika Sekta ya Kilimo matumizi ya bioteknolojia ni pamoja na:-

- Kuongeza tija kwa kuzalisha aina za mazao yenye (a) kustahimili ukame, (b) kustahimili magonjwa, (c) ukinzani dhidi ya wadudu na viuamagugu, (d) virutubisho zaidi (e) sifa ya kukaa muda mrefu bila kuoza na kupoteza ladha, (f) upungufu wa sumu asilia kwa mfano kwenye tumbaku na mihogo;

- Kuwezesha kutambua na kutofautisha nasaba za mimea na wanyama kwa uhakika na ufanisi;

- Kuhifadhi nasaba za mimea na wanyama;

- Kuzalisha kwa wingi miche yenye kutoa mazao mengi na isiyokuwa na magonjwa kwa njia ya tishu;

- Kuhifadhi nasaba za mimea na wanyama; na

- Kuzalisha kwa wingi miche yenye kutoa mazao mengi na isiyokuwa na magonjwa kwa njia ya tishu.

Hata hivyo, wapinzani wa teknolojia hii wamekuwa na mashaka katika maeneo makuu yafuatayo; usalama wa chakula kwa binadamu na wanyama na athari hasi kwa mazingira, kiuchumi na biashara, kimaadili, mila na desturi.

Taarifa kutoka Mashirika mbalimbali ya Kimataifa zinaonesha kwamba hakuna madhara yoyote kwa binadamu, wanyama wala mazingira, ambayo yamewahi kutokea katika nchi zinazozalisha mazao ya *GMO* baada ya kuidhinishwa na vyombo husika. Kwa mfano, taarifa kutoka Shirika la Afya la Dunia *(WHO)* zinaonesha kwamba, vyakula vitokanavyo na mazao ya *GMO* vilivyoko katika soko havina madhara yoyote kwa watumiaji kwa kuwa vimethibitishwa na kupasishwa na vyombo vinavyosimamia matumizi salama ya *GMOs* katika nchi husika. Aidha, hakuna taarifa zozote kutoka nchi zinazozalisha mazao ya *GMO* zinazoonesha kuwa wananchi wake wamewahi kudhurika kiafya kutokana na mazao hayo.

Kwa kutambua umuhimu na mchango wa bioteknolojia, Serikali ilianza mchakato kuhakikisha Taifa linafaidika na uhawilishaji *(technology transfer)* na uendelezaji wa matumizi ya bioteknolojia hapa nchini kwa kufanya yafuatayo:-

- Iliridhia kujiunga na *International Centre for Genetic Engineering and Biotechnology - ICGEB)* mwaka 2002;

- Iliunda Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Bioteknoloja *(National Biotechnogy Advisoty Committee - NBAC)* mwaka 2002;

- Iliridhia Itifaki ya Cartagena ya Mkataba wa Bioanuai *(Cartagena Photocol on Biosafety, CPB to the Convention on Biological Biodiversity, CBD)* mwaka 2003. Madhumumi ya Itifaki hii ni kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia usalama katika usafirishaji, *"handling"* na matumizi ya viumbe watokanao na bioteknolojia ya kisasa zinazoweza kuathiri bioanuai au afya ya binadamu;

- Iliunda mfumo wa Taifa wa Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia *(National Biosafety Framework)* mwaka 2005 kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004;

- Ilipitisha Mwongozo wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia *(Biosafety Guidelines)* wa mwaka 2005;

- Ilitengeneza Kanuni za Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia mwaka 2009;

- Iliunda Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia *(National Biosafety Committee)* mwaka 2009;

- Ilipitisha Sheria ya Matumizi ya Vinasaba *(The Human DNA Regulation Act)* mwaka 2009; na

- Ilipitisha Sera ya Taifa ya Bioteknolojia mwaka 2010 ambayo inatoa miongozo ya uhawilishaji na uendelezaji wa matumizi ya bioteknolojia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuandaa Mfumo wa Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia (mwaka 2003 – 2005), kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi za Afrika, Tanzania tulijiwekea kwa makusudi mazingira magumu *(precautionary principle* na *strict liability)* ili kudhibiti uingizaji na matumizi ya bidhaa zitokanazo na bioteknolojia ya uhandisi jeni *(genetic engineering).* Kanuni za *strict liability* zinaifanya sheria iwabane wahusika katika mlolongo mzima wa kutafiti, kuendeleza, kusafisha na kutumia teknolojia hii, wahusike moja kwa moja na madhara ambayo yanaweza kutokea hata kutokana na makosa ya watu wengine au hata kama hayatakuwa yamesababishwa na teknolojia yenyewe. Sababu ya msingi ya kuweka mazingira hayo magumu wakati huo ilitokana na kutokuwa na uwezo na utaalamu wa kutosha wa kufanya tathmini na udhibiti madhara *(risk assessment and risk management).*

Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika imekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza matumizi ya bioteknolojia ya uhandisi wa jeni katika Sekta ya Kilimo hapa nchini kama ifuatavyo:-

(1) Kujenga maabara ya kisasa katika Kituo cha Utafiti cha Mikocheni ya kufanya utafiti wa uhandisi jeni

kwa msaada wa asasi mbalimbali, zikiwemo *Rockefeller Foundation, Association to Strengthening Agricultural Research in East and Central Africa – ASARECA, Bill and Melinda Gates Foundation* na *Danforth Centre* ya Marekani. Maabara hii imeanza kufanya utafiti wa aina bora za mihogo yenye uwezo wa kuhimili magonjwa ya batobato *(cassava mosaic disease)* na michirizi ya kahawa *(cassava brown steak disease – CBSD)* baada ya kupata kibali kutoka kwa Waziri wa Mazingira.

(2) Wizara inashirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* katika kutekeleza Mradi wa *Water Efficient Maize for Africa* wenye lengo la kuongeza na kuimarisha uhifadhi wa chakula kwa kuzalisha mbegu bora za mahindi yanayostahimili ukame. Aidha, matokeo ya mradi huu yatachangia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu ulianzishwa mwaka 2008 na unashirikisha Nchi za Uganda, Kenya, Msumbiji, Afrika Kusini na Tanzania. Mradi umejenga uwezo wa wataalamu na kuweka miundombinu kwa ajili ya kuanza utafiti huo. Mradi umeongeza uelewa wa wananchi juu ya masuala ya bioteknolojia kutokana na warsha za wadau katika ngazi za kitaifa, Mkoa (Dodoma) na Kata ya Makutupora na vile vile kwa kushiriki katika Maonesho ya Nanenane.

(3) Mradi wa WEMA una mpango wa kuanzisha utafiti wa kumdhibiti funza wa mahindi kwa kutumia mahindi yaliyofanyiwa mabadiliko ya jeni *(Bt-maize).* Kwa kufanya hivyo, Mradi wa WEMA unatarajia kuzalisha na kuwapatia wakulima aina ya mahindi

yenye sifa ya kustahimili ukame pamoja na funza wa mahindi.

(4) Mradi wa kutafiti mbegu za mahindi inayostahimili ukame kutumia jeni inayotokana na mmea wa jangwani *(resurrection plant).* Mradi unashirikisha Nchi za Sudan, Ethiopia, Kenya na Tanzania chini ya ufadhili wa *ASARECA.* Mtafiti kutoka Wizara ya Kilimo amelazimika kufanyia utafiti wake Nchini Kenya.

Changamoto kuu: Kanuni za *strict liability* zinawanyima watafiti uhuru na fursa ya kufanya na kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa matokeo yake kwa kuwa zinakwaza upatikanaji wa rasilimali na ubadilishanaji wa utaalamu na uzoefu.

Kanuni za *strict liability* zinawakwaza washirika wetu na wadau wa maendeleo wanaofadhili tafiti za uhandisi jeni pamoja na wawekezaji katika Sekta ya Kilimo kwa kuwa sheria inaweza kuwatia hatiani hata kama madhara ambayo yanaweza kutokea yanatokana na makosa ya watu wengine au hata kama hayatakuwa yamesababishwa na teknolojia yenyewe.

Athari hasi zitakazoletwa na kuendelea na mfumo tulionao sasa ni:-

(1) Kudhoofisha juhudi za Serikali za kujijengea uwezo wa kutumia sayansi, teknolojia na uvumbuzi katika utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza na

Mapinduzi ya Kijani ili kuongeza tija na maendeleo ya Taifa na wananchi wake kwa jumla.

(2) Taifa kukosa fursa ya kutumia na kufaidika na teknolojia bora zenye uwezo wa kuimarisha uhakika wa chakula na kuongeza kipato. Kwa mfano, wakulima wadogo wa pamba Nchini Burkina Faso, Afrika ya Kusini, China na India wameweza kuongeza tija na uzalishaji wa pamba kutokana na kupanda *Bt-cotton.* Aina hii ya pamba imefanyiwa mabadiliko ya jeni kuiwezesha kujikinga kwa kiasi kikubwa na funza wa vitumba na kumfanya mkulima kutumia kiasi kidogo cha viuatilifu. Kwa hiyo, gharama za uzalishaji zinapungua na madhara yatokanayo na matumizi ya viuatilifu kwa binadamu na mazingira yanapungua. Aidha, faida kama hizi zinapatikana kwa kutumia aina ya mahindi ya *bt-maize* yenye ukinzani dhidi ya funza wa mahindi.

(3) Pamoja na kwamba sheria itatumika kudhibiti uingizaji wa mazao na bidhaa za *GMO,* kukwama kwa tafiti za *GMO* kutokana na Kanuni za Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia, kunaikosesha nchi fursa na uwezo wa kufanya tathmini ya madhara na udhibiti wake *(risk assessment and risk management).* Kwa kuwa kuna uwezekano wa mazao na bidhaa za *GMO* kuingizwa nchini kwa njia zisizo halali, sisi kama nchi tutakuwa hatujajiandaa kujua kama mazao hayo yatakuwa na madhara au la. Uwezekano huu ni mkubwa kwa sababu nchi jirani za Kenya na Uganda zinafanya tafiti za aina hii katika mazao ya mihogo, mahindi, migomba, viazi vitamu na pamba na mwaka huu Kenya inatarajia kuwa nchi ya nne Afrika, baada

ya Afrika ya Kusini, Misri na Burkina Faso, kuidhinisha uzalishaji wa pamba *(Bt-cotton)* kibiashara.

(4) Kusitishwa kwa miradi ya utafiti inayoendelea nchini. Hii ni pamoja na mradi wa utafiti wa aina bora za mihogo yenye uwezo wa kuhimili mradi wa utafiti wa aina bora za mihogo yenye uwezo wa kuhimili magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia pamoja na Mradi wa WEMA unaolenga kuzalisha miwa, mihogo na mahindi kama ilivyoelezwa hapo juu mwaka huu; unatarajia kuzalisha na kuwapatia wakulima aina ya mahindi yenye sifa ya kustahimili ukame pamoja na funza wa mahindi.

(5) Watafiti wetu kukatishwa tamaa na kushawishika kuhamia nchi za nje, zikiwemo nchi jirani kufanya tafiti hizo. Kwa mfano, watafiti wetu wamelazimika kufanya utafiti wa pamba *(Bt-cotton)* na mahindi nchini Kenya.

(6) Kupunguza kasi ya sekta binafsi katika kuwekeza kwenye miradi ya uwekezaji kama vile *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)* ambayo inatarajia kutumia teknolojia mpya.

(7) Kudhoofisha azma ya Serikali katika ushirikishaji wa Sekta Binafsi *(Public – Private – Partnerships)*, asasi za Kikanda na Kimataifa katika utafiti na maendeleo hapa nchini. Sekta binafsi ni mdau muhimu kutokana na umiliki wake wa teknolojia mpya *(proprietary technologies)* ambazo zitachangia juhudi za kuleta Mapinduzi ya Kijani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba ili kuweka mazingira mazuri ya kuhawilisha na kuendeleza utafiti na matumizi ya *GMO* hususan katika Sekta ya Kilimo na kuweza kunufaika na matokeo ya tafiti mbalimbali zinazohusu mahindi, mihogo, pamba, migomba na kadhalika, tunaishauri Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka za kufanya marekebisho ya Kanuni hizi.

Tunapendekeza Kanuni hizi zirekebishwe ili uwajibikaji wa wahusika uzingatie kosa litakalotendeka na mhusika atakayekuwa amelitenda, yaani *fault based liability.*

Zifuatazo ni Kanuni zinazopendekezwa zifanyiwe marekebisho:-

*Regulation No. 6: Strict Liability Statement:*

- *All approvals for introduction of GMO or their products shall be subjet to a condition that the applicant is strictly liable for any damage caused to any person or entity.*

*Implication:*

- *The principal of strict liability is not fault-based and may apply despite the exercise of utmost care on the part of the alleged offender. According to this provision, the applicant would be liable in cases where damage is not necessarily caused as a result of the applicant's actual negligence or intent to harm.*

- *Almost all countries in the world have their own legislation usually based on a fault based liability system for technologies that have already been shown to be safe to humans, animals and the environment.*

*Regulation 56 (1,2,3): Strict liability*

*Statement:*

- *56 (1). Any person or his agent who imports, transits, makes contained or confined use of, releases, carries out any activity in relation to GMOs or products thereof, places on the market a GMO shall be strictly liable for any harm, injury or loss caused directly or indirectly by such GMOs or their products or any activity related to GMOs.*

- *56 (2). The harm, injury or loss includes personal injury, damage to property, financial loss and damage to the environment or to biological diversity as well as taking into account socio-economic, cultural and ethical concerns.*

- *56 (3). Liability shall be attached to the applicant, the person responsible for the activity which results in the damage, injury or loss, as well as the provider, supplier or developer of the GMOs or their products.*

*Implication:*

- *The expressions of these provisions are too broad, not functional and not enabling. They cover products there of, indirect effects of GMOs and products there of, socio-economic, cultural and ethical*

*concerns. This provision provides room for the alleged offender to be held guilty without proof of association of the observed injuries or losses to the GMO activities.*

*Regulation 57 (1): Liability of Officer of Corporation*

*Statement:*

- *Any director, manager, secretary or similar officer of a corporation shall similarly be held liable unless he can show he did everything in his power to prevent the import, release, etc. that caused the damage.*

*Implication:*

- *No fault liability may scare decision makers to take actions in favour of promoting GMO activities even when benefits may outweigh perceived risks.*

*Regulation 59: Liability for socio-economic harm or damage.*

*Statement:*

- *Liability also extends to damage caused directly or indirectly to the economy, social or cultural principles, livelihoods, indigenous knowledge systems or indigenous technologies. Harm includes disrupt or damage to production systems, agricultural systems, reductions in yield, and damage to the economy of an area or community.*

*Implication:*

*- Theoretically, this provision could make applicants, promoters, investors, innovators, collaborating partners and sponsoring agencies, liable if farmers of non-GMO traditional variety in a particular region of Tanzania lose market share to smallholder farmers using the GM crop variety.*

*Regulation 60: Indemnification by Applicant.*

*Statement:*

*- The application shall indemnify any other person who deliberately releases or markets GMOs or products thereof and any person who manufactures, processes or markets food, food ingredients or animal feed containing or derived from GMOs against any civil liability where the GMO or their products were first imported, released, used in contained conditions, or placed on the market etc. by the applicant.*

*Implication:*

*- The effect of an indemnification provision is that the indemnifying party (applicant) will compensate the indemnified party for any loss or damage that may be suffered as a result of the actions of the applicant. Indemnification may work by either direct compensation to the injured or by reimbursement for any loss incurred by the indemnified party. As stated above, the indemnifying party will be compelled to compensate the indemnified party regardless whether there is or no proof of injury or loss suffered by the indemnified party to have directly or indirectly been caused by GMO activities by the indemnifying party.*

*Regulation 62 (1): Right of individual and legal persons to sue.*

*Statement:*

- *Any person may bring a claim and seek relief for any breach or threatened breach of the Regulations if in his own or the public interest. The NBFP also may initiate actions for compensation of any inhabitants or organisations in Tanzania that may suffer damage as a consequence of exposure to imported GMOs and their products. Art. 8(h).*

*Implication:*

- *This provision is potentially problematic because of two reasons. First, the highlighted expression is too broad and speculative especially in view of the fact that a guiding principle of the Regulations is the provision that the lack of scientific evidence is not a basis for not taking preventive measures. Second, the above provision grants any anti-GMO grop the right to institute a speculative lawsuit against the Applicant and collaborating partners on the pretext that they are protecting the interests of a particular person or group of persons.*

*Regulation 64 (2) (a) & (b): Protection for reasonable.*

*Statement:*

- *Under the Regulations, no person is liable or may be dismissed, disciplined or prejudiced on account of having disclosed information to*

*governmental authorities or the news media, if the person in good faith reasonably believed at the time of the disclosure that he was disclosing evidence of any risks posed by GMOs or their products.*

*Implication:*

- *While it is difficult to argue with the good faith disclosure of information to government authorities, the provision allowing disclosure of information to news media outlets could lead to violations of the confidentiality agreements, e.g. disclosure of Confidential Business Information (CBI).*

*Regulation 35 and 72 (1): Insurance against liability.*

Statement:

- *The applicant must have an insurance policy that covers liability to pay compensation for damages. The NBFP must be satisfied that the policy covers the risks likely to arise out of the activities.*

*Implication:*

- *Liability insurance for GMOs is not widely available in Africa, including Tanzania and the costs of such insurance could increase operational and product costs.*

*Article 73: Environmental Impact Assessment.*

*Statement:*

- *An application for field trial or release of GMO shall not be permitted or licensed under the Regulations unless an Environmental Impact Assessment under these regulations has been carried*

*out in accordance with the Act and the Environmental Impact Assessment and Audit Regulations, 2005.*

*Implication:*

*- This provision should not apply to research under confined field trials because these are normally small experimental plots designed with adequated risk management measures to evaluate the GMO in question and to collect additional risk assessment data.*

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwanza, kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji umakini wa hali ya juu katika utekelezaji wake na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano ni muhimu sana kwa Watanganyika na Wazanzibari mbali ya mambo mengine yote, kubwa zaidi tumekuwa damu moja. Pili, Sera yetu ya Chama cha Wananchi *(CUF)* ni Muungano wa Serikali tatu, ndiyo kilio chetu, hivyo Muungano udumu lakini unahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa ya kuwa ndugu, damu moja, zipo changamoto nyingi zilizojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo wa masuala ya Muungano na utekelezaji wa masuala ya Muungano hasa katika kipindi hiki cha uundwaji wa Katiba Mpya, lakini pia Muungano sasa hivi una umri mrefu, vijana wengi

hawana uelewa wa Muungano huo, wanahitaji elimu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, changamoto kubwa kabisa iliyopo ambayo ni kero kubwa kwa Wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla wao ni mfumo tofauti wa sheria kwa pande mbili za Muungano; hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika kutatua changamoto za Muungano kama suala la usajili wa magari na kodi mbalimbali ambazo hazina utaratibu maalum au hazieleweki hasa unapotoa vitu Zanzibar kuja Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu; elimu kuhusu Muungano ni muhimu sana kwa njia zote, kuuelimisha umma kwa ufafanuzi mzuri kabisa, elimu hiyo ieleze wazi kwa nini tuliungana, umuhimu wa Muungano, tumeungana kwenye mambo gani na faida za Muugano. Pia Serikali zetu zishirikiane katika kutatua suala la kodi zinazotozwa ovyo bila wananchi kuelewa sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni muhimu sana vikao vinavyoendelea vya kutatua kero za Muungano vifanyike kwa umakini na kuhakikisha kero hizo zinapatiwa ufumbuzi kwani ni kilio kikubwa kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaelekea kuwa jangwa kutokana na ukataji miti hovyo bila kupanda mingine. Miji yetu ni michafu sana. Dar es Salaam peke yake ni hatari, kuna *pollution* kila kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika wazi kuwa, ukataji miti na uchomaji wa misitu Tanzania umeendelea kwa kiwango kikubwa sana. Lazima kuwe na mikakati madhubuti ya kufuata Sera yetu ya Taifa ya Kata Mti Panda Mti ili kuepusha jangwa linalotaka kutokea nchini kwetu.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kupongeza juhudi ambazo Serikali inachukua kukabiliana na changamoto za kimazingira hadi sasa. Juhudi hizi ni pamoja na ripoti mbalimbali, sheria, sera, tafiti mbalimbali, machapisho, kijarida, kanuni mbalimbali, miradi mbalimbali, mipango kadhaa ambayo ni pamoja na MKUHUMI kuhusiana na udhibitri wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, naipongeza Serikali kwa kukamilisha kanuni zitakazoipa uwezo kupiga marufuku mifuko ya plastiki, isipokuwa ile ya kuhifadhia maziwa na chakula, ambayo kwa muda mrefu imekuwa ni kero katika maeneo yetu. Hata hivyo, Serikali lazima iwe na mpango madhubuti wa namna ya kuchakata aina ya plastiki ambazo zitaendelea kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Serikali bado inakabiliwa na changamoto nyingi, baadhi ya changamoto hizo ni:-

(i) Serikali Kuu na za Mitaa hazijawa na mipango madhubuti ya kuweka mazingara yetu katika usafi

unaostahili. Maeneo yetu; mijini na vijijini ni machafu sana. Kwa ujumla, tatizo ni uelewa na wananchi kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira na wajibu wa kila mtu kuweka mahali pake katika usafi. Kadhalika, Serikali haijahamasisha vya kutoka usafi katika nchi nzima.

(ii) Hatua za utunzaji wa mazingira ambazo Serikali imekuwa ikichukua hazitoshelezi kuleta mabadiliko yanayohitajika hasa kuhusiana na upandaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na upandaji wa miti, napendekeza Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

- Iwe ina miradi na Mipango ya Kitaifa ambayo inafaa ienezwe katika kila Wilaya. Miradi ya Kitaifa iwe ni mifano ya kuigwa na watu katika maeneo husika.

- Iwe na miradi na mipango katika kila Halmshauri. Hii itekelezwe kwenye ngazi ya vijiji.

Tujifunze kutoka kwa wenzetu wa Rwanda kuhusu usafi wa mazingira na kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti.

Mwisho, nataka kuuliza kwa nini Tanzania ilipinga Muswada wa Sheria ya Mazingira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mapema mwaka huu (2012)? Muswada huu ulihusu mazingira yanayovuka mpaka wa nchi. Licha ya Tanzania kuupinga, Muswada huo uliungwa mkono na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Je, Muswada huo

wa Sheria umeshaidhinishwa na Marais wa Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano; nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Wataalamu wa Wizara. Nampongeza pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii, Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa Hotuba zao zilizowasilishwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wa Nchi za Afrika kuwa Taifa moja ilikuwa ndoto ya Baba yetu wa Taifa, Marehemu Mwalimu Nyerere na hadi kufa kwake tarehe 14 Oktoba 1999 aliutetea bila kutetereka. Mwalimu Nyerere hakudhani hata kidogo kuwa Muungano utakuwa na changamoto hizo na alizisemea; la msingi zaidi alisisitiza manufaa ya Muungano.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Nchi za Afrika kuungana, Muungano wetu ni mfano bora wa utekelezaji wa nia ya Waafrika kuungana.

Juhudi za Serikali ya SMZ na SMT kushughulikia changamoto mbalimbali za Muungano kupitia Kamati ya Pamoja zinastahili pongezi. Licha ya juhudi za Kamati hii, bado kuna changamoto zifuatazo:-

(i) Malalamiko ya Wazanzibari kuwa bado wanaonewa na Tanzania Bara. Mathalani, wengi hawajaridhika na gawio la asilimia 4.5 la Pato la Taifa ingawa vigezo vilivyotumika ni thabiti na vya Kimataifa.

Malalamiko mengine ya baadhi ya Wazanzibari ni kuwa hawanufaiki na Muungano, kwa hiyo, hawautaki.

(ii) Malamamiko ya upande wa Tanzania Bara kuwa Tanganyika yao ilifutwa ilhali Zanzibar haikufutwa. Majina “Tanzania Visiwani na “Tanzania Zanzibar” ambayo kwa nyakati mbalimbali yalipendekezwa hayakupata mashiko; jina la Zanzibar limeendelea kutumika.

(iii) Changamoto kubwa zaidi inahusiana na Katiba ya Zanzibar (2010). Katiba hii ina vipengele vinavyopingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mathalani, Katiba ya Zanzibar (2010) inasema kuwa, Zanzibar ni nchi, jambo ambalo linapingana na Katiba ya Muungano inayosema: “Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto hizo, mchakato wa kuandika Katiba Mpya ni fursa nzuri kwa Watanzania kuutafakari Muungano. Ninaungana na Kambi ya Upinzani na wengine wote wanaopendekeza kuwa “Muungano” na “aina ya Muungano” yawe ni maswali yatakayopigiwa kura za maoni Tanzania Bara na Zanzibar. Watu waulizwe kama wanautaka Muungano, na kama wanautaka uwe wa muundo gani; Serikali mbili, tatu au moja? Kura hiyo ya maoni ndiyo itakayotupa majibu ya kudumu kuhusiana na suala zima la Muungano.

**MHE. SAID SULEIMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam Mkataba wa Muungano na Sheria ya Muungano zipo, ni vizuri sasa kufanya rejea

kuona wapi tumepotoka na wapi panahitajika kuimarishwa ili kukomesha umbeya na uzushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kero za Muungano hazina mtatuzi. Kwa maoni ya Tume ya Nyalali ni kwamba, kwa kuwa Tanganyika ilifutika kufuatia Muungano na Zanzibar ikabaki ni wazi kuwa Zanzibar ilikosa mweza wa kujadiliana naye kwa hali ya usawa kuhusu matatizo ya Muungano kadiri yanavyojitokeza tokea 1964 mpaka hii leo. Nasema Zanzibar haina mweza kwa sababu Tanzania ndiyo Tanganyika na Tanganyika ndiyo Tanzania wakati Zanzibar ni sehemu tu ya Tanzania ambayo ndiyo Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira hayo ambayo Serikali ya Muungano si Serikali mwenza wa Serikali ya Zanzibar, kwa hivyo basi, kero za Muungano hazina mtatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari ni lazima tuwe na msimamo mmoja, fikra moja na sauti moja, juu ya Katiba Mpya na kura yake ya maoni. Kura hiyo itakuwa na lengo la kutaka kuihalalisha Katiba Mpya pamoja na Muungano ambao haujawahi kupata kamwe kukubaliwa na wananchi au na taasisi yoyote ya kizanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe hii si mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa na mchakato wa kutunga Katiba au kupitia upya Katiba ya Nchi. Hapo ninawajibika kukumbusha namna CCM ilivyoandika na kuishurutisha Katiba ya Mwaka 1977, ambayo ndiyo inayotumika sasa. CCM iliyofanya hayo kwa njia isiyo

halali. Ninasema hivi kwa sababu Hati za Muugano za Aprili 1964 kati ya Tanganyika na Zanzibar zilikuwa bayana kwamba, Bunge la Katiba litaundwa kabla ya mwezi Aprili 1965, likiwa na idadi sawa ya wawakilishi kutoka Zanzibar na Tanganyika kuzingatia mfumo wa kudumu wa Muungano na Katiba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tujuavyo, hayo hayakutendeka. Kwa hiyo basi, CCM iliweza kuishurutisha Katiba Mpya kwa sababu Taifa lilikuwa na mfumo wa Chama kimoja tu cha siasa na chama ndicho kilichokuwa taasisi adhimu nchini kushinda taasisi yoyote ile nchini. Kwa hiyo basi, Kanuni ya kutetea na kulinda maslahi ya Zanzibar ni muhimu sana wakati huu wa mchakato wa kutunga Katiba Mpya.

Kwa hakika, miongoni mwa mambo ambayo Wazanzibari wanapaswa kuyazingatia wakati wa mchakato huu ni hili suala la maslahi ya jumla ya nchi yetu na Kanuni ya Kimsingi ya kwamba Taifa letu ni muhimu zaidi kushinda kitu chochote kingine. Hivyo, maslahi ya nchi yetu ni muhimu zaidi kuliko maslahi ya Vyama vyetu vya Kisiasa; kiwe CUF, CCM, CHADEMA au chama chochote kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari hatutoweza kuyatetea na kuyalinda maslahi ya nchi yetu endapo tutagawanyika. Kwa sababu hiyo basi, lazima tuwe waangalifu, tusibabaishwe na kugawanywa kama tulivyokuwa tukigawanywa huko nyuma. Tukijiachia tukagawanywa itakuwa ni rahisi sana kwa wasioitakia heri nchi yetu ya Zanzibar kuacha mifumo ya utawala itakayodharau maslahi ya nchi yetu. Hali hii ikitoea na

tukijikuta tumegawanyika tena, basi sisi wenyewe ndiyo wa kulaumiwa na vizazi vijavyo vya Wazanzibari kwa kuiuza nchi yao.

Mheshimiwa Spika, tunataka nchi yetu iwe na uhuru wa kujiamulia mambo yake yenyewe bila kuingiliwa. Tunataka nchi yetu iwe na sarafu yake. Tunataka nchi yetu iwe na Benki kuu yake. Tunataka pia nchi yetu iwe na uhusiano na Tanganyika katika mfumo unaoshabihiana na uhusiano wa nchi zilizomo katika Jumuiya ya Ulaya.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya ukuaji wa Sayansi na Teknolojia Duniani leo na hasa ukizingatia Lengo la Nane la Milenia *(Global Partnership)* ni kwamba, rasilimali watu ndiyo rasilimali kubwa kuliko zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar ni tunu ya kuendeleza. Mfumo wetu wa Muungano ni mzuri sana na wa kuigwa hapa Barani Afrika. Zipo changamoto ndogo ndogo za kufanyia kazi hasa suala la Muundo wa Muungano na namna bora ya kuzitumia rasilimali tulizonazo kwa maslahi ya pamoja yenye kuzingatia maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utu wa mwanadamu hupimwa zaidi na uelewa wa kujitambua kuhusu thamani ya uhai wa binadamu. Uelewa huu unatakiwa utiliwe mkazo kwenye mifumo yetu ya Elimu (Elimu inayojali utu wa mwanadamu). Nashauri kwa kuwa sisi ni Taifa moja, elimu inayotolewa iwe moja

(mitaala inayofanana na miongozo inayosabihiana). Hii itasaidia kuwa na Taifa lenye uelewa na fikra zenye kudumisha Uzalendo wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya msingi kuhusu umri wa Muungano wetu wa miaka 48, ambayo yamefanikiwa kufikiwa (chanya), yawekwe wazi na kufundishwa katika shule zetu ili kizazi kilichopo kiweze kufahamu umuhimu wa Muungano wetu. Pia yapo mambo ambayo ni hasi yaliyotokea katika kipindi hicho nayo yawekwe wazi kama changamoto za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni dhana pana. Mwenyezi Mungu, alimuumba mwanadamu ili aweze kutawala vitu vyote vilivyopo Duniani. Mharibifu mkubwa wa mazingira ni binadamu, hasa katika kuichokonoa asilia ya uumbaji. Lengo la Saba la Milenia ni la Uhifadhi wa Mazingira *(Sustainability and Environmental Protection).* Nashauri vigezo vilivyowekwa maalum vifikiriwe vitatumikaje ifikapo mwaka 2015 katika kupima Malengo ya Milenia. Elimu ya mazingira ni muhimu ikapewa kipaumbele katika taasisi zote za elimu, pia kwa kutumia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ya utabiri wa hali ya hewa ni vyema likasisitizwa katika ufahamu wa jamii nzima ya Watanzania kwa ajili ya maandalizi ya kilimo, pia namna bora ya kupambana na majanga ya ukame na mafuriko yanapotokea.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataasafu kusema kwamba, uundwaji wenyewe wa Kamati inayoshughulikia Kero za Muungano imeundwa katika misingi ambayo haina nia njema ya kumaliza Kero hizo kwa wakati unaostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema mfumo huu haulengi kumaliza Kero hizo kutokana na sababu zifuatazo:-

Makamu wa Rais kawekwa Mwenyekiti, Makamu wa Pili wa Rais kutoka Zanzibar (SMZ), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ambaye anatoka Zanzibar. Mfumo huu unaelekea kwamba, unalenga kabisa kutomaliza Kero za Muungano kwa haraka, lolote ambalo litapelekwa litaonekana kwamba Wajumbe wanaotoka Zanzibar wameamua wao na kwa hiyo halina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kero za Msingi za Muungano hazijatatuliwa na wala hazijatamkwa kabisa lakini kero za msingi za Muungano ni namna ya Muungano wenyewe juu ya namna gani pande mbili za Muungano huu wananchi wake walishirikishwa katika kuunganishwa kwao. Lililokuja kuvuruga zaidi ni uvunjwaji wa Mkataba wa Muungano ambao uliweka misingi maalum katika kujenga na kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero moja ya msingi katika Muungano wetu ni kumwondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, jambo ambalo liliondoa kabisa dhana

nzima ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Suala la kumwondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni sawa na kuifanya Zanzibar kwamba siyo Mshirika wa Muungano na limeipa nguvu Katiba ambayo ilivunja Mkataba wa Muungano, kifungu cha kwanza, ukurasa wa 18 kinasema; Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano. Kitendo cha kumfanya Rais wa Zanzibar kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri ni kitendo cha dharau kwa Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ambayo ina wajibu wa kushughulikiwa ni Akaunti ya Pamoja na Mfuko wa Pamoja wa Fedha, haya yametamkwa katika ukurasa wa 176 na 177, kifungu cha 133 na 134 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Toleo la Mwaka 1977, kutokupatiwa ufumbuzi suala hili kunaonesha hakuna nia ya dhati ya kutatua Kero za Msingi za Muungano huu. Kwa nini Katiba imevunja Mkataba na hatimaye isitekeleze hata yale ambayo ilijiamulia kuyaweka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, SMT imechangia kwa kiasi kikubwa kuwafanya Wazanzibari kuukataa na kuuchukia Muungano kwa kuwavunja nguvu na madaraka ya Rais wa Zanzibar. Kama hilo halitoshi kuua hata nguvu za uchumi wa Zanzibar juu ya ukusanyaji wa mapato na wafanyabiashara kutozwa ushuru mara mbili linaonesha nia ya SMT kudhoofisha upelekaji wa mizigo moja kwa moja Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha ilikaa kikao chake tokea mwaka 1996 na

mapendekezo hayo yalishafikishwa Serikalini; kwa nini halijapatiwa ufumbuzi hadi leo? Tujiulize ni kweli SMT iko *serious* katika kutatua Kero za Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu akiwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati inayoshughulikia Kero za Muungano, wakati akijibu hoja za Wabunge waliogusia fedha za rada alisema kwamba, fedha za rada hazihusiani na Muungano, ikiwa rada iliyokusudiwa ni chombo cha ulinzi na ulinzi ni suala la Muungano na zaidi ya asilimia 85 ilichukuliwa kutoka katika Ulinzi na si zaidi ya asilimia 15 iliyochukuliwa kutoka Wizara ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitaja. Inakuwe fedha za rada haziwahusu Wazanzibari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanzanzibari wanaambiwa fedha za rada haziwahusu na pesa za *EPA* vile vile tutaambiwa hazituhusu. Kwa misingi hiyo, SMT itakuwa inajenga na kuimarisha Muungano au ndiyo walio mstari wa mbele wanaovuruga Muungano?

Ieleweke kwamba, Muungano huu ni wa nchi mbili, ni lazima heshima ya Zanzibar itambuliwe, ithaminiwe na haki za Wazanzibari zitokanazo na Muungano wasidhulumiwe kwa kutumia kivuli cha Wizara zisizokuwa za Muungano ndani ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo pale aliposema kuwa Mfuko wa Bunge wa Muungano kupitia Zanzibar umesaidia Shule ya Msingi Simai, Wingwi; je, fedha hizi ni pamoja na

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kupitia Mbunge wao au vipi? Ikiwa kuna Mfuko mwingine mbona mimi kama Mbunge wa Jimbo husika sina taarifa nao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Hotuba ya Upinzani iliyowasilishwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, *page 4 of 22, paragraph* ya kwanza, namjibu kama ifuatavyo:-

Kwamba, Zanzibar ipo na ipo hai na kuwepo kwa Tannganyika ni kuonesha uwepo wa Wizara 20 ambazo hasihusiani na Muungano na Wizara sita tu ambazo ni za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *page 6 of 22* ya Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imesema kwamba, Katiba ya Zanzibar ni batili. Ukweli kwamba, Katiba ya Zanzibar imetungwa, ni Chombo halali kinachochaguliwa na Wananchi wa Zanzibar na Bunge hili halina uwezo wa kujadili na kuhalalisha jambo lolote ambalo mamlaka yake yako chini ya Kifungu cha 64 (2) cha Katiba ya Muungano.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri wa Muungano na Mzingira, kwa kuwasilisha Hotuba yao nzuri ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni kila kitu katika maisha ya binadamu, kwa kuwa shughuli zote za binadamu zinafanywa katika mazingira hivyo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie namna ya kushiriana na Viongozi wa Serikali wa Mkoa wa Dar es Salaam na Jiji hilo kwa ujumla ili kukuza hadhi ya Jiji hilo kimazingira, ambalo kwa sasa linakithiri kwa uchafuzi wa mazingira. Jiji la Dar es Salaam ni taswira ya Mikoa yote ya Tanzania ambapo endapo litakuwa safi na ni dhahiri kuwa litailetea sifa nchi yetu kuwa ni nchi nzuri, inayopendeza, lakini kwa hali ilivyo sasa, Jiji la Dar es Salaam ni chafu sana. Uchafuzi wa mazingira kwa taka ngumu, mifuko ya plastiki, maji taka kuelekeza baharini na kipindi cha muvua maeneo mengine ya Dar es Salaam wanafungulia uchafu wa vyoooni na kuacha utitirike na maji ya mvua. Hali hiyo husababisha Jiji kuendelea kuwa chafu, hewa nzito na kukosekana kwa hewa safi na harufu kali; nashauri Wizara iandae Mkakati Maalum na kuwashirikisha Viongozi wa Serikali wa Dar es Salaam kuweka Sheria ndogo ndogo za kuliondoa Jiji katika hali hiyo ya uchafu uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayochimbwa madini yanaathirika kwa kiasi kikubwa, katika maeneo hayo machimbo yanatisha na kutokuwepo jitihada za makusudi za kuotesha uoto wa asili na upandaji wa miti katika maeneo ya machimbo yanatishia mazingira. Nashauri Wizara isisitize taasisi zinazofanya tathmini ya uharibifu wa mazingira ziwe zinasimamiwa na kuhakikisha zinafanya kazi yake vizuri; vinginevyo, athari zake na mabadiliko ya tabia ya nchi hazikwepeki katika maeneo mengi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni uchafuzi wa mazingira unaofanywa na wasafiri wa mabasi na magari madogo unaofanywa kwa kutupa mifuko ya plastiki na chupa za maji, wanapokuwa katika safari zao wanatupa barabarani au pembeni, bila kujali kwamba kwa kufanya hivyo wanachafua mazingira yetu. Ni vyema Serikali ikaona namna ya kuweka sheria kali zitakazowabana wasafiri kuchafua mazingira kwa kutupa taka hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la ukataji wa matawi ya miti na kutumika kama alama kwa magari yanayoharibika barabarani; ni dhahiri kuwa matawi ya miti haya yanakatwa na kuachwa barabarani mara baada ya wahusika kumaliza kurekebisha magari yao wanaacha matawi hayo barabarani na kufanya barabara zetu kuwa na matawi hayo mengi ambayo hayapendezeshi bali kuchafua mazingira. Wizara inaliona tatizo hili; na kama ndiyo utaratibu gani unafanyika ili tabia hii iachwe mara moja? Kwa kuwa vipo vifaa maalum vinavyopaswa kutumika kuwekwa barabarani magari yanapoharibika *(triangle)* zinapaswa kutumika siyo majani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri, lakini kwa upande wa mazingira nauliza Serikali; je, ina mkakati gani wa kuzuia viwanda vyetu hasa vile vilivyo karibu na wananchi kutokana na kemikali zinazotumika na kuchafua mazingira na

kusababisha athari na madhara mbalimbali hasa kupitia kwenye visima kuharibu maji; pia kutuama maji machafu na kuzidisha mazalia ya wadudu wabaya kama mbu na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mkakati wa kupanda miti kupitia Wizara ya Mazingira na inapofikia wakati wa kuadhimisha Siku ya Mazingira itolewe taarifa ya miti mingapi iliyopandwa kwa mwaka na mingapi imekufa. Hii itatujenga heshima ya kupanda miti na baadaye kuishughulikia siyo kudharau na kunyauka au kufa kabisa baada ya muda mfupi. Miti yote inayopandwa na Viongozi iwe inawekewa kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia mbaya sana kwa baadhi ya watu kujisaidia haja ndogo hovyo (kukojoa) mahali popote na hivyo kusababisha hatari kiafya, kuchafua mazingira na kuua nyasi. Tabia hii inawahusu baadhi ya wanaume, tena bila aibu utamkuta mtu na heshima zake anakojoa hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatunga Sheria ya kuwachukulia hatua na adhabu kali watu hawa? Nchi kama UK anayeruhusiwa ni mtoto wa miaka mitano kurudi chini na wote wanatii Sheria.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi sana kwa Mawaziri wote wawili,

kwa uhodari wao wa kazi hasa ukizingatia ni wanawake.

Mheshiiiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni nyeti sana nchini na Duniani kote. "Tusipoyatunza mazingira nayo hayatatutunza." Bado binafsi nashauri kuwepo na jitihada zaidi.

Changamoto ni kuwa watu wanahitaji mbao au kuni na kadhalika mkaa, lakini Halmashauri zetu hazijafanya jitihada za kutenga maeneo maalum ya kuruhusu kukata miti na maeneo ya kuchoma mkaa. Matokeo yake wanakata miti ovyo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua Halmashauri zetu kama Makete, Njombe, Rujewa na Iringa yametengwa wapi. Hii ni sample tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi wa Barabara – *Environmental Audit;* Wakandarasi hawa wanakata miti ovyo bila kushirikisha Wataalamu wa Mazingira na Serikali ya Kijiji mfano ujenzi wa Dodoma – Iringa kuelekea Mtera unaoendelea sasa. Lazima tuwe na *Recycleling Policy.* Mazingira yakitunzwa vyema na vyanzo vya maji hutunzwa vyema, bado tatizo la maji nchini ni kubwa sana vyanzo vya maji (mazingira) vinaharibiwa. Tunapaswa kuwa na kilimo cha umwagiliaji *(irrigation).* Tunayo miti mingi sana. Vijiji vingi havina maji mfano, Ilininda, Mudilu na Manda Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingi za Kimataifa za Mazingira hazijawa *Domesticated - signed or relified*

tu. Naomba kujua ni Sheria zipi *International Conventions* zimekuwa *ratified* na *domesticated* na zipo bado *and why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Mazingira ijiandae vyema kuweka haki na wajibu wa mazingira katika Katiba Mpya, kwa sasa hakuna suala la mazingira katika Katiba. Milipuko ya magonjwa mbalimbali kutokana kutotunza mazingira siyo sawa. Maeneo ya mikusanyiko kuwepo na mikakati maalum hususan stendi. Mfano, Ubungo, Kariakoo, stendi zote za mikoa zingine hazina vyoo, tuweke *strategic* na mabasi yapigwe marufuku kuchimba dawa barabarani. Wizara ingieni PPP. Wakija watalii hakuna vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Europe/Ulaya wametunza mazingira kiasi kwamba maji ya bomba unaweza kunywa bila kuchemsha maeneo kama *airport,* lakini kwetu maji ni biashara kubwa sana. Maji yanauzwa kwa shilingi 700, 1000 mpaka 1500; maji siyo maziwa. Sasa mwananchi wa chini akishindwa kununua atakunywa maji ya kawaida anaweza kupata tatizo. Wizara ya Mazingira ishirikiane na Wizara ya Maji tupate mazingira safi na maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyuo/hosteli wanafunzi hawawezi kunywa maji ya bomba mfano, Wanafunzi wa Mzumbe, Tumaini, UDOM, UDSM na shule za sekondari mfano Manda, Ilininda, tutunze mazingira nayo yatatutunza. Hata maeneo ya hospitali mfano Kibena, Makete, Ludewa, Lugarawa, mazingira hayaruhusu usafi wa maji watu wapate

kunywa maji, kutokana na kutolinda mazingira. Matokeo yake, watu wanahama vijijini kuja mijini, watu wanatoka Mtera, Ismani, mvua hazinyeshi kilimo kinagoma wanakuja kuishi mijini. Matokeo yake nyumba zinajengwa kienyeji na miundombinu hafifu, lazima tuwe *Health Environmental Health Initiatives.* Je, Tanzania tuna mikakati gani ya *Environmental Health Initiatives.* Eneo la Njombe, Makete na Ludewa watu tunapanda sana miti, tunaomba wataalamu wa *carbon credit* waje tena waanze Wilaya ya Ludewa ambako tumeanzisha vitalu vingi sana vya miti waje watupe elimu; watakuja lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano hili ni jambo muhimu, maoni yatatolewa katika Katiba Mpya, tunahitaj maamuzi ya Ushauri wa Tume ya JFC yafanyike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutunze mazingira nayo yatatutunza.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa kuandika. Pia nikushukuru wewe Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ulivyowasilisha hotuba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano ni jambo muhimu katika nchi yoyote ile kwani huongeza nguvu na ufanisi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umekumbwa na wimbi la kutojali upande mwingine wa

Muungano katika suala zima la uchumi na maendeleo na kwa maana hiyo upande mmoja wa Muungano kupoteza haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nzima ya muundo wa Muungano imechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kero za Muungano. Kwanza ni lazima tuelewe kuwa ndani ya Bunge hili, limegawika sehemu mbili(2), zipo Wizara za Muungano na zipo Wizara zisizokuwa za Muungano. Muundo huu unaleta utata kiutekelezaji, kwa maana hiyo haieleweki Wizara ambazo sio za Muungano bajeti yake inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kuwe na Mfuko miwili ya fedha kuwepo Mfuko wa Wizara ya Muungano kuna kifungu 133 cha Katiba kinachoelezea, lakini pia kuwe na Mfuko wa Wizara zisizokuwa za Muungano, hii italeta ufanisi na kuweza kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ni kumrejesha Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano kama ilivyokuwa zamani. Hii itasaidia kusimamia Zanzibar na kuitetea akiwa na nguvu kama Rais aliyeunganisha nchi yake. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa kero za Muungano na kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mgao wa mapato na uhusiano wa mambo ya nje ya nchi. Suala hili ni muhimu sana, ni lazima lipatiwe ufumbuzi kwani hapo ndipo penye chimbuko la kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii iliyowasilishwa na Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Muungano na Daktari Terezya Luoga Huvisa Mazingira pamoja na wataalam wote kwa kuwasilisha vizuri hotuba zao. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu katika ofisi hii ya Makamu wa Rais itakuwa katika maeneo yafuatayo: hasa katika eneo la mazingira, uharibifu wa mazingira katika maeneo mengi ya nchi yetu imekuwa ni janga la Kitaifa. Serikali bado haijachukua hatua za kutosha kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira kwa mfano, barabara zetu nchini zimekuwa dampo kubwa la wasafiri kutupa takataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iandae utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu mazingira kila basi linalochukua abiria kuwe na utaratibu kabla ya basi kuondoka, kondakta awaelimishe abiria kutotupa takataka nje. Kazi hiyo ya kuwaelekeza wamiliki wa mabasi hayo inahitaji fedha kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mita 15 zilizoainishwa na Wizara kwamba ziwe ndiyo mwisho kulima katika

maeneo ya vyanzo vya maji ni kidogo sana katika suala la kuhifadhi vyanzo vya maji. Serikali izitathmini mita hizo kama zinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji wa miti katika Wilaya zetu umekuwa wa wastani na sioni kama Wizara imehamasisha vya kutosha. Pamoja na kwamba inatoa motisha kwa wale waliopanda miti mingi lakini bado upandaji wa miti umekuwa na mwitiko mdogo sana angalia jedwali lote namba moja katika hotuba ukurasa 125-129. Naiomba Serikali kuwa karibu na Halmashauri ili kuona kama kweli kazi hiyo inapewa umuhimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iviwezeshe vikundi mbalimbali vilivyoko Wilayani vinavyojishughulisha na kuhamasisha upandaji wa miti. Serikali iwaangalie kwa ukaribu wakulima wanaohama hama maana nao ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru baadhi ya miradi katika Jimbo langu imefanyika, lakini baadhi haijatekelezwa kabisa. Katika ripoti yako imeandika visima vitatu Kirando vimekamilika, lakini Kirando vilichimbwa visima viwili tu. Kwa hiyo, naomba hicho cha tatu kikamilike katika Kijiji cha Kirando, kama ulivyoeleza pia mradi wa Mwalo Kirando sikuona sehemu yoyote na mwaka jana ulikuwepo, lakini naomba huo mradi ukamilike mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa kuhesabu wavuvi na zana zao hapa katika Wilaya yangu ya Nkasi, nilijulisha kuwa kuna wizi mkubwa ulifanyika na mratibu wake, wizi mkubwa wa mafuta lakini nimejitahidi sana, lakini mpaka sasa afisa huyo na mfanyabiashara aliyemsaidia kuiba yaani aliyempa risiti hewa wala haulizwi. Yaonesha huo ni mtandao wa wizi, maana wote ni wezi tu maana huo wizi wa kuiba pesa za wafadhili watachoka, risiti hewa mradi wa kusaidia miundombinu ya barabara ili wavuvi wafike kwenye masoko mpaka mzabuni alipewa taratibu lakini hakuna hata senti iliyofika Wilayani. Tuliahidiwa shilingi 507,457,250 kwa ajili ya km 29.1 kwa ajili ya barabara za:-

(i) Kipili – Karungu km 8;

(ii) Mwangamilulu- Korogwe km 5; na

(iii) Korogwe- Mpenge-Kachui-Kabwe km16.1 pamoja na daraja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo barabara ni muhimu sana kusaidia wavuvi wanaoishi mwambao mwa ziwa Tanganyika yaani hakuna barabara kabisa wana shida kubwa sana maana wanavua samaki lakini hawana pa kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mwaka huu zipatikane hizo pesa maana ziliahidiwa na mimi kama Mbunge nilipita katika vijiji hivyo kuwaeleza huu mwaka ni ukombozi wao. Sasa nimeonekana mwongo

maana hakuna hata kilomita moja iliyotengenezwa Serikali isitoe ahadi ambazo hazitekelezeki, hala hala mwaka huu naomba sana ahadi hiyo itekelezwe ili nisionekane mwongo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera na Sheria ya Mazingira, kwa sasa sijaona juhudi za dhati za kuhifadhi mazingira hasa kwa namna ambayo vifungashio vya chakula na *plastic* laini. Magari yanayotokea mikoani kwenda Jijini Dar es Salaam, zinabeba kiwango kikubwa cha mifuko. Je, Wizara ina mkakati gani kudhibiti wingi wa taka ngumu zinazoingia Dar es Salaam kila siku.

Je, Serikali inaweza au iko tayari kuagiza Serikali za Wilaya ili zihusike kwa karibu kudhibiti watu wanaolima karibu na vyanzo vya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa na mitaala maalum katika shule zetu kuanzia shule za msingi hadi sekondari ili vijana wetu waanze tangu utoto wao kuelewa umuhimu wa kutunza mazingira katika maisha yao hadi utu uzima wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mbalimbali ya nchi yetu yako karibu na misitu ya asili na kwa namna moja au nyingine wanashiriki katika utunzaji wa misitu au mazingira ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Serikali iandae utaratibu wa kuwapatia huduma za kijamii kama kuchimbiwa visima, visima vya maji, kupatiwa madawati au misaada ya kujengewa

zahanati ambazo zitaendeshwa na Halmashauri za Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ya abiria (mabasi) yanapofika kwenye hoteli na kuwaruhusu abiria wapate chakula, wawape abiria muda wa kutosha ili wapate chakula bila kuwalazimisha kubeba chakula katika vifungashio vigumu na kula chakula ndani ya basi na kisha kutupa taka hizo kupitia madirishani na taka hizo kuzagaa barabarani kila mahali jambo ambalo lina athari nyingi kwa jamii na Taifa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri na kutoa maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kero za Muungano; napenda kutoa ushauri kwamba maagizo yote yaliyotolewa mwaka jana yafanyiwe kazi ili kuepusha vurugu zinazoweza kujitokeza kama vikundi vya Uamsho na kadhalika. Pia Serikali iongeze kasi katika mambo yanayohusu pande zote mbili za Muungano hasa yale ambayo hayapaswi kusubiri Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa wa faida za Muungano na hasara zake endapo kero zilizopo hazitatatuliwa, napenda kuishauri Serikali kwamba uelewa wa Muungano ufafanuliwe sana kwa upande wa Tanganyika na Zanzibar ili wananchi wajue faida na hasara za kuvunjika kwa Muungano. Pia napenda kuishauri Serikali juu ya *Double taxation* kwa upande

wa Zanzibar litatuliwe haraka ili kuepusha tatizo hili, katika mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mazingira, napenda kuishauri Serikali mambo mbalimbali juu ya ofisi hii, kwanza mazao ya misitu kama mbao na mkaa katika Mikoa ya Kigoma hususani Wilaya ya Kibondo; Rukwa, Shinyanga, Kagera na kadhalika. Kumekuwa na ukataji mkaa na kusababisha uharibifu wa Mazingira mfano, katika jedwali (kiambatanisho Na. 1) kwenye hotuba ya Waziri inaonesha Wilaya ya Kibondo ni asilimia 68 ya miti iliyopandwa ndiyo ilipona lakini napenda kutoa taarifa kwamba ukataji wa miti ni mkubwa kuliko upandaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mifugo mingi kuliko malisho na kilimo holela, napenda kuishauri Serikali kuweka utaratibu na kutenga maeneo kwani vurugu za Rufiji zinaweza kutokea maeneo mengine ya nchi kama Kibondo, Kasulu, Biharamulo, Karagwe, Ngara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, usafi wa Mazingira mijini, napenda kuishauri Serikali kuwa na utaratibu mpya wa usafi katika majiji yetu na kuwepo siku ya usafi kila mwezi nchi nzima kama ilivyo Burundi na Rwanda.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu kuboresha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano,

nashauri suala hili lipewe uzito na mazungumzo ya pande mbili yapewe uzito, yaharakishwe na uamuzi ufikiwe mapema iwezekanavyo ili Tume ya Pamoja ya Fedha itoe maamuzi muafaka kwa pande zote kuhusu mapato, uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano, ni muda mrefu mijadala ya pande mbili za Muungano inaendelea ila hadi hii leo basi hoja mbili hazijapatiwa ufumbuzi, hivi itachukua miaka mingapi kupatiwa ufumbuzi? Hebu tuelezwe. Je watendaji kweli wako *serious* katika kuona *solution* inapatikana? Katika maeneo mbalimbali baadhi ya watendaji kwa makusudi wanasaidia kuweka vikwazo visivyo na sababu, kukataliwa kulipwa msindikizaji wangu katika tiba yangu ya nje ya nchi, wakati wakijua mimi nilikuwa ni Naibu Waziri wa Muungano na kutakiwa kurejesha fedha alizopewa msindikizaji wangu wa SMT. Hii si haki kwani viongozi wa SMT wote waliougua na kupelekwa nje wasindikizaji wao wanalipwa na SMT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ndogondogo na usumbufu usiofaa kwa wafanyabiashara toka Zanzibar wanapopita Bandari za Tanzania bara vema ziondoshwe. Mapato na mgawanyo wa 4.5% (gawio) la misaada ya wahisani na mikopo ya kibajeti kwa SMZ ni ndogo sana hasa kutokana na hali halisi ya uchumi na changamoto zilizoko kwa sasa. Ni vyema vikao vya pamoja vya kuratibu na kubuni mbinu mpya za kuongeza mapato vifanyike ili pande zote zifaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ufuatiliwe *(evaluation)* ili kuona iwapo uliwafikia kweli walengwa, aidha miradi ya *MACEMP*, nayo tufanye *evaluation* kuona ni kwa kiasi gani miradi hii iliwasaidia wanyonge kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya magazeti yaache kuisemea SMZ kuwa inaunga mkono kikundi cha Uamsho, hayo waliyapata wapi? Je, wanaweza kututhibitishia au wana uhakika na wanayoyaandika? Wasichochee ugomvi hauna tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, uchafu unaotokana na utupaji taka holela na bila Manispaa kukemea au kuchukua hatua kumeleta athari kubwa katika miji mbalimbali. Mitaro ya maji kuziba baada ya mifuniko ya chuma kuibiwa na takataka na machupa matupu kuziba *drainage system*. Aidha, wenye mabasi wengi kudharau maagizo ya kuweka ndoo na mifuko mikubwa ya kuweka takataka mbalimbali zinazotokana na vyakula wanavyokula abiria. Hakuna sheria zozote au ni *laws* ambazo zinaweza kuzuia suala hili. Uuzaji vyakula madafu kando kando ya fukwe zetu na bila kuwekewa utaratibu mzuri wa usafi baada ya kuuza bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko katika fukwe zetu sasa unatishia sana nyumba zilizo karibu na fukwe hizo, *it is high time* sasa watu washirikishwe katika kutafuta mbinu za haraka za udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala sugu la magugu maji bado halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa masikitiko yangu na masikitiko ya Wazanzibar wote kutokana na kauli za dharau na kebehi kwa Wazanzibar zinazoendelea kutolewa hapa Bungeni na baadhi ya Wabunge lakini pia hata baadhi ya Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba ukiacha Wabunge wa kawaida lakini hata Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Utawala Bora pia naye kwa masikitiko makubwa jana alipokuwa akichangia hoja ya Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma akifanya majumuisho katika kujibu hoja za Wabunge mbalimbali alisema na akitoa mifano ya utawala bora kwamba isingekuwapo Muungano, pasingekuwepo Ubunge toka Pemba hapa, lakini pia Wapemba wako mpaka Mtwara na kwamba hii shauri ya utawala bora chini ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke pia kwamba ndani ya Muungano pana Wachina, Wahindi, Wazungu, Wajerumani, Wamsumbiji, Wasomali na kadhalika. Wote hao wanaishi wanafanya biashara na vibarua ni vijana wetu wa Kitanzania na wala hao hatukuungana, lakini pia Wamakonde wako Zanzibar na wanaishi bila bughudha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi si hoja za kusherehesha au kuwashawishi Watanzania waamini kwamba Tanzania pana utawala bora na kwamba tunaishi chini ya misingi ya utawala bora kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusherehesha na kuonesha vigezo vya utawala bora, nilitegemea Mheshimiwa Mkuchika angesema kwamba, mgawanyo wa mapato yatokanayo na Benki Kuu *(BOT) JFC*. Sasa jambo hili limekwisha kwa kuwa ni la muda mrefu sana. Chini ya Utawala bora, Zanzibar itaachiwa iwe huru kiuchumi kwa kuwa ni nchi chini ya Utawala bora, nafasi za ajira katika Muungano ziwe sawa, Tume ya Uchaguzi iwe huru tofauti na ilivyo sasa, chini ya utawala bora. Nafasi za kuiwakilisha Tanzania nje ya nchi Mabalozi, ziwe sawa, angesema pia kwamba katika kuimarisha utawala bora Tanzania pia:-

(i) Nafasi ya Rais wa Zanzibar ndiye atakayekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;

(ii) Angesema pia katika suala la utawala bora, rasilimali (madini) na kadhalika zitasimamiwa vema ili ziwafaidishe Watanzania kuliko hivi sasa ambapo wageni (wawekezaji) ndiyo wanaofaidika na kufaidisha nchi zao; na

(iii) Angesema kwamba kwa kuwa kwa muda mrefu sasa vyombo vya ulinzi vimekuwa vikiongozwa na watu toka bara kwamba sasa ni zamu ya Wazanzibar na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Muungano huu ndiyo uliomfanya Mbunge toka Pemba kuwepo hapa na kwamba hii ni moja ya utawala bora, ieleweke pia kwamba hata Mheshimiwa Mkuchika yupo hapa kwa sababu hiyo? Lakini pia kama si Muungano basi naye

angekuwa hapa kwa Bunge la Tanganyika na sio la Muungano hali ambayo kwa Zanzibar tayari tunalo Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Wabunge hutumia udogo wa eneo la Zanzibar na uchache wa Wazanzibari kama hoja ya kuidharau na kuikebehi Zanzibar. Naomba ieleweke kwamba Muungano huu haukuzingatia na wala haikua kigezo suala la ukubwa wa ardhi na wingi wa watu wa kila nchi katika nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere na Mzee Karume walielewa wazi kwamba kwa wakati ule Zanzibar ilikuwa na watu wasiozidi 400,000 lakini wakaona ni vema waunganishe nchi hizi na katika misingi ya kuheshimiana na kugawana haki sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mbunge atokaye bara bila aibu anathubutu kusimama na kuifananisha Zanzibar na Jimbo fulani la bara kwa vigezo vya eneo na watu waliomo, hii ni dharau kwa Zanzibar na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya nchi ya Zanzibar, watu walipata uhuru baada ya kumwaga damu, lakini Tanganyika, uhuru wao ni wa kalamu hivyo si vema kudharauliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa

mchango wangu katika hotuba iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Muungano. Kutoa elimu kwa umma, ukurasa wa 15 wa hotuba yake kipengele a,b,c. Ofisi iliandaa na kusoma nakala 8,000 za jarida la Muungano wetu, nakala 9,000 za vipeperushi na nakala 2,000 za kitabu cha miaka 50 ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania walio wengi hasa vijijini hawana utamaduni wa kusoma vijarida na vipeperushi napendekeza, elimu ya masuala ya Muungano yapatiwe kipaumbele kwa kutengewa kiasi cha fedha za kutosha hivyo kutumia njia za *TV* na *Radio*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha sh. 24,000,000 zilizoombwa kwa ajili ya elimu ya masuala ya Muungano ni kiwango kidogo sana na hakiwezi kutosha kutoa elimu hata kwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika utekelezaji wa masuala ya Muungano changamoto kubwa iliyojitokeza ni pamoja na uelewa mdogo wa masuala ya Muungano na utekelezaji wake hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa uundwaji wa Katiba mpya. Napendekeza kama nilivyoandika hapo juu kwamba kizazi cha leo kipatiwe elimu ya kutosha juu ya faida za Muungano wetu tulikotoka, hapa tulipo na tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanapenda muziki na michezo ya kuigiza, elimu ya kutosha itolewe kupitia muziki na michezo ya kuigiza kupitia televisheni na redio. Hivyo kama nilivyosema

hapo awali fedha iliyotengwa ni kidogo na haitoshi hivyo inastahili kuongezwa ili kizazi cha leo kipate elimu na hivyo kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa 27, anasema kwamba, baadhi ya Halmashauri hapa nchini tayari zimeandaa Sheria Ndogo na zimeanza kutumika kwa mfano, Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza na Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, wale wote waliobanika kufanya uchafuzi wa mazingira katika Halmashauri hizo wamechukuliwa hatua gani za kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi unatekelezwaje hapa nchini? Je, kuna taka zozote za sumu zimewahi kukamatwa zikiwa katika usafirishaji hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ya wafugaji na wananchi kwa ujumla wawekewe programu ya elimu ya matumizi ya *biogas* kwa kutumia kinyesi cha wanyama na binadamu kama nishati mbadala hivyo kupunguza kasi ya ukataji miti ya utengenezaji mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupanda miti katika kila maeneo yaliyotengwa ni la kila mwaka, naomba nipewe takwimu za fedha

ambazo zimetumika kukamilisha zoezi hilo? Ni miti mingapi imeshapandwa tangu zoezi hili kuanza na ni mikoa ipi inaongoza? Ili kuboresha zoezi la upandaji miti, je, ni semina ngapi ziliendeshwa kwa wanaokata miti kwa kutengeneza mkaa kama zao la biashara ili waepukane na kuacha nchi kwenye jangwa? Ni mikoa mingapi na ni wangapi walipata mafunzo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kumekuwa na fungu la kupanda miti, wakata mkaa wamehusikaje na fungu hilo ili wanapokata miti kwa ajili ya mkaa, pia wajiajiri kwa kupanda miti tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zinakwamia wapi za nishati mbadala kwa ajili ya kupikia ili kuokoa miti? Je, ni tuzo ngapi zimetolewa kwa wahifadhi na watunza mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *TMAA* inaingilia kazi za *NEMC?* Kwa nini wataalam walioko *TMAA* wasirudishwa *NEMC* ili wakawe na kitengo cha kushughulika masuala ambayo wanayafanya *TMAA?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri na wasaidizi wake wote kwa bajeti nzuri ila ni ndogo, majukumu ni mengi kuliko fedha zilizotengewa. Tunashauri mwaka kesho bajeti hii iongezwe, hii ni finyu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa mipango mizuri ya upandaji miti ili kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji, *well done.* Pongezi kwa ukusanyaji wa mapato wa kiwango cha juu. Elimu kwa wananchi kwa njia mbalimbali juhudi ziongezwe hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa jengo jipya la Ofisi ya Makamu wa Rais lililo Tunguu, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba hii inakidhi, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Kuna kero nyingi za mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni uharibu mkubwa wa Mazingira Kilombero. Mifugo ni mingi mno kiasi ambacho uharibu wa Mazingira Kilombero ni mkubwa, naona wa kutisha. Waziri Mkuu aliamuru mifugo iondoshwe Kilombero kwa sababu ni Wilaya ya ghala la chakula. Ni nini kinazuia amri hii haitekelezwi? Wafugaji waelimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugomvi kati ya wafugaji na wakulima, wananchi wanapigana hadi kuuana. Jambo hilo la mifugo lilikuwa kero sasa limekuwa janga, tunaomba Wizara walipe kipaumbele suala la mifugo Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu mkubwa wa mashamba na mazingira na wanyamapori kutoka hifadhi ya jamii Udzungwa, Mang'ula, wanyama pori kama tembo wanaharibu mashamba kwa sana tu, tembo hushambulia hata mashamba 10-20 bado fidia *TANAPA*, hawalipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chatu ni waharibifu wa mifugo, chatu huingia kijijini na kumeza mifugo kama mbuzi kuku na kadhalika. Wananchi hawaruhusiwi kuua maana ni wanyama wa hifadhi, hivyo chatu na tembo wao wana haki kuliko wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati mbadala kwa wanawake wa kilombero, elimu itolewe kwa akina mama wa Kilombero ili wapate nishati ya kupikia chakula badala ya kuni au mkaa. *TANAPA* wamepiga marufuku kuokota kuni kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba msaada.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa shukurani njema kwa Mwenyezi Mungu kuniwezesha mimi na Wabunge wenzangu kuwa salama katika Bunge hili la bajeti. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mazingira nachukua fursa hii kupongeza Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa uboreshaji wa maji safi na salama katika Jimbo langu la Nungwi. Kwa kuchimba kisima katika Kijiji cha Kilimani Tazari ambacho kitasaidia sana wananchi wa Nungwi na kuondokana na tatizo sugu na la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fukwe za bahari katika Mji wa Nungwi, Kendwa, Fukuchani zimekuwa katika mazingira magumu, kwa sababu Bahari imekuwa ikipanda juu kwa nguvu na kuathiri mazingira katika mji wa Nungwi, juhudi zimechukuliwa kujenga ukuta kuzuia

maji yasipande lakini juhudi hii haijasaidia kwa sababu ukuta umevunjwa na Maji ya Bahari yenye nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri anayehusika alione hili katika Mji wa Nungwi, juhudi za makusudi zichukuliwe kudhibiti hali hii ya uharibifu wa Mazingira, naomba Waziri utakaposimama kujibu hoja za Wabunge toa kauli namna gani utasaidia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia Muungano. Nadhani Serikali ya Muungano haiko tayari kuimarisha Muungano wenyewe, kwa sababu kero za Muungano zinajulikana na zina muda mrefu lakini hazipatiwi ufumbuzi. Tukiangalia hoja kumi na tatu za Tume ya Shelukindo tangu 1996 hadi leo hazijapatiwa ufumbuzi, kama sikosei ni miaka kumi na sita, kama ni sahihi miaka kumi na sita ni miaka mingi sana kwa matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari masikitiko yao makubwa ni kero ambazo zinagusa uchumi wa Zanzibar halafu zikabaki bila ufumbuzi mfano, ushiriki wa Zanzibar na taasisi za nje, ajira katika taasisi za Muungano, mgawanyo wa mapato yatokanayo na Benki Kuu *(BOT)*, hisa za Zanzibar zilizokuwa Bodi ya Afrika ya Mashariki, kodi nyinginezo, *Payee*, *Withholding Tax* (ZUIO), mafuta ya gesi, usajili wa vyombo vya moto na wafanyabiashara kulipa mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo matatizo ya Muungano wetu upande mmoja unadhoofika kiuchumi, wala si hoja ya msingi kwamba Wazanzibar wana fursa kuishi popote Tanzania Bara na kufanya

biashara, ni sawa, lakini hujaondoa tatizo kwa hili isipokuwa kujenga hoja za ubaguzi. Kwa sababu Watanzania wapo nchi mbalimbali duniani wanaishi na kufanya biashara wala hatukuungana. Vilevile hapa Tanzania wapo watu wa nchi mbalimbali wanaishi na kufanya biashara za kutembeza mikononi na hatukuungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoe matatizo ya Muungano ili uwe madhubuti ubaguzi utaliangamiza Taifa. Mwisho naomba Tume ya kuratibu Katiba mpya iwe huru na ifanye haki kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Muungano udumu na kero zipate ufumbuzi.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwanza nauelekeza kwenye suala zima la Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964. Muungano wetu ni wa mafanikio na ni mfano au ni kama mwamvuli wa usalama ambao unatufunika vema katika kulinda usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kusema kwamba Muungano wetu umekuwa ni wa mafanikio makubwa. Kutokana na mafanikio mengi ya Muungano wetu, kumekuwa na ishara mbalimbali za wale ambao hawaitakii mema nchi hii kwa kuleta chokochoko mbalimbali juu ya Muungano huu. Naishauri Serikali

kuwa makini na watu hao na kuzima dhamira mbaya za watu hao juu ya Muungano. Ikiwa duniani watu wanatafuta njia za kuungana pamoja, iweje leo watokee watu wavunje dhamira hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, penye mafaniko hapakosi matatizo, ni kweli Muungano wetu umekabiliwa na changamoto nyingi kwa maneno mengine ni kero za Muungano. Pamoja na Serikali kuziona na kuchukua hatua mbalimbali kwa baadhi ya kero bado kuna malalamiko mengi hasa kwa upande wa pili wa Muungano. Naishauri Serikali bila kuchukua muda mrefu ishughulikie na kero zilizobaki kwa kina kabisa ili kumaliza malalamiko juu ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za msingi ni kutatuliwa kero za Muungano mfano, ushiriki wa Zanzibar na taasisi za nje, ajira katika taasisi za Muungano, mgawanyo wa mapato yatokanayo na Benki Kuu *(BOT)*, hisa za Zanzibar zilizokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, wafanyabiashara kulipa kodi mara mbili na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuzitatua kero hizi kwa haraka sana ili kuepusha malalamiko ya upande wa pili na kufuta kabisa maneno ya wale wanaoutazama kwa jicho la husuda Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vema kwa baadhi ya viongozi kusema kwamba Muungano ukivunjika Wazanzibar watarudi kwao, kwani Wazanzibar walioko

Tanzania Bara ni sawa na Watanzania wengine wanaishi na kulipa kodi za nchi kisheria kama watu wengine. Siombi na wala sishabikii hata kidogo kuvunjika kwa Muungano wetu, lakini najiuliza hawa raia wa kigeni waliopo Tanzania na wanafanya biashara hata za Machinga mfano Wachina kwani hawa nchi zao tumeungana? Au Watanzania wanaoishi nchi za nje mfano, Uingereza, Marekani Canada na nyingine, je, nchi hizi zina Muungano na Tanzania? Hivyo mtu kuishi katika nchi nyingine ni haki yake ya kibinadamu ili mradi havunji sheria za nchi ile na wala si lazima kwamba nchi yake iwe imeungana na nchi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mazingira, Mazingira ni suala mtambuka na walio wengi wanaona Mazingira ni usafi wa mzunguko wa nyumba tu pale anapoishi, lakini kiujumla wake mazingira ni kila kitu kinachomhusu binadamu mfano, maji, Bahari Misitu, Ardhi, Mito na Maziwa na vyote vilivyomzunguka binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira ni suala zima la ukataji wa miti katika njia mbalimbali mfano kuchoma mkaa kukata kuni kupasua mbao na kwa njia mbalimbali za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi ni changamoto kubwa kwa Serikali kwani zimegusa maslahi ya watu kimaisha, watu wanafanya hayo kwa kukidhi haja zao za kimaisha na watoto wao. Hii ni kwa sababu watu hawana shughuli mbadala za kufanya ili

kukidhi haja zao za kimaisha. Hatuwezi kuwalaumu kwani wanayofanya ni kuokoa maisha yao na walio chini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kujitahidi kuleta mambo ya nishati mbadala ili kunusuru misitu. Pia Serikali kutilia maanani upatikanaji wa ajira ili watu wanaotegemea kuhujumu miti kukidhi maisha yao wapate ajira ili kuacha kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha Muungano wetu, undugu baina yetu unaongezeka na kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, maoni ya Kamati mbalimbali zilizoundwa ni vyema yakafanyiwa kazi ili kuondoa dhana ya kutoaminiana baina ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, nashauri Wizara ijikite kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi katika kushiriki kuhifadhi kikamilifu na kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi waishio kando kando ya Bahari ya Hindi hasa Vijiji vya Mchinga, Mvuleni, Ruvu na Kijiweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidumu Chama cha Mapinduzi, *viva* CCM *viva*.

**MHE. PROF ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga

mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, amefafanua hoja yake vizuri kwa ukweli na uwazi. Amekiri historia ya Muungano imekuwa na changamoto zilizoibuka kulingana na nyakati na kufanyiwa kazi ili kuziboresha. Hili ni jambo la kawaida katika Muungano wowote ule kwa mfano wanandoa wana historia ya *honeymoon*, halafu kulea watoto na changamoto zake ili ndoa idumu inabidi wanandoa wajadiliane, warekebishe hata wakati mwingine kuweka ahadi upya au mpya ili kulinda ndoa yake. Hivyo hivyo basi, changamoto za nyakati hizi si tishio kwa Muungano kwani kuna mwanya au *opportunity* ya kurekebisha na kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupinga Muungano ni kukosa maono, kutojua cha kufanya na kudai tuangalie yaliyojili kabla ya Muungano ni kupotea kwenye historia. Waasisi wa Muungano waliofanya kazi nzuri walitengeneza historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalotakiwa sasa ni kuendeleza si kuvunja. Kwa mantiki hiyo wakati huu wa kuandika upya Katiba ya Muungano wa Tanzania tuwe na ujasiri na ubunifu, kufanyia kazi yale maeneo yenye utata. Tuondoe kero lakini tutambue tutajidanganya kudhani tutakaa tuwe na Muungano usiokuwa na *Limitations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupata faida tu ambayo haina gharama. Muungano huwa na faida nyingi na kubwa hizi nazo tusizisahau na kuangalia

gharama (*costs)* tu zinazoitwa kero kwani tutakuwa tunapotosha ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitoe nafasi kwa majambazi na wahuni wasiotutakia mema sisi na vizazi vijavyo, kuingiza hoja za udini katika Muungano wetu. Kwa kikundi cha Uamisho kufanya hamasa zenye mlengo wa dini ni hatari ambayo haiwezi kufumbiwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochoma Makanisa Zanzibar sharti wasakwe na kuadhibiwa vikali ili tulinde umoja wetu na Muungano. Makanisa au Misikiti vimekuwepo kabla ya Muungano na vitaendelea kuwepo hata Muungano ukivunjika. Hii ni ishara tosha kuwa tuwe macho na wahuni, *criminasl* tusiwape nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano ni lulu tuulinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ukataji miti na uchomaji moto vinavyoendelea katika Mlima Kilimanjaro katika hifadhi yake ni ishara tosha inayoonesha hatari kubwa ya uharibifu wa mazingira na hujuma za makusudi kwa Mlima Kilimanjaro, sanjari na hayo ujangili wa uvunaji miti katika hifadhi hiyo ya msitu inatoa ishara mbaya kwa uhai na usalama wa mlima huu pamoja na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko kubwa la minara ya Kampuni za Simu vijijini ambalo upatikanaji wa nishatri ya umeme umekosekana na kulazimika kwa makampuni hayo kutumia majenereta kwa uzalishaji umeme. Hili ni moja kati ya yale yanayosababisha mabadiliko ya tabia nchi kutokana na umwagiliaji wa vilainishi *(oil)* ovyo na utoaji holela moshi kutoka katika majenereta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumiaji na usafirishaji wa kemikali kama vile zebaki zitumikazo katika migodi ya uchimbaji madini kwa kampuni kubwa na wachimbaji wadogo mbali na kuhatarisha afya ya wanadamu na wanyama pia ni moja ya yale yanayochukua nafasi kubwa katika uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maoni yangu ni kwamba:

- Serikali iuangalie Mlima Kilimanjaro na hifadhi yake kwa ukaribu zaidi na ikiwezekana kuunda kikosi kazi cha udhibiti wa mazingira *(especial)* kwa ajili ya Mlima huo.

- Serikali ieleze ni namna gani makampuni ya simu ambayo hujenga minara inavyochangia katika Mfuko wa kuhifadhi Mazingira nchini.

- Serikali ifanye utafiti wa mabaki ya kemikali zilizotumika katika migodi nchini ili itafute utaratibu wa kuyahifadhi au kuyaangamiza. Ni vema Serikali kupitia Wizara husika kutueleza mpango mkakati walionao katika suala hili.

- Ili kuwaondolea adha wananchi na kutaka kutambua wale wanaohujumu miundo yetu kwa kungoa vyuma barabarani, ni vema Wizara ikayataja kwa majina makampuni ambayo yamepewa leseni ya ukusanyaji chuma chakavu. Hii itasaidia kuwatambua matapeli wote ambao hufanya biashara hii.

- Kwa kuwa baadhi ya wananchi wameamua kukusanya chupa za plastiki ambazo zimeshatumika (za maji) na kuuza kwa makampuni yenye viwanda vya ku-*cycle*, je, Wizara kupitia NEMC ina mpango gani mkakati wa kuwasaidia vijana hao ambao mbali ya kujipatia ajira, lakini wanahifadhi mazingira?

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye ukarimu, kunijalia kuwepo katika Bunge lako Tukufu nami nikiwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Bunge lako naomba na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti iliyopo mezani katika baadhi ya vipengele vilivyomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze mchango huu kwa kulielewesha Bunge hili kuhusu wajibu wetu sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano tukiwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Bunge lako tukufu tuna wajibu wa kuisimamia Serikali pamoja na kuishauri katika mambo yote yanayo husu uchumi, siasa na kijama kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla nyanja tatu hizi nilizozitaja pamoja na majukumu mengine mambo hayo matatu ndiyo yamekusanya wajibu wetu sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri. Pili, sasa nataka nianze mchango wangu katika suala linalohusu kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoukabili Muungano zimekuwa gumzo la muda mrefu kwa sababu nataka nilieleze Bunge lako kwamba tangu mwaka 1995 lianze Bunge la mfumo wa Vyama Vingi hapa nchini, changamoto hizi zinajadiliwa na Wabunge hadi leo. Sasa ni Bunge la nne katika mfumo wa Vyama Vingi inaonekana suala limekuwa zito bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Hii ni dalili tosha kwamba Serikali ya CCM kupitia ilani yake haina nia ya kuondoa tatizo hili lililotopea na kuota mizizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizitaje baadhi ya kero hizi, ni kama vile, mgawanyiko wa mapato; inasikitisha kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano imeshindwa kupeleka mapendekezo yake kwenye Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Zanzibar, Serikali imeshatoa mapendekezo yake kuhusu suala la mgawanyo wa mapato katika Tume. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ni ile wafanyabishara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na suala hili limekwishaulizwa Bungeni mara chungu

nzima. Majibu ya Serikali hueleza watachukua hatua za haraka kuliondoa tatizo, hadi leo bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ni ile ya ufunguaji wa akaunti ya pamoja hadi sasa bado. Hii ni dhuluma na jambo hili sasa lazima lieleweke. Katika mchango wangu huu wa maandishi nitamtaka Waziri husika alitolee ahadi Bunge lako. Wakati wa majumuisho katika kipindi kifupi ni lini ndani ya bajeti hii masuala haya yatapitiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii tena kuelewesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano mbele ya Bunge lako kwamba Zanzibar ni nchi, haikuungana na Tanganyika ya Nyerere kwa dhiki, la hasha! Iliungana kwa nia njema kupitia faida za umoja na sio iwe ni kosa kwa Zanzibar kuamua kuungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupitia chombo chako hiki cha sheria yaani Bunge, hoja za Muungano zinazotolewa humu Bungeni kama ni kero katika Muungano, Serikali ithamini na Zanzibar imechoshwa na dharau na kejeli, lolote ambalo litakuja kutokea Wazanzibar watakuwa na haki ya kuishtaki Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu makadirio ya matumizi

ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pili, nampongeza kwa utendaji makini wa majukumu yake na uvumilivu wa hali ya juu alionao. Nampongeza pia Mheshimiwa Daktari Terezya Luoga Huviza, Waziri kwa utendaji mzuri na ameonesha ni jinsi gani yupo makini maana ni kipindi chote cha utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watu ambao kwa makusudi wanakosoa Muungano na wanafikia hatua kuhatarisha amani ya nchi kwa kushiriki kuchoma Makanisa, Misikiti na hata kuharibu mali za watu ili kufikisha ujumbe wao kuwa Muungano una matatizo. Serikali ihakikishe inachukua hatua za haraka kuhakikisha tatizo hili linapata ufumbuzi pamoja na wahusika kuchukuliwa hatua stahiki na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea kero na matatizo ya Muungano pamoja na yale ambayo yamekuwa yakiyumbisha utendaji wa Serikali na taasisi nyinginezo za umma. Miongoni mwa hayo ni umeme, umefika wakati sasa kuwepo na utaratibu unaowezesha Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO* kufua umeme yenyewe kwa kuweka kituo Zanzibar au hata upande wa bara hasa ikizingatiwa sasa fursa za gesi asilia na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafuta ya gesi asilia pamoja na ufuatiliaji mzuri wa viongozi wa Wizara hizi, naishauri Serikali ihimize mchakato wa kutengeneza kanuni ama sheria za mgawanyo wa mapato haraka na pia ielezwe bayana ni sababu zipi ambazo zinapelekea Zanzibar isijihusishe na biashara ya mafuta na gesi asilia bila kuingizwa kwenye Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yanayohusu mahusiano ya kibiashara, ikumbukwe Zanzibar ni kisiwa ambacho bila ya kufanya biashara kwa uhuru wake hakuna njia nyingine za kuingiza kipato cha nchi hasa ukizingatia ukuaji wa idadi ya watu na mahitaji. Fursa za kilimo ni chache kutokana na ukubwa wa eneo na hakuna vyanzo vinginevyo vya asilia kama madini, misitu na milima. Hakuna tija itakayopatikana kwa kuingilia uhuru wa mahusiano ya kibiashara baina ya Zanzibar na nchi nyingine za kigeni. Pale ambapo panaonekana ni tatizo basi ziainishwe bayana athari zake, si kwa kusema hapana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Muungano sasa uangaliwe ili kuwe na maridhiano kwa kuwa tumeingia katika mchakato wa Katiba mpya, ni kheri yale ambayo yamekuwa yakitiliwa mashaka yakaondolewa ili kuufanya Muungano wetu uwe imara na bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, eneo hili ni muhimu sana katika maisha na ustawi wa viumbe vyote. Matatizo kadhaa yamekuwa yakiainishwa ili kuyapatia ufumbuzi lakini naona jitihada hizi hazijakidhi

haja. Tatizo la kilimo cha kuhama hama ni kubwa sana hasa katika Mikoa ya Kusini mwa nchi ikiwemo Kilwa Kaskazini. Wananchi hawajapata elimu ya kutosha kuhusiana na umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Miradi mingi iliyoorodheshwa *MACEMP, TCMP, WIOMPH* na ile ya *WWF* haimfikii moja kwa moja mwananchi kwa kutoshirikishwa badala yake kuwanufanisha wachache hasa watumishi wa Idara za Misitu na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba Waziri, pamoja na kunukuu Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kuna mambo kumi yameainishwa ili kukabiliana na tatizo la uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Naishauri Serikali iongeze kipengele kimoja kuwa miti, vyanzo vya maji, mito, maziwa, mabonde pamoja na viasilia vyote ni sehemu ya mali za nchi. Watumishi kuanzia ngazi ya Kijiji pamoja na viongozi wengine wanakabidhiwa kama wanavyokabidhiwa dhamana nyingine. Pale ambapo wanahama hama kumaliza utumishi wao basi wanakabidhi kama walivyokabidhiwa na ikiwa kuna mapungufu, wachukuliwe hatua kali za kinidhamu. Hii ni kutokana na watendaji wengi vijijini kushiriki moja kwa moja katika kuhujumu maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uvuvi haramu wa kutumia mabomu limekuwa kubwa sana, Serikali ishirikiane na Jeshi la Polisi na JWTZ kukomesha matendo haya maovu hasa eneo la Somanga, Kivinje na Masoko. Imebainika kuwa wengi wa wanaofanya kazi hizi si Watanzania bali ni wageni kutoka Kenya na Msumbiji ambao wanakuja kwenye Pwani zetu na kufanya uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupokelewa maoni yangu na naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya, mahali penye Muungano kwa kitu au jambo lolote ni wazi panakuwa na msuguano na panastahili uvumilivu na ustahimilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa Muungano uliozaa Taifa la Tanzania bado ni muhimu kwetu na kwa vizazi vyetu. Tunafahamu kuwa changamoto za Muungano huu ni kubwa, lakini ni mambo ambayo yako ndani ya uwezo wetu. Kadri Tanzania inavyoendelea ndiyo hivyo hivyo Muungano na mambo yahusuyo Muungano yanavyokuwa na kubadilika, cha msingi ni wajibu wa sisi tubadilike na watu ndani ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la rasilimali ni muhimu kuwa nje ya Muungano, naliona kama mwiba ambao tukiuendekeza utaleta matatizo makubwa. Hii itaruhusu Mataifa makubwa kupata mwanya wa kutuunga ili waweze kuzifaidi rasilimali hizi, si wote wanaoitakia Tanzania mema. Migogoro mikubwa duniani hivi sasa inatokana na rasilimali na hususani rasilimali ya nishati. Ni wazi kama tutakuwa tumefarakana au kutengana katika hili basi itakuwa rahisi kuvurugwa na wakubwa kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa mazingira ya pwani bado ni hafifu sana. Fukwe ni sehemu ambazo kila Mtanzania ana haki ya kufika kuona na hata kupata burudani, leo hii fukwe zetu kwa asilimia

kubwa zinamilikiwa na watu binafsi na hazitoi fursa kwa wananchi wote. Yale maeneo yaliyobaki hayana *plan* nzuri ya ufukweni kama njia za miguu, matunzo ya bustani za ufukweni, huduma kwa wanaopumzika na hata ulinzi na uhifadhi wa fukwe zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunasafiri na tunaona wazi fukwe za wenzetu katika nchi mbalimbali jinsi zilivyochorwa na kujengwa na ambavyo kweli zinaleta burudani na pia kipato kwa mamlaka husika. Kuna nini hapa kwetu wataalam wetu hawaoni wala kupanga mipango kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kupitia Serikali za Miji, Manispaa na Halmashauri za miji sasa kuwa na mpango kabambe wa kuboresha fukwe zote za Bahari na Maziwa na hata Mito mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mazingira llitaweza tu kuona na kushauri mambo ya kuzingatia lakini mwenye jukumu la kupanga, kuchora na kutekeleza mipango ni Serikali zetu za Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji. Tutoe msukumo wa makusudi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mambo yanayoleta shida na kero katika Muungano ni kutekeleza kutatua kero za Muungano taratibu. Napendekeza tatizo la mgao wa

fedha za Mfuko wa Pamoja urekebishwe na asilimia zirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chenji ya Rada, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kuwa fedha za manunuzi zimetokea mawasiliano, hili jambo litaleta changamoto na kuongeza chuki na kero za Muungano sababu inafahamika kuwa usalama wa Anga, Jeshi, *Metrology* yote hayo ni mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Double Taxation* pia ni jambo ambalo linasumbua na inafaa lifanyiwe marekebisho ili kero zipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mikataba na sheria zitakazosimamia mambo ya Muungano, kuna matatizo yanajitokeza ya kupitisha sheria ndani ya Bunge bila ya kupeleka Baraza la Wawakilishi. Lakini pia hata zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki nazo zijadiliwe ndani na Mabunge yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye hotuba hii. Naomba niwapongeze Mawaziri na Naibu pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na iliyowasilishwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utangulizi huo, naomba sasa nichangie katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni Muungano, Tanzania madhubuti ni ya Muungano imara na sio vinginevyo. Pamoja na ukweli huu katika siku za hivi karibuni kumeongezeka matishio ya kuudhofisha kwa lengo la kuuvunja. Naomba nitoe rai kwamba ipo haja ya kuwa makini zaidi kuhusu Muungano na njia pekee ya kunusuru Muungano na matishio ya kuuvunja ni kutatua matatizo au kero zilizopo. Katika uzoefu wangu wa kufanya kazi kwenye Serikali zote mbili nimegundua kwamba baadhi ya watendaji na hata wanasiasa hawana utashi na mara nyingine hufanya maamuzi ambayo hayasaidii kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio la hivi karibuni ni hili la Uamsho, nashauri, jitihada zote zifanywe ili kudhibiti taasisi hii ambayo malengo yake sio ya kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu mazingira, tabia nchi ni tatizo kubwa sana ambalo linatishia mustakabali wa maisha ya wananchi wa Tanzania na mambo haya ya kuharibu mazingira yakiachwa yaendelee nina hakika malengo yetu ya maisha bora hayawezi kupatikana. Ni lazima tusaidie kuhifadhi ili iwe nyenzo ya maendeleo na kwa hiyo nashauri mambo yafuatayo yafanywe:-

(i) Gesi ambayo imegunduliwa isambazwe haraka ili iweze kutumika hasa kama nishati hususan katika shughuli za kupikia.

(ii) Matumizi ya nishati mbadala kama *solar* na *biogas* ili kupunguza uharibifu wa mazingira yakomeshwe.

(iii) Elimu ya kutunza mazingira isambazwe kwa wananchi ili shughuli zao za kila siku zisiondoe uwezo wa jamii ya baadaye kujikimu.

(iv) Mpango wa *carbon credit* upewe nafasi ili watakaojihusisha na upandaji na ukuzaji wa miti wafidiwe kwa jitihada zao. Sheria ya Uhifadhi wa Maliasili za Mipakani *(Cross Border Resources)* iliyopitishwa na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki isikubaliwe na Tanzania. Sheria hii inapora madaraka ya Tanzania kusimamia rasilimali zake. Sheria hii ikiachiwa kufanya kazi ni dhahiri kwamba maliasili zilizopo hasa mipakani zitatoweka bila kutuarifu.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu uharibifu wa mazingira katika Jimbo langu la Mpwapwa. Miaka ya nyuma kulikuwepo na mwamko nzuri wa utunzaji wa mazingira kwa kupitia utaratibu mzima wa *HADO* katika mkoa mzima likiwemo na Jimbo la Kondoa. Miti mingi ilipandwa katika Jimbo la Mpwapwa ikizunguka pande zote za mto mkubwa unaopita katikati ya Mji wa Mpwapwa. Miti hii kwa kiasi kikubwa sana imesaidia sana kuzuia kupanuka kwa mto huu ambao hivi sasa umeendelea kupanuka na kusambaza maji kuelekea

kwenye makazi ya watu na kutishia au kuleta uharibifu wa makazi ya watu kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti yote iliyopandwa ili kuokoa na kulinda ardhi na mmomonyoko wa udongo katika kingo za Mto imetoweka kwa wingi. Naleta kilio hiki ili Jimbo la Mpwapwa lifikiriwe kama ilivyokuwa zamani enzi ya *HADO* kupewa semina, kutembelewa na viongozi wa mazingira wa ngazi mbalimbali na kujionea wenyewe uharibifu wa mazingira kandokando ya Mto huu unaopita katikati ya Mji wa Mpwapwa na kuleta hofu kwa wananchi wa Mji wa Mpwapwa kwa kubomolewa makazi yao ya kuishi. Hali hii inajitokeza sana wakati wa msimu wa mvua. Katika msimu wa mvua wa mwaka 2011/2012 yametokea maafa ya mafuriko makubwa ambayo yameongeza hofu zaidi kwa makazi na nyumba za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuomba semina kuhusu utunzaji mazingira kwa viongozi na wananchi wa Jimbo la Mpwapwa kutembelewa na viongozi, ningeomba kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kupatiwa msaada wa ufumbuzi wa tatizo la uharibifu wa mazingira katika mto unaopita katikati ya Mji wa Mpwapwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti zao hapa Bungeni. Nianze kwa kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane kabisa na wale wote wanaounga mkono suala la Muungano. Wapo watu wachache wasioutakia mema huu Muungano wetu. Jambo muhimu ni vema sasa elimu itolewe kwa pande zote mbili ili watu waeleweshwa *advantage* na *disadvantage* za Muungano. Pia kama kuna kero basi kero hizo Serikali ijaribu kutoa ufumbuzi na pande zote mbili zielimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nchi yetu imetoa uhuru wa vyombo vya habari. Lakini wakati mwingine vyombo hivi vinatumika vibaya na hasa hii midahalo mingine imekuwa chachu ya uchochezi wa upotoshaji kwa wananchi, pengine ingesdhibitiwa ili ijadiliwe kwa ku-*balance issue* inayotaka kuzungumziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuchangia kuhusu mazingira. Kuna uharibifu na uchafuzi wa mazingira umesababisha mabadiliko ya tabia nchi ambayo jumla huathiri mfumo mzima wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa asilimia kubwa ya ardhi ya zamani imezungukwa na madini ya aina mbalimbali. Shughuli hizi za uchimbaji huu wa madini hapa nchini mwetu zinachangia kiasi kikubwa katika kuharibu mazingira yetu. Kumekuwepo na athari kubwa sana kwa wananchi na viumbe hai vinavyoishi karibu na machimbo hayo,

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Ni ukweli

usiofichika kuwa Muungano wetu ni mzuri na hatuwezi kukaa miaka hamsini, ambayo umedumu Muungano huu leo sisi watoto ambao tumeukuta tukaushupalia uvunjike itakuwa hatuwatendei haki wazee wetu waliounganisha nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano una kasoro nyingi ambazo huwa tunazipigia kelele sana tunaomba kasoro hizi zirekebishwe, kuna kero ambayo ni sugu ambayo ni moja kati ya sababu kubwa ambayo vijana wetu wengi imewafanya wavunjike moyo na kuwepo Muungano huu. Sababu mojawapo ni wafanyabiashara wa Zanzibar wanapokuja Tanzania bara wanalipishwa ushuru mara mbili. Sababu nyingine kubwa ambayo sisi Wazanzibar tunaona ni kero kubwa kwetu ni ile ya kutaka ifunguliwe Akaunti ya Pamoja ambayo ingeleta maslahi kwa pande zote mbili, lakini mpaka leo Serikali haijakubali kufunguliwa, kila siku tunaambiwa mchakato bado unaendelea, mpaka lini tuambiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali itatue kero zote za Muungano ili tunusuru huu Muungano wetu usivunjike na udumu daima na milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo la mafuta lipatiwe ufumbuzi haraka sana, kila upande naishauri Serikali ichimbe mafuta yao na gesi yao ili haya malumbano yamalizike yasiendelee kila siku yataleta sura mbaya kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa mapato 4.5% sasa haukidhi haja, urekebishwe.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa hotuba yake nzuri, yenye maana nzuri na yenye kuvutia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri, hizi changamoto za Muungano zitatuliwe kwa kadri inavyowezekana, mfano, malalamiko ya wafanyabiashara na kadhalika.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(FYDPI)* hauhitaji moja kwa moja suala la mazingira. Hata hivyo, maeneo ya vipaumbele vyote isipokuwa moja, yanahusika moja kwa moja na changamoto za mazingira kama Miundombinu; Nishati, Bandari, Reli, Barabara, Viwanja vya Ndege, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu *(Innovation);* Kilimo; Viwanda na Maji na Maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

Wizara ishirikiane na Wizara zote za kisekta zinazotekeleza vipaumbele vya Mpango wa miaka mitano kwa kuainisha matokeo ya athari za kimazingira ufumbuzi wake *(mitigation)* na kadhalika.

Pia Wizara inayohusika na mazingira iweke bayana katika kila Mpango wa mwaka shughuli zote za mazingira ikiwemo miradi inayojitegemea na ile inayotokana na utekelezaji wa miradi mingine mikubwa ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi Idara na Wizara zote ziliripoti katika Ofisi ya Makamu wa Rais namna ambavyo zinatekeleza *components* za mazingira katika miradi na shughuli zote husika.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la utunzaji mazingira nchini liende sambamba na mabadiliko ya tabia nchi, dunia inatilia maanani juu ya utunzaji wa mazingira duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ujoto ambayo inatokana na tabia nchi imechangia kwa kiasi kikubwa kuleta athari kutoka kwenye kina kikubwa cha bahari na athari hizo kuishia nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya matatizo yanayotukabili Watanzania ni utaalam wa kuandika na kusema bila ya matendo mfano, suala zima la utunzaji wa vyanzo vya maji bila ya kuviathiri vyanzo hivyo, lakini ni Watanzania wenyewe wanaoviathiri vyanzo hivyo kwa kulima bila ya kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la upandaji wa miti ni suala la lazima na sio kupanda tu, lakini pia miti hiyo iwe na ulinzi wa kutosha ili kuhakikisha kwamba kile ambacho kimepandwa hakiathiriwi ama kwa kutumia mifugo ambayo inatembea hovyo. Lakini vile vile kuondoa suala zima la ukataji miti ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukosekana kwa nishati ya umeme kunachangia kwa kiasi kikubwa

uharibifu wa mazingira katika nchi yetu. Kwani wananchi wanakata miti kwa ajili ya kupata mkaa kwa ajili ya kupikia, kuna haja ya Serikali kuweka utaratibu maalum juu ya wakataji na ukatwaji wa miti kwa ajili ya mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa kutozingatia umuhimu wa utunzaji wa Mazingira kumepelekea sehemu kubwa ya nchi yetu kuwa jangwa na hata baadhi ya vivutio vya nchi yetu kuanza kuathirika ikiwemo Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandaji wa miti kulinda misitu yetu, kutunza vyanzo vya maji na kuuhami Mlima wa Kilimanjaro na hata mbuga zetu za wanyama kama vile Serengeti, Ngorongoro, Manyara na Mikumi ni sehemu moja ya utunzaji wa mazingira yetu na ni kitu muhimu cha kuenziwa duniani kote.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchafuzi wa mazingira imekithiri katika Jiji la Dar es Salaam na kupelekea maafa makubwa wakati wa mafuriko ya mwezi Desemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababishwa kwa kiasi kikubwa na Baraza la Mazingira *(NEMC)* kutoa vibali na kuruhusu ujenzi holela katika maeneo ya kando kando ya Mto Msimbazi ama kuacha ujenzi huo bila kuzuia wakati wanafahamu ni kuhatarisha usalama wa wananchi wetu. Mfano, ujenzi mkubwa pale Kigogo Sambusa eneo ambalo maji yalikuwa yanakaa na kuelekea Baharini kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni msitu wa Kifo uliopo Bonde la Mkwajuni, maeneo ya Magomeni, kuna msitu ambao kunafanyika maovu mbalimbali kama wizi, ubakaji, mauaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa maeneo hayo wameomba kuondoa msitu huo lakini *NEMC* wanakataa. Hivyo, naomba Serikali iwaruhusu wananchi wa eneo hilo kuondoa msitu huo ambao umepewa jina la Msitu wa Kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani zangu za dhati ziende katika ofisi yako kwa kuruhusu uchangiaji wa maandishi katika mada hii. Nimesoma ukurasa 10 -11 wa hotuba hii kuhusu kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja zenye lengo la kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na jitihada za pande mbili hizi za miradi ya MKUKUTA katika SMT na MKUZA katika SMZ, mapato ya Muungano yanagawiwa kwa upungufu na punjo kubwa kupewa Zanzibar, 4.5% ya misaada ya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari walichangia 11.2% ya mradi wa Benki Kuu, mbali na kuwa Zanzibar sio Mkoa wa Tanzania Bara, bali ilisabilia Utaifa wake kwa nguvu sawa na Tanganyika. Kuna haja ya kugawa sawa mapato hayo kwa nchi hizi mbili, Zanzibar na Tanganyika kama usawa huo ni shida

tungefanya angalau 60% kwa Bara na 40% kwa Zanzibar na mgao huo uendelee kwa mapato yote ya Taifa kwa sababu mapato ya nchi ni suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari wanahoji mambo mengi; mgawanyo wa madaraka usiojali haki sawa ya nchi mbili Tanzania Bara na Zanzibar, si Rais, si Waziri Mkuu, si Mkuu wa Majeshi na kadhalika. Wote wanatoka Tanzania Bara! Migogoro au kero zimezidiwa idadi na hili la chenji ya Rada! Mwalimu J.K. Nyerere alisema Serikali ya Tanganyika imevua madaraka yake kwa Jamhuri ya Muungano. Je, inakuwaje Mwanasheria Mkuu wa SMT aseme chenji ya rada ni mali ya Serikali ya Tanzania Bara. Je, Muungano wetu ni wa Serikali tatu? Mbona anadai hivi ina maana kuna Serikali hiyo ya Tanzania Bara, ya SMZ na ya Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo sahihi unaotufaa ni wa Serikali mbili za mkataba au Serikali tatu. Wingi na ukubwa wa Serikali hizo ni jambo la kujadili. Inashangaza kuwa mambo ya Anga ni Muungano, Ulinzi ni mambo ya Muungano na mapato ni mambo ya Muungano, vipi rada iwe ya Tanzania Bara tu?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais Daktari Mohamed Gharib Bilali kwa uongozi wake uliotukuka. Nawapa hongera nyingi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Daktari Terezya Luoga Huvisa, Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira sawia

kwa hotuba nzuri sana. Aidha, nimpongeze pia Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Naibu Waziri, Mazingira kwa kazi nzuri, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia imekumbwa na mabadiliko makubwa ya tabia nchi *(climate)* katika maeneo mengi yaliyokuwa na uhakika wa mvua za vuli kama Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Kilimanjaro, sasa yamekumbwa na ukame na wananchi wamepoteza mazao kwa miaka mitano mfululizo. Katika maeneo mengine mabadiliko ya tabia nchi yameleta mvua nyingi sana na kuleta maafa ya mafuriko. Vimbunga vikali vilivyofuatana na mvua kubwa sana. Matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa mazingira, makazi ya watu na hata miji kama uharibifu wa Kimbunga cha Katrina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasayansi wa *Ecology, atmospheric sciences* na hali ya hewa wamekusanya takwimu zinazoonesha kuwa ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya mbao, mkaa na kuni katika Milima ya Tao ya Mashariki ndiyo unaoleta ukame katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na sehemu ya Mkoa wa Tanga na Morogoro. Aidha, ukataji mkubwa wa miti katika misitu ya Miombo katikati ya Afrika, Kusini mwa *Equator* kunapunguza nguvu ya *Inter Tropical Convergence Zone (ITCZ)* na hivyo kuchelewa kwa mvua, kupungua kwa kiasi cha mvua na msimu wake kuwa mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuchukue hatua kungali mapema. Tusimamie kwa karibu sana na tuhifadhi misitu yetu ya Milima katika Milima ya Tao ya

Mashariki, Miombo katikati ya Tanzania katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Mtwara, Lindi na Pwani. Sisi Watanzania tumejaliwa sana. Mwenyezi Mungu katupatia utajiri wa gesi ya asilia na makaa ya mawe. Tuchukue hatua za haraka kuendeleza matumizi ya rasilimali hizi kwa ajili ya kupikia majumbani ili kuondoa kabisa matumizi ya mkaa majumbani, Viwandani na kwengineko. Tutumie magogo ya mbao toka kwenye mashamba ya miti ya kupanda ya *pine cypress na teak*. Tupunguze kabisa uvunaji wa miti ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ni vizuri tujiandae pia katika Kilimo. Hivi sasa tumepiga hatua kubwa katika kuandaa mbegu zinazohimili ukame kwa mazao ya mahindi, pamba na kukabiliana na magonjwa ya mihogo. Maendeleo haya yameletwa na utafiti unaotumia *biotechnology* na kubadili vinasaba vya viini vya mazao hayo. Katika pamba mabadiliko hayo yanaongeza urefu na ubora wa nyuzi za pamba yanaongeza tija ya uzalishaji toka kilo 300/*ha* za sasa mpaka kilo 2000/3000 *ha*, zinapunguza kupulizia dawa na kuhimili magonjwa na wadudu wa pamba, lakini kwa kanuni za biotechnolojia tulizonazo mbegu hizi haziwezi kutumika nchini Tanzania.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Naomba kushauri mambo yafuatayo:-

Kwanza naunga mkono Serikali ya Muungano. Aina ya Muungano ambao utakuwa wa manufaa kwa

Watanzania wote na ambao utakuwa wa gharama nafuu kuendesha ni wa Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kutatua kero za Muungano zilizobaki, jitihada za Serikali kutatua kero zilizobaki ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee na mchakato wa Katiba mpya ili wananchi watoe kero zao ambazo zinaweza kusaidia kuimarisha Muungano.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hotuba hizi mbili, Muungano na Mazingira. Kwanza napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili. Mheshimiwa Samia na Mheshimiwa Terezya kwa kuwasilisha hotuba zao, hii inadhihirisha wazi kuwa wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na mazingira, kuna uharibifu mkubwa wa mazingira hasa katika migodi yetu. Wawekezaji wanapochimba migodi na mara nyingi hubeba hadi mchanga, hivi hatuoni kama tunaachiwa mashimo ambayo hatuwezi kuyafukia mpaka kiama. Wizara ya Mazingira itatuambia nini? Ambapo sasa tuna mashimo ya kutosha hata iweje kuyafukia haitowezekana. Pia utafiti wa *uranium* huko Namtumbo ni kwa kiasi gani Watanzania wako salama na ni nani anayesimamia hayo kwa kina? Tumeona wananchi wa Nyamongo walivyoathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pale watu wanyonge wanapojaribu kujitafutia nishati mbadala ya kupikia,

hapo ndipo utapowaona maafisa wa maliasili na mazingira wanapowasumbua raia hao. Ni vizuri kuhimiza kupanda miti mara mbili zaidi ya sasa tunavyopanda kuliko kuwazuia watu hasa wa vijijini kushindwa kutumia kuni na mkaa kama nishati mbadala. Vijijini hakuna umeme, hiyo gesi hata mjini inatushinda kutoa zuio la kutumia kuni na mkaa bila kuwasaidia nishati ya uhakika ya kupikia, ni kuwaongezea matatizo, Maafisa wa Maliasili na Mazingira wanapowakamata huwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mazingira inayo kazi ya kuelimisha Wizara zingine kama Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Elimu ili ziweze kutoa elimu. Mfano, ukosefu wa maji karibu na vyanzo vya maji unapelekea matatizo makubwa. Watu wanaoishi jirani mfano, Ziwa Victoria hupelekea watu kufua hapo ndani ya Ziwa na hivyo sabuni na taka zingine huingia ziwani na kusababisha uchafuzi wa mazingira, ha pale akina mama wanapofua nguo za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati ni upande hasa wa migodi pale wanapochimba na kutumia kemikali kali ambazo husambaa kwa mtiririko wa maji na kuwaathiri wanavijiji jirani na migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu kutoa mafunzo kikamilifu kwa wanafunzi juu ya utunzaji wa mazingira ili watoto wetu waweze elewa tangu wakiwa wadogo umuhimu wa kutunza mazingira, ni wajibu wetu kama nchi tutunze mazingira na pia kuangalia changamoto zake wakati wa utekelezaji. Tuyatunze mazingira ili nayo yatutunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano ni muhimu sana kwetu, hivyo ni bora tofauti za Muungano zikashughulikiwa kwa haraka na umakini mkubwa, Muungano umetuunganisha leo miaka 48, kwa hiyo, ni bora tukaulinda. Wanaodai wao hawakuulizwa hiyo ni sawa na baba anapoumwa mama hawaulizi wanafamilia wote na hasa mtoto ambaye hajazaliwa ataulizwa vipi? Muungano sio siasa, Muungano ni kwa ajili ya Umoja wa Watanzania walipoamua kuunganisha Tanganyika na Zanzibar. Muungano mzuri ni wa Serikali tatu; Tanganyika, Zanzibar na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu ni utatuzi wa kero za Muungano wenyewe. Ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Mchango wangu utaweza kuzungumzia kujadili mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira, zoezi la upandaji miti halisimamiwi vizuri. Agizo hili likisimamiwa vizuri kwa kila mtu katika eneo lake mazingira yanaweza kutunzwa, miti inapandwa na mashule na Serikali za vijiji, lakini haitunzwi hivyo juhudi ipo ila tija hakuna. Ibuniwe njia itakayohakikisha miti inayopandwa kila mwaka inakua na kila mtu awajibike hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za vijiji na ziwe na sheria na zisimamie Sheria za Mazingira kikamilifu. Nishati mbadala ni suluhisho la mazingira na

changamoto zake, *biogas*, gesi asili na *solar* vikiendelezwa maeneo ya vijijini ambako hakuna umeme itaweza kusaidia kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo, Mawaziri, Wabunge, na viongozi mbalimbali wanamiliki mifugo kupita kiasi na hivyo mipango mizuri ya kuhifadhi na kutunza mazingira kunakohimizwa na Serikali inashindikana. Jambo la uharibifu wa mazingira kwa ufugaji tunaofanya leo na kuufumbia macho tutasutwa na vizazi vijavyo, hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe kunusuru uharibifu huu unaofanywa na jamii ya wafugaji ambao kwa sehemu kubwa hawana kabisa elimu juu ya utunzaji mazingira, itungwe sheria na isimamiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadilko ya Tabianchi, kutokana na hali ya kuongezeka kwa uharibu wa mazingira kuongezeka kwa gesi joto duniani, nchi ambazo zina uchumi ulio nyuma zina changamoto kubwa sana katika kuendeleza uchumi wake. Ni vizuri kuwepo *adaptation programmes* ili kuziwezesha kusonga mbele kiuchumi kwa kujenga uchumi wa kijamii kwa vile uwezo ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea kwa vile zilitumia rasilimali zetu zisaidie katika mipango hii ya *adaptation programmes*, kunusuru uchumi wa nchi nyingi za kiafrika na dunia ya tatu na dunia yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Ziwa Tanganyika unaoshirikisha nchi zipatazo nne, Tanzania, Burundi, Zambia na Kongo, utekelezaji kwa upande wa Tanzania nashauri miradi inayotekelezwa iwe na mgawanyo wa kutambua mipaka ya kiutawala na kisiasa. Mfano, eneo lote linalopakana na Ziwa changamoto zake zinafanana. Tungependa kuona miradi inazingatia uwepo wa Mikoa, Wilaya, na Majimbo isitokee wilaya X ambayo ina Majimbo zaidi ya moja, miradi inajazana kwenye Jimbo moja kama Jimbo la Nkasi Kusini, naona lina mradi mmoja tu wa pale Wampembe, lakini ndiyo Jimbo pekee lenye mtandao mrefu wa Ziwa japo miradi ya barabara, bweni na nyumba ya Mwalimu na ujenzi wa Mialo upo Wilaya ya Nkasi, miradi yote karibu iko katika Jimbo moja. Hii haiwezi kukubalika hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, uwanda wa Ziwa Tanganyika unakabiliwa na umaskini mkubwa licha ya kuzungukwa na utajiri wa maliasili zilizopo. Hii imesababishwa na eneo hilo kutofikika kwa urahisi. Mradi ufungue barabara zilizoko mwambao kama vile (km 67) Nkana- Kala; (km 68) Kitosi – Wampembe. Barabara hizi zikifunguka wananchi wa Tarafa ya Wampembe yote watapata fursa ya mwingiliano *(interaction)* na wenzao wa maeneo ya ukanda wa juu na hivyo kubadili mitazamo yao na kutambua vema suala la utunzaji Bonde lenyewe barabara zipewe kipaumbele kuliko chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama , eneo la Ziwa hasa Tarafa ya Wampembe hakuna mawasiliano ya simu wala barabara na hivyo wananchi,

hawatembelewi na viongozi wao hata kidogo. Wanavamiwa na majambazi na kuwanyang'anya zana za uvuvi na mali kadhaa. Katika kipindi cha miaka miwili tu, wamevamiwa mara nne na kunyang'anywa mali. Mradi usaidie mawasiliano ya mitandao ya simu za mkononi ili kunusuru wananchi hawa na watakapojua mkombozi wao watatoa ushirikiano sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zana za uvuvi, katika kuwaelimisha wananchi juu ya zana zisizotakiwa kutumika kwa sababu baada ya elimu hii kuanza kuenea kwa kasi, wananchi wamekuwa wakinyang'anywa zana zao walizozizoea na hivyo kurudi katika umaskini wa ujima. Ningeshauri mradi ununue zana za kisasa na kubadilishana na zile walizokuwa nazo ili wasibaki hohehahe au basi mradi ulete zana na wapunguze bei kwa asilimia 50% na kuwa sifa ya kupata ni kusalimisha nyavu zisizotakiwa, lakini kuwanyang'anya na kuchoma ni aibu na kuwatia katika umaskini wananchi wetu kwani walizinunua pasipo kuwa na uelewa ambapo ni kazi ya Serikali kuwapa elimu.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuelekeza mchango wangu kuhusu suala la mazingira katika sehemu kuu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na uharibu wa mazingira unaofanywa na kampuni zinazotengeneza barabara. Kwa kweli hali inasikitisha sana kuona miradi mikubwa kama hii ambayo Serikali

inatumia kiasi kikubwa cha pesa kulipa, lakini miradi hii si rafiki hata kidogo wa mazingira. Mara nyingi wanakuwa katika usanifu wa mradi wanakuwa na kambi na wapole sana, lakini pale wanapoanza uchimbaji wa vifusi suala la mazingira halina tena nafasi yake. Ukweli ni kwamba miti iliharibiwa na kukatwa hovyo, pale watakapofanikiwa kuchimba changarawe na kifusi hakuna hatua za makusudi za kurudi nyuma na kufukia mashimo yale. Hii ni hatari kwa maisha ya wanyamapori na hata kwa maisha ya binadamu. Ni ukweli usiopingika, hakuna sehemu wanapotekeleza mradi wa ujenzi wa barabara wanapokumbuka suala la utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa Serikali kuwa katika suala zima la mikataba wanayopewa, basi suala la utunzaji wa mazingira lazima lipewe kipaumbele na lizingatiwe na ikiwezekana malipo ya mwisho yasifanyike mpaka amefukia mashimo yaliyopo ili kunusuru maisha ya viumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu suala zima la wachimbaji wadogo wadogo, imekuwa ni tabia ya muda wote pale yanapogundulika machimbo ya madini, hili kundi bila ya kujali athari za mazingira watachimba kila kona na kuharibu uoto wa asili pasipo kujali. Mara nyingi inawezekana kitengo cha mazingira aidha, hakioni kuwa hili nalo ni suala muhimu au ofisi haipewi mafungu ya kutosha kufuatilia sehemu zote ambazo shughuli hizi za uchimbaji mdogo mdogo unafanyika na kufanya tathmini ya mazingira. Sasa ili kufanikisha azma ya kulinda mazingira yetu ni muhimu

Kitengo cha Mazingira kikawa na mpango mkakati madhubuti na wa kina katika suala zima la ulinzi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la ufugaji usiozingatia taratibu na kanuni. Kuna kundi au makundi ya wafugaji ambao hawajali suala la mazingira wanayofugia bali wao wanajali kiasi cha ng'ombe kuongezeka, hapa kinachoendelea ni uharibifu wa uoto wa asili na vyanzo vya maji, maana kundi kubwa la mifugo wakati eneo husika ni dogo. Mifugo hii haitoi nafasi kwa mimea kuota wala kurudia hali yake ya ustawi. Hii itapelekea uharibifu mkubwa na muda mrefu wa nyasi kuota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa ofisi husika kuwa na mikakati ya makusudi ya kunusuru hali hii, kwa kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ni suala Mtambuka, basi Ofisi ya Mazingira ishirikiane na wahusika huko Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano na Mazingira ni masuala tata na tete. Naomba Serikali izingatie masuala yafuatayo kuhusu mapitio ya utekelezaji na bajeti ya 2011/2012 ya Ofisi ya Makamu wa Rais( Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mosi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Baraza la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, baada ya kufanya ukaguzi wa uchafuzi wa mazingira Jimboni Ubungo katika maeneo

mawili niliyoyataja. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira katika maeneo hayo umeendelea kwa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuelezwa hatua iliyofikiwa na *NEMC* kwenye kuwezesha ahadi ya kiwanda cha Mkoani *Traders* na Azania *Wheat Floor*, kutafuta eneo mbadala na Shirika la Hifadhi ya Jamii kuweka mfumo mbadala wa uondoaji wa maji taka toka hosteli za Chuo Kikuu Mabibo bila kutiririsha maji taka katika mto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pamoja na hatua zilizochukuliwa kuhusu uchafuzi wa mazingira unaofanywa na mgodi wa *North* Mara, unaomilikiwa na kampuni ya *African Barrick Gold*, ili Wabunge tuweze kupima iwapo masuala yote yamezingatiwa. Narudia ombi langu la kutaka tupewe taarifa ya kina ya *NEMC* na ripoti za Kamati maalum za Bunge zilizotumwa kufuatilia malalamiko katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mpaka sasa sijapewa nakala ya taarifa ya hali ya mazingira Dar es Salaam iliyoandaliwa na *NEMC* kupitia Mradi wa Programu ya Mtandao wa Taarifa Afrika ambayo ilipaswa kukamilishwa katika mwaka 2011/2012. Ili ituwezeshe Wabunge kufuatilia masuala yanayohusu Serikali kuwa na yale yanayohusu Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali ieleze imefikia wapi kuhusu ombi la kutoa baadhi ya nyaraka za siri *(declassification)* ili zisaidie katika kupata rejea ya historia ya Taifa letu na dhamira ya waasisi wa Taifa

kuhusu Muungano katika wakati huu ambapo nchi ipo kwenye mchakato wa Katiba Mpya. Aidha, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inahitaji kufanyiwa marekebisho kuhusu Bunge na kwa kura za maoni. Kwa upande wa makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2012/2013, hususani kuhusu fungu 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi katika utekelezaji wa mradi wa kifungu 5306, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais iingize Manispaa ya Kinondoni katika kazi zake za kujumuisha kutathmini kujenga uelewa na mikakati ya masuala ya tabia nchi katika Serikali za Mitaa ikiwemo Jimbo la Ubungo kutokana na athari ambazo zinaanza kutokea. Kama ikishindikana kwa mradi huo hatua hizo zichukuliwe kupitia mradi wa kifungu 5301, ambapo Wilaya zote tatu zilizotajwa kuwa majaribio *(pilot projects)* hakuna Wilaya ya Mjini wakati Miji imeanza kupata athari za mabadilko ya tabia nchi ikiwemo mafuriko. Mradi huo pamoja na kushughulikia masuala ya mipango miji uhusishe pia uhamasishaji wa matumizi ya gesi asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu mradi wa kifungu 6571 na matumizi ya kawaida ya kifungu 5001, kasma 270800 juu ya *NEMC* na usimamizi wa Sheria ya Mazingira, vitumike kuamisha viwanda vinayochafua mazingira Dar es Salaam, ikiwemo Ubungo kuweka mkakati wa usafirishaji wa Mito na Vijito. Kushirikiana na Wizara za Maji na TAMISEMI kuwa na mpango kabambe wa uzoaji maji taka na takataka katika Jiji la Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naendelea kupata Mwongozo hapa. Kwa kadiri ya muda ulivyo, nafikiri kwa kweli, naomba nikubali tu tuishie hapo. Tunapoishia hapo, huyu Mheshimiwa Waziri aliyetoa hoja anatakiwa apate saa moja ya kujibu hoja. Kwa hiyo, tuna saa moja nyingine. Tukitoka hapo, tuingie kwenye vifungu. Kwa hiyo, nafikiri tuishie hapa sasa, kusudi tuanze kuipa Serikali nafasi, iweze kujibu hoja.

Sasa, Mwongozo nilioupata, hiyo saa moja ambayo Serikali imepewa na kama mnavyofahamu, Ofisi ya Makamu wa Rais, hapa inawasilishwa na eneo la Muungano na Mazingira. Sasa Mawaziri hawa wawili, anayesimamia Muungano na Mazingira, wao wamegawana dakika 20, 20. Lakini nafasi nyingine kwa Serikali, wamempa Mheshimiwa Shamsi Nahodha, Waziri wa Ulinzi, lakini wamempa nafasi nyingine ya dakika 10, Mheshimiwa *AG,* ili na yeye atoe ufafanuzi wa masuala kadhaa, yakiwemo masuala ya Katiba na masuala ya Kisheria.

Kwa hiyo, nitaanza kumpa nafasi Mheshimiwa Shamsi Nahodha, kwa dakika 10, Mheshimiwa *AG,* ajiandae na yeye dakika 10 na baada ya hapo, sasa nitarudi kwa Waheshimiwa Mawaziri na wao wataniongoza utaratibu wa kufanya.

Mheshimiwa Shamsi Nahodha.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Tundu Lissu - Msemaji wa Kambi ya

Upinzani, nimebaini mambo matatu katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kazi nzuri ya kufanya utafiti. Kama bidii hii aliyoitumia katika kufanya utafiti angeilekeza katika kila eneo linalohusu maendeleo ya nchi yetu, basi bila shaka nchi yetu ina hazina kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hotuba yake imejaa hadaa, ulaghai na udanganyifu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, ametoa tu malalamiko kuhusu Zanzibar, Tanzania Bara, akinukuu Wanasheria, Maprofesa na Wanazuoni mbalimbali wa Taaluma ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa na Msomi na Mweledi wa kiwango cha Mheshimiwa Tundu Lissu, ningemtarajia angetupa sasa mapendekezo yake ni nini, juu ya kasoro hizi ambazo tunakabilianazo katika Muungano. Lakini nitafanya hivyo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza kasoro nyingi, lakini mimi nitataja nne. La kwanza, amesema Mamlaka ya Zanzibar, inachukuliwa kwa kuongeza orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningemtarajia basi angetoa jibu, lakini si neno tutamsaidia sasa. Nadhani

jibu la kuondokana na utaratibu huu wa kuongeza orodha ya mambo ya Muungano mambo ambayo inaelekea upande fulani hauridhiki dawa yake ni hii ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefanya kwa kupitia Tume ya Kukusanya Maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Wazanzibar wa Bara na Visiwani watapata fursa hiyo ya kutoa mapendekezo juu ya muundo wa Muungano wanaoutukana na mimi ningeulizwa ni muundo gani wa Muungano naupenda kwa dhati ya moyo wangu nasema kama ulivyo msimamo wa Chama changu naupenda Muungano wenye muundo wa Serikali mbili na nitaeleza baadaye kwa nini. *(Makofi)*

Lakini pia Wazanzibar na Watanzania watapata fursa ya kutoa na kueleza utaratibu wa kubainisha mambo ambayo wanadhani yatakuwa muafaka kubakishwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano na hapa nitatoa maoni yangu; kwa maoni yangu na kwa maoni ya Serikali. Naamini kwamba tunapaswa kuwa na maeneo machache sana katika Muungano, maeneo ambayo tunaweza tukayasimamia vizuri na ni maeneo hayo tu:-

(i) Ni eneo la ulinzi na usalama;

(ii) Ni Polisi;

(iii) Uraia;

(iv) Sarafu;

(v) Mambo ya nje;

(vi) vyama vya siasa; na

(vii) Masuala ya anga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** eneo la pili, ambalo katika hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu naona halikuelezwa vizuri, ni suala la badiliko la kumi la Katiba ya Zanzibar ambayo anahisi kwamba yameashiria kutoa tafsiri mpya ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alitoa mifano. Mfano wa kwanza, alisema mabadiliko haya ya kumi yamebadilisha ibara ya kwanza ya Katiba ya Zanzibar ambayo mwanzo ilikuwa inasema Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa inasema Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** sasa hili ni suala la lugha, wako watu Kiswahili ni lugha yao ya pili, wamejifunza shuleni lakini kwa watu ambao lugha ya Kiswahili ni lugha yao ya kwanza ya asili kama nilivyo mimi hiki ni kitu kimoja. Ukisema Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano maana yake Jamhuri ya Muungano huu ina maana umeundwa na sehemu zaidi ya moja. Kwa hiyo, sehemu moja iko Zanzibar na sehemu moja iko Tanzania Bara na kwa maana ile ya pili ambayo anasema yeye inahoji Muungano wa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili, sasa tunakataa nini na huu unakuwaje ni Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa Kigoma ni miongoni mwa nchi mbili, nadhani hilo lingekuwa tatizo lakini kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili nafikiri hilo halina utata liko sahihi. Lakini kwa watu ambao wanajifunza Kiswahili, wanapata tabu kati ya nchi, Taifa na dola. Hata wanaojifunza Kiingereza wanapata matatizo hayo hayo, wanapata tatizo; *State* kwa maana ya Kiswahili nchi, *a Nation* kwa maana ya Taifa na Dola kwa maana ya *Sovereignity*. Sasa nafikiri rafiki yangu Mheshimiwa Tundu Lissu, nafikiri akaangalie vizuri kwenye Kamusi ili aweze kupata maana halisi, sioni kama kuna utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** suala la mwisho, ni suala la Katiba ya Zanzibar kuruhusu kura ya maoni. Kwa maoni yake anahisi kwamba, Katiba ya Zanzibar kuruhusu kura ya maoni inatoa nafasi kwa Uamsho na vikundi vingine vinavyopinga Muungano kupata nafasi ya kufanya kura za maoni juu ya suala la kuwepo kwa Muungano.

Mheshimiwa Tundu Lissu yeye ni Mwanasheria, nakumbuka tafsiri ya sheria inasema ukitaka kujua tafsiri halisi ya sheria unaangalia vitu viwili; cha kwanza tafsiri ya maneno na cha pili dhamira ya watu walioitunga hiyo sheria. Sasa kwa bahati nzuri nilikuwa miongoni mwa watu waliohusika na mabadiliko ya Kumi nikiwa Waziri Kiongozi wakati ule. Kwa hiyo, dhamira ya jambo hili naweza kulifahamu zaidi kuliko Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yake ilikuwa ni kuleta umoja na maelewano Zanzibar, lakini hili suala la

kura ya maoni halikukusudiwa kuhusiana na masuala ya Muungano, kura ya maoni ilikuwa *specifically* kwa ajili ya maeneo mahususi yanayohusu mamlaka ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekit, la mwisho, napenda kutoa ushauri, Waheshimiwa viongozi tunajua mjadala wa mambo ya Muungano unapita katika kipindi kigumu sana na wakati mwingine suala la Muungano linajadiliwa kwa hisia kali sana. Maoni yangu, Kiongozi mzuri ni yule ambaye anatumia hekima na busara na kujua wapi anasema nini na wakati gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali, tunapaswa kusema ukweli, lakini kuna wakati ukweli huu unaweza kuleta maangamizi na madhara makubwa sana kwa Taifa letu. Kwa hiyo, ushauri wangu tutoe maoni yetu kwa uhuru tuseme kweli pale inapobidi lakini tukielewa kwamba tuitendee haki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wananchi wa Tanzania...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Wasiingie kwenye matatizo. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Shamsi Nahodha kwa mchango wako kwa niaba ya Serikali. Sasa naomba nimwite Mwanasheria Mkuu wa

Serikali naye tunampa dakika kumi na baada ya hapo nitawaita watoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kama nilivyokwishawahi kusema mwanzoni nilipokuwa naingia kwenye Bunge hili nilikiombea Kiti afya ya akili, afya ya mwili na sasa nakiombea tena afya ya roho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini sana hotuba zote asubuhi na nawashukuru sana Mawaziri wanaohusika na sekta hii na kabla sijaenda mbali naunga mkono hoja hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitaweza kuzungumzia vitu vyote lakini niombe radhi kwa Ndugu yangu Jaddy Simai Jaddy kwamba sitaongelea suala la rada. Si kwa sababu sina majibu, lakini ni kwa sababu rada kama rada ni suala la Muungano, lakini fedha zilizoinunua hiyo rada inawezekana likawa si jambo la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa sababu moja tu. Wakati Mheshimiwa Tundu Lissu anahitimisha hotuba yake alisema kwamba, Bunge hili liazimie kutumia mamlaka ambayo linayo ya Ibara ya 46 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kumshtaki Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu gani? Eti mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Jamhuri ya Zanzibar yamevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Lissu inahitaji vitu ambavyo tunaviita kisomi kuweka

*footnote* au maelezo ya ziada au *endnotes* likiwemo hili la kusema kwamba historia halisi ya Muungano haifahamiki kwa wananchi walio wengi. Kazi niliyofanya kama mwalimu kumbe ni bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** pia kuna mkanganyiko, kwamba kunapotokea mkanganyiko tofauti kati ya Sheria ya makubaliano ya Muungano na Katiba basi makubaliano au Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Sura 577 ni lazima yafuatwe. Lipo jambo lingine la Zanzibar kutoridhia makubaliano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Labda nikiri kwamba mimi mwenyewe sijaona *decree,* sijaona tamko la Baraza la Mapinduzi Zanzibar kuridhia mkataba wa makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesoma, tena nimesoma vizuri. Tarehe 25 Aprili, 1964, Baraza la Mapinduzi Zanzibar lilikaa mjini Zanzibar likifanya nini? Likipitia makubaliano hayo na jioni hiyo Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo ni pamoja na Wawakilishi kutoka Baraza la Mapinduzi lilipitisha makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata kama hakuna hati ya uridhio unataka kusema Muungano ni batili? Kama umekwenda shule vizuri utakuwa umepitia Mkataba wa Kimataifa wa Mikataba ya Kimataifa, unaoitwa *Vienna Convention on Treates*. Nimeusoma na nimeuhariri. Tabia ya nchi au uwezo wa nchi fulani baada ya kufanya tendo inaonyesha kwamba mmekubali na ndiyo msingi wa kupata *pacta sunt servanda* yaani makubaliano ya mkataba lazima

yaheshimiwe, kwa hiyo, mikataba inabana na bahati nzuri msomi uliyerejea Mheshimiwa Lissu anakubali hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msomi aliyerejewa na Mheshimiwa Lissu, Profesa Shivji naye alikuwa *academic advisor* wangu, ni msomi naye anakubali kwamba *principle of acquiescence* (yaani kuridhia kwa tabia mwenendo na vitendo bila maandishi) katika hali hii inakubalika. Kwa hiyo hakuna kichaa atakayesema kwamba Muungano wetu batili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la msingi, la watu wanaohoji Muungano siyo hilo na ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa na nje na kwenye makongamano ya kisomi pamoja na ambayo siyo ya kisomi, kwenye mabasi ya UDA, kwenye vituo vya mabasi, kwenye mabaa, tatizo siyo hilo, tatizo ni nini? Tatizo wanataka kuweka na kubainisha wazi au kama wanavyosema neno la asili ya Kisukuma kinagaubaga. Nimesema na Kiswahili pia hakikuanzia kwetu Ukuriani lakini nimekisoma, tena nimekisoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zile haki na wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ziwekwe wazi kwenye Katiba, hilo linakosekana kwenye Katiba yetu, hicho ndicho watu wanachosema. Sasa kupandisha mbavu hapa kusema kwamba haya mambo ni batili nafikiri si jambo jema, Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Muungano na SMT na SMZ wamejaribu, lakini kujaribu huku kunakwamishwa na msingi wa Katiba kwa sababu huwezi kuondoa suala la mafuta hivi hivi,

lazima uende kwenye Katiba, ubadilishe Katiba ndiyo uliondoe lakini ukiliondoa lina athari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika pia kusikia kwamba, kifungu cha tano cha Sheria ile ya Muungano hakijaguswa. Angekuwa anasema mtu mwingine ningeshangaa, lakini kwa sababu amesema msomi mwenzangu nafikiri ni upotoshaji. Labda mimi ni mwalimu nafikiri ni suala la elimu, kama utapenda kufahamu nikufahamishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kifungu kile cha tano hakiwezi kuwa kinaguswa kwa sababu baada ya Katiba ya muda ya 1965 na Katiba ya kudumu 1977 kutungwa tunarudi tena kwenye kifungu hicho? Je, ndiyo hoja ya kusema kwamba, kunapotokea mgongano kati ya Sheria ya Muungano na Katiba ya basi sheria ile ya Muungano ya 1964 inafuatwa, nafikiri kama ni utovu wa kufikiri, samahani neno hilo nisilitumie ni makosa. *(Makofi)*

Unamkariri Profesa Shivji anasema hivyo, mimi ni msomi pia, mimi sisemi hivyo, angalia Maprofesa wengine; Profesa Sriva Stava katika ile mada yake ya *The Constitution of United Republic of Tanzania, 1977 its Riddles et cetera*, angalia mada za Profesa Paramaganda Kabudi, angalia mada za Daktari Harisson Mwakyembe... *(Makofi)*

Katika watu hawa, watu wote wamesomea elimu ya Katiba, huyu mwingine unayemsema amesoma elimu ya Katiba ya kuandika, kwa hiyo ni vizuri kujua

kwamba kunapotokea hitilafu hiyo kinachoongoza ni Katiba na nafahamu unajua hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yaliyofanywa na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar hayakuvunja Katiba yoyote na alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi yanasema Zanzibar ni nchi. Ndiyo Zanzibar ni nchi, Zanzibar si dola, Zanzibar si Jamhuri, Zanzibar ni nchi na msingi wa nchi hiyo ndiyo unaoleta Muungano kwa sababu bila nchi hakuna Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nchi hizi mbili nchi hii ya Tanganyika na nchi hii ya Zanzibar zilizaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga tena mkono hoja lakini nina mengi ya kusema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* tunakushukuru sana kwa mchango wako kwa niaba ya Serikali. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri Kitwanga, yeye atatumia dakika 15 atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mazingira, Mheshimiwa Daktari Huvisa na atafuatiwa na Waziri mwenye dhamana ya Ofisi ya Rais masuala ya Muungano, Mheshimiwa Kitwanga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuitumikia tena nchi yangu katika nafasi ya Unaibu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Nimshukuru sana Makamu wa Rais Daktari Mohamed Gharib Bilali kwa uongozi wake mzuri sana na maelekezo yake ambayo yote yamenifanya niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Misungwi. Niwaeleze tu kwamba, tuendelee na kauli mbiu yetu ya Mawe Matatu kwa maana ya msimamo, mshikamano na mnato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru familia yangu kwa msaada wao na sala zao siku zote katika kuniombea ili niweze kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende moja kwa moja kwenye hoja na nitajaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao nawashukuru sana kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakinipa tangu nikiwa Wizara nyingine mpaka hapa nilipo.

Hoja ya kwanza ambayo imezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ni sekta ya mazingira ambayo inasema msisitizo mkubwa unaonekana ni wa kinadharia, lakini utendaji ni

mdogo. Lakini hapo hapo vilevile niweze kujibu kwa ujumla, wanazungumzia zaidi kwamba, sheria iliyopo nayo haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nitalizungumzia dunia yetu iko hapa duniani na jua liko juu na katikati kuna hewa. Hewa kwa asilimia mia moja (100%) imegawanyika, asilimia 78 *Nitrogen*, asilimia 21 ni *Oxygen* na inayobaki watu wengi wanaita *green house gases* kwa Kiswahili tunasema gesi joto. Mwanga wa jua unapotua duniani unaleta joto, lakini miale mingine inapaswa irudi juu kwenye hewa kama *reflection*. Sasa kinachotokea hii gesi joto ndiyo inayozuia kwa kiwango kinachotakiwa kubakiza joto hapa duniani. Sasa inapokuwa gesi joto imeongezeka basi joto nalo linaongezeka na ndipo hapo mazingira yetu tunaanza kuyaharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nilivyojibu swali linalohusu Mlima Kilimanjaro wiki iliyopita, Mheshimiwa Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni nilisema kwamba, sisi kama Watanzania tunachangia kwa asilimia 18 mpaka 20 kwa sababu ya uharibifu wa mazingira na asilimia 78 mpaka 80 inachangiwa na nchi zilizoendelea. Sasa kama viongozi na Watanzania tuna chombo au sheria ambayo inatufanya tuweze kudhibiti hii asilimia 18 yaani Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na ndiyo inatutaka tutunze mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitalijibu hili kwa ujumla kwa sababu wengi tunasema tukate miti tupande miti, kuna uharibifu wa mazingira.

Kinachosababisha tusitekeleze hii sheria ni pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge. Sheria kifungu cha 33 mpaka 41 vinaelezea utaratibu ambao sisi kama viongozi na sisi kama wananchi wa Tanzania tunatakiwa tufuate. Kifungu cha 33, kinazungumzia sekta mbalimbali katika Serikali. Lakini vifungu vya 34 na 35 vinatuelezea ni kwa namna gani wengine tunavyoweza kuunda Kamati zetu katika Sekretarieti za Mikoa. Lakini kifungu cha 36 ndicho ambacho nataka nisisitize kwa sababu kinatutaka sisi Waheshimiwa Madiwani kupitia Halmashauri zetu tuweze kuwa na Wataalam watakaosimamia mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ndipo wengi tunashindwa, halafu tukifika hapa Bungeni wote tunazungumza. Mimi nazungumza, wewe unazungumza, lakini kama sote kwa pamoja hatutachukua, hakuna kitu ambacho tutakitekeleza kwa sababu *section* 37 inatoa mamlaka mpaka kwenye kitongoji. Msimamizi wa mazingira katika Kata, Kijiji na Kitongoji sisi kama wananchi wa Tanzania na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tumefanyia nini hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jambo ambalo inabidi tujiulize kwa sababu tunapokata miti, tunapolima kila mahali, mabadiliko haya lazima yatokee. Sasa tusimamie na tutafanya hivyo kwa kuanzia katika nyumba zetu. Hivi nani unataka aje afagie nyumbani kwako? Hivi nani unataka aje atengeneze vizuri shimo la kuchomea takataka nyumbani kwako? Serikali itaendelea kusimamia na

kutoa sera na kuhakikisha kwamba, inafanya *oversight* kwa watu ambao wanakiuka taratibu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimejaribu kulielezea hilo ili sote tusiwe walalamikaji tu, tuwe watendaji. Kuna mikakati ambayo imetengenezwa na Serikali. Kuna mkakati wa kuzuia uharibifu wa ardhi na mazingira wa mwaka 2006 na bahati nzuri tunatumia huo huo hata kushindanisha Vijiji vyetu, kushindanisha Halmashauri zetu na ndiyo huo msingi tunaoutumia hata kutoa tuzo za Rais za Mazingira. Sasa nawaomba sana Watanzania hili tulichukulie kwa umakini na undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende haraka haraka katika jambo lingine ambalo limezungumziwa na Wabunge wengi, la *Genericallly Modified Organisms (GMO)*. Hili nalo Waheshimiwa Wabunge na ndugu zangu Watanzania tuwe makini nalo. Unapobadilisha mbegu ya asili ni lazima uwe umefanya utafiti wa kutosha. Sisi sote wakulima wetu wanatumia mbegu za pamba kwa mfano; zote *either* zinatoka Ukiriguru au Ilonga. Sasa kama tutaweza kuzibadilisha hizi mbegu zikatoka mahali pengine na wananchi wetu wakawa hawana uwezo wa kuzinunua itakula kwa nani? Ndugu zangu Watanzania twendeni kwa mpangilio, nakumbuka ndugu zetu wa Benki Kuu walipoambiwa ku-*liberalise capital account* walisema tunakwenda polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tunakwenda hivyo polepole na ndiyo sababu tumetoa kibali kwa *COSTECH* kupitia mradi wa

*WEMA* kufanya utafiti pale Makutopora. Ndiyo sababu tumetoa kibali kule Mikocheni ili tuweze kufanya utafiti wa zao la mhogo. Tutaangalia hilo kama Serikali tuone kama tunaweza tukaanzia kwenye katani au pamba, lakini kwenye chakula ni vizuri tukaliangalia hili. Wenzetu wanaona mbali zaidi. Kwa hivyo, ni lazima tufanye utafiti wa kutosha na huo utafiti ufanywe na Wataalam wetu kwa kushirikiana nao ili *ownership* ya hizo mbegu iwe ni ya Watanzania ambao watahakikisha kwamba, wakizipanda leo mwaka kesho zitaota na mwaka unaofuatia zitaota pia.

Kuna sehemu ambapo walifanya hivyo, baada ya kupanda mara mbili mbegu zote zikawa haziwezi kuota. Sasa kama na sisi tunataka tuingie huko kichwa kichwa nadhani tutakuwa hatutendi haki. Tuwaruhusu wataalam wetu katika vituo vyetu vya utafiti waweze kufanya utafiti *step by step*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzania amezungumzia *North* Mara, Geita *Gold Mine* kuhusu *cyanide*. Niseme tu kwamba kwa *system* ya uzalishaji au viwanda vya *Gold there is no way cyanide can go out of the cycle. There is no way*! Lakini nakubaliana kuna zebaki, *yes I'm a scientist as others* nakubaliana na hii tunayoita *mercury* kwa sababu inatumika na wachimbaji wadogo wadogo na *in actual sense* ina-*extract gold* katika udongo *not more than twenty two percent* (22%) ndiyo sababu ukienda kwenye mradi wa wachimbaji wadogo wadogo wale wengine wananunua yale mabaki ya mchanga wanakwenda wana- *process* kwa kutumia *Cyanide* na

wanapata *gold* zaidi. Ni vema tukalitambua na kulijua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatukatai kwamba, kutokana na watu kutumia zebaki kulitokea uharibifu na tutaendelea kufuatilia na kuhakikisha kwamba kila sehemu inayofanya uchimbaji iko salama. Lakini tunahitaji ushirikiano wa Halmashauri husika kwa kutumia sheria hii hii na kutumia kifungu cha 36 mpaka 41. Tukitumia vifungu hivyo tutashirikiana na tutaweza kuondoa tatizo hili. Tatizo hili haliwezi kutatuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais pekee. Lakini kwa kutumia sheria hii ambayo ina-*empower* hata Halmashauri zetu tutaweza kusaidia sana Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia ambalo Mheshimiwa amesema *twenty two billion* (22,000,000,000/=) kwa watu 474 alichosema na tulichoandika kwenye randama yetu ni kweli na alichosema Naibu Waziri wa Nishati na Madini ni kweli kwa sababu *at that time* kwa sababu hizi *compensation* ni *company and the person* wana-*negotiate* wanakubaliana. Kama utaangalia vizuri alisema kuna wengine wamekataa, *but time has changed*. Sasa *time* ikipita mazungumzo yakaendelea wakakubaliana na wakalipana hizo takwimu za sasa kwa nini unazikataa? *Is a fact, You can not be rigid*! Sasa kama ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Kitwanga, maarufu mawe matatu. Nafikiri na sisi kule Peramiho tutaanzisha mawe manne sasa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri, Daktari Huvisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Masuala ya Mazingira. Yeye pia atatumia dakika 15.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Vile vile nimshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunipa dhamana tena kusimamia masuala ya mazingira. Shukrani za pekee kwa Makamu wa Rais, Daktari Mohammed Gharib Bilali, kwa ushauri na miongozo anayotupatia mara kwa mara ili kuweza kutekeleza majukumu ya ofisi. Vile vile niwashukuru wapiga kura wangu wa UWT ambao wameweza kunifikisha mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee zimwendee Mama yangu mzazi, watoto wangu, ndugu na rafiki kwa kuniombea kila siku na hivyo kuniwezesha nizidi kupata afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja za Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambayo iliwakilishwa na Daktari Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum. Hoja ya kwanza ilisema kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha zitakazowezesha Ofisi ya Makamu wa Rais kutoa elimu, lakini vile vile bajeti iongezwe ili majukumu ya Baraza yaweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi itaendelea kuwasiliana na mamlaka husika ili kutenga fedha za kutosha katika Ofisi ya Makamu wa Rais na vilevile kuwezesha Baraza kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine Kamati inatoa ushauri kwa Serikali itumie utaratibu mzuri ili Mfuko wa Mazingira usimamiwe na watendaji waadilifu, makini na wenye weledi. Nitoe tu taarifa kwamba Mfuko huo tayari tumeshauzindua na tunahakikisha kabisa tunaweka watu maalum ambao wataufuatilia na kuutekeleza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kirekebishwe ili kutoa mamlaka ya Wizara husika kuajiri Wataalam wenye taaluma za mazingira kuwa waratibu wa mazingira na kusimamia kama inavyotakiwa. Tunazingatia suala hilo na Ofisi ya Makamu wa Rais itaandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mazingira ikiwa ni pamoja na kurekebisha kifungu Namba 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, Ofisi ya Makamu wa Rais ikutane na Halmashauri nyingi zaidi ili

ziweze kuhusisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo. Mkiangalia kile kitabu changu cha bajeti mwaka huu tumeongeza bajeti kwa ziara za ndani. Lengo ni kuweza kuzifikia Halmashauri nyingi zaidi na kutoa elimu zaidi ili ziweze kusimamia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, Ofisi ya Makamu iainishe maeneo ya kipaumbele na kutenga fedha za kutosha. Ushauri tunauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, Kamati inashauri suala la upandaji miti liwe kipaumbele hasa siku ya upandaji miti. Suala hili tunalizingatia, lakini vile vile tumeweka mkakati kwamba, pamoja na Halmashauri kupanda miti milioni moja na nusu (1, 500,000) kila mwaka, vile vile tunawasiliana na TAMISEMI upande wa elimu kuhakikisha kuwa shule zote za Kata kwa sababu Kata zote zina shule za *primary schools* na, *secondary schools* zishiriki zoezi hili la kupanda miti. Kama tutaweza kuhakikisha kila mwanafunzi wa *primary* na *secondary* anaweza kupanda miti angalau 10 kila mwaka tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwa sababu *primary schools* ziko pia karibu katika kila Kijiji, tunafikiria kila shule ipate chanzo kimoja cha kuhifadhi maji. Sasa tukifanya hivyo na kuwashirikisha wananchi tunadhani suala hili tutalitekeleza kwa uzuri zaidi kuliko ambapo sasa hivi tumesema Halmashauri tu. Lakini vile vile tunaomba Halmashauri kwa sababu ndizo zenye kazi ya kupanda miti ziandae vitalu vya kutosha

kuweza kugawa miche kwa shule zote za *Secondary* na *Primary School* ili kila shule iweze kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Kitaifa yafanyike katika mikoa ambayo iko nyuma. Hilo tunalizingatia kwa sababu mwaka jana tulifanya Mkoa wa Ruvuma na mwaka huu tumefanya Kilimanjaro kwa sababu ya Mlima Kilimanjaro, kila mmoja anajua ule mlima jinsi ambavyo tunauzungumzia. Kwa hiyo, tulitoa kipaumbele ili kuweka msisitizo katika kuhifadhi Mlima Kilimanjaro na namshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Kambi ya Upinzani ambayo iliwasilishwa na Mchungaji Peter Msigwa, hoja ya kwanza ilikuwa ni Serikali iandae mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na vile vile Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira imelisemea suala hilo. Napenda kutoa taarifa kwamba utekelezaji wa mradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi iko katika sekta mbalimbali kama Sekta ya Kilimo, Maji, Afya, Wanyamapori, Misitu, Mifugo na Ardhi na zimetolewa kwa kina katika kitabu cha hotuba yangu *paragraph* 88 na 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zinahusisha miradi ya majaribio katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya ya Mbinga, Igunga, Misenyi na Kaskazini A. Vilevile maandalizi ya mwongozo wa kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabia nchi katika sera, mipango na programu za Wizara za Kisekta na Serikali za Mitaa, maandalizi ya mwongozo wa tathmini

ya ufuatiliaji wa shughuli za kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Wilaya. Vile vile miradi na miongozo hii imelenga kuboresha juhudi za Serikali na jamii katika kuhimili mabadiliko ya tabia nchi katika sekta husika yaani kilimo, maji, afya, wanyamapori na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kambi ya Upinzani imezungumzia suala la Mkutano wa Rio + 20 na wametaka tueleze tumejiandaa namna gani. Labda kwa kifupi tu nieleze Rio + 20. Mkutano wa Kwanza wa Rio ulikuwa mwaka 1992 na baada ya Mkutano ule Serikali ilikuwa imejiandaa vizuri na ndiyo maana mwaka 1997 tulikuwa na Sera ya Mazingira kwa mara ya kwanza. Ilikuwa ni utekelezaji wa Rio ya kwanza. Vile vile Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ilizingatia utekelezaji huo pamoja na kuanzisha kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, yote hayo yalikuwa ni maandalizi. Kwa hiyo, sasa hivi huo Mkutano wa Rio + 20 ulikuwa unaangalia nchi mbalimbali zimetekeleza nini.

Sisi tulitoa taarifa ya mambo hayo niliyoyasema ambayo tumeyatekeleza, lakini pia miongozo tuliyopewa tutaendelea kuizingatia kwa kufuatia bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, kuanzia bajeti ya Serikali ya mwaka huu na miaka inayoendelea tutaendelea kufuatilia maagizo ya utekelezaji ya Rio + 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia imetaka Serikali kueleza kiasi cha fedha shilingi bilioni 178 za Halmashauri. Tunashukuru kwa taarifa hii na tutaifuatilia kwa sababu bila Halmashauri kutekeleza

masuala ya hifadhi ardhi pamoja na misitu nchi yetu itajikuta kwenye janga. Kwa hiyo, naahidi kwamba tutazifuatilia hizi fedha na kuangalia kwanza kwa nini hawajafanya, lakini pia kusisitiza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi ya Upinzani imezungumzia athari zinazotokana na uchimbaji wa madini nchini, tafiti mbalimbali zifanyike na pia wananchi wahamasishwe katika maeneo yao ya asili kupisha uchimbaji wa madini holela na vilevile kampuni za Madini kuwajibika kurekebisha mazingira baada ya kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba Serikali itoe ufafanuzi katika suala la fidia kwa kuainisha viwango. Suala lingine ni kwamba Serikali ijumuishe katika sheria ya nchi suala la ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa ujumla ni kwamba, tafiti zinazohusu mazingira kama zilivyo tafiti nyingine hufanywa na wataalam wanaoaminika na tayari Baraza limesajili hao wataalam katika uchimbaji wa madini mbalimbali. Hadi sasa jumla ya wataalam 125 wameshasajiliwa kwa mujibu wa taratibu za kanuni hizo. Miongoni mwa wataalam hao wapo wataalam waliobobea katika masuala ya uchimbaji madini na mazingira ambao hufanya tafiti hizo.

Ushauri huu utazingatiwa na suala la kampuni za uchimbaji madini kuwajibika pia katika tathmini huwa

wanapewa taratibu za kufanya baada ya kufungwa mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia, ninachoweza kusema ni kwamba, inapothibitika wananchi wameathirika na sumu zinazotokana na shughuli za uchimbaji wa madini sheria zinazingatiwa kuhusu suala la fidia na wale wote wanaoathirika wanapewa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa sera, sheria na taratibu zinazohusu uchimbaji wa *Uranium* tumeshafanya maandalizi. Serikali inatambua changamoto za uchimbaji wa *Uranium* na nimeielezea katika vifungu vya 156, 157 na 158 vya hotuba yangu katika ukurasa wa 101, lakini vile vile Tume ya Nguvu za Atomiki wameshaanza kuandaa kuanzisha Kituo cha Kupima Mionzi, Namtumbo. Kwa hiyo, hayo yote ni maandalizi pamoja na sheria na kanuni mbalimbali za nguvu za *Atomic* na nyingine zipo chini ya Wizara ya Nishati na Madini, zote hizo ni kwa ajili ya maandalizi.

Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja nao wameweza kuchangia nikianza na Daktari Kebwe S. Kebwe ambaye amezungumzia Magugupori yanayoishambulia Serengeti. Tunashukuru kwa taarifa hiyo na Baraza italifuatilia. Vile vile amezungumzia ukataji miti ambayo nimeshaeleza jinsi ambavyo tunaendelea kuweka mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mchungaji Luckson N. Mwanjale na Mheshimiwa Agnes Hokororo wamezungumzia utupaji wa taka na matumizi mabaya

ya matawi ya miti barabara. Elimu itaendelea kutolewa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri na hilo tunalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Andrew amezungumzia uchafuzi wa mazingira kutokana na ujenzi wa viwanda, tatizo hili linajitokeza kutokana na ujenzi holela usiozingatia mipangomiji au kutokuwepo kwa mipangomiji inayotenganisha maeneo ya makazi na yale ya viwanda. Lakini la msingi, tunawaomba wananchi wasiweze kuuza maeneo yao holela kwa viwanda kwa sababu unakuta kiwanda sasa kinakuwa katikati ya watu. Kwa hiyo, tunaomba sana watu binafsi wasiuze maeneo kwa viwanda au wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cecilia D. Pareso amesema Baraza kuwezesha zaidi kufanya ukaguzi katika maeneo. Ushauri huo tunauzingatia, lakini pia Serikali imetunga kanuni ya tozo ya mwaka 2008 inayowataka wenye miradi kulipa tozo ya kila mwaka ili kuchangia gharama za ukaguzi. Tozo hizo zitatuwezesha kufanya ukaguzi mara kwa mara.

Mheshimiwa Aliko N. Kibona yeye anazungumzia uchafuzi unaotokana na matumizi ya *plastic*. Nimeshaelezea hayo katika ukurasa wa 74 aya ya 114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallack naye anazungumzia uharibifu unaotokana na wachimbaji wadogo wadogo. Kinachohitajika ni elimu na tutaendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Israel Y. Natse amezungumzia uharibifu wa chanzo cha maji kwa *DED* Karatu. Tunaomba uzungumze na Halmashauri ya Wilaya ili utekelezaji ufanyike na sisi tutafuatilia.

Mheshimiwa Agness Hokororo amezungumzia pia uchafuzi wa Jiji la Dar es Salaam na majiji mengine. Lakini nitoe tamko kwamba nawashukuru Wakuu wa Mikoa wote kwani kwa kiasi kikubwa wameweza kuendeleza hili zoezi la usafi, lakini naomba tushirikiane nao ili tuweze kuendelea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa msitu wa Shengena. Tatizo hili Baraza imelifuatilia kwa karibu sana na tuligundua kuna makampuni matatu, kampuni ya *Wiley Enterprise*, *Mamuya Partners* na *Amanyambo Enterprise* na Baraza lilianza kufuatilia mwezi Januari 2012 kwa sababu uchimbaji ule ulianza bila tathmini Baraza lilitoa agizo kwamba wafanye tathmini ya mazingira ili wapeleke kwenye Baraza lakini hawakufanya hivyo, kwa hiyo, mwezi Juni mwanzoni Baraza lilikwenda tena na kutoa katazo na sasa hivi wale wote wamekatazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni kengele ya pili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Vile vile nimewasiliana na Mheshimiwa Mbunge Anna Malecela Kilango na baada ya hapo tutakwenda kufuatilia huo uchimbaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hiyo ni kengele ya pili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumalizie na mtoa hoja ambaye ni Mheshimiwa Samia ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais lakini anayeshughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Samia!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutumia muda wetu leo kuzungumzia hoja hii.

Nichukue nafasi hii kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati kwa kuchambua hoja yetu na kutoa maoni na hoja ambazo walitaka Serikali izifanyie kazi. Lakini pia kwa hatua hiyo hiyo niwashukuru sana Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani na wenyewe wametoa maoni yao na kutaka Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge waliochangia hoja hii kwa kusema ni Wabunge 14 na

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba sasa nianze kuwataja waliochangia kwa kusema ambayo ni Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mheshimiwa Daktari Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Shawana B. Hassan, Mheshimiwa Daktari Dalali P. Kafumu na Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse. (*Makofi*)

Pia, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Nasseb S. Omar, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Chiligati, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Frederick M. Werema ambaye ni Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Charles Kitwanga ambaye ni Naibu Waziri na Mheshimiwa Terezya L. Huvisa ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Charles J. Mwijage, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Daktari Christine G.

Ishengoma, Mheshimiwa Daktari Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Rashid A. Abdallah, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Leticia Nyerere mara mbili, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Daktari Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Hamad A. Hamad. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Mchungaji Daktari Getrude P. Rwakatale, Mheshimiwa Yussuph Haji Khamis, Mheshimiwa Abdallah Haji Ally, Mheshimiwa Ally Juma Haji, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Ameir, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mheshimiwa Anna Marystella J. Mallack, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa Felister A. Bura na Mheshimiwa Margaret S. Sitta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine ni Mheshimiwa Kheri Khamis Ameir, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Cecilia D. Pareso, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ally, Mheshimiwa Suleiman Said Jafo, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Agness E. Hokororo, Mheshimiwa Amina A. Clement, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Waride Bakar Jabu, Mheshimiwa Juma Athman Ally, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Mohamed

Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Daktari David M. Malole, Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Mheshimiwa Ally Khamis Seif, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba na Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Daktari Seif Said Rashid, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Daktari Dalali P. Kafumu, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, Mheshimiwa Thuwayba Idriss Mohamed, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Daktari Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine ni Mheshimiwa Daktari Anthony Mbassa, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Engeneer Ramo Makani, Mheshimiwa Idd Azan, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Hadhi Juma Maalim, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Pereira Silima, Mheshimiwa Abdallah Juma Abdallah, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutaja majina hayo, sasa naomba niingie katika ufafanuzi wa hoja na naomba nianze na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo imetoa maoni yake na imegusia maeneo mengi ila walihimiza tu kwamba ufumbuzi wa matatizo ya Muungano ufanywe kwa haraka, lakini pia walisisitiza suala la kufanyiwa kazi kwa ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walitaka kuharakishwa kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha. Nataka niseme hili lipo ndani ya mikono ya Wizara ya Fedha na tulishawaandikia na tutachukua hatua ya kuwakumbusha ili wafanye marekebisho ya Sheria ya Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia walitaka elimu kwa Muungano iendelee kutolewa, tunakubali kufanya hivyo. Lakini pia suala la wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, suala ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alilisema hapa na kueleza kwamba wamepania au wamedhamiria kulikamilisha suala hilo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye hoja za Kambi ya Upinzani na hapa nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Ndugu yangu Tundu Lissu, amefanya utafiti wa kina hasa wa Mheshimiwa Issa Shivji kwamba ilikuwa ndiyo *main reference*. Lakini nataka niseme kwamba, nilidhani Kambi ya Upinzani wangeifanyia uchambuzi hotuba ya bajeti ya Idara ya

Muungano, lakini kwa bahati mbaya kilichotokea ni kujadili vifungu vya Katiba na marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, katika yaliyozungumzwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani labda la kwanza ambalo nataka ku-*comment* ni lile la kusema kwamba Waziri wakati wa hotuba yake hakutaja changamoto zinazowakabili katika Muungano. Nataka kusema kwamba changamoto katika ukurasa wa 22 *paragraph* ya 37 zimetajwa, inawezekana kabisa labda hazikutajwa zile ambazo msemaji alitegemea kuziona, lakini hapa tumetaja zile ambazo tunakumbana nazo katika kufanya kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani pia kulikuwa na vipengele kadhaa ambavyo vilitakiwa Serikali itoe maelezo, lakini sidhani kwamba maelezo haya tunaweza kuyatoa hapa kwa sababu hapa ni kikao cha kujadili bajeti na siyo kikao cha kujadili marekebisho ya Katiba au vifungu vya Katiba. Kwa maana hiyo, nitafanya dondoo moja moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifanye dondoo katika kifungu alichokitaja cha 123 cha Katiba mpya ya Zanzibar kwamba kwa nini SMT imeruhusu Zanzibar kujinyakulia madaraka juu ya mambo ya Ulinzi na Usalama. Namuomba Msemaji arudie Ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba hakuna ruhusa mtu yeyote kuunda vikosi vya ulinzi isipokuwa Serikali na Serikali imeelezwa katika ngazi tofauti tofauti. Lakini ukienda kwenye tafsiri ibara ya 151 neno Serikali ni Serikali ya

Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, ina haki ya kufanya vikosi hivyo.

Lakini ukiacha hilo ni kwamba kwa sasa hivi kuna mashirika ambayo yanaunda vikosi vya Ulinzi, mimi nalindwa na Kigeni *Security Game,* kuna *Ultimate Security* na kadhalika na vikosi hivi vingine wanashika silaha kabisa. Sasa je, Zanzibar kulinda *territorial* mipaka ambayo Zanzibar inaizunguka nadhani si jambo baya na wala hawakuvunja Sheria katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo Msemaji wa Kambi ya Upinzani alitaka litolewe ufafanuzi ni kuanikwa kwa hizo nyaraka za Muungano wakati huo zilisainiwa, nadhani Mwanasheria Mkuu amelizungumza vizuri suala hili.

Mengine yote ambayo yameelezwa kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ningependa sana kuyajadili, lakini siyo hapa. Napenda kuwa *discussant* wa *paper* hii nje ya muda huu wa kuzungumza makisio ya bajeti na matumizi kwa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa katika hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyowataja Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia hoja nyingi lakini yote waliyoyataja nimeyagawa katika mafungu matatu. Kwanza kuharakishwa kwa kero za Muungano, lakini lingine ni elimu kwa umma kuhusu Muungano na maswali mengine madogo madogo kama Zanzibar kujiunga na *OIC* na mengine ambayo nitayataja kwa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla nataka niseme kwamba, kama nilivyotoa ufafanuzi juzi wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu kwamba utekelezaji wa kero za Muungano tunajitahidi, katika 15 tumeshafanya tisa (9) na nyingine sita (6) zilizobaki zipo kwenye hatua nzuri. Kama nilivyosema nyingine tunategemea ufafanuzi wake uletwe hapa, lakini nyingine tunaendelea nazo polepole kama Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha walivyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kufanyiwa kazi kwa Tume ya Pamoja ya Fedha. Nadhani Wizara ya Fedha walishaji–*commit* hapa kwamba sasa wako tayari kuyafanyia kazi matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala mengi yalikuwa ni kuhimiza utekelezaji wa Kero za Muungano, masuala ya ajira katika utumishi wa Muungano ambayo nayo *report* yake tutaileta karibu na mengi ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, kuna Waheshimiwa kama sikosei Mheshimiwa Shawana na Mheshimiwa Pareso, walisema basi kile kilichofanyika na yale yaliyobakia yaletwe rasmi Bungeni. Nataka nichukue ahadi kwamba nitafanya hivyo, tutakwenda kuandika waraka na tutauleta rasmi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hayo ndiyo yaliyochangiwa, kero, hati za Muungano, lakini pia kuna hili ambalo amelichangia Mheshimiwa Clara

Diana Mwatuka kwamba matumizi ya majengo ya Muungano na yeye alizungumzia kuhusu jengo la Bunge, Zanzibar kwamba halitumiki na wakati mwingine vikao vinafanywa katika kumbi za kukodi lakini kumbe wangepelekwa Zanzibar wangefanyia kwenye jengo lao. Kwa hiyo, hilo nalo nadhani Ofisi ya Bunge wamelisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine ambayo yapo *specific* kuna mmoja ameulizia itifaki ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Hadhi ya Rais wa Zanzibar kwamba imeteremshwa, *again* ni masuala ya marekebisho ya Katiba. Niwaombe tu ndugu zangu Wabunge kwamba tuitumie nafasi hii ya marekebisho ya Katiba kuweka yale ambayo tunaona yana kasoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo *specific* kwa Mheshimiwa Kahigi, yeye alisema pamoja na yote aliyoyasema, lakini alisema matumizi ya neno Tanzania Zanzibar na Tanzania Visiwani yamekuwa yamependekezwa muda mrefu, lakini hayajashika mashiko. Sasa hili naomba nitoe ufafanuzi kwamba tu ukisema Tanzania Visiwani kwa maana ya Zanzibar, Tanzania Visiwani inajumlisha Visiwa vingi ikiwa ni pamoja na Ukerewe na Mafia na kwingineko. Kwa hiyo, ukisema Tanzania Visiwani kidogo inaleta utata. Lakini nataka nimhakikishie kwamba neno Tanzania Zanzibar hili linatumika sana, sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la Mheshimiwa Nassibu ambaye amesema katika kueleza basi mafanikiko na changamoto tutaje basi viongozi waasisi

wa Muungano. Niseme tu kwamba tunalichukua, hotuba ijayo tutaanza na dibaji hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali au hoja Sylvester Mabumba na naomba niombe radhi kwamba sikumtaja kwenye *list* na amechangia kwa maandishi. Hoja yake alikuwa anaulizia je, ni lini Serikali itasaidia Makanisa yaliyochomwa na wafuasi wa Kikundi cha Uamusho kule Zanzibar. Nataka niseme tu kwamba kitakachofanywa na Serikali hapa ni kuwachukulia hatua wale waliofanya uovu huo. Lakini sioni kwamba Serikali inapaswa sasa kulipa fidia kwa tendo lililofanywa na waovu labda ni hao waovu kulazimishwa kulipa wao fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine alisema kwamba niliambie Bunge lako Tukufu kwa nini Serikali ya Zanzibar haijawachukulia hatua kali. Nina hakika hatua kali zimechukuliwa kwa hao waliohusika, sasa kama ni kali au ni nyepesi nadhani ni muono wa mtu, lakini hatua zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo Mheshimiwa Sylvester ametaka kujua ni lile ni hatua gani zinachukuliwa kwa kulinda wananchi wenye asili ya Tanzania Bara wanaoishi Zanzibar ambao kwa sasa wananyanyasika sana huko Zanzibar hata kunyimwa haki za ajira, kumiliki ardhi, uhuru wa kuabudu, nafasi za masomo ya juu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nilimuuliza ndugu yangu Sylvester nilijibu akaniambia nilijibu. Nataka niseme kwamba yeye mwenyewe ndugu yangu

Sylvester Mabumba ni mfano wa hili kwamba yeye amepata kusoma akiwa Zanzibar na sasa ana *hold Masters Degree* ya *Economics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, ana ardhi kule alikotoka, Jimboni kwake amejenga nyumba yake na ana ardhi kwa ajili ya kilimo na kwa upande wa ajira, Mheshimiwa Sylvester aliajiriwa, mimi nikiwa *Manpower Planning Officer* pale Wizara ya Mipango na amepanda mpaka alipofika. Kwa hiyo, na *scholarship* ndiyo hizo amepata. Sasa huu unyanyasaji wa juzi kwa Uamsho kuleta vurugu sidhani kwamba unafaa ku-*generalize* kwamba Watanzania Bara walioko Zanzibar wananyanyasika. Kuna Watanzania Bara wanaishi vizuri kabisa na wako *very happy* na wala hawana haja ya kurudi walikotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa mujibu wa Kanuni sasa tutaendelea na hatua inayofuata.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Bunge limeingia katika hatua ya Kamati Matumizi ili tuweze kupitisha mafungu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

## FUNGU 26 - MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 - *Administration and HR Managt. ... ... Shs.* 4,653,309,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felix Mkosamali tumemaliza. Haya Mkosamali naomba muwe *sharp* jamani.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahoji *Vote* 26, kasma 210100, *Basic Salaries*, nimesoma nimeona fedha zimeongezeka sana za mishahara karibu milioni 129 na ukisoma kwenye randama inaonekana kwamba mtumishi aliyeajiriwa ni mmoja tu. Sasa nataka kupata ufafanuzi huyo mtumishi analipwa kiasi gani kutokana na ongezeko hilo maana ni mmoja na fedha zilizoongezwa ni nyingi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo linajumuisha nyongeza ya mishahara na ajira mpya kwa sababu majengo mawili Dar es Salaam na Tunguu yamekamilika na tunategemea tuanze kuyatumia mwaka huu. Kwa hiyo, hizo ni ajira mpya zitakazohusisha hayo majengo mawili Dar es Salaam na Tunguu Zanzibar.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 31 - OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 – *Administration and HR Managt ... ..Shs.* 2,280,338,000/=

**MWENYEKITI:** Tutaanza na Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua Wizara inashirikiana vipi na Wizara ya Uvuvi katika suala nzima la uhifadhi wa mazingira baharini hususan katika ukanda wa Bahari ya Hindi unaojumuisha maeneo ya Jimbo langu la Mchinga kwa sababu wale wananchi wamekuwa ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda kifungu gani?

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Fungu gani?

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 1001.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda naomba ukae kwanza. Waheshimiwa Wabunge, naomba mfanye maandalizi vizuri tumeshakuwa wazoefu sana wa kutumia hivi vitabu. Kwenye kifungu 1001 pale hakuna mshahara wa Waziri. Kifungu 1001 lile ni fungu la jumla na pale chini kuna zile *sub-vote*. Kwa hiyo, Mbunge anapotaka kujikita atumie zile *sub-vote* na aeleze moja kwa moja anakwenda wapi? Kwa hiyo, nitamwita anayefuata Mheshimiwa Sanya. Ama umeondoa jina.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 210100.

**MWENYEKITI:** Hapa hakuna Mshahara wa Waziri, mshahara wa Waziri tumemaliza katika fungu lililopita. Hili fungu halina mshahara wa Waziri, lile fungu tulilomaliza ndiyo lina mishahara wa Mawaziri. Hapa tunaingia moja kwa moja kwa Makamu wa Rais.

Sasa sijui kama ni mshahara wa Makamu wa Rais. Sasa kuna *sub-vote* nyingine ama na wewe unataka mshahara wa Waziri hapo hapo. Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Mnyaa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, ngoja tuendelee nitaita mmoja, mmoja. Wewe si umejiorodhesha hapa, tunaendelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika hatuna taarifa hapa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Fungu 26 lilikuwa ni Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika naomba ukae kwanza. Haya Leticia Nyerere.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze nini tofauti kati ya kasma hizo mbili?

**MWENYEKITI:** Nimekuelewa Mheshimiwa. Haya Mheshimiwa Waziri tofauti ya kasma hizo mbili ni nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ya *hospitality* inahusu *food refreshment* na gharama zimepanda ni kwa ajili ya Ofisi zote, Mawaziri tupo watatu. Halafu hiyo nyingine ya *other supplies and services* kuna mambo ya *sundry, barrier* na kuna mambo ya *fumigation, up keep maintenance*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christowaja. Mheshimiwa Rajab hukusimama mwanzo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama mwanzo na ulinitaja mtu wa mwanzo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rajab mwanzo hukusimama. Aliyesimama mwanzo alikuwa Mheshimiwa Sanya. Mheshimiwa Christowaja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba swali kwenye kifungu 1001, kasma ya 210100. Katika mchango wangu wa maandishi nilichangia kuhusu masuala ya Muungano; nilisema kwamba Tanzania Zanzibar inawakilishwa na Wabunge 50 wa Majimbo, ina Wabunge wa Viti Maalum, ina Wabunge wa kuteuliwa na pia ina Wabunge wa Baraza la Wawakilishi ambao wanashiriki katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo wanalinda maslahi ya Zanzibar. Lakini nilipenda

kwamba kwa nini Bunge la Jamhuri ya Muungano upande wa Bara halipeleki angalau Wabunge watano kwenye Bunge la Baraza la Wawakilishi ili kuwasilisha maslahi ya Tanzania Bara na ndiyo maana tumeona matatizo ya Katiba ya Zanzibar jinsi ambavyo imeweza kukiuka hati za Muungano. Kwa hiyo, nataka kupata ufafanuzi kwa nini Zanzibar inawakilishwa Wabunge hapa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Tanzania Bara hawawakilishwi kwenye Baraza la Wawakilishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa ndugu yangu Christowaja angeniambia kifungu gani anachozungumzia. Lakini la pili, hayo ni maamuzi ya Bunge kwa sababu wamekuja kwa sheria ya Bunge na ni matakwa ya Kikatiba. Kwa hiyo, kama kuna muono mwingine wowote nafasi mzuri ipo, tunaomba atoe maoni yake. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Fungu 31, *programme* 10, kifungu 1001, kasma 210100, ningeomba kupewa ufafanuzi kuhusu jambo la kisera linalohusu mazingira na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ninukuu Ibara ya 99 ya Katiba ya Jamhuri ya

Muungano ya Tanzania, inasema: “Bunge halitashughulikia jambo lolote kati ya mambo yasiyohusika na Ibara hii isipokuwa kama Rais amependekeza kwamba jambo hili lishughulikiwe na Bunge na pendekezo hilo la Rais liwe limewakilishwa Bungeni na Waziri na mambo yasiyohusika na Ibara hii ni yafuatayo:- Muswada wa Sheria kwa ajili ya jambo lolote kati ya mambo yafuatayo:- Kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna yoyote nyingine isipokuwa kupunguza.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna jambo lilijitokeza kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani na kwenye mchango wangu juu ya athari za uharibifu wa mazingira kutokana na kupandishwa kwa kodi kwenye mafuta ya taa na kuna kauli ilitolewa kwamba jambo hili limefanywa na Bunge. Lakini ukiangalia Ibara hii ya Katiba pendekezo la kupandisha kodi linaanzia kwa Serikali, linapitishwa kwa Bunge lakini linakwenda kuridhiwa na Mheshimiwa Rais.

Ningependa kupata ufafanuzi tu wa kisera kwa kuwa, Kamati Kuu ya Serikali ilitangaza kwenye Vyombo vya Habari kwamba uamuzi huu haukuwa sahihi. Je, Serikali sasa ipo tayari kukubaliana na mapendekezo ambayo tumeyatoa mara kadhaa kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha urudishwe na gharama za kodi kwenye mafuta ya taa zipunguzwe ili kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi, lakini kuepuka vilevile uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya mkaa hasa Dar es Salaam?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kwa mujibu wa Kanuni 104(1), naomba nitumie mamlaka yangu kuongeza muda angalau nusu saa ili tuweze kuendelea na kazi hii. Sasa Mheshimiwa Waziri hili swali kwa kweli, sasa hizo taarifa za Kamati Kuu sijui Mheshimiwa Mnyika amezipataje. Lakini Mheshimiwa Waziri nisikujibie ujibu mwenyewe. Anajibu nani? Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Mnyika kwamba maamuzi ya Bunge ni ya Bunge ndiyo sababu huwa hatukai humu kama Chama. Maamuzi ya Chama yalikuwa yanashauri Wabunge wa CCM, lakini maamuzi halali yaliyopitishwa, yalipitishwa na kikao cha Bunge kihalali kabisa, naomba itambulike hivyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Naomba uende moja kwa moja kwenye fungu na kwenye hoja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Sina fungu ila naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Hatuna mwongozo kipindi hiki jamani Mheshimiwa Mnyaa, mbona mnajua Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Natse!

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhoji vote 31, *programme* 10 *sub-vote* 1001, kasma 210100. Katika mchango wangu nilihoji uharibifu wa mazingira mkubwa unaofanyika katika Mgodi wa dhahabu pale Mweusi Mwendamashi, Karatu; sikupata kauli ya Serikali na hatua ambazo Serikali inachukua kuokoa mazingira yale.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA)** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu tulikuwa nayo lakini muda haukutosha.

**MWENYEKITI:** Naomba uende kwenye jibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni kwamba, Baraza limepokea hiyo taarifa kwa mara ya kwanza tutalifuatilia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanya.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunikumbuka na kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi narejea tena kwenye kauli aliyoitoa Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Naomba utuelekeze kwa kifungu. Mheshimiwa Kifungu gani?

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA**: Cha Mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Wewe soma kifungu tu hapa tutapeana maelekezo.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** *Sub vote* 210100. Tayari sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *don't take by Surprise* unajua tena kama huna uzoefu. Nasemaje kuhusu habari ya *change* ya Rada. Rada bado ni chombo cha Muungano ukichukua sehemu yoyote ile. Kama utakwenda kwenye ulinzi ni ya Muungano, ukienda *Metrology* unakwenda kwenye Muungano, ukiwa kwenye Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni chombo cha Muungano. *Change* iliyorejeshwa imerejeshwa kwa ajili ya Tanzania. Tanzania ni Jamhuri ya Muungano wa nchi mbili Tanzania Bara na Zanzibar, haikusema kwamba inarejeshwa Tanzania Bara. Hilo moja.

Kama kuna...

**MWENYEKITI:** Ni moja tu Mheshimiwa Sanya.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Naelezea bado, hilo hilo na kama kuna matatizo kwamba Zanzibar haikushirikishwa haikutoa fedha ya kununua hicho chombo, sio makosa ya Zanzibar ni makosa ya waliokinunua. Lakini kinapoingia katika sehemu ya Muungano kinabakia kwamba ni cha Muungano. Hapo hapo kama ukiangalia leo unaweza ukasema

silaha nyingi zinanunuliwa na upande wa Bara. Je, unaweza ukasema wakati wa vita, wakati wa lindo Polisi utamwambia kwamba usichukue bunduki kwa sababu Serikali yako haikushiriki katika kutoa fedha za kununulia silaha hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna kifungu ambacho kinahusikana na rada kwenye kitabu hiki. Ukweli ni kwamba *of course* rada ni suala la Muungano, lakini fedha yule aliyelipa si ndiye anarudishiwa fedha kama aliyekopa ndiye anarudishiwa fedha. Sasa hili lisitutenganishe sisi ndugu wa Tanzania Bara na ndugu wa Tanzania Visiwani kwa sababu hili linaweza kushughulikiwa kwa njia nyingine kama ni fedha tukazungumza na tukapeana, lakini sio suala la kukunjiana uso.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye *Vote* 31, *sub vote* 1001, Kasma 210500.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninachotaka kuangalia hapa kwamba hizi fedha zinavyoonyesha *trend* yake inapanda na kushuka mwaka hadi mwaka. Lakini kwa kuangalia Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu amesema kwamba tunafikiria kufanya *research* zaidi kwenye *genetically modify organs.* Huu utaratibu hautufai kwa sababu *organical food* ni *affordable* na ndiyo ambayo ina ubora katika nchi zote duniani. Kwa nini tunataka kuingia kwenye *genetically engineered food*. Hili sio jambo jema na sio jambo ambalo linakubalika. Nchi kama Marekani ambao ndio

wakulima wameanza hii na wanaona kwamba wanafeli sasa hivi kwenda kwenye hizo *non organic food*. Kwa hiyo Serikali kama mmetenga fedha hizi basi ziwe *allocated* kwenye mambo mengine muhimu kuliko kuingia katika hilo.

**MWENYEKITI:** Ni fedha gani hizo unazozihoji Mheshimiwa?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Hiyo *sub vote* 210500 ambazo ni *allowances.* Sasa nimezi-*treat* kwamba pengine zinatumika kwa ajili ya hizo *research* ambazo zinafanyika.

**MWENYEKITI:** Haya majibu Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *sub vote* haihusiani na *research* kabisa. Lakini kwa kumtoa woga tu Mheshimiwa Mbunge nimesema na nimejibu nikisema kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais itakwenda pole pole kwa kufanya *research* katika hayo mambo ya GMO. Ni kwa sababu tunatambua tatizo, tunajua madhara yanaweza kutokea, lakini hatuwezi tukakaa nyuma bila ya kufanya *research* na sisi tuwe tayari pale ambapo tutaona kwamba inafaa kuingia katika mbegu za namna hiyo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote* 31 program 10 *sub vote* 1001 na *item* 210100, Mshahara wa Waziri lakini sina haja ya mshahara wake, nataka tu ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema siungi mkono hoja hii kwa sababu ya mambo mawili. Moja ni hili la kuhusu uanzishwaji wa Mfuko wa Pamoja wa Fedha ambao niseme kwa aibu kubwa umechukua miaka mingi wakati Serikali zote mbili ni za CCM, inatia aibu kweli.

Sasa Mheshimiwa Waziri ametoa jawabu la mkato kwamba wameshapeleka Wizara ya Fedha na majibu hayo yanatolewa miaka yote. Sasa tutegemee nini? Tutegemee yale yale yaliyokuwa yakitendeka kwenye miaka ya nyuma au kuna mabadiliko katika hili. Kwa sababu msimamo wa Wizara ya Fedha inapokea lakini haifanyi lolote. Hapa kuna matatizo ya utendaji kati ya Serikali mbili. Naomba maelekezo kama kuna nia sahihi ya kuleta marekebisho, sawa. Kwa kweli niendelee na msimamo wangu kwamba siungi mkono hoja hii. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hii hoja inashughulikiwa na Wizara ya Fedha, lakini kuna hatua imeshapigwa tayari kwamba waraka ule umeshajadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu na sasa uko mikononi kwa *Cabinet Secretariet*. Kuanza leo tarehe 04, 05 na 06 Julai, 2012 Mawaziri *Cabinet* tunakaa hapa Dodoma. Kwa hiyo *hopefully* ni katika siku hizi huu Muswada pamoja na ule Muswada wa Kodi za Watumishi wa Taasisi za Muungano na *Withholding Tax* yote italetwa na vitazungumzwa. Kwa hiyo, hatua imeshapigwa tayari.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naenda moja kwa moja katika *sub vote* 210100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu uchafuzi wa mazingira na nimesikitika sana Serikali kusema kwamba uchafuzi wa mazingira ulitokana na kuvuja kwa zile tindikali kuwa-*affect* wananchi wa Nyamongo na mimea na kuna tafiti zingine zimefanywa na wanasayansi na zinaonesha kuna madhara. Lakini baada ya uchafuzi wa maji, pia kuna uchafuzi wa kelele kwa maana ya *noise pollution* na kuna uchafuzi wa *air pollution* kwa maana ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Serikali imeshafanya jitihada gani au tafiti zipi kujua ni kwa kiasi gani wananchi wa Nyamongo wanaozungukwa na mgodi wa *North Mara* wanaathirika na shughuli za ule mgodi mpaka sasa hivi na wakituonesha hizo tafiti zao. Pia ningependa kujua wale watu watakuwa *compesated* vipi maana yake wameathirika na kuna wengine mpaka wamekuwa viziwi kwa sababu ya kelele zile za mgodi.

**MWENYEKITI:** Maswali yako matatu Mheshimiwa Waziri utajibu moja kwa mujibu wa kanuni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Matiko na tumekubaliana kwanza niseme kwamba tutakwenda kutembelea Tarime yeye pamoja na wataalam kuhakikisha kwamba zile ahadi zote

zilizotolewa na Mwekezaji kama zinatekelezwa na nimemwonesha orodha yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *pollution* ya hewa. Katika hotuba ya Wizara yetu imeelezwa wazi kabisa kwamba kuna kanuni (*regulations*) ambazo tayari ziko mbioni kukamilishwa ili tuweze kuhakikisha kwamba watu wote wanazifuata kuweza kuhakikisha kwamba watu hawapati madhara.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo mtakwenda pamoja na wewe mwenyewe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Ndiyo na mimi mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Ukiambatana na Mheshimiwa Matiko?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Aaah! Sio na Mheshimiwa Matiko. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tumekuelewa Mheshimiwa Naibu Waziri, tunawatakia safari njema na utatuzi bora kabisa wa tatizo hilo.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami natumia *Vote* ya 31, programu ya 10, *sub vote* 1001, kasma 210100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kumekuwa na tatizo hususan kwenye Serikali za Mitaa katika Sheria Ndogo za Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira hasa hasa katika kusimamia utekelezaji wake ama *enforcement*. Kwa mfano, mtu anapochafua mazingira labda mtu amekwenda kujisaidia kichakani, mgambo hawezi kumkimbiza hususan akiwa mtoto wa kike anaweza akasingiziwa amebakwa. Lakini hata kwa wenzetu wa magari, mgambo hawezi kuona gari zima watu wametoka kuchimba dawa akasema awakimbize.

Sasa nilitaka *commitment* ya Waziri kwamba je, yuko tayari kukaa yeye na Waziri wa Serikali za Mitaa na Waziri wa Mambo ya Ndani kuhakikisha kwamba kunafanyika *enforcement* ya kutosha ya *Local Government Subsidiary Legislation* ili sheria hizi ziwe na tija kwa wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge Sabreena kama ifuatavyo:-

Sheria za usafi wa mazingira katika Serikali za Mitaa kwanza zinatungwa na Serikali za Mitaa zenyewe na wanapendekeza adhabu gani watatoa kwa mtu atakayevunja zile sheria. Kwa hiyo usimamizi wa sheria za usafi wa mazingira uko chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa inayohusika ambayo kama ni kule Kigoma basi na yeye Mheshimiwa Mbunge naye anakaa katika Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ziko Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafanya vizuri sana katika usimamizi wa usafi wa mazingira. Mwanza kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, wameshinda hata mashindano ya Bara la Afrika katika usafi wa Miji. Udhaifu tulionao ni baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa na sheria lakini kutoisimamia ile sheria. Nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu suala la usafi wa mazingira, lakini pia kuwataka Waheshimiwa Madiwani ambao wamependekeza sheria zile basi wahakikishe kwamba zinatekelezwa kama walivyozitunga na kukubaliwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujikwaa si kuanguka. Maelezo ya Mwanasheria Mkuu leo ni ya hekima na yameleta...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa kifungu gani?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Fungu hilo hilo nililosimama mwanzo 210100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli angalau nimeridhika kidogo kwa busara alizozitumia Mwanasheria Mkuu, lakini nataka ufafanuzi na kwa ushauri huu ninaotaka kuutoa. Baada ya ku-*sight* vipengele vyote vya Katiba kuhusu hii fedha ya rada na baada ya majibu yaliyotoka kule, na baada ya msimamo wa Serikali ya Zanzibar aliyotoa Waziri kule anayehusika. Sasa kero hizi nyingine za Muungano *solution* yake ni majadiliano ya Katiba mpya. Lakini

kero hii ya rada na sasa naongeza na fedha za *EPA* zinahusika. Je, Mheshimiwa Waziri unayehusika na mambo ya Muungano uko tayari kuichukua sasa uwe ni mjadala wa mwanzo wa kero ya kutafutiwa suluhu *immediately* kwa sababu hili ndio limetukera kwa muda huu huu haliwezi kusubiri mabadiliko ya Katiba?

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo sasa ni lipi, ni hilo la kwanza au ni hilo la pili. Nafikiria sasa tunahamia kwenye *EPA*. Ni moja tu Mheshimiwa Mnyaa. Haya utajibu unalolipenda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Ofisi yangu huwa inapokea kero za Muungano kutoka Serikali zote mbili. Aidha, Serikali ya Muungano au Serikali ya Zanzibar. Sasa kama itawasilishwa na Serikali ya Zanzibar tutaipokea na kwenda nayo kama kero.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts... ... ... ... ...*Shs. 271,340,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 230400, *Routine Maintenance and Repair of Vehicle and Transportation Equipment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuhoji *vehicles* na *transportation equipment,* lakini baadaye nikagundua

kwamba kwa kuwa ziko kwenye kasma moja Mheshimiwa Waziri hana sababu ya kutoa maelezo ya tofauti ya mambo haya mawili *vehicles* na *transportation of equipment.*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo hakuna swali? (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Leticia ebu naomba tuheshimu taratibu za Bunge. Kama huna maswali kwa nini unatumia muda wa Bunge kimchezo namna hiyo Mheshimiwa Leticia.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijagundua kwamba ni kasma moja. Samahani sana.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza kasma 220900, *training foreign.* Nimeona kwamba hizi fedha ambazo zimetengwa kwa mwaka huu 2012/2013 ni ndogo sana shilingi 2,000,000/=. Nilitaka kujua je hizi shilingi 2,000,000/= zinatosha kusomesha watu nje ya nchi au ni makosa ya kiuchapaji. Kwa sababu kwa maoni yangu ni kwamba ni fedha ndogo sana. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na ukomo wa bajeti hatutapeleka mfanyakazi kusoma nje isipokuwa zimewekwa kidogo kwa ajili ya *upkeep* ya wale walioko kule nje.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning Division... ... ...* ...Shs. 728,022,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit...* Shs. 220,817,000/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit... ... ... ... ... ... ...*Shs. 170,948,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit... ...* Shs. 169,266,000/=
Kif. 1007 - *Information and Comm. Techn. Unit...* Shs. 97,980,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit ... ... ... ... ...* Shs. 82,510,000/=
Kif. 2001 - *Union Secretariat ... ... ... ...* Shs. 33,301,101,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Environment ... ... ... ... ... ... ... ...*Shs. 5,372,218,000/=

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo kwenye programu ya 50 *sub vote* 5001, kifungu kidogo cha 270800 (*Current Grant to Non Financial Public Units (General).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nipate ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, wakati nachangia nilizungumza kwamba ukikata mkaa ni biashara, yaani ni ajira. Sasa sijui kifungu hiki kama kinaweza kikawapa mbadala wa ajira wale wakata

mkaa kwamba watakapokuwa wanakata mkaa, lakini bado kifungu hiki kiwawezeshe kuweza kutunza mazingira kwa ajili ya kupanda miti pale wanapokuwa wamemaliza kukata mkaa. Naomba ufafanuzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kifungu hicho kina kazi gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni pesa zanazopelekwa kwenye Baraza la Hifadhi yaani *NEMC*.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niende moja kwa moja kwenye kasma ya 221600 kwenye *printing advertising and information supplies and services*. Kuna usemi unaosema kwamba information is power. Sasa hapa tunasema kwamba, tunataka Watanzania wapate elimu ya mazingira, lakini tukiangalia *source of information* kwa mwaka jana, tunaona kabisa waliwekewa milioni 12/=, lakini mwaka huu wamewekewa milioni 3/=. Nataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kweli milioni 3/= itaweza kufanya kazi hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukomo wa bajeti, lakini vilevile ukiangalia kifungu 221300 *education materials, supplies and services,* kwa hiyo vifungu hivi viwili vitasaidia kutoa elimu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakwenda moja kwa moja vote 31, programu 50 na *sub-vote* 270200, *current grant international organisations*. Ukiangalia katika kipengele hiki fedha ambayo kimetengewa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimetoa ushauri kwamba, fedha kwa ajili ya elimu kwa vyombo vya habari iongezwe zaidi kwa sababu ni ndogo zaidi kuliko kiwango hiki kilichopo hapa. Sasa napenda Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba, hizi *International Organisations* ni zipi ambazo zimepata kutengewa kiwango hiki cha pesa na ni kwa ajili gani? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha tunazolipa kwenye Mikataba ya Kimataifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kasma 270800, *current grant to non financial public unit*. Ambayo kimsingi ndiyo ya ruzuku ya *NEMC* ambayo ndiyo mhimili wa kusimamia Sheria za Mazingira. Nieleze kwamba masikitiko yangu ni kwamba, ruzuku hii imepungua kutoka bilioni nne mpaka bilioni 3.7. Naelewe ukomo ulikuwa bilioni nne lakini bado ruzuku imepungua, sasa ningependa kupata ufafanuzi kuhusu jambo moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wa maandishi niliomba kwamba kwa kuwa Mkoa wa Dar

es Salaam ulikumbwa na mafuriko hivi karibuni na sababu mojawapo ikiwa ni mabadiliko ya tabia nchi na Mkoa wa Dar es Salaam una mito na vijito. Kwa Jimbo la Ubungo peke yake kuna Kibangu, kuna Mburahati, kuna Ubungo na mito mbalimbali. Sasa nikaomba kwamba *NEMC* iandae mradi wa kuweza kufanya menejimenti ya mito na vijito kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na mamlaka nyingine za Kiserikali. Ningeomba kauli ya Ofisi ya Makamu wa Rais kama *NEMC* iko tayari kuandaa mradi maalum kwa ajili ya jambo hili kwa sababu ya Fungu hili la *NEMC*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika lakini maswali ya *development* hayapo kwenye *vote* hii. Hilo sio suala la kisera bwana, hilo suala la Ubungo sio, suala la kisera linatakitwa li-*cut across* nchi nzima kama sera. Mheshimiwa Waziri hebu mjibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuriko yaliyotokea Dar es Salaam tumelielezea kwa kina, lakini vilevile limesababishwa na wananchi waliojenga kandokando mwa fukwe na tuliahidi kwamba tutabomoa, zoezi hili tumelifanya mwaka mzima la kufanya tathmini na kuhakikisha kwamba wale tunaowabomolea ni kweli wamekiuka Sheria za Mazingira. Kwa hiyo, kuanzia sasa wakati wowote tutabomoa ili kuongeza upana wa ule mto unaoelekea baharini.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika hiyo progamu 50

ningependa kupata ufafanuzi. Katika mchango wangu wa maandishi kifungu hicho cha 270800 kwamba Serikali sasa iweke jitahada za makusudi kushirikiana na Baraza la Mazingira kwa ajili kuwashirikisha wananchi katika utunzaji wa mazingira badala ya kutumia mfumo uliokuwepo sasa hivi, elimu inapitia kwenye radio na mipango inayowekwa inakuwa haiwagusi na kuwashirikisha moja kwa moja wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nieleze kwamba tuna mpango mahususi kabisa wa kutoa semina katika Halmashauri na kama ataangalia kwenye kitabu chetu ataona jinsi ambavyo mwaka jana tumezitolea semina Halmashauri mbalimbali. Lakini tuchukue ushauri wake na tutaona namna tutakavyokuwa tunautekeleza mwakani.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumebakiza dakika kumi kufika saa mbili na dakika 15 ambao ndiyo mwisho wa dakika zangu 30. Kwa hali hiyo sasa tutahoji mafungu yote kwa jumla wake kwa mujibu wa Kanuni na mamlaka niliyopewa.

## MIPANGO YA MAENDELEO

## FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 - *Administration and HR Managt. ... ...* Shs 3,200,000,000/=

Kif. 5001 - *Environment ... ... ... ... ... ... ... ...* Shs 7,070,000,000/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia makadario ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi za Makamu wa Rais, Fungu -,26 Makamu wa Rais na 31 Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili na Naibu Waziri kwa kazi hii ambayo tumeikamilisha, basi niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa Majukumu katika Ofisi hiyo ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha uliotajwa ili shughuli hizo ziweze kwenda sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hapa Taarifa kutoka Ofisi ya Kambi ya Upinzani niwatangazie kwamba Kiongozi wa Ofisi ya Kambi ya Upinzani alikuwa nje ya Shughuli za Bunge kikazi sasa amerejea na ataendelea kuwepo tena. Kwa hiyo naomba nitangaze tangazo hilo.

Vile vile nimepokea tangazo kutoka *Bunge Sports Club*. Wachezaji wa *Bunge Sports Club* wahudhurie mazoezi kesho asubuhi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo kati ya Washabiki wa Yanga na wale wa Simba tarehe 7/7/2012, huko Dar es Salaam. Wanasema lengo kuu la mchezo huu ni kuchangia gharama za ujenzi wa mabweni ya wasichana kwenye shule za sekondari zenye upungufu huo nchini kote. Mamlaka ya Elimu Tanzania wakishirikiana na *Global Publishers* ndiyo walioandaa mchezo huu pamoja na michezo mingine. Kwa hiyo Wachezaji wote wameombwa tafadhali sana kesho wahudhurie kwenye mazoezi kwa sababu baada ya mazoezi kesho asubuhi timu hizo zote mbili na wameomba hapa nizisome kama nitakuwa na muda zitaelekea katika maeneo ya kambi ambazo zimeandaliwa kwa ajili yao.

Timu ya Yanga baada ya mazoezi ya kesho asubuhi wataelekea Namanyere, Sumbawanga na

timu ya Simba wao wamesema wataelekea Chambani, Pemba. *(Kicheko)*

Sasa nimeombwa niwataje wachezaji wenyewe kusudi wajijue kwa ajili ya hayo maandalizi. Timu ya Yanga itaongozwa na Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mkuu wa Msafara, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mwanakhamis Said na kila timu ina watumishi hawa wa Yanga watumishi wake ni Helen Mbeba, Michael Kadebe, Christopher Kannonyele na Paul Chima.

Kikosi cha Simba kitaongozwa na Iddi Azan, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Kocha Mkuu na ambaye ni Naibu Waziri; Mheshimiwa Amos Makala, Naibu Waziri; Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri na Wabunge wengine ambao ni Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Joshua Nasari, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Yusuph Masauni, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Raya Ibrahim Hamis, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Daktari Hamis Kigwangala na watumishi wa Bunge ni Waziri Kizingiti, Abeid Kikula na Yona Kirumbi.

Waheshimiwa Wabunge mtaanza kuzipima timu hizi na kambi zao wanazokwenda kuziweka huko wanakoelekea na mnaweza kutabili ushindi wa shughuli hiyo ya ljumaa kwa kadiri ya muonekano.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema haya nawashukuru sana, tumekamilisha shughuli za leo. Naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asabuhi.

*(Saa 2.15 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 5 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*